	Robo ya tatu	214.8	195.8	227.8	295.3	134.3	179.6	172.9	170.3	131.5	195.1	203.3	114.4	206.9
	Robo ya nne	224.0	196.2	270.1	306.8	136.8	178.6	157.2	187.4	129.7	193.8	217.2	118.9	213.8
FAHIRISI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAFANYAKAZI WA KIMA CHA KATI DAR ES SALAAM (DEC. 2015 = 100)														
Mwaka	Vyakula na vinywaji baridi	Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku	Mavazi ya nguo na viatu	Nishati, Maji na Makazi	Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba	Gharama za Afya	Usafirishaji	Mawasiliano	Utamaduni na Burudani	Elimu	Hoteli na Migahawa	Bidhaa na huduma nyinginezo	FAHIRISI BIDHAA ZOTE	
2010	Robo ya kwanza	64.9	67.0	70.8	49.0	75.0	77.1	68.2	96.9	73.3	67.4	68.5	69.7	63.9
	Robo ya pili	66.0	66.2	71.4	49.6	74.5	77.1	68.2	96.8	73.0	67.4	68.6	69.4	64.6
	Robo ya tatu	66.3	67.3	71.8	50.8	75.4	77.1	68.4	97.3	75.4	67.4	69.2	69.5	65.1
	Robo ya nne	66.7	68.9	72.1	51.7	75.9	77.1	68.8	97.3	75.2	67.4	69.4	69.1	65.6
2011	Robo ya kwanza	69.8	69.5	74.0	54.2	78.8	79.0	70.2	97.3	75.8	67.1	68.6	70.9	67.9
	Robo ya pili	70.9	70.1	75.9	56.5	81.3	80.6	71.0	97.3	76.8	67.0	69.5	73.4	69.3
	Robo ya tatu	72.1	71.3	75.9	57.6	82.0	80.8	71.1	97.4	77.0	67.2	70.0	75.1	70.3
	Robo ya nne	75.1	72.0	76.3	58.1	82.5	80.8	71.6	97.6	77.7	67.3	70.0	75.9	72.1
2012	Robo ya kwanza	82.9	76.0	84.8	64.1	83.8	83.0	73.6	97.9	81.3	73.8	74.4	79.5	78.4
	Robo ya pili	85.9	78.7	87.6	67.5	87.9	87.0	78.2	98.3	86.3	79.1	77.0	81.9	81.6
	Robo ya tatu	87.1	81.2	89.5	68.4	89.0	87.9	78.5	98.4	89.2	81.3	78.6	83.1	82.7
	Robo ya nne	87.6	82.2	91.9	69.4	89.6	88.8	78.1	98.5	89.4	82.7	79.5	84.6	83.4
2013	Robo ya kwanza	94.6	82.5	94.0	70.7	90.1	90.0	78.0	98.7	90.0	83.5	80.0	85.4	87.6
	Robo ya pili	94.6	83.5	94.7	73.7	90.4	90.1	83.6	99.0	90.8	84.2	80.7	86.0	88.6
	Robo ya tatu	92.7	86.2	95.6	76.2	90.8	91.3	88.0	99.2	91.5	85.9	81.6	88.2	88.5
	Robo ya nne	91.7	88.0	95.7	77.5	91.3	91.7	89.5	99.2	92.2	86.8	82.5	88.8	88.4
2014	Robo ya kwanza	98.1	88.8	96.0	80.3	92.1	92.2	93.5	99.3	92.6	91.8	83.5	90.2	92.8
	Robo ya pili	99.1	89.0	96.6	82.8	93.2	94.8	94.2	99.5	93.2	94.3	85.8	90.6	94.2
	Robo ya tatu	97.3	92.9	97.3	86.8	96.7	97.0	96.3	100.0	95.0	95.9	88.0	93.6	94.5
	Robo ya nne	93.7	97.0	98.0	89.6	99.0	97.8	97.7	100.0	97.2	95.9	90.5	95.7	93.5
2015*	Robo ya kwanza	97.3	97.9	98.5	93.4	99.6	97.8	98.6	100.2	97.2	99.0	93.8	96.0	96.5
	Robo ya pili	100.1	98.1	98.9	96.7	99.3	97.8	99.3	100.3	97.3	99.9	96.4	96.6	98.9
	Robo ya tatu	101.8	98.9	99.0	99.4	99.4	98.4	100.5	100.2	98.2	100.0	98.0	96.7	100.6
	Robo ya nne	100.4	100.0	99.8	99.5	99.9	99.6	100.1	100.0	100.1	100.0	99.0	99.2	100.0
2016	Robo ya kwanza	101.81	100.94	99.84	108.37	99.89	106.44	99.44	100.00	100.34	97.77	100.70	101.37	102.05
	Robo ya pili	104.35	100.23	100.67	111.35	101.13	111.18	99.79	100.65	100.98	97.34	105.93	102.20	104.35
	Robo ya tatu	103.90	101.28	99.83	107.36	100.24	113.92	100.57	101.22	101.05	97.34	106.92	102.16	103.81
	Robo ya nne	102.52	102.55	100.25	110.34	102.43	114.81	99.94	101.34	101.94	97.34	105.83	103.52	103.79

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Dec. 2015=100

Fahirisi za Bei kuanzia mwaka 2004 hadi 2009 zilitumia mgawanyo wa makundi kwa tafsiri ya Kitaifa (National Classification) hivyo fahirisi hizi hazizewezi kuungwa na fahirisi zilizozia mwaka 2010 zilizotumia mgawanyo wa makundi kwa mfumo wa kimataifa wa COICOP

FAHIRISI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WENYE KIPATO CHA JUU DAR ES SALAAM (2001=100)

Jedwali Na.12

Mwaka	Chakula	Vinyaji na Sigara	Kodi ya Nyumba	Umeme, Mafuta ya Taa, Maji	Nguo na Viatu	Fenicha, Vyombo Vya Ny-	Huduma Mahitaji ya Nyumbani	Huduma za Afya	Michezo na Starehe	Usafiri	Elimu	Vinginevyo	Fahirisi Bidhaa Zote
2008 Machi	177.3	172.0	160.0	253.9	135.2	130.2	142.4	125.8	124.5	178.7	185.1	79.3	174.6
Juni	184.2	171.4	173.3	260.0	135.3	133.8	146.7	128.2	129.5	181.5	185.1	86.1	179.1
Septemba	191.6	182.0	180.0	270.7	128.8	140.5	155.8	131.3	131.8	217.1	188.9	91.1	192.6
Desemba	198.3	192.3	186.7	301.4	130.9	149.4	164.2	135.8	135.4	214.2	190.9	91.8	198.0
2009 Machi	219.8	198.3	200.0	275.0	130.0	157.4	169.0	149.3	191.2	212.7	193.0	92.0	206.3
Juni	225.3	199.3	200.0	275.2	134.5	163.9	170.7	155.0	193.1	210.2	193.3	93.0	208.7
Septemba	237.8	237.8	200.0	293.0	139.7	176.4	180.1	172.5	190.8	225.0	193.5	94.9	220.2
Desemba	247.4	207.4	200.0	305.1	147.2	137.0	163.7	185.5	189.4	228.1	195.9	94.7	225.9
FAHIRISI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WENYE KIPATO CHA JUU DAR ES SALAAM (Dec. 2015=100)													
Mwaka	Vyakula na vinywaji baridi	Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku	Mavazi ya nguo na viatu	Nishati, Maji na Makazi	Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba	Gharama za Afya	Usafirishaji	Mawasiliano	Utamaduni na Burudani	Elimu	Hoteli na Migahawa	Bidhaa na huduma nyinginezo	FAHIRISI BIDHAA ZOTE
2010 Robo ya kwanza	54.8	68.9	75.2	63.9	82.3	84.4	67.3	94.3	82.5	82.1	65.4	83.0	63.4
Robo ya pili	57.0	72.3	74.7	65.1	82.8	84.4	67.8	94.7	84.8	82.1	65.7	85.2	64.9
Robo ya tatu	56.8	72.4	78.6	68.2	85.5	84.4	68.5	94.9	87.1	82.1	66.3	86.7	65.8
Robo ya nne	57.7	72.6	81.1	67.7	84.6	84.4	69.1	94.9	88.2	82.1	65.9	87.1	66.3
2011 Robo ya kwanza	61.1	73.8	80.7	70.9	86.7	85.2	70.8	94.9	89.3	82.1	67.5	83.9	68.7
Robo ya pili	62.4	74.8	83.8	72.0	89.5	87.7	77.2	94.9	91.2	82.1	72.2	85.6	70.8
Robo ya tatu	64.5	76.7	84.2	74.4	88.9	87.7	80.5	95.2	91.8	82.5	76.4	86.9	72.8
Robo ya nne	68.8	77.3	85.7	76.4	90.3	89.5	82.9	95.4	92.0	82.7	77.2	88.4	75.7
2012 Robo ya kwanza	72.8	78.2	88.7	77.3	92.9	91.5	82.4	95.4	92.8	82.7	78.7	91.3	78.0
Robo ya pili	74.2	78.6	89.2	79.8	94.2	91.9	83.3	95.4	93.0	82.7	79.6	95.4	79.5
Robo ya tatu	74.9	80.5	91.0	81.8	95.0	92.0	83.3	95.5	93.3	82.7	81.5	95.7	80.4
Robo ya nne	77.3	81.4	93.0	83.1	95.7	93.3	85.2	95.6	93.4	82.7	82.9	96.1	82.2
2013 Robo ya kwanza	83.1	81.4	93.8	83.9	96.1	94.8	86.4	95.5	93.9	84.4	84.9	96.4	85.5
Robo ya pili	81.7	82.1	95.2	83.4	96.3	94.8	94.1	95.7	96.1	84.4	85.3	96.8	85.6
Robo ya tatu	82.8	87.7	96.3	84.3	97.1	94.8	95.6	95.7	96.3	84.4	85.8	97.2	86.6
Robo ya nne	84.2	90.4	96.4	86.4	97.7	94.8	96.2	95.7	96.0	84.7	87.4	97.2	87.9
2014 Robo ya kwanza	88.5	90.4	97.5	87.6	97.7	95.5	96.6	95.7	98.8	95.7	87.9	99.0	90.6
Robo ya pili	87.9	90.4	97.6	88.1	98.5	97.7	97.6	95.7	98.9	98.6	88.0	99.8	90.7
Robo ya tatu	88.0	92.9	97.5	92.7	97.8	97.5	98.7	95.7	99.3	98.6	90.4	101.2	91.8
Robo ya nne	89.7	95.6	97.3	95.1	98.2	97.3	99.3	95.6	99.8	98.6	92.5	99.9	93.3
2015* Robo ya kwanza	92.5	96.7	97.8	95.2	98.3	97.5	101.2	97.6	99.7	100.0	95.4	100.2	95.1
Robo ya pili	95.1	98.1	97.8	96.0	98.2	97.5	102.5	97.7	100.0	100.0	97.5	98.6	96.8
Robo ya tatu	97.6	99.0	98.5	97.1	98.7	98.4	102.6	98.5	100.2	100.0	97.5	98.7	98.3
Robo ya nne	100.0	99.6	99.3	101.1	99.6	99.3	99.9	100.0	100.1	100.0	98.4	99.6	100.0
2016 Robo ya kwanza	102.6	100.4	99.8	105.2	100.2	107.3	98.6	100.0	100.4	98.6	100.4	101.4	101.0
Robo ya pili	105.3	100.9	100.7	107.2	103.0	111.9	98.9	100.6	101.3	98.4	103.1	102.0	102.5
Robo ya tatu	106.0	102.3	99.7	104.3	100.1	114.0	99.7	101.2	101.0	98.4	102.9	102.7	102.4
Robo ya nne	104.4	102.8	100.2	106.9	104.4	115.0	99.8	101.3	101.9	98.4	102.4	105.0	102.8

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Dec. 2015=100

Fahirisi za Bei kuanzia mwaka 2004 hadi 2009 zilitumia mgawanyo wa makundi kwa tafsiri ya Kitaifa (National Classification) hivyo fahirisi hizi haziziwezi kuungwa na fahirisi zilizozia mwaka 2010 zilizotumia mgawanyo wa makundi kwa mfumo wa kimataifa wa COICOP

**FAHIRISI YA GHARAMA YA MAISHA YA WATU WENYE KIPATO
CHA JUU DAR-ES-SALAAM (Dec. 2015=100)**

Jedwali Na. 13

Mwaka	M I E Z I				Wastani	Badiliko Asilimia
	Machi	Juni	Sept.	Desemba		
2000	24.18	24.18	25.27	25.83	24.87	6.2
2001	30.87	28.15	27.03	25.83	27.97	12.5
2002	28.96	28.88	28.93	28.89	28.91	6.6
2003	29.92	30.22	30.19	30.24	30.14	4.2
2004	30.98	31.77	32.30	33.02	32.02	6.2
2005	33.62	33.88	34.76	36.80	34.77	8.6
2006	37.88	38.51	38.90	40.13	38.86	11.8
2007	42.19	43.45	44.68	45.76	44.02	13.3
2008	48.86	50.13	53.91	55.41	52.08	18.3
2009	57.72	58.40	61.62	63.21	60.24	15.7
2010	63.41	64.89	65.82	66.29	65.10	8.1
2011	68.73	70.77	72.83	75.67	72.00	10.6
2012	78.04	79.50	80.40	82.20	80.04	11.2
2013	85.48	85.58	86.64	87.93	86.41	8.0
2014	90.61	90.68	91.84	93.27	91.60	6.0
2015*	95.14	96.78	98.27	100.00	97.55	6.5
2016	101.02	102.52	102.43	102.81	102.20	4.8

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Dec. 2015=100

FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI - TANZANIA BARA (2001=100)

Jedwali Na.14

Mwaka	Chakula	Vinywaji na Sigara	Kodi ya Nyumba	Umeme, Mafuta ya Taa, Maji	Nguo na Viatu	Fenicha, Vyombo Vya Nyumbani	Huduma Mahitaji ya Nyumbani	Huduma za Afya	Michezo na Starehe	Usafiri	Elimu	Vinginevyo	Fahirisi Bidhaa Zote
2008 Robo ya kwanza	163.4	146.8	138.9	161.6	105.3	116.6	115.1	113.6	110.0	132.9	106.2	103.4	149.2
Robo ya pili	165.1	148.5	139.5	172.0	106.4	118.1	117.1	114.7	111.4	136.5	107.8	103.9	151.7
Robo ya tatu	164.5	149.7	141.6	179.2	106.4	120.1	116.8	117.4	114.5	141.0	110.8	104.2	152.8
Robo ya nne	175.0	152.1	141.6	172.5	108.6	122.1	119.1	120.3	117.6	139.6	112.7	105.2	158.4
2009 Robo ya kwanza	193.5	154.8	156.4	164.5	109.7	124.8	120.7	122.3	121.4	137.7	116.9	106.9	168.7
Robo ya pili	194.0	158.2	156.5	158.7	112.5	126.1	122.7	125.9	121.4	135.3	122.4	108.6	168.9
Robo ya tatu	193.6	165.7	159.4	168.9	115.7	128.0	123.0	126.1	124.6	140.3	122.4	108.3	170.6
Robo ya nne	203.8	170.9	159.6	181.7	115.6	127.1	126.0	126.1	127.6	140.3	122.7	106.3	178.2

FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI - TANZANIA BARA (Dec. 2015=100)

Mwaka	Vyakula na vinywaji baridi	Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku	Mavazi ya nguo na viatu	Nishati, Maji na Makazi	Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba	Gharama za Afya	Usafirishaji	Mawasiliano	Utamaduni na Burudani	Elimu	Hoteli na Migahawa	Bidhaa na huduma nyinginezo	FAHIRISI BIDHAA ZOTE
2010 Robo ya kwanza	54.4	66.1	68.2	54.3	72.0	84.6	79.4	101.3	81.7	83.4	69.5	72.4	61.3
Robo ya pili	55.2	64.8	68.4	57.2	72.9	84.8	79.2	102.0	82.7	83.4	69.5	72.9	62.1
Robo ya tatu	54.2	66.2	70.2	58.1	74.1	84.9	78.9	102.2	84.2	81.9	69.8	74.6	61.9
Robo ya nne	54.9	66.6	71.7	58.1	74.8	84.6	78.9	102.3	83.9	81.3	68.9	74.5	62.4
2011 Robo ya kwanza	59.0	67.7	73.6	61.9	80.5	85.7	80.4	100.2	84.7	85.6	72.4	74.6	65.8
Robo ya pili	61.2	68.7	75.0	66.2	83.1	86.2	84.5	99.9	85.2	85.9	73.9	75.4	68.2
Robo ya tatu	64.4	69.7	76.9	70.3	84.6	86.5	86.6	100.7	86.1	85.9	75.9	77.9	71.0
Robo ya nne	69.0	70.3	79.5	71.8	86.1	87.6	88.1	100.7	86.3	85.9	78.0	80.3	74.2
2012 Robo ya kwanza	74.7	73.1	83.8	73.4	88.9	88.2	88.8	99.6	90.9	89.2	83.7	82.9	78.6
Robo ya pili	76.3	75.5	86.5	76.3	90.7	89.0	90.4	99.1	93.7	90.0	87.3	85.2	80.5
Robo ya tatu	76.3	83.3	87.8	80.4	91.8	89.4	90.5	99.1	96.0	90.0	88.5	85.9	81.4
Robo ya nne	78.5	85.4	89.0	84.1	93.1	90.1	90.5	98.9	95.7	90.0	90.5	87.1	83.4
2013 Robo ya kwanza	83.4	87.6	90.5	86.1	94.4	91.0	90.7	98.7	95.6	91.7	91.8	88.6	86.7
Robo ya pili	82.9	88.3	91.2	90.1	94.6	91.7	96.1	98.5	96.0	91.9	92.2	89.4	87.3
Robo ya tatu	81.6	92.4	92.3	90.7	95.0	91.9	97.8	99.0	96.4	92.1	92.3	90.9	86.9
Robo ya nne	83.7	93.5	92.8	92.0	95.6	92.0	98.4	99.1	96.4	92.1	92.9	91.7	88.4
2014 Robo ya kwanza	88.9	93.8	93.8	96.8	96.1	92.8	98.8	99.2	96.6	96.8	93.3	92.6	91.9
Robo ya pili	89.7	93.8	94.1	98.7	96.8	95.2	99.4	99.5	96.7	96.8	94.5	96.6	92.9
Robo ya tatu	88.6	96.8	94.5	100.5	96.9	95.8	100.0	99.9	96.9	96.8	95.2	96.6	92.7
Robo ya nne	89.2	98.6	95.5	101.1	96.9	96.2	99.6	99.7	97.0	96.8	96.1	96.7	93.3
2015* Robo ya kwanza	93.5	98.8	97.0	101.6	97.4	96.6	97.5	99.8	97.1	98.6	97.6	97.4	95.7
Robo ya pili	97.3	98.8	97.8	99.8	97.4	97.1	97.6	99.8	97.5	100.0	98.9	97.8	97.8
Robo ya tatu	97.5	99.4	99.1	101.1	98.7	98.4	100.3	99.7	98.9	100.0	99.8	98.5	98.5
Robo ya nne	98.9	99.8	99.7	100.9	99.3	99.5	99.8	100.0	100.1	100.0	100.0	99.8	99.4
2016 Robo ya kwanza	102.1	100.4	101.0	103.8	100.5	101.6	99.1	99.5	100.4	101.8	100.5	100.8	101.4
Robo ya pili	104.2	103.2	101.9	107.3	101.5	103.2	98.9	98.8	100.9	102.3	103.6	101.4	103.0
Robo ya tatu	103.9	104.4	102.8	107.8	101.9	104.0	99.8	99.1	101.2	102.6	104.4	101.9	103.3
Robo ya nne	105.1	104.9	103.3	110.1	103.1	104.6	100.0	99.1	101.7	102.6	104.1	102.6	104.2

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Dec. 2015=100

Fahirisi za Bei kuanzia mwaka 2005 hadi 2009 zilitumia mgawanyo wa makundi kwa tafsiri ya Kitaifa (National Classification) hivyo fahirisi hizi hazizewezi kuungwa na fahirisi zilizonzia mwaka 2010 zilizotumia mgawanyo wa makundi kwa mfumo wa kimataifa wa COICOP

**FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO
NA WAKAZI WA MIJINI TANZANIA BARA (Dec 2015=100)**


Jedwali Na.15

Mwaka	R o b o y a M w a k a				Wastani wa Fahirisi	Badiliko Asilimia
	Robo ya Kwanza	Robo ya Pili	Robo ya Tatu	Robo ya Nne		
2000	33.2	33.0	31.8	32.3	32.6	6.0
2001	35.0	34.7	33.4	33.8	34.2	5.1
2002	35.4	35.6	35.5	36.3	35.7	4.3
2003	37.1	37.6	37.4	38.3	37.6	5.3
2004	39.0	39.0	39.1	40.4	39.4	4.7
2005	40.6	41.2	41.3	42.4	41.4	5.0
2006	43.8	44.9	43.7	45.1	44.4	7.3
2007	46.9	47.5	47.4	48.2	47.5	7.0
2008	51.1	51.9	52.3	54.2	52.4	10.3
2009	57.7	57.8	58.4	61.0	58.7	12.1
2010	61.3	62.1	61.9	62.4	61.9	5.5
2011	65.8	68.2	71.0	74.2	69.8	12.7
2012	78.6	80.5	81.4	83.4	81.0	16.0
2013	86.7	87.3	86.9	88.4	87.3	7.9
2014	91.9	92.9	92.7	93.3	92.7	6.1
2015*	95.7	97.8	98.5	99.4	97.9	5.6
2016	101.4	103.0	103.3	104.2	102.9	5.2

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Dec. 2015=100

MWENENDO WA KASI YA UPANDAJI BEI - Tanzania Bara



**FAHIRISI MBALIMBALI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO
NA WAKAZI WA MIJINI-TANZANIA BARA (Dec.2015=100)**

Jedwali Na.16

Mwaka	F A H I R I S I			WAKAZI MIJINI TANZ. BARA	B A D I L I K O %			WAKAZI MIJINI TANZ. BARA
	KIPATO CHA				KIPATO CHA			
	CHINI	KATI	JUU		CHINI	KATI	JUU	
2000	23.8	27.9	24.9	32.6	1.7	2.5	6.2	6.0
2001	25.9	29.1	28.0	34.2	8.5	4.5	12.5	5.1
2002	26.9	30.2	28.9	35.7	3.8	3.5	3.3	4.3
2003	28.4	30.8	30.1	37.6	5.8	2.3	4.3	5.3
2004	30.2	33.4	32.0	39.4	6.4	8.2	6.2	4.7
2005	32.7	36.0	34.8	41.4	8.3	7.9	8.6	5.0
2006	36.5	39.3	38.9	44.4	11.5	9.2	11.8	7.3
2007	39.9	43.9	44.0	47.5	9.3	11.5	13.3	7.0
2008	46.8	50.6	52.1	52.4	17.3	15.3	18.3	10.3
2009	54.7	58.9	60.2	58.7	16.8	16.4	15.7	12.1
2010*	61.9	64.8	65.1	61.9	13.2	10.0	8.1	5.5
2011	66.5	69.9	72.0	69.8	7.4	7.9	10.6	12.7
2012	79.0	81.5	80.0	81.0	18.8	16.6	11.2	16.0
2013	86.3	88.3	86.4	87.3	9.3	8.3	8.0	7.9
2014	93.0	93.7	91.6	92.7	7.7	6.2	6.0	6.1
2015*	98.0	99.0	97.5	97.9	5.4	5.6	6.5	5.6
2016	102.2	103.5	102.2	102.9	4.3	4.5	4.8	5.2

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Dec. 2015=100

SURA YA 2

HALI YA UCHUMI WA DUNIA NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

HALI YA UCHUMI WA DUNIA

Ukuaji wa Uchumi

31. Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia iliendelea kusuasua na kutoridhisha kwa mwaka 2016 ikilinganishwa na miaka iliyotangulia. Mwaka 2016, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia ilikuwa asilimia 3.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.2 kwa mwaka 2015. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia ni matokeo ya kupungua kwa ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizoendelea ambapo ukuaji wa uchumi kwa nchi zinazoendelea haukubadilika.

32. Mwaka 2016, kasi ya ukuaji wa pato la nchi zilizoendelea ulipungua ikilinganishwa na kipindi kilichotangulia. Hali hiyo ilitokana na kupungua kwa ukuaji wa uchumi wa Marekani, Ulaya na Japani. Kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizoendelea kilikuwa asilimia 1.6 mwaka 2016 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.1 mwaka 2015. Kasi ndogo ya ukuaji ilitokana na kudhoofu kwa mahitaji ya bidhaa na huduma kutoka nje, kupungua kwa tija kwenye uzalishaji na kupungua kwa kasi ya uwekezaji.

33. Mwaka 2016, kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi zinazoendelea ilikuwa asilimia 4.1 kama ilivyokuwa kwa mwaka uliotangulia. Ukuaji huu kwa nchi zinazoendelea ulichangiwa zaidi na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi kwa nchi za China na Nchi za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara. Hali hiyo ilichangiwa na bei ndogo za bidhaa katika soko la dunia, kupungua kwa uwekezaji kutoka sekta binafsi na kupungua kwa uhitaji wa bidhaa kutoka nje. Aidha, uwepo wa ukame kutokana na El Nino uliathiri shughuli za kilimo na uzalishaji wa umeme wa maji na hivyo kupunguza uzalishaji wa bidhaa na huduma. Kutokana na athari hizo, kasi ya ukuaji wa pato la nchi za Asia zinazoendelea ikijumuisha China na India ilikuwa asilimia 6.3 mwaka 2016 ikilinganishwa asilimia 6.7 mwaka 2015. Kwa upande wa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara kasi ya ukuaji wa uchumi ilipungua hadi asilimia 1.6 mwaka 2016, kutoka ukuaji wa asilimia 3.4 mwaka 2015.

Jedwali Na 2.1: Pato la Dunia 2009 – 2016

	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016
<i>Ukuaji kwa asilimia</i>								
Pato la Dunia	0.0	5.4	4.2	3.5	3.3	3.4	3.2	3.1
Nchi Zilizoendelea	-3.4	3.1	1.7	1.2	1.2	1.9	2.1	1.6
Nchi Zinazoendelea	3.1	7.4	6.3	5.3	4.9	4.6	4.1	4.1
Nchi za Asia Zinazoendelea	7.5	9.6	7.8	6.9	6.9	6.8	6.7	6.3
Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara	4.0	6.6	5.0	4.3	5.2	5.1	3.4	1.6

Chanzo: Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Januari 2017

34. Mwaka 2016, mfumuko wa bei wa dunia uliongezeka na kuwa wa wastani wa asilimia 2.9 kutoka wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2015. Mwenendo huu uliongezeka kutokana na kulegezwa kwa sera za bajeti na fedha kwa baadhi ya nchi, ukame uliotokana na mabadiliko ya tabia nchi pamoja na uwepo wa El nino ambao uliathiri upatikanaji wa mvua. Ongezeko hili liliwiana na mfumuko wa bei ya mlaji wa mwisho kwa nchi zilizoendelea, zinazoendelea za Asia na nchi zilizo Kusini mwa Bara la Afrika. Mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea uliongezeka na kuwa asilimia 0.8 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 0.3 mwaka 2015. Katika kipindi hicho, mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea za Asia uliongezeka hadi asilimia 3.1 ikilinganishwa na asilimia 2.7 mwaka 2015.

Mwenendo wa Biashara Duniani

35. Mwaka 2016, ukuaji wa shughuli za biashara duniani uliendelea kudhoofika ambapo kasi yake ilikuwa asilimia 1.3 ikilinganishwa na asilimia 2.6 mwaka 2015. Ukuaji huo ni matokeo ya kupungua kwa ukuaji wa uchumi duniani ukiambatana na mabadiliko ya muundo katika bidhaa za biashara na uzalishaji wa bidhaa zenyewe. Aidha, matatizo katika taasisi za fedha za kimataifa yaliathiri kwa kiasi kikubwa shughuli za biashara nchini China na kwa washirika wake wa kibiashara ambapo kulijitokeza hofu ya kuporomoka kwa thamani ya sarafu zao.

Jedwali Na.2.2: Mwenendo wa Biashara Duniani 2016 (USD bilioni na Asilimia)

	Mauzo ya Nje					Manunuzi kutoka Nje				
	<i>Thamani</i>	<i>Badiliko kwa mwaka (Asilimia)</i>				<i>Thamani</i>	<i>Badiliko kwa mwaka (Asilimia)</i>			
	2016	2010-16	2014	2015	2016	2016	2010-16	2014	2015	2016
Dunia	15,464	0.6	0.3	-13.5	-3.3	15,799	0.7	0.6	-12.5	-3.2
Amerika ya Kaskazini	2,219	2.1	3.1	-8.0	-3.2	3,067	2.3	3.4	-4.5	-2.9
Marekani	1,455	2.2	2.6	-7.3	-3.2	2,251	2.3	3.6	-4.0	-2.8
Canada	390	0.1	3.9	-13.9	-4.8	417	0.6	0.9	-9.1	-4.5
Mexico	374	3.8	4.4	-4.1	-1.8	398	4.2	5.3	-1.5	-1.9
Amerika ya Kusini na Kati	511	-2.4	-7.0	-21.1	-5.6	533	-1.5	-4.0	-16.4	-14.5
Brazil	185	-1.4	-7.0	-15.1	-3.1	143	-4.7	-4.5	-25.2	-19.8
Nchi nyingine za Amerika ya Kusini na Kati	326	-2.9	-6.9	-24.1	-6.9	389	-0.2	-3.7	-12.3	-12.4
Ulaya	5,942	0.8	0.5	-12.5	-0.3	5,920	0.0	1.2	-13.2	0.2
Umoja wa Nchi za Ulaya	5,373	0.6	1.3	-12.5	-0.3	5,330	-0.3	2.2	-13.4	0.1
Ujerumani	1,340	1.0	3.4	-11.2	1.0	1,055	0.0	2.2	-12.9	0.3
Ufaransa	501	-0.7	-0.1	-12.9	-0.9	573	-1.1	-0.7	-15.3	-0.1
Uholanzi	570	-0.1	0.2	-15.3	0.0	503	-0.4	0.0	-12.9	-1.9
Uingereza	409	-0.3	-6.6	-8.9	-11.0	636	1.2	4.6	-9.3	1.5
Italia	462	0.5	2.2	-13.7	0.9	404	-3.0	-1.1	-13.3	-1.6
Jumuiya ya Madola ya Nchi huru (CIS)	419	-5.5	-5.8	-13.9	-16.2	333	-3.6	-11.7	-32.4	-2.6
Shirikisho la Urusi	282	-5.7	-4.8	-31.3	-17.5	191	-4.3	-9.8	-37.3	-0.8
Afrika	346	-6.6	-7.6	-29.6	-11.5	501	0.7	0.4	-13.8	-9.5
Afrika ya Kusini	75	-3.2	-4.1	-11.7	-7.8	92	-0.9	-3.5	-14.2	-12.5
Afrika bila Afrika ya Kusini	271	-7.4	-8.2	-33.2	-12.5	409	1.1	1.3	-13.8	-8.8
Wauza mafuta Nje	113	-14.4	-13.6	-44.6	-27.6	143	-0.7	1.2	-19.1	-12.6
Wasiouza Mafuta Nje	158	1.7	1.6	-15.4	2.8	266	2.2	1.3	-10.4	-6.6
Mashariki ya Kati	766	-2.8	-4.3	-34.4	-9.5	665	2.3	2.1	-7.7	-7.2
Asia	5,262	1.9	2.6	-7.9	-3.7	4,781	0.9	0.1	-14.5	-4.7
China	2,098	4.9	6.0	-2.9	-7.7	1,587	2.2	0.5	-14.3	-5.5
Japan	645	-2.9	-3.5	-9.5	3.2	607	-2.2	-2.5	-20.2	-6.3
India	264	2.6	2.5	-17.1	-1.3	359	0.4	-0.5	-15.1	-8.6
Nchi zinazochipukia kiviwanda	1,131	0.3	1.3	-11.1	-3.5	1,041	-0.9	1.1	-16.6	-5.8
Nchi Masikini Duniani	145	-1.8	-3.5	-23.5	-6.0	228	5.1	6.5	-9.7	-3.0

Chanzo: Shirika la Biashara Duniani (WTO) Aprili 2016

36. Mwaka 2016, thamani ya mauzo ya bidhaa nje kwa nchi za Afrika ilipungua hadi dola za Marekani bilioni 346 ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 391.0 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 11.5. Aidha, thamani ya manunuzi ya bidhaa kutoka nje ilipungua hadi dola za Marekani bilioni 501 mwaka 2016 kutoka thamani ya manunuzi ya dola za Marekani 553.6 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 9.5. Kulingana na mwenendo huo wa biashara, nchi za Afrika zilipata nakisi kwenye urari wa biashara ya bidhaa nje yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 155 mwaka 2016 ikilinganishwa na urari wa biashara wenye nakisi ya dola za Marekani bilioni 162.6 mwaka 2015

Hali ya Uchumi wa Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara

37. Mwaka 2016, ukuaji wa Pato la nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ulikuwa asilimia 1.6 ikilinganishwa na asilimia 3.4 mwaka 2015. Ukuaji huo ni matokeo ya kuporomoka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi ambazo zinazuza mafuta kutoka wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2015 hadi asilimia 1.3 mwaka 2016. Hali hii ilitokana na bei ya bidhaa ghafi hususan mafuta katika soko la dunia kuwa chini na mazingira ya kiuchumi duniani kutokuwa rafiki kwa nchi hizo. Aidha, kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi nyingine kusini mwa Jangwa la Sahara ulipungua kutokana na kutokuwepo kwa hali nzuri ya hewa. Kwa nchi za kipato cha kati, kasi ya ukuaji wa uchumi ilipungua kutoka asilimia 2.7 mwaka 2015 hadi asilimia 0.4 mwaka 2016. Vile vile, kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za kipato cha chini ilipungua na kuwa asilimia 4.7 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 5.6 mwaka 2015.

38. Mwaka 2016, kutokana na uhaba wa mvua uliosababishwa na El nino kasi ya ukuaji wa bei kwa nchi za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara iliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 11.3 kutoka asilimia 7.0 mwaka 2015. Ongezeko la mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ulichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mfumuko wa bei kwa nchi zinazouza mafuta kutoka wastani wa asilimia 8.8 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 18.2 mwaka 2016. Aidha, mfumuko wa bei kwa nchi za kipato cha kati na cha chini uliongezeka hadi wastani wa asilimia 11.8 na asilimia 9.5 mwaka 2016 kutoka asilimia 7.2 na asilimia 6.3 mwaka 2015, kwa mtiririko huo.

**Jedwali Na.2.3: Mwenendo wa Baadhi ya Viashiria vya Uchumi kwa
Baadhi ya Nchi Kusini mwa Jangwa la Sahara: 2014 – 2016**

	Pato halisi la Taifa			Bei za Mlaji			Urari wa Biashara ya Nje		
	Ukuaji kwa mwaka			Ukuaji kwa mwaka			Sehemu ya pato la taifa		
	2014	2015	2016	2014	2015	2016	2014	2015	2016
Nchi Kusini mwa Jangwa la Sahara	5.1	3.4	1.6	6.3	7.0	11.3	-3.7	-5.9	-4.5
Nchi zinazouza mafuta	5.9	2.6	-1.3	7.1	8.8	18.2	-0.6	-4.7	-2.2
Nigeria	6.3	2.7	-1.7	8.0	9.0	15.4	0.2	-3.1	-16.6
Angola	4.8	3.0	0.0	7.3	10.3	33.7	-2.9	-8.5	-5.4
Equatorial Guinea	-0.5	-7.4	-9.9	4.3	1.7	1.5	-5.6	-16.8	-11.8
Gabon	4.3	4.0	3.2	4.5	0.2	2.5	8.1	-2.3	-5.3
Republic of Congo	6.8	2.3	1.7	0.9	2.0	4.0	-3.3	-21.0	-8.2
Chad	6.9	1.8	-1.1	1.7	3.7	0.0	-9.0	-12.4	-8.7
Cameroon	5.9	5.8	4.8	1.9	2.7	2.2	-4.3	-4.2	-4.2
South Sudan	2.9	-0.2	-13.1	1.7	52.8	476.0	2.1	-11.1	-0.5
Nchi za Kipato cha Kati	4.6	2.7	0.4	7.0	7.2	11.8	-2.4	-4.5	-3.0
Botswana	3.2	-0.3	3.1	4.4	3.0	3.2	15.6	7.2	4.1
Cape Verde	1.9	1.5	3.6	-0.2	0.1	0.1	-9.0	-4.3	-7.7
Ghana	4.0	3.9	3.3	15.5	17.2	17.0	-9.6	-7.5	-6.3
Kenya	5.3	5.6	6.0	6.9	6.6	6.2	-10.3	-6.8	-6.4
Lesotho	3.4	2.8	2.4	4.0	5.3	8.6	-7.9	-8.7	-8.0
Mauritius	3.6	3.5	3.5	3.2	1.3	1.5	-5.7	-4.9	-4.3
Namibia	6.5	5.3	4.2	5.3	3.4	6.6	-10.7	-12.9	-12.4
Senegal	4.3	6.5	6.6	-1.1	0.1	1.0	-8.9	-7.6	-8.4
Seychelles	6.2	5.7	4.9	1.4	4.0	-0.8	-12.0	-18.6	-18.7
South Africa	1.6	1.3	0.1	6.1	4.6	6.4	-5.3	-4.3	-3.3
Swaziland	2.5	1.7	0.5	5.7	5.0	7.0	3.3	9.2	-4.9
Zambia	5.0	3.0	3.0	7.8	10.1	19.1	2.1	-3.5	-4.5
Nchi za Kipato cha Chini	6.6	5.6	4.7	4.2	6.3	9.5	-8.8	-10.7	-9.3
Benin	6.5	5.0	4.6	-1.1	0.3	0.6	-8.7	-10.5	-10.0
Burkina Faso	4.0	4.0	5.2	-0.3	0.9	1.6	-8.0	-6.4	-6.0
Ethiopia	10.3	10.2	6.5	7.4	10.1	7.7	-7.9	-12.0	-10.7
Gambia	-0.2	4.4	2.3	6.2	6.8	8.3	-10.9	-15.2	-12.7
Madagascar	3.3	3.1	4.1	6.1	7.4	6.7	-0.3	-1.9	-2.3
Malawi	5.7	2.9	2.7	23.8	21.9	19.8	-8.5	-8.3	-15.8
Mali	7.0	6.0	5.3	0.9	1.4	1.0	-4.7	-5.1	-6.0
Mozambique	7.4	6.6	4.5	2.3	2.4	16.7	-38.2	-39.0	-33.5
Niger	7.0	3.5	5.2	-0.9	1.0	1.6	-14.1	-17.2	-17.8
Rwanda	7.0	6.9	6.0	1.8	2.5	5.3	-10.5	-13.5	-16.6
Sierra Leone	4.6	-21.1	4.3	8.3	9.0	9.7	-18.2	-15.5	-16.2
Tanzania	7.0	7.0	7.2	6.1	5.6	5.5	-9.5	-8.8	-8.8
Uganda	4.9	4.8	4.9	3.1	5.5	5.5	-8.7	-9.4	-8.7

Chanzo:-Shirika la Fedha Duniani (IMF) Oktoba 2016.

USHIRIKIANO WA UCHUMI KIMATAIFA

Jumuiya ya Afrika Mashariki

39. Kikao cha kawaida cha 17 cha Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kilifanyika katika Jiji la Arusha, Tanzania mwezi Machi 2016. Pamoja na mambo mengine, kikao hicho kilipokea taarifa ya mwaka ya Baraza la Mawaziri wa Jumuiya kwa kipindi cha Novemba 2014 hadi Novemba 2015 na hivyo kuridhishwa na maendeleo mazuri ya utekelezaji wa programu za Jumuiya. Aidha, kikao hakikuridhishwa na utekelezaji wa baadhi ya maagizo kwa baadhi ya nchi, mathalani, katika kuridhia itifaki mbalimbali. Sekretarieti ilielekezwa kuandaa orodha ya itifaki ambazo hazijaridhiwa ili nchi wanachama waziridhie na kuziwasilisha kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ifikapo tarehe 30 Julai 2016.

40. Kwa upande mwingine, kikao cha wakuu wa nchi za Jumuiya kililiagiza Baraza la Mawaziri wa Jumuiya kuipitia hati ya uanzishwaji wa Benki ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EADB) na kuijumuisha kwenye muundo wa Jumuiya. Aidha, Sekretarieti ilielekezwa kuandaa miongozo ya taasisi mbalimbali za Jumuiya kuhusiana na uanzishaji, utawala na utoaji wa taarifa. Vile vile, Baraza la Mawaziri wa Jumuiya liliagizwa kukamilisha kazi ya kutafuta mbinu thabiti za namna ya kugharamia shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuzingatia mapendekezo mbalimbali. Wakuu wa nchi za Jumuiya walipokea taarifa ya maombi ya uanachama wa nchi ya Sudani ya Kusini ambapo ombi hilo lilipitishwa na hivyo nchi ya Sudani ya Kusini kukubaliwa kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hati ya uanachama ilitiwa sahihi na Mwenyekiti wa Jumuiya Mhe. Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Rais wa Sudani ya Kusini Mhe. Generali Salva Kiir Mayardit.

41. Mwaka 2016, kikao cha 17 cha ziada kwa wakuu wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kiliitishwa katika Jiji la Dar es Salaam. Kikao hicho kilijadili taarifa ya Baraza la Mawaziri wa Jumuiya kuhusu makubaliano ya ushirikiano wa kiuchumi (EPA) baina ya Umoja wa Ulaya na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, nchi mbili wanachama zilikuwa zimetia sahihi makubaliano hayo ambazo ni Rwanda na Kenya. Hata hivyo, wakuu wa nchi za Jumuiya waliamua kujipa muda zaidi wa kuelewa mpango huo kabla ya kutoa maamuzi yao kama Jumuiya. Halikadhalika, taarifa ya mazungumzo ya usuluhishi wa mgogoro wa

Burundi ilipokelewa kutoka kwa Rais mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na mapendekezo yake yalikubaliwa. Kwa kufanikisha jambo hilo, wakuu wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki waliliagiza Baraza la Mawaziri wa Jumuiya kuandaa bajeti ya mazungumzo ya usuluhishi wa mgogoro wa Burundi.

Umoja wa Afrika na Tume ya Uchumi ya Bara la Afrika

42. Mkutano wa pamoja wa 9 wa kila mwaka kwa mawaziri wa fedha na uchumi wa Umoja wa nchi za Afrika na Tume ya Uchumi ya Afrika ulifanyika tarehe 31 Machi hadi 5 Aprili 2016 katika jiji la Addis Ababa, Ethiopia. Lengo la mkutano huo lilikuwa kutatua changamoto zilizomo kwenye mada kuu ya mikutano “*Kuelekea kwenye utaratibu jumuiishi na madhubuti katika utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya Ajenda za 2063 na Malengo Endelevu ya Maendeleo (SDGs)*”. Kwa mantiki hiyo, nchi za Afrika zinakabiliwa na mambo mawili ya mpito ambayo ni mpito kwa ngazi ya dunia kutoka malengo ya maendeleo ya milenia hadi Ajenda 2030 na mpito wa kikanda kuelekea Ajenda 2063.

43. Kutokana na mada hiyo kuu, jambo lililotiliwa mkazo lilikuwa utangamano wa kikanda ambapo utekelezaji wake kwa nchi za Afrika unatofautiana. Utangamano wa kikanda unaambatana na usafirishaji huria wa bidhaa, rasilimali za fedha na watu kutoka nchi moja ya Afrika hadi nchi nyingine, ambapo Afrika inajitahidi kutekeleza mambo yote matatu kwa wakati mmoja. Aidha, utekelezaji huo ni maamuzi ya nchi zote za Afrika ambapo waafrika wanaweza kusafiri kwenda nchi yoyote ya Afrika bila vikwazo vyovyote. Baadhi ya nchi za Afrika zinatekeleza lengo hili kwa kutoa viza ya siku thelathini kwa raia wa nchi za Afrika wanapowasili katika nchi hizo. Vile vile, wakuu wa nchi za Afrika watakuwa wanapatiwa hati za kusafiria nje ya nchi kuanzia Julai 2016 katika jiji la Kigali, Rwanda.

Shirikisho la Biashara Duniani (WTO)

44. Shirika la Biashara Duniani liliandaa pendekezo la Itifaki ya Marekebisho ya Makubaliano ya Haki Miliki ya Ubunifu kwenye masuala mbalimbali ya biashara mwaka 2015. Dhumuni kuu la Itifaki hiyo lilikuwa kuziwezesha nchi masikini wanachama wa WTO kupata madawa kwa bei nafuu. Kufanikisha hilo, pendekezo la Itifaki lilikuwa kila nchi mwanachama wa WTO kuwasilisha hati ya kukubali utekelezaji wa mageuzi hayo. Itifaki hiyo itanza kufanya kazi ikiwa

idadi ya nchi zitakazo wasilisha hati ya kukubali itafikia theluthi mbili ya wanachama wa WTO.

45. Mwaka 2016, Tanzania iliwasilisha hati ya kukubaliana na pendekezo la Itifaki ya Marekebisho ya Makubaliano ya Haki Miliki ya Ubunifu ya Biashara, kama nchi nyingine wanachama wa WTO. Aidha, Itifaki hiyo itakapopitishwa itaziwezesha nchi zinazouza dawa kutoa leseni kwa wazalishaji na wasambazaji kuziuzia nchi ambazo haziwezi kutengeneza dawa hizo. Tofauti na ilivyo Kwa sasa, ambapo leseni za biashara zinawataka watengeneza dawa kuzisambaza katika soko la ndani.

SURA YA 3

SEKTA YA NJE

Utangulizi

46. Mwaka 2016, mwenendo wa biashara ya bidhaa na huduma kati ya Tanzania na nchi mbalimbali uliendelea vizuri. Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje iliongezeka kwa asilimia 4.1 na kufikia dola za Marekani milioni 9,285.6 mwaka 2016 ikilinganishwa na Dola milioni 8,918.1 mwaka 2015. Aidha, thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma nje kwa mwaka 2016 ilipungua kwa asilimia 15.2 na kufikia dola za Marekani milioni 10,604.9 kutoka Dola milioni 12,528.2 mwaka 2015. Punguzo hilo lilitokana na kupungua kwa thamani ya bidhaa zote zilizoagizwa kutoka nje isipokuwa malighafi za viwandani, sambamba na kupungua kwa malipo ya usafirishaji, malipo ya huduma za kiserikali, na huduma za biashara nyingine.

Bidhaa Zilizouzwa Nje

47. Thamani ya mauzo ya bidhaa nje iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 5,688.8 mwaka 2016 kutoka Dola milioni 5,402.3 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 5.3. Kiasi hiki kinajumuisha bidhaa ambazo hazikurekodiwa zenye thamani ya Dola milioni 517.2. Ongezeko hili lilichangiwa na kukua kwa kiasi cha mauzo ya bidhaa asilia na zisizo asilia ambapo bidhaa asilia zilichangia asilimia 15.6 na bidhaa zisizo asilia zilichangia asilimia 75.3 ya mauzo yote.

Bidhaa Asilia

48. Mwaka 2016, thamani ya mauzo ya bidhaa asilia iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 885.6 kutoka Dola milioni 793.3 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 11.6. Hii ilitokana na kuimarika kwa bei katika soko la dunia hususan kwa mazao ya korosho, pamba na tumbaku.

Kahawa

49. Mwaka 2016, thamani ya mauzo ya kahawa ilipungua kwa asilimia 4.9 na kufikia dola za Marekani milioni 154.2, kutoka dola milioni 162.2 mwaka 2015. Punguzo hilo lilichangiwa zaidi na kushuka kwa bei ya kahawa katika soko la dunia, kutoka wastani wa dola 3,123.0 kwa tani mwaka 2015 na kufikia wastani wa dola 2,556.7 kwa tani mwaka 2016, sawa na punguzo la asilimia 18.1.

Pamba

50. Thamani ya mauzo ya pamba iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 46.8 mwaka 2016, ikilinganishwa na dola milioni 30.2 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 55.0. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa wingi wa pamba iliyouzwa nje pamoja na kupanda kwa wastani wa bei ya pamba katika soko la kimataifa. Aidha, kiasi cha pamba kilichouzwa nje kilikuwa tani 33,046 mwaka 2016 ikilinganishwa na tani 29,086 mwaka 2015. Vile vile, wastani wa bei ya pamba katika soko la dunia uliongezeka kwa asilimia 36.4 hadi wastani wa dola za Marekani 1,415.9 kwa tani mwaka 2016 kutoka dola 1,037.8 kwa tani mwaka 2015.

Katani

51. Mwaka 2016, thamani ya katani iliyouzwa nje ilipungua kwa asilimia 35.1 kutoka dola za Marekani milioni 26.5 mwaka 2015 hadi Dola milioni 17.2. Upungufu huo ulitokana na kupungua kwa kiasi cha katani kilichouzwa nje kutoka tani 1.5 mwaka 2015 hadi tani 1.4 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 6.7. Aidha, wastani wa bei ya katani uliongezeka kwa asilimia 14.5 kutoka dola za Marekani 1,748.8 kwa tani mwaka 2015 hadi Dola 2002.1 kwa tani mwaka 2016.

Chai

52. Thamani ya mauzo ya chai ilikuwa dola za Marekani milioni 44.7 mwaka 2016 ikilinganishwa na Dola milioni 44.0 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 1.6. Ongezeko hili lilitokana na kupanda kwa wastani wa bei ya chai katika soko la dunia kutoka wastani wa dola za Marekani 1,600.9 kwa tani mwaka 2015 hadi dola 1,695.7 kwa tani mwaka 2016. Hata hivyo, kiasi cha chai kilichouzwa nje mwaka 2016 kilipungua na kufikia tani 26,374 ikilinganishwa na tani 27,480 mwaka 2015.

Tumbaku

53. Mwaka 2016, thamani ya mauzo ya tumbaku iliongezeka kwa asilimia 8.7 na kufikia dola za Marekani milioni 312.7 ikilinganishwa na dola milioni 287.6 mwaka 2015. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa wastani wa bei ya tumbaku katika soko la dunia kutoka dola 4,336.5 kwa tani mwaka 2015 hadi wastani wa dola 4,732.0 kwa tani mwaka 2016. Kwa upande mwingine, kiasi cha tumbaku iliyouzwa nje ilipungua hadi tani 66,091 mwaka 2016 kutoka tani 66,326 mwaka 2015.

Korosho

54. Mwaka 2016, thamani ya mauzo ya korosho iliyouzwa nje ilikuwa dola za Marekani milioni 270.6 ikilinganishwa na dola milioni 218.8 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 23.7. Ongezeko hili lilichangiwa na kupanda kwa bei ya korosho katika soko la dunia kutoka dola za Marekani 1,273.8 kwa tani mwaka 2015 hadi dola za Marekani 1,599.2 kwa tani mwaka 2016.

Karafuu

55. Mwaka 2016, thamani ya karafuu iliyouzwa nje iliongezeka kwa asilimia 63.1 na kufikia dola za Marekani milioni 39.3 kutoka dola milioni 24.1 mwaka 2015. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa kiasi cha karafuu kilichouzwa nje kutoka tani 2,783 mwaka 2015 hadi tani 4,925 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 77.0. Aidha, wastani wa bei ya karafuu ulipungua kwa asilimia 7.8 kutoka dola za Marekani 8,653.1 kwa tani mwaka 2015 hadi dola za Marekani 7,976.0 kwa tani mwaka 2016.

Bidhaa Zisizo Asilia

56. Thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia zilizouzwa nje iliongezeka kwa asilimia 4.1 hadi dola za Marekani milioni 4,286.0 mwaka 2016 kutoka dola za Marekani milioni 4,117.9 mwaka 2015. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na kukua kwa mauzo ya madini hususani dhahabu, maua pamoja na mauzo mengine, wakati mauzo ya bidhaa za viwandani yalipungua.

Madini

57. Thamani ya mauzo ya madini nje iliongezeka kwa asilimia 22.5 hadi kufikia dola za Marekani milioni 1,574.5 kutoka Dola milioni 1,285.4 mwaka 2015. Aidha, thamani ya mauzo ya dhahabu iliongezeka kwa asilimia 22.5 na kufikia dola za Marekani milioni 1,449.4 ikilinganishwa na Dola milioni 1,183.3 mwaka 2015. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha dhahabu iliyouzwa nje pamoja na kupanda kwa bei ya madini hayo katika soko la dunia. Katika kipindi hicho, bei ya dhahabu katika soko la dunia iliongezeka kwa asilimia 7.6 na kufikia dola za Marekani 1,248.9 kwa kila wakia mwaka 2016 kutoka dola za Marekani 1,160.7 kwa wakia mwaka 2015.

Bidhaa za Viwandani

58. Thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani zilizouzwa nje ilipungua kwa asilimia 20.0 kutoka dola za Marekani milioni 1,364.5 mwaka 2015 hadi Dola milioni 1,092.1 mwaka 2016.. Hali hii ilitokana na kushuka kwa thamani ya mauzo ya bidhaa za chuma, mafuta ya kula, pamoja na kioo na bidhaa zake.

Samaki na Mazao ya Samaki

59. Mwaka 2016, thamani ya mauzo ya samaki na mazao yake ilipungua na kufikia dola za Marekani milioni 142.5 kutoka dola za Marekani milioni 173.5 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 17.9. Hii ilitokana na kupungua kwa kiasi cha samaki na mazao ya samaki kilichouzwa nje.

Mazao ya Mboga na Maua

60. Thamani ya mauzo ya mazao ya mboga na maua ilikuwa dola za Marekani milioni 24.8 mwaka 2016 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 24.4 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 1.6. Ongezeko hili lilitokana na kukua kwa mauzo ya bidhaa za maua kufuatia ukuaji wa shughuli za uzalishaji wa maua katika miaka ya hivi karibuni.

Bidhaa Nyinginezo Zilizouzwa Nje

61. Mwaka 2016, thamani ya mauzo ya bidhaa nyinginezo zilizouzwa nje iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 972.2 kutoka dola za Marekani milioni 884.3 mwaka 2015. Aidha, bidhaa za mbegu za mafuta, kakao, ngozi na nafaka zilichangia karibu asilimia 75 ya mauzo yote katika kundi hili.

Jedwali Na.3.1: Thamani, Kiasi na Bei ya Bidhaa Zilizouzwa Nje

Bidhaa	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	Badiliko, %
Bidhaa Asilia								
Kahawa								
Thamani (US\$ milioni)	101.6	142.6	186.6	171.0	121.5	162.2	154.2	-4.9
Kiasi ('000 tani)	35.6	39.0	54.8	59.5	44.1	51.9	60.3	16.2
Bei (US\$ kwa tani)	2853.1	3654.9	3403.2	2872.7	2756.2	3123.0	2556.7	-18.1
Pamba								
Thamani (US\$ milioni)	84.0	61.6	164.9	111.7	54.7	30.2	46.8	55.0
Kiasi ('000 ttani)	67.6	40.3	132.0	89.0	49.5	29.1	33.0	13.4
Bei (US\$ kwa tani)	1241.9	1529.0	1249.7	1256.0	1104.9	1037.8	1415.9	36.4
Katani								
Thamani (US\$ milioni)	10.9	16.9	18.4	16.9	16.8	26.5	17.2	-35.1
Kiasi ('000 tani)	11.6	13.8	13.5	12.6	11.5	1.5	1.4	-6.7
Bei (US\$ kwa tani)	939.8	1223.5	1357.1	1341.6	1459.7	1748.8	2002.1	14.5
Chai								
Thamani (US\$ milioni)	49.8	47.2	56.1	56.9	45.7	44.0	44.7	1.6
Kiasi ('000 tani)	27.1	27.1	27.2	28.8	29.2	27.5	26.4	-4.0
Bei (US\$ kwa tani)	1840.2	1739.7	2061.2	1977.9	1568.1	1600.9	1695.7	5.9
Tumbaku								
Thamani (US\$ milioni)	232.4	281.2	350.1	307.0	315.0	287.6	312.7	8.7
Kiasi ('000 tani)	53.6	73.3	105.6	67.8	67.4	66.3	66.1	-0.3
Bei (US\$ kwa tani)	4337.0	3839.4	3316.0	4526.1	4,673.5	4,336.5	4,732.0	9.1
Koroshu								
Thamani (US\$ milioni)	96.9	107.0	142.6	162.4	222.2	218.8	270.6	23.7
Kiasi ('000 tani)	100.6	96.4	130.9	147.3	172.2	171.7	169.2	-1.5
Bei (US\$ kwa tani)	963.2	1110.0	1089.3	1102.5	1290.7	1273.8	1599.2	25.5
Karafuu								
Thamani (US\$ milioni)	7.6	28.9	38.1	43.0	52.9	24.1	39.3	63.1
Kiasi ('000 tani)	2.2	2.2	3.4	4.1	4.7	2.8	4.9	75.0
Bei (US\$ kwa tani)	3449.6	13162.9	11198.5	10562.8	11231.3	8653.1	7976.0	-7.8
Jumla (Bidhaa Asilia)	583.2	685.5	956.7	868.9	828.8	793.4	885.5	11.6
Bidhaa Zisizo Asilia								
Madini	1561.2	2283.4	2197.8	1782.1	1466.7	1285.4	1574.5	22.5
Dhahabu	1516.6	2224.1	2117.4	1644.8	1321.6	1183.3	1449.4	22.5
Almasi	11.1	10.2	30.2	48.8	78.2	53.2	77.5	45.7
Madini mengine	33.5	49.2	50.2	88.5	66.9	48.9	47.6	-2.7
Bidhaa za Viwandani	964.0	861.5	1037.3	1072.1	1239.7	1364.5	1092.0	-20.0
Nyuzi za Pamba	11.5	4.8	5.8	10.9	10.8	11.9	9.6	-19.3
Kahawa Iliyozalishwa	0.7	1.1	1.0	1.1	1.2	0.3	0.1	-66.7
Tumbaku ilizalishwa	10.5	16.7	24.6	32.2	33.6	33.0	25.4	-23.0
Mazao ya Katani	9.0	11.8	9.1	9.7	10.5	17.4	24.9	43.1
Mazao mengine ya Viwandani	932.4	827.1	996.8	1018.2	1183.6	1301.9	1032.0	-20.7
Samaki na Mazao ya Samaki	150.4	137.7	160.6	130.6	195.1	173.5	142.5	-17.9
Mazao ya mboga na Maua	30.8	36.4	31.3	28.1	30.5	24.4	24.8	1.6
Bidhaa zilizouzwa tena (re-exports)	338.2	330.2	555.7	172.8	177.0	385.8	480.0	24.4
Bidhaa nyinginezo	132.5	98.3	181.7	517.6	687.2	884.3	972.2	9.9
Jumla (Bidhaa zisizo Asilia)	3177.0	3747.5	4164.4	3703.3	3796.2	4117.9	4286.0	4.1
Bidhaa zisizorekodiwa	564.0	664.9	768.2	685.8	693.8	491.1	517.2	5.3
JUMLA KUU (BIDHAA ZOTE)	4324.3	5097.9	5889.2	5258.1	5318.8	5402.4	5688.7	5.3

Chanzo: Benki Kuu na Wizara ya Fedha na Mipango

Mapato ya Huduma

62. Mwaka 2016, mapato yatokanayo na biashara ya huduma yalikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 3,596.8 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,515.8 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 2.3. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na utalii na huduma ya usafirishaji. Mapato ya utalii yaliongezeka kwa asilimia 9.0 na kufikia dola za Marekani milioni 2,073 ikilinganishwa na dola milioni 1,901.9 mwaka 2015. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa idadi ya watalii kufuatia juhudi za Serikali na wadau wengine kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi. Aidha, mapato yatokanayo na huduma ya usafirishaji yalikuwa dola za marekani milioni 1,044.0 mwaka 2016 ikilinganishwa na dola za marekani milioni 1,012.3 mwaka 2015.

Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje

63. Mwaka 2016, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ilipungua kwa asilimia 14.0 na kufikia dola za Marekani milioni 8,463.7 kutoka dola za marekani milioni 9,843.1 mwaka 2015. Hali hii ilitokana na kupungua kwa thamani ya bidhaa zote zilizoagizwa kutoka nje isipokuwa malighafi za viwandani.

Bidhaa za Kukuza Mitaji

64. Mwaka 2016, thamani ya bidhaa za kukuza mitaji zilizoingizwa nchini ilipungua na kufikia dola za Marekani milioni 3,497.4 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,812.9 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 8.3. Hii ilitokana na kupungua kwa thamani ya mitambo iliyoagizwa toka nje pamoja na thamani ya bidhaa za ujenzi na vyombo vya usafirishaji iliyochangiwa na kumalizika kwa miradi mikubwa kama vile ujenzi wa kiwanda cha saruji, mitambo ya kuzalisha umeme na kukamilika kwa shughuli za makampuni makubwa ya utafiti wa gesi asilia.

Bidhaa za Kati

65. Thamani ya bidhaa za kati zilizoingizwa kutoka nje ilikuwa dola za Marekani milioni 2,863.2 mwaka 2016 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,696.7 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 22.5. Hali hii ilitokana na kupungua kwa thamani ya bidhaa za mbolea na mafuta zilizoagizwa ambapo thamani ya uagizaji wa mbolea kutoka nje ilipungua kwa asilimia 18.6 na kufikia dola za Marekani milioni 118.6 mwaka 2016. Kwa upande wa bidhaa

za mafuta ya petroli thamani ya uagizaji ilipungua kwa asilimia 34.5 kufikia dola za Marekani milioni 1,807.7 mwaka 2016 kutoka dola za Marekani milioni 2,760.7 mwaka 2015, kutokana na kupungua kwa bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia. Aidha, thamani ya uagizaji wa malighafi za viwandani iliongezeka kwa asilimia 18.5 na kufikia dola za Marekani milioni 937.0 mwaka 2016 kutoka dola za Marekani milioni 790.4 mwaka 2015, sambamba na ukuaji wa shughuli za uzalishaji viwandani.

Bidhaa za Matumizi ya Kawaida

66. Mwaka 2016, thamani ya uagizaji wa bidhaa za matumizi ya kawaida ilipungua kwa asilimia 10.0 na kufikia dola za Marekani milioni 2,100.9 kutoka dola za Marekani milioni 2,333.5 mwaka 2015. Hii ilitokana na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa za chakula pamoja na bidhaa nyingine za matumizi ya kawaida. Kupungua kwa uagizaji wa bidhaa za chakula kulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji na kuimarika kwa usambazaji wa chakula katika soko la ndani.

Malipo ya Huduma

67. Mwaka 2016, malipo ya huduma yalikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 2,141.3 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,669.7 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 19.8. Hii ilitokana na kupungua kwa malipo ya usafirishaji, malipo ya huduma za kiserikali, na huduma za biashara nyingine. Kupungua kwa malipo ya usafirishaji kulienda sambamba na kushuka kwa uagizaji bidhaa nje ya nchi.

Jedwali Na. 3.2: Thamani ya Bidhaa Zilizoaagizwa kutoka Nje (Dola za Marekani)

Bidhaa	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	Badiliko
BIDHAA ZA KUKUZA MITAJI	2,715.2	3,560.5	3,686.5	3,460.4	3,598.2	3,812.9	3,497.4	-8.3
Vifaa vya Usafirishaji	901.1	1,008.5	1,158.2	1,160.2	1,214.8	1,096.5	907.7	-17.2
Majengo na Ujenzi	610.6	757.7	805.8	959.8	1,032.4	908.0	817.2	-10.0
Mitambo	1,203.4	1,794.3	1,722.5	1,340.5	1,351.0	1,808.4	1,772.5	-2.0
BIDHAA ZA KATI	2,741.2	4,139.0	4,320.2	5,205.2	4,663.6	3,696.7	2,863.2	-22.5
Uagizaji Mafuta	2,024.2	3,228.7	3,380.6	4,308.6	3,656.8	2,760.7	1,807.7	-34.5
Mbolea	115.0	176.6	133.9	160.1	122.8	145.6	118.6	-18.6
Malighafi za Viwandani	602.0	733.7	805.7	736.6	884.0	790.4	937.0	18.5
BIDHAA ZA MATUMIZI YA KAWA	1,709.2	2,128.0	2,312.5	2,363.5	2,656.0	2,333.5	2,100.8	-10.0
Bidhaa za Vyakula	461.6	603.1	656.6	646.4	632.6	541.7	445.5	-17.8
Bidhaa nyingine za Vyakula	1,247.5	1,524.9	1,655.9	1,717.1	2,023.4	1,791.8	1,655.4	-7.6
JUMLA KUU (F.O.B)	7165.5	9827.5	10319.1	11029.1	10917.8	9843.1	8463.7	-14.0

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Mwenendo wa Biashara Baina ya Tanzania na Nchi Mbalimbali

68. Mwaka 2016, Tanzania iliendelea kuwa na mahusiano mazuri ya kibiashara na nchi mbalimbali duniani zikiwemo nchi za Afrika, Ulaya, Marekani, Asia, Australia, pamoja na Jumuiya za ushirikiano kikanda kama Jumuiya ya Umoja wa nchi za Ulaya, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika. Katika kipindi hicho, sehemu kubwa ya mauzo nje yalikwenda katika nchi ya Uswisi iliyochangia asilimia 16.2 ya mauzo yote, India (asilimia 12.4), Afrika ya kusini (asilimia 12.2), China (asilimia 6.2), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (asilimia 5.6) na Kenya (asilimia 5.5). Aidha, bidhaa zilizouzwa Uswisi na India ni pamoja na dhahabu, mbegu za mafuta, vito vya thamani na mbogamboga. Bidhaa zilizouzwa Kenya zilikuwa chai, mahindi, vifaa vya ushonaji, mbogamboga na nafaka nyinginezo. Vile vile, bidhaa zilizouzwa Afrika ya Kusini zilikuwa dhahabu, madini ya shaba na chai.

69. Kwa upande wa bidhaa zilizoagizwa kutoka nje, kiasi kikubwa kilitoka katika nchi za China, India, Ufalme wa nchi za Kiarabu, Afrika ya Kusini, Japani na Kenya ambazo kwa pamoja zilichangia asilimia 60.6 ya bidhaa zote zilizoagizwa. Aidha, bidhaa zilizoagizwa kutoka China ni pamoja na mitambo na bidhaa za marumaru, Ufalme wa nchi za Kiarabu (mafuta ya petrol na sukari) na Japani na Afrika ya Kusini (magari na bidhaa za chuma).

Jedwali Na. 3.3: Uagizaji wa Bidhaa Kutoka Nchi Mbalimbali Duniani (USD in Million)

JUMUIYA/ NCHI	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2015/16 (Badiliko, %)
JUMUIYA YA ULAYA NA USWISI	1074.4	1536.9	2759.4	2795.0	1006.5	977.8	-2.9
NCHI NYINGINE ZA ULAYA	647.1	1756.3	218.0	499.1	673.6	323.6	-52.0
JUMLA - BARA LA ULAYA	1721.5	3293.2	2977.4	3294.1	1680.1	1301.4	-22.5
AFRIKA							
JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)							
Afrika ya Kusini	676.5	920.8	660.1	603.3	514.1	472.2	-8.2
Zimbabwe	1.0	2.9	3.4	4.8	5.7	2.1	-63.2
Zambia	27.0	39.6	46.2	63.3	32.6	33.5	2.8
Msumbiji	16.9	11.0	66.9	18.3	33.3	12.0	-64.0
Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo	1.0	0.9	0.1	0.8	0.6	0.4	-33.3
Swaziland	29.0	34.6	33.9	47.1	37.3	41.2	10.5
Nchi nyingine za SADC	29.9	83.3	25.3	35.3	45.6	54.2	18.9
JUMLA -SADC	781.3	1093.1	835.9	772.9	669.2	615.6	-8.0
JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)							
Burundi	0.6	3.8	1.5	0.6	1.1	0.8	-27.3
Kenya	246.1	555.8	303.6	379.6	238.6	267.7	12.2
Rwanda	1.2	2.1	1.5	3.2	1.1	1.1	0.0
Uganda	15.9	106.7	52.5	48.0	39.4	30.7	-22.1
JUMLA -EAC	263.8	668.4	359.1	431.4	280.2	300.3	7.2
Nchi nyingine za Afrika	53.2	60.5	60.6	53.3	62.7	69.0	10.0
JUMLA NCHI ZOTE ZA AFRIKA	1098.3	1822.0	1255.6	1257.6	1012.1	984.9	-2.7
BARA LA AMERIKA							
Marekani	138.5	235.5	211.9	269.8	323.3	252.0	-22.1
Canada	33.1	110.1	91.8	93.7	60.2	100.9	67.6
Nchi nyingine za Bara la Amerika	68.6	199.1	34.5	44.4	47.3	48.6	2.7
JUMLA - BARA LA AMERIKA	240.2	544.7	338.2	407.9	430.8	401.5	-6.8
ASIA							
China	787.6	1145.4	1444.2	1571.1	1699.7	1638.4	-3.6
India	784.5	867.4	2088.2	1748.6	1154.1	1428.7	23.8
Japan	502.9	510.5	466.7	559.3	363.0	371.0	2.2
Hong Kong	21.1	52.5	32.7	53.2	41.6	51.6	24.0
Singapore	390.4	145.6	200.7	39.2	84.3	52.6	-37.6
Umoja wa Falme za Kiarabu	590.9	1010.3	1079.3	1095.1	769.0	592.3	-23.0
Nchi nyingine za Asia	959.9	2024.9	1871.2	1052.4	2497.1	1566.6	-37.3
JUMLA - ASIA	4037.3	5756.6	7183.0	6118.9	6608.8	5701.2	-13.7
NCHI NYINGINEZO	2730.2	-1097.4	-725.1	3.4	111.3	74.6	-33.0
JUMLA KUU	9827.5	10319.1	11029.1	11081.9	9843.1	8463.6	-14.0

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Fedha na Mipango

70. Mwaka 2016, thamani ya mauzo ya bidhaa kwa nchi za Jumuiya ya Ulaya iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 630 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 615.5 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 2.4. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa katika nchi za Jumuiya ya Ulaya hasa Ujerumani na Ubelgiji. Aidha, thamani ya bidhaa zilizoagizwa ikijumuisha gharama za bima na usafirishaji (*c.i.f*) kutoka nchi za

Jumuiya ya Ulaya ilipungua hadi dola za Marekani milioni 978 mwaka 2016 kutoka dola za Marekani milioni 1,006.5 mwaka 2015.

71. Thamani ya mauzo ya bidhaa kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ilipungua hadi dola za Marekani milioni 430.6 mwaka 2016, kutoka dola za Marekani milioni 862.0 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 50.0. Hii ilitokana na kupungua kwa mauzo nchini Kenya kwa asilimia 57.1. Mauzo kwa nchi ya Kenya yalipungua kutoka dola za Marekani milioni 731.4 mwaka 2015 hadi dola za Marekani milioni 313.8 na yalichangia asilimia 72.9 ya mauzo yote kwa nchi za Jumuiya. Aidha, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki iliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 280.2 mwaka 2015 hadi dola za Marekani milioni 300.3 mwaka 2016.

72. Mwaka 2016, thamani ya mauzo kwa nchi za SADC ilipungua hadi dola za Marekani milioni 1,112.7 kutoka dola za Marekani milioni 1,028.1 mwaka 2015. Vile vile, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za SADC ilipungua hadi dola za Marekani milioni 615.6 mwaka 2016 kutoka dola za Marekani milioni 669.2 mwaka 2015. Hata hivyo, mauzo ya bidhaa kwa nchi ya Afrika Kusini pekee yaliongezeka kwa asilimia 2.8 kufikia dola za Marekani milioni 692.2, sawa na asilimia 62.2 ya mauzo yote kwa nchi za SADC.

Jedwali Na. 3.4: Mauzo ya Bidhaa Kwenda Nchi Mbalimbali Duniani (Dola milioni)

JUMUIYA/ NCHI	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2015/16 (Badiliko %)
JUMUIYA YA ULAYA NA USWISI	553.5	745.4	898.4	791.7	615.4	629.8	2.3
NCHI NYINGINE ZA ULAYA	828.5	816.8	16.9	77.5	176.4	784.7	344.8
JUMLA - BARA LA ULAYA	1382.0	1562.2	915.3	869.2	791.8	1414.5	78.6
(SADC)							
Afrika ya kusini	831.1	967.9	760.0	689.1	673.2	692.2	2.8
Zambia	47.1	71.4	90.6	135.3	44.1	35.7	-19.0
Swaziland	12.5	2.2	4.0	1.2	9.1	0.1	-98.9
Zimbabwe	4.1	4.7	6.5	7.1	6.3	7.0	11.1
Msumbiji	61.9	53.1	66.4	68.1	18.6	13.5	-27.4
Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo	119.5	181.6	236.2	281.5	197.7	319.8	61.8
Nchi nyingine za SADC	82.6	141	44.9	53.7	79.1	44.4	-43.9
JUMLA- SADC	1158.8	1421.9	1208.5843	1236.0	1028.1	1112.7	8.2
JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)							
Burundi	30.8	45.8	45.0	43.0	39.1	52.1	33.2
Kenya	211.2	330.9	227.1	445.9	731.4	313.8	-57.1
Rwanda	65.8	72.8	81.1	35.8	41.2	6.5	-84.2
Uganda	44.6	65.8	66.1	73.3	50.3	58.2	15.7
JUMLA – EAC	352.4	515.3	419.3	598	862	430.6	-50.0
Nchi nyingine za Afrika	67.9	47.7	3.5	219.1	337.5	202.8	-39.9
JUMLA –AFRIKA	1579.1	1984.9	1631.4	2053.1	2227.6	1746.1	-21.6
BARA LA AMERIKA							
Marekani	47.5	66.8	60.5	143.0	50.6	57.0	12.6
Canada	5.0	25.2	12.9	7.1	6.0	4.7	-21.7
Nchi nyingine za Bara la Amerika	7.4	1.7	2.7	6.2	84.7	9.3	-89.0
JUMLA- BARA LA AMERIKA	59.9	93.7	76.1	156.3	77.1	71.0	-7.9
ASIA							
China	659.2	520.4	307.8	583.9	560.5	354.1	-36.8
India	202.7	476.5	748.2	1084.1	1145.8	702.8	-38.7
Japan	346.8	296.5	220	247.8	229.7	138.5	-39.7
Umoja wa Falme za Kiarabu	74.9	93.2	84.2	85.5	157.1	63.5	-59.6
Hong Kong	11.1	23.1	30.4	35.6	33.9	30.0	-11.5
Singapore	10.9	24.3	55.7	15.9	6.6	10.5	59.1
Nchi nyingine za Asia	109.1	210.4	64.7	121.9	160.2	193.0	20.5
JUMLA- ASIA	1414.7	1644.4	1511	2174.7	2293.8	1492.4	-34.9
NCHI NYINGINEZO	662.2	604.0	1124.3	65.5	12.0	964.8	7940.0
JUMLA KUU	5,097.9	5,889.2	5,258.1	5,318.8	5,402.3	5,688.8	5.3

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Fedha na Mipango

Mizania ya Malipo na Nchi za Nje

Urari wa Biashara ya Bidhaa

73. Mwaka 2016, urari wa biashara ya bidhaa ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,774.8 ikilinganishwa na nakisi ya dola milioni 4,440.7 mwaka 2015, sawa na upungufu wa nakisi kwa asilimia 37.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa nje kwa asilimia 5.3 sambamba na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa kutoka nje kwa asilimia 14.0.

Urari wa Biashara ya Huduma

74. Mwaka 2016, urari wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 1,455.5 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 846.0 mwaka 2015, sawa na ongezeko la ziada kwa asilimia 72.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za usafirishaji na usafiri hususan biashara ya utalii sambamba na kupungua kwa malipo ya usafirishaji kufuatia kupungua kwa uagizaji bidhaa kutoka nje.

Urari wa Biashara ya Huduma na Bidhaa

75. Mwaka 2016, urari wa biashara ya bidhaa na huduma ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,319.3 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 3,594.7 mwaka 2015, sawa na upungufu wa nakisi kwa asilimia 63.3. Upungufu huo wa nakisi ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na mapato ya huduma.

Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi

76. Mwaka 2016, urari wa mapato ya vitega uchumi ambayo yanajumuisha malipo kwa wafanyakazi, mapato ya uwekezaji na malipo ya riba ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,066.7 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 900.2 mwaka 2015, sawa na ongezeko la nakisi kwa asilimia 18.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa malipo ya riba.

Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida

77. Mwaka 2016, urari wa uhamisho mali wa kawaida unaojumuisha uhamisho wa fedha unaofanywa na sekta binafsi, misaada na unafuu wa kulipa deni ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 372.3 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 532.0 mwaka 2015, sawa na upungufu wa ziada kwa asilimia 30.0. Hali hiyo ilitokana na kupungua kwa misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo ambayo ilishuka hadi dola za Marekani milioni 63.3 mwaka 2016 kutoka dola za Marekani milioni 246.9 mwaka 2015.

Urari wa Malipo ya Kawaida

78. Mwaka 2016, urari wa malipo ya kawaida unaojumuisha biashara ya bidhaa, huduma, mapato ya vitega uchumi na uhamisho mali wa kawaida ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,013.8 kutoka nakisi ya dola za Marekani milioni 3,962.9 mwaka 2015, sawa na upungufu wa nakisi kwa asilimia 49.2. Upungufu huo ulitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na mapato ya

huduma pamoja na kupungua kwa uagizaji bidhaa kutoka nje na malipo ya huduma.

Urari wa Uhamisho wa Mitaji

79. Mwaka 2016, urari wa uhamisho wa mitaji unaojumuisha misaada ya vitega uchumi na misamaha ya madeni ya nje kutoka kwa washirika wa maendeleo ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 327.8 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 354.4 mwaka 2015, sawa na upungufu wa ziada kwa asilimia 7.5. Hali hiyo ilitokana na kupungua kwa misaada ya kawaida ya kibajeti kutoka washirika wa maendeleo.

Urari wa Malipo ya Fedha katika Uwekezaji

80. Mwaka 2016, nakisi katika urari wa malipo ya fedha katika uwekezaji, unaojumuisha uwekezaji wa mitaji ya kigeni ya moja kwa moja na mikopo ya fedha kutoka nje ilipungua kufikia dola za Marekani milioni 2,059.1 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 3,157.6 mwaka 2015, sawa na upungufu wa nakisi kwa asilimia 34.8. Hii ilichangiwa na kupungua kwa uwekezaji wa moja kwa moja na uwekezaji mwingine usio wa moja kwa moja kama vile amana kutoka nje.

Urari wa Malipo Yote

81. Mwaka 2016, urari wa malipo yote ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 305.5 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 199.1 mwaka 2015. Hali hii ilichangiwa na kupungua kwa nakisi ya urari wa malipo ya kawaida.

Akiba ya Fedha za Kigeni

82. Akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani milioni 4,325.6 mwezi Desemba 2016 ikilinganishwa na dola milioni 4,093.7 Desemba 2015 bila kujumuisha bidhaa na huduma ambazo zinalipiwa na fedha za uwekezaji wa moja kwa moja. Kiasi hicho kilikuwa na uwezo wa kulipia bidhaa na huduma kwa miezi 4.6 ikilinganishwa na miezi 5.2 iliyofikiwa mwaka 2015. Aidha, akiba ya fedha za kigeni katika benki za biashara ilikuwa dola za Marekani milioni 768.2 mwaka 2016 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,012.1 zilizoripotiwa Desemba 2015.

Soko la Fedha za Kigeni kwa Mabenki

83. Mwaka 2016, viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni viliendelea kuamuliwa na nguvu ya soko. Kiasi cha fedha za kigeni zilizouzwa katika soko la fedha za kigeni kilikuwa Dola za Kimarekani milioni 1,710.1 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 2,203.2 mwaka 2015. Kati ya mauzo yote yaliyofanyika mwaka 2016, Dola za Kimarekani milioni 261.0 (sawa na asilimia 15.3) ziliuzwa na Benki Kuu na kiasi kilichobaki kiliuzwa na benki za biashara ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 844.0 (sawa na asilimia 38.3) zilizouzwa mwaka 2015.

Thamani ya Shilingi ya Tanzania

84. Mwaka 2016, thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani imeendelea kuimarika baada ya kupungua thamani kwa kasi ndogo ya wastani wa asilimia 8.8 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 16.8 mwaka 2015. Hii ilitokana na usimamizi madhubuti wa sera za fedha na za bajeti. Dola moja ya Marekani ilinunuliwa kwa wastani wa Shilingi 2,177.07 ikilinganishwa na shilingi 1,985.39 mwaka 2015. Aidha, mwishoni mwa mwaka 2016, Dola moja ya Marekani iliuzwa kwa Shilingi 2,172.6 ikilinganishwa na Shilingi 2,148.5 mwishoni mwa mwaka 2015.

THAMANI YA BIDHAA ZA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA NCHI ZA NJE

Jedwali Na.17

Shs. Milioni

Aina ya Bidhaa	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016
Zilizouzwa Nje	2628866	3194929	3671935	4050561	7331020	8658371	8223206	11366504	10725753	12387829
Bidhaa Halisi	2413809	2992530	3568071	3921648	7175377	8368496	7012100	9429220	9959761	11342534
Zilizouzwa Tena	215057	202399	103864	128913	155643	289875	1211106	1937284	765992	1045294
Zilizoagizwa	7296763	8839274	8446721	11086891	17217173	18275893	19904472	20977105	21475090	20660282
Jumla	9925629	12034203	12118656	15137452	24548193	26934264	28127678	32343609	32200843	33048110
Urari	-4667897	-5644345	-4774785	-7036330	-9886153	-9617522	-11681266	-9610601	-14659582	-14962132
Thamani ya Fedha (Shs/US\$)	1232.80	1196.31	1320.30	1395.68	1557.43	1571.71	1598.66	1652.51	1985.39	2177.59

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Idara ya forodha na Benki Kuu ya Tanzania

KIASI NA THAMANI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 18

Bidhaa	Kiasi(000 ⁰ Tani)							Thamani(sh. Milioni)						
	2011	2012	2013	2014	2015	2016	Badiliko(%) 2015/16	2011	2012	2013	2014	2015	2016	Badiliko (%) 2015/16
Kahawa	39.0	54.8	59.5	44.1	51.9	60.3	16.2	225748	292787	259132	204301	315921	335629	54.6
Pamba	40.3	132.0	89.0	49.5	29.1	33.0	13.6	61636	164926	137663	558404	62959	101816	-88.7
Katani	13.8	13.5	12.6	11.5	1.5	1.4	-2.8	16931	18369	25396	111323	53927	37524	-51.6
Chai	27.1	27.2	28.8	29.2	27.5	26.4	-4.0	72257	87359	86810	72784	86285	97381	18.5
Tumbaku	73.3	105.6	67.8	67.4	66.3	66.1	-0.4	189834	348062	159454	319295	568812	680453	78.1
Korosho	96.4	130.9	147.3	172.2	171.7	169.2	-1.5	162715	221971	301212	647936	430023	587849	-33.6
Karafuu	2.2	3.4	4.1	4.7	2.8	4.9	77.0	48362	58281	68429	50880	48912	85454	-3.9
Almasi (Carat)	417000	411000	-	-	-	-	-	16976	-	63584	166107	65636	-	-
Dhababu(gms)	40400000	37900000	35100000	41813100	-	-	-	3463813	3410746	2768481	2812561	2717187	-	-

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Idara ya forodha, TRA

- Takwimu hazikupatikana


KIASI NA THAMANI YA BIDHAA ZA ASILIA NA ZISIZO ZA ASILIA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 19


Bidhaa	Kiasi (000" Tani)						Badiliko(%)	Thamani (Milioni US\$)						Badiliko (%)	
	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2015/16	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2015/16	
Bidhaa Asilia:															
Kahawa	39.0	54.8	59.5	44.1	51.9	60.3	16.2	142.6	186.6	171.0	121.5	162.2	154.2	-4.9	
Pamba	40.3	132.0	89.0	49.5	29.1	33.0	13.6	61.6	164.9	111.7	54.7	30.2	46.8	55.0	
Katani	13.8	13.5	12.6	11.5	1.5	1.4	(2.8)	16.9	18.4	16.9	16.8	26.5	17.2	-35.1	
Chai	27.1	27.2	28.8	29.2	27.5	26.4	(4.0)	47.2	56.1	56.9	45.7	44.0	44.7	1.7	
Tumbaku	73.3	105.6	67.8	67.4	66.3	66.1	(0.4)	281.2	350.1	307.0	315.0	287.6	312.7	8.7	
Koroshho	96.4	130.9	147.3	172.2	171.7	169.2	(1.5)	107.0	142.6	162.4	222.2	218.8	270.6	23.7	
Karafuu	2.2	3.4	4.1	4.7	2.8	4.9	77.0	28.9	38.1	43.0	52.9	24.1	39.3	63.1	
Jumla								685.5	956.7	868.9	828.8	793.3	885.6	11.6	
Bidhaa zisizo asilia:															
Madini								2283.4	2197.8	1782.1	1469.2	1285.4	1574.5	22.5	
Bidhaa za Viwanda								861.5	1037.3	1072.1	1239.6	1364.5	1092.1	-20.0	
Samaki na Mazao ya Samaki								137.7	160.6	130.6	195.0	173.5	142.5	-17.9	
Mazao ya Mboga na Maua								36.4	31.3	28.1	30.5	24.4	24.8	1.4	
Bidhaa zilizouzwa tena								98.3	181.7	172.8	177.0	385.8	480.0	24.4	
Bidhaa nyinginezo								330.2	555.7	517.6	687.2	884.3	972.2	9.9	
Jumla								3747.5	4164.4	3703.3	3798.6	4117.9	4286.0	4.1	
Bidhaa Zisizorekodiwa								664.9	768.2	685.8	694.1	491.1	517.2	5.3	
JUMLA KUBWA								5097.9	5889.2	5258.1	5321.5	5402.3	5688.8	5.3	

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Idara ya forodha, TRA


I: BIDHAA ASILIA NA ZISIZO ASILIA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE
(US\$ Milioni)




**II: PAMBA NA KAHAWA ILIYOUZWA NCHI ZA NJE
(Kiasi kwa Tani '000)**



IIIA: MCHANGO WA BIDHAA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE - 2015



IIIB: MCHANGO WA BIDHAA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE - 2016



WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 20

Sh./Tani*

Bidhaa	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	Badiliko (%)
											2015/16
Kahawa	2668414	2642540	2628934	4069399	5580087	5400679	4135909	4284297	6084327	5563694	-8.6
Pamba	1222475	1767694	1462236	1775008	1431997	1724164	2016331	4196444	2164592	3080982	42.3
Katani	1047444	946323	1951011	1986211	2091121	2102332	2129059	2052892	3554124	2473086	-30.4
Chai	1581921	1861435	2373683	2501897	2664933	3144333	3392989	2617376	3139968	3543747	12.9
Tumbaku	2869021	4593309	4970800	2586996	2564562	3145641	2237711	4172482	8576002	10259213	19.6
Korosho	2278459	1356504	950656	1284308	1636560	1695963	1943340	3255142	2503867	3422830	36.7
Karafuu	3321160	4202786	4008131	4390290	20972246	9783616	16735615	17997878	17576080	30707266	74.7
Almasi (kwa carat)	156300	157692	157319	38695	40709	99809	353966	317548	-	-	-
Dhahabu (kwa gramu)	9982	34504	40826	60038	85738	89993	78874	64709	-	-	-

Chanzo: Idara ya Forodha, Mamlaka ya Mapato Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

* Isipokuwa kwa almasi na dhahabu

WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE


Jedwali Na. 21

Bidhaa	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	US\$/Tani*
											Badiliko(%) 2015/16
Kahawa	2165	2203	1991	2853	3655	3403	2873	2756	3123	2557	-18.1
Pamba	992	1321	1108	1242	1529	1250	1256	1105	1038	1416	36.4
Katani	850	1251	980	940	1224	1357	1342	1460	1749	2002	14.5
Chai	1283	1575	1542	1840	1740	2061	1978	1568	1601	1696	5.9
Tumbaku	2327	3041	3762	4337	3839	3316	4526	4673	4336	4732	9.1
Korosho	1848	730	720	963	1110	1089	1103	1291	1274	1599	25.5
Karafuu	2694	3578	3036	3450	13163	11199	10563	11231	8653	7976	-7.8
Almasi (kwa carat)	127	133	1193	3028	2395	2188	208	187.0	-	-	-
Dhahabu (kwa gramu)	8.10	1.78	35.34	43	55	57	35	38	-	-	-

Chanzo: Idara ya forodha, TRA

* Isipokuwa kwa almasi na dhahabu

- Takwimu Hazikupatikana



AINA NA THAMANI YA BIDHAA ZILIZOAGIZWA TOKA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 23

Sh. Milioni

Mwaka	Bidhaa za Matumizi ya Kawaida	Bidhaa za Kati	Bidhaa za Viwanda	Jumla
2000	401612	222399	444427	1068438
2001	468173	386317	648361	1502851
2002	499346	408872	697209	1605426
2003	654630	705729	846251	2206610
2004	917953	1024705	1029389	2972046
2005	937031	1451062	1341462	3729555
2006	1068550	1977695	1799855	4846100
2007	1393799	2441781	2186910	6022490
2008	1703932	3217747	3537543	8459222
2009	1836142	2471066	3319331	7626538
2010	2385447	3825823	3789528	10000799
2011	3314193	6446217	5545242	15305652
2012	3634506	6790046	5794109	16218662
2013	3778395	8321394	5532070	17631859
2014	4389188	7706688	5945855	18041732
2015	4632916	7339405	7570108	19542430
2016	4870477	8536607	6603856	20010939

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania


*Angalia: Kuanzia mwaka 1990, thamani ya bidhaa zilizoagizwa ni f.o.b. badala ya c.i.f.

MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 24	US \$ milioni									
	2007 Halisi	2008 Halisi	2009 Halisi	2010 Halisi	2011 Halisi	2012 Halisi	2013 Halisi	2014 Halisi	2015 Halisi	2016 Matarajo
Urari wa Biashara	-2634.1	-3433.5	-2536.1	-2841.2	-4729.6	-4429.9	16287.2	16111.9	15245.4	14322.6
Zilizouzwa nje (fob)	2226.6	3578.8	3298.1	4324.3	5097.9	5889.2	5258.1	5194.1	5402.3	5688.8
Zilizonunuliwa toka nje (fob)*	4860.6	7012.3	5834.1	7165.5	9827.5	10319.1	-11029.1	-10917.8	-9843.1	-8633.8
Urari wa Huduma	462.1	336.9	132.7	156.9	92.2	427.5	713.2	727.3	846.0	1455.5
Mapato	1875.7	1998.8	1854.6	2045.7	2300.3	2786.4	3201.7	3396.0	3515.8	3596.8
Malipo	1413.7	1661.9	1722.0	1888.9	2208.1	2358.9	2488.5	2668.7	2669.7	2141.3
Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi	-282.1	-314.3	-297.8	-577.6	-645.8	-574.0	-705.7	-824.7	-900.2	-1066.7
Yaliyoingia	107.3	122.7	161.1	160.1	184.2	131.1	130.1	118.4	110.3	93.5
Yaliyotoka	389.4	437.0	458.9	737.651	830.0	705.1	835.8	943.1	1010.5	1160.2
Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida	651.5	833.8	891.2	1051.2	902.2	807.5	931.4	593.7	692.3	514.8
Iliyoingia	724.0	913.4	959.7	1130.2	994.9	913.0	869.6	535.6	612.2	443.5
Serikalini	626.9	588.5	658.4	798.1	609.7	544.3	517.9	178.0	246.9	63.3
Sekta nyingine	97.1	324.9	301.3	332.1	385.2	368.7	351.7	357.6	365.3	380.2
Iliyotoka	72.5	79.6	68.4	79.0	92.7	105.4	-61.8	-58.2	-80.2	-71.2
Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali	-1802.6	-2577.1	-1809.9	-2210.8	-4381.0	-3768.9	17226.0	16608.2	15883.5	15226.1
Urari wa Uhamisho wa Mitaji	938.5	524.2	442.2	537.9	690.9	777.2	658.8	522.2	354.4	327.8
Iliyoingia	938.5	524.2	442.2	537.9	690.9	777.2	658.8	522.2	354.4	327.8
Iliyotoka	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Urari katika uwekezaji	873.0	2592.8	1984.4	3063.7	2843.3	3879.6	5021.0	3499.9	3157.7	2059.1
Uwekezaji katika miradi	581.5	1383.3	952.6	1813.2	1229.5	1799.6	2087.3	1672.6	1604.6	1365.4
Uwekezaji katika hisa	4.3	1.8	3.5	3.1	11.3	6.1	4.5	11.5	27.6	-5.0
Uwekezaji aina nyingine	287.1	1207.8	1028.3	1247.4	1602.5	2073.9	2929.3	1815.9	1525.5	698.8
Makosa na Masahihisho	307.8	-391.9	-250.5	-1282.3	644.8	-561.8	-216.1	1069.8	251.7	102.5
Urari wa Malipo yote	316.7	148.0	366.2	108.5	-202.0	326.2	22689.7	21700.1	19647.3	17715.6

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

* Kuanzia mwaka 2006 bidhaa zilizouzwa nje zinajumuisha pia zile zisizorekodiwa (Unrecorded trade)



SURA YA 4

FEDHA ZA SERIKALI

Utangulizi

85. Bajeti ya mwaka 2016/17 ililenga kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015 – 2020, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21 na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ili kukidhi kiu na matarajio ya Watanzania. Bajeti ililenga kuimarisha miundombinu ya msingi ikiwemo ya maji, umeme na usafirishaji kwa ajili ya kuhakikisha maendeleo ya viwanda na kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo yanayotumika kama malighafi viwandani.

86. Pamoja na mambo mengine, Bajeti ya mwaka 2016/17 ilijielekeza katika kufikia shabaha na malengo yafuatayo: mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri kufikia asilimia 16.9 ya Pato la Taifa; mapato ya kodi kufikia asilimia 13.8 ya Pato la Taifa; matumizi ya Serikali kufikia asilimia 27.0 ya Pato la Taifa ; na nakisi ya bajeti kuwa asilimia 4.5 ya Pato la Taifa.

87. Katika kipindi cha mwaka 2016/17, Serikali ilipanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 29,539.6 kutoka kwenye vyanzo vya ndani na nje. Sera za mapato ya ndani katika mwaka 2016/17 zililenga kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya shilingi bilioni 17,798.1 sawa na asilimia 16.3 ya Pato la Taifa. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi ni shilingi bilioni 15,105.1 na mapato yasiyo ya kodi ni shilingi bilioni 2,693.0. Aidha, mapato yanayotokana na vyanzo vya halmashauri yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 665.4 sawa na asilimia 0.6 ya Pato la Taifa. Vile vile, mikopo ya ndani ilikadiriwa kuwa shilingi bilioni 5,374.3; misaada na mikopo yenye masharti nafuu kutoka nje ilikadiriwa kuwa shilingi bilioni 3,600.8; na mikopo ya kibiashara kutoka nje shilingi bilioni 2,100.9.

Mwenendo wa Mapato

Mapato ya Ndani

88. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, makusanyo ya ndani ikijumuisha mapato ya halmashauri yalifikia shilingi bilioni 12,465.8, sawa na asilimia 91 ya makadirio ya shilingi bilioni 13,752.1 katika kipindi hicho.

Mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 10,626.3 ikiwa ni asilimia 95 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 11,233.4 kwa kipindi hicho. Mwenendo huu umetokana na usimamizi madhubuti wa makusanyo kwenye malimbikizo ya kodi, kupanua wigo wa kodi kwa kusajili walipa kodi wapya, pamoja na utekelezaji wa mikakati ya kuongeza makusanyo ya kodi. Hata hivyo, kutofikiwa kwa malengo ya mapato ya kodi yaliyokusudiwa katika kipindi hicho kulitokana na: kushuka kwa mauzo ya baadhi ya bidhaa katika soko la ndani katika kipindi husika kama vile, vinywaji hususan bia na bidhaa nyinginezo za jumla na reja reja; mabenki makubwa kufanya marekebisho ya makisio yao ya kulipa kodi kutokana na kushuka kwa mapato ya riba kulikosababishwa na kupungua kwa utoaji wa mikopo katika sekta hii; kupungua kwa huduma zinazotolewa kwenye utafiti na uchimbaji wa madini, mafuta na gesi asilia ambako kuliathiri kodi ya zuio; kutoongezeka kwa ajira kama ilivyotarajiwa na hivyo kuathiri kodi ya mapato; kutotumika kikamilifu kwa mashine za kielektroniki; na sekta isiyo rasmi kuendelea kuwa kubwa.

89. Kwa upande wa maduhuli hadi Machi 2017, lengo lilikuwa ni kukusanya shilingi bilioni 2,019.6 ambapo makusanyo halisi yalifikia shilingi bilioni 1,484.9 sawa na asilimia 73.5 ya lengo. Sababu za kutofikia lengo kwa makusanyo yasiyotokana na kodi ni pamoja na baadhi ya mashirika kutowasilisha michango yao ya asilimia 15 kwa wakati. Vile vile, baadhi ya Wizara na Idara zinazojitegemea ziliendelea kutumia mifumo isiyo ya kielektoniki katika kukusanya maduhuli na hivyo kusababisha upotevu wa mapato.

90. Mapato yanayokusanywa na halmashauri yalifikia shilingi bilioni 354.6 sawa na asilimia 71 ya makadirio ya shilingi bilioni 499.1 kwa kipindi hicho. Sababu ya kutofikiwa kwa malengo ya mapato ya halmashauri ni pamoja na kutokutumika kikamilifu kwa mifumo ya kiutawala iliyopo katika kukusanya mapato na kuchelewa kuanza kwa ukusanyaji wa kodi ya majengo kwa baadhi ya halmashauri, hususan zilizochukuliwa na Mamlaka ya Mapato kupisha kipindi cha mpito cha maandazi ya taratibu za ukusanyaji wa kodi hiyo.

Misaada na Mikopo Nafuu

91. Hadi kufikia Machi 2017, shilingi bilioni 2,247.9 zilipokelewa sawa na asilimia 68.9 ya ahadi za shilingi bilioni 3,263.3 katika kipindi hicho. Kati ya

hizo, misaada na mikopo nafuu ya kibajeti ilikuwa shilingi bilioni 111.4 ikiwa ni asilimia 43.2 ya makadirio ya kipindi hicho ya shilingi bilioni 258.0, mifuko ya kisekta shilingi bilioni 292.9 ambayo ni asilimia 78.9 ya makadirio ya shilingi bilioni 372.1 katika kipindi hicho na miradi ya maendeleo shilingi bilioni 1,843.6 sawa na asilimia 70.0 ya makadirio ya shilingi bilioni 2,633.2.

92. Kupungua kwa misaada na mikopo nafuu kutoka nje kunafuatia kudorora kwa uchumi kwa baadhi ya nchi zinazotoa misaada na mtazamo mpya kuhusu mfumo wa ushirikiano baina ya mataifa hayo na Afrika. Aidha, sababu nyingine za kuchelewa kutolewa kwa fedha zilizoahidiwa ni pamoja na washirika wa maendeleo kufanya mabadiliko ya ahadi za awali na kuingiza masharti ambayo hayakuwepo kwenye makubaliano ya awali na hivyo kusababisha baadhi yao kupunguza ahadi na wengine kutotoa kabisa.

Mikopo ya Ndani

93. Hadi Machi 2017, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 4,296.1 ikiwa ni asilimia 118.8 ya kiasi kilichopangwa kukopwa katika kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 3,657.8 zilikopwa kwa ajili ya kulipia dhamana za Serikali zilizoiva (rollover) na shilingi bilioni 638.4 kwa ajili ya mikopo mipya, sawa na asilimia 87.1 ya kiasi kilichopangwa kukopwa kwa kipindi hicho. Aidha, mikopo kutoka kwenye chanzo hiki ilielekezwa kulipia sehemu ya madeni ya wakandarasi wa barabara na maji, ujenzi wa mitambo ya kufua umeme wa Kinyerezi III pamoja na ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

Mikopo yenye Masharti ya Kibiashara

94. Mwaka 2016/17, Serikali ilipanga kukopa mikopo yenye masharti ya kibiashara kutoka nje kwa kiasi cha shilingi bilioni 2,100.9 ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Hata hivyo, hadi kufikia Machi, 2017 Serikali haikuweza kukopa kutoka katika chanzo hiki kutokana na hali ya soko la fedha la kimataifa kutokuwa nzuri.

Matumizi

95. Sera za matumizi kwa mwaka 2016/17 zililenga kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya Serikali. Sera hizi zilikusudia kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, kuziba mianya ya uvujaji wa fedha za umma na kuelekeza kiasi kikubwa

cha fedha kwenye miradi ya maendeleo. Aidha, sera zililenga kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/17 wenye maeneo makuu manne (4) ya vipaumbele, ambayo ni: (i) Viwanda vya kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda; (ii) Kufungamanisha Maendeleo ya Uchumi na Rasilimali Watu; (iii) Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji wa Biashara na Uwekezaji na (iv) Usimamizi wa Utekelezaji wa Mpango.

96. Mwaka 2016/17, Serikali ilikadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni 29,539.6 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi bilioni 17,719.1 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 11,820.5 kwa matumizi ya maendeleo, sawa na asilimia 40 ya bajeti yote. Kwa kipindi cha Julai, 2016 – Machi, 2017 jumla ya shilingi bilioni 19,010.1 zilitolewa kwa ajili ya matumizi mbalimbali kwa wizara, idara zinazojitegemea, sekretarieti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 14,027.8 zilizotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 4982.3 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

97. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, malipo ya riba kwa madeni ya ndani na nje yalifikia shilingi bilioni 1,342.4 ambayo ni asilimia 95.9 ya makadirio ya shilingi bilioni 1,399.6 kwa kipindi hicho. Aidha, malipo ya mkopo yalifikia shilingi bilioni 4,544.1 ikiwa ni asilimia 121.9 ya lengo la shilingi bilioni 3,726.2. Kati ya malipo hayo, shilingi bilioni 886.3 zilikuwa malipo ya mkopo wa nje sawa na asilimia 105.2 ya lengo la kulipa shilingi bilioni 842.4. Shilingi bilioni 3,657.8 zilikuwa malipo ya dhamana za Serikali zilizoiva (rollover) ikiwa ni asilimia 126.8 ya lengo la shilingi bilioni 2,883.7 kwa kipindi hicho. Matumizi mengine ya Mfuko Mkuu (CFS Others) yalikuwa shilingi bilioni 927.3 ikiwa ni asilimia 82.6 ya makadirio ya shilingi bilioni 1,122.7 ya kipindi hicho.

98. Hadi Machi 2017, malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali yalikuwa shilingi bilioni 4,793.0 sawa na asilimia 96.9 ya lengo la shilingi bilioni 4,945.1. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1,465.9 zililipwa kwa watumishi wa Serikali Kuu, shilingi bilioni 110.0 zililipwa kwa watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na shilingi bilioni 2,638.2 kwa watumishi wa halmashauri za majiji, manispaa, miji na wilaya. Aidha, Serikali ililipa mishahara ya Taasisi na Mashirika ya Umma jumla ya shilingi bilioni 578.9.

99. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, Serikali ilipanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 8,775.0 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali, ambapo shilingi bilioni 5,657.2 zilikuwa fedha za ndani na shilingi bilioni 3,117.8 fedha za nje. Hadi Machi, 2017, shilingi bilioni 4982.3 sawa na asilimia 56.8 ya makadirio zilitolewa. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 3,352.3 zilikuwa fedha za ndani sawa na asilimia 59.3 na shilingi bilioni 1,630.0 fedha za nje sawa na asilimia 52.3. Miradi iliyopewa kipaumbele kwenye mgao ni pamoja na maeneo yenye vyanzo vyake vya mapato ikiwa ni pamoja na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Umeme vijijini, Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Reli na Mfuko wa Maji Vijijini. Maeneo mengine ni ulipaji wa madeni ya wakandarasi.


100. Baadhi ya mahitaji yaliyopewa kipaumbele zaidi katika utoaji wa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo kwa kipindi cha Julai, 2016 – Machi, 2017 ni pamoja na: ununuzi wa ndege mbili za Serikali na malipo ya awali ya ununuzi wa ndege 4 shilingi bilioni 227.6; elimu msingi bila malipo shilingi bilioni 159.8; upanuzi wa uwanja wa ndege wa Dodoma na Mwanza shilingi bilioni 12.4; uzalishaji wa umeme, uboreshaji wa njia za kupitisha umeme na usambazaji wa umeme vijijini shilingi bilioni 389.2; ujenzi na ukarabati wa barabara kuu za mikoa na halmashauri shilingi bilioni 1,133.5; usambazaji wa maji mijini na vijijini shilingi bilioni 175.9; mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu shilingi bilioni 375.2; Mfuko wa Reli shilingi bilioni 111.7 na malipo ya awali ya ujenzi wa reli kwa kiwango cha ‘standard gauge’ shilingi bilioni 300; uboreshaji wa huduma za afya katika ngazi zote ikiwemo ununuzi wa dawa na vifaa tiba shilingi bilioni 256.1; na uendeshaji wa shughuli za Mfuko wa Bunge shilingi bilioni 60.8.

Deni la Taifa

101. Hadi kufikia Machi 2017, deni la Taifa lilifikia shilingi bilioni 42,883.59 ikilinganishwa na shilingi bilioni 38,071.58 Machi 2016, sawa na ongezeko la asilimia 12.6. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 12,073.68, sawa na ongezeko la shilingi bilioni 2,070.83 na deni la nje lilikuwa

shilingi bilioni 30,809.91, sawa na ongezeko la shilingi bilioni 2,741.25 ikilinganishwa na kipindi kama hicho Machi 2016 (Kielelezo 4.1).

Kielelezo Na. 4.1: Mwenendo wa Deni la Taifa kwa kipindi cha Machi 2011 - Machi, 2017 (Tsh Bilioni)



Deni la Nje

102. Hadi Machi 2017, deni la Taifa la nje lilikuwa dola za Marekani milioni 13,783.90 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 12,814.40 mwezi Machi 2016, sawa na ongezeko la asilimia 7.6. Ongezeko hilo lilitokana na kupokelewa kwa mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo na malimbikizo ya riba kwa nchi ambazo si mwanachama wa kundi la Paris. Kiasi hicho cha malimbikizo ya riba kilifikia dola za Marekani 772.00 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 723.60 Machi 2016.

Deni la Nje kwa Wakopeshaji

103. Hadi kufikia Machi 2017, mashirika ya fedha ya kimataifa yalichangia asilimia 56.8 ya deni la nje ikilinganishwa na asilimia 55.3 Machi 2016, mikopo yenye masharti ya kibiashara ilichangia asilimia 29.3 na mikopo kutoka nchi wahisani ilichangia asilimia 13.8 ya mikopo yote ya nje. Aidha, Serikali imedhamiria kuendelea kukopa kutoka kwenye vyanzo nafuu na kuhakikisha kuwa mikopo hiyo inatumika kugharamia miradi ya maendeleo inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi.

Jedwali Na.4.1:- Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Wakopeshaji


Taasisi	Machi 2015	Mchango kwa %	Machi 2016	Mchango kwa %	Machi 2017	Mchango kwa %
Mashirika ya Fedha	6,196.8	52.8	7,084.0	55.3	7,834.4	56.8
Washirika wa Maendeleo	1,866.5	15.9	1,732.0	13.5	1,905.3	13.8
Benki za Kibiashara	3,665.6	31.3	3,998.4	31.2	4,044.2	29.3
Jumla	11,728.9	100	12,814.4	100	13,783.9	100

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

Deni la Ndani

Hadi Machi 2017, deni la ndani lilifikia shilingi bilioni 12,074.60 ikilinganishwa na shilingi bilioni 10,002.85 Machi 2016, sawa na ongezeko la asilimia 20.7. Ongezeko la deni la ndani lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya Serikali kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kielelezo Na. 4.2 Mwenendo wa Deni la Ndani kwa kila Dhamana.



Deni la Ndani kwa Wakopeshaji

104. Hadi kufikia Machi 2017, benki za biashara zilikuwa zinaongoza kwa kuhodhi asilimia 49.14 ya deni la ndani ikilinganishwa na asilimi 59.74 ya kipindi kama hicho mwaka 2016. Mifuko ya hifadhi ya jamii ni ya pili kwa kuhodhi asilimia 32.15 ikifuatiwa na kampuni za bima asilimia 11.87.

Jedwali Na. 4.2: Deni la Ndani kwa Wakopeshaji hadi Machi 2017

Taasisi	Machi 2015	Mchango kwa %	Machi 2016	Mchango kwa %	Machi 2017	Mchango kwa %
Benki za Biashara	4,446.27	64.81	4,859.48	59.74	4,578.83	49.14
Taasisi za Fedha	111.32	1.62	117.63	1.45	145.75	1.56
Mifuko ya Jamii	1,383.98	20.17	1,383.98	17.01	2,995.30	32.15
Kampuni za Bima	676.49	9.86	798.75	9.82	1,105.75	11.87
Mashirika Madogo	106.56	1.55	187.12	2.49	193.83	2.08
Watu Binafsi	136.04	1.98	175.55	2.12	297.7	3.2
Jumla	6,860.66	100	7,522.52	100	9,317.16	100

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

Tathmini ya Uhimilivu wa Deni

105. Matokeo ya tathmini ya uhimilivu wa deni la Taifa iliyofanyika Novemba, 2016, ilionesha kuwa deni la Taifa ni himilivu. Viashiria vya deni vinaonesha kuwa: thamani ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 19.9 ikilinganishwa na ukomo wa asilimi 40; thamani ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 97.7 ikilinganishwa na ukomo wa asilimi 150; thamani ya deni la nje kwa mapato ya ndani ni asilimia 145.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 250; na ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato ya ndani umefikia asilimia 7.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 20. Viashiria hivyo vinaonesha uwezo wa nchi kukopa na kulipa deni. Kwa kuzingatia vigezo hivyo, Tanzania bado ina uwezo wa kuendelea kukopa kutoka ndani na nje ya nchi ili kugharamia shughuli zake za maendeleo na pia ina uwezo wa kulipa mikopo inayoiva kwa kutumia mapato yake ya ndani na nje kwa wakati.

Jedwali Na. 4.3: Viashiria vya Uhimilivu wa Deni hadi mwaka 2035/36

VIASHIRIA VYA DENI LA NJE	2015/16	2016/17	2017/18	2018/19	2020/21	2025/26	2035/36	Ukomo
Deni (PV[1]) /Pato la Taifa	19.9	19	18.8	18.6	20.1	18.9	14.4	40
Deni (PV) / uuzaji wa bidhaa nje	97.7	94.2	98.2	100.6	107.4	95.5	71	150
Deni (PV) / Mapato ya ndani	145.3	111.5	114.3	107.6	98.7	91.8	68.4	250
Ulipaji wa deni la nje/Uuzaji wa bidhaa nje	7.8	9.2	8.4	8.7	8.0	7.9	8.0	20
Ulipaji wa deni/ Mapato ya ndani	11.5	11.0	9.7	9.3	7.3	7.6	7.7	20
VIASHIRIA VYA DENI LA NJE NA LA NDANI	2015/16	2016/17	2017/18	2018/19	2020/21	2025/26	2035/36	Ukomo
Deni (PV) /Pato la Taifa	34.2	32.5	31.2	30.8	32.7	29.4	23.3	56
Deni (PV) / Mapato ya ndani	249.6	178.5	177.6	168.3	153.9	137	108	
Ulipaji wa deni/ Mapato ya ndani	30.8	21.1	23.4	20.6	16.9	16.6	16.1	

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

PV = Present value


MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI

Jedwali Na. 25

Sh.milioni

	2011/12	2012/13	2013/14	2014/15	2015/16	2016/17	2016/17	2016/17
	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Bajeti	Matokeo hadi Machi	Matarajio hadi Juni
A. MAPATO YA NDANI (yakijumuisha Halmashauri)	7221409	8442611	10182455	10957765	14048034	18463533	12465835	16880361
MAPATO YA NDANI	7025884	8221776	9867227	10597681	13622182	17798118	12111235	16348029
1. Mapato yatokanayo na Kodi	6480478	7729986	9294417	9891680	12410951	15079514	10626287	14243469
Ushuru wa Forodha na Excise Duty	1538617	1845218	2243413	2495082	3090110	3547600	2460771	3421769
Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)	2072621	2374977	2647665	3031828	3553637	4635666	3000190	4311169
Bidhaa toka nje	1082918	1240149	1329477	1519939	1717902	2102428	1346196	1955258
Bidhaa za ndani	989703	1134829	1318188	1511889	1835735	2533238	1653994	2355911
Kodi ya Mapato	2311350	3036110	3791713	3727934	4608245	5325815	3505666	4793233
Kodi nyingine	732303	706910	1123779	1278648	1921459	2336938	1749129	2100551
Marejesho (Refunds Accounts)	-174414	-233231	-512153	-641811	-762499	-766504	-89469	-383252
2. Mapato yasiyotokana na Kodi	545406	491790	572810	706001	1211231	2718604	1484948	2104560
3. Mapato ya Halmashauri	195525	220835	315228	360084	425852	665415	354600	532332
B. JUMLA YA MATUMIZI	10764528	13543018	13958162	14603714	17759598	24796623	14466058	25940743
1. Matumizi ya Kawaida	6989807	9043323	10032120	10893486	13420045	12976120	9483752	17669341
2. Matumizi ya Maendeleo	3774722	4499695	3926042	3710228	4339553	11820503	4982306	8271402
Fedha za ndani	1872312	2314718	2121212	2264506	2904530	8702697	3352302	6326290
Fedha za nje	1902410	2184977	1804831	1445722	1435023	3117805	1630003	1945113
C. NAKISI/SALIO (A-B)	-3543120	-5100407	-3775707	-3645949	-3711564	-6333090	-2000223	-9060383
D. KUZIBA NAKISI	3543120	5100407	3775707	3830651	6281252	4895700	2298195	3606135
1. Fedha kutoka nje	3590357	3942498	3858785	3030875	3982100	4735934	1463243	2732209
Ruzuku	1855097	1447013	1399025	896496	1349799	1244380	619973	793560
Basket support	172212	280936	188623	127637	81073	178675	89078	142940
Mikopo ya uagizaji bidhaa/OGL	246850	543817	733822	537881	546846	497149	279201	312239
Mikopo ya miradi	595414	734389	524019	640724	344800	1680603	1259715	1008362
Mikopo ya masharti ya kibiashara	801282	1063006	1194516	1054803	2142469	2100995	101526	1313684
Kulipia madeni ya nje (Amortization Foreign)	-80497	-126663	-181220	-226667	-482887	-965868	-886250	-838577
2. Fedha za Ndani	-47237	1157910	-83078	799776	2299151	159766	834952	873926
Mikopo isiyo ya mabenki	263614	401391	21216	0	776945	0	0	87393
Mikopo ya mabenki	71250	667930	205526	799776	1522207	159766	834952	786534
Mikopo ya ndani (Rollover)	1326852	1734535	1528153	2064756	2600000	3777112	3657800	4615670
Mapato ya Ubinafsisishaji	0	0	0	0	0	0	0	0
Marekebisho (Adjustment to Cash)	-198539	439984	300810	0	0	0	0	0
Kulipia madeni ya ndani (amortization)	-1326852	-1734535	-1528153	-2064756	-2600000	-3777112	-3657800	-4615670
Expenditure float	-183562	-351395	-610630	0	0	0	0	0

Chanzo: Wizara ya Fedha



MGAWANYO WA MATUMIZI YA SERIKALI KWA HUDUMA ZA SERIKALI													
Fungu	Maelezo	2014/2015 (Hali)						2015/2016 (Bajeti)			TShs Milioni		
		2014/2015 (Hali)			2015/2016 (Bajeti)			2016/2017 (Makadirio)					
		Matumizi ya kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla	Matumizi ya kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla	Matumizi ya kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla			
701	Huduma za Kawaida	6,926,356	413,831	7,340,188	8,256,128	1,172,472	9,428,601	9,367,231	1,586,950	10,954,181			
70111	Utawala na Shughuli za Bunge	571,204	123,557	694,761	674,594	178,301	852,895	589,713	470,881	1,060,594			
70112	Fedha na Masuala ya Kodi	252,478	23,664	276,143	688,577	667,716	1,356,293	354,026	726,170	1,080,196			
70113	Mambo ya Nje	194,291	16,656	210,946	130,847	10,079	140,926	132,024	10,521	142,546			
70121	Misaada ya Kiuchumi kutoka Nje	1,420	0	1,420	1,928	0	1,928	0	0	0			
70122	Misaada ya Kiuchumi kupitia Mashirika ya Kimataifa	51	0	51	193	0	193	348	0	348			
70131	Huduma za Umma	56,611	1,632	58,243	54,162	5,811	59,973	54,629	27,708	82,337			
70132	Huduma za Mipango na Takwimu	75,129	36,955	112,083	68,512	14,933	83,445	170,953	30,014	200,966			
70133	Huduma nyingine za Kawaida	32,959	205,692	238,651	31,266	282,816	314,081	30,662	306,639	337,301			
70140	Utafiti wa Msingi	0	0	0	32	0	32	18	0	18			
70150	Utafiti na Maendeleo Huduma za Umma	0	0	0	0	0	0	549	0	549			
70160	Huduma za Umma zisizotajwa hapo juu	248,729	4,123	252,852	211,382	11,765	223,147	21,780	11,863	33,643			
70170	Deni la Taifa	5,490,511	0	5,490,511	6,390,465	0	6,390,465	8,009,341	0	8,009,341			
70180	Uhamishaji Fedha Ndani ya Serikali	2,974	1,552	4,527	4,171	1,050	5,221	3,188	3,154	6,341			
702	Ulinzi	1,144,361	73,450	1,217,811	1,440,925	231,205	1,672,130	1,485,916	247,750	1,734,474			
70210	Huduma za Ulinzi wa Kijeshi	1,144,361	73,450	1,217,811	1,440,925	231,205	1,672,130	1,485,916	247,750	1,734,474			
70220	Huduma za Ulinzi wa Kiraia	0	0	0	0	0	0	238	0	238			
70230	Misaada ya Nje ya Ulinzi	0	0	0	0	0	0	0	0	0			
70240	Utafiti na Maendeleo ya Ulinzi	0	0	0	0	0	0	570	0	570			
70250	Huduma za Ulinzi zisizotajwa hapo juu	0	0	0	0	0	0	0	0	0			
703	Usalama wa Raia	628,342	61,223	689,564	748,974	27,600	776,575	746,633	66,597	813,230			
70310	Huduma za Polisi	567,648	60,335	627,983	542,766	12,311	555,077	595,429	14,870	610,299			
70320	Huduma za Zimamoto	7,719	0	7,719	12,401	0	12,401	9,754	0	9,754			
70330	Mahakama	35,248	888	36,136	176,143	13,689	189,833	116,271	48,727	164,998			
70340	Magereza	15,811	0	15,811	15,706	1,600	17,306	23,844	3,000	26,844			
70350	Huduma za utafiti na Maendeleo Usalama wa Raia	0	0	0	0	0	0	0	0	0			
70360	Huduma Usalama wa Raia zisizotajwa hapo juu	1,915	0	1,915	1,959	0	1,959	1,335	0	1,335			
704	Shughuli za Kiuchumi	3,605,754	1,914,033	5,519,788	4,456,780	2,970,060	7,426,840	4,501,045	7,420,827	11,921,872			
70411	Shughuli za Kiuchumi na Biashara	29,628	2,429	32,057	43,363	14,892	58,255	35,733	10,765	46,498			
70412	Masuala ya Kazi	11,145	1,399	12,544	19,578	21,810	41,388	16,602	20,580	37,182			
70421	Kilimo	3,238,802	428,036	3,666,838	3,953,779	733,652	4,687,431	4,065,233	1,381,761	5,446,993			
70422	Misitu	17,696	2,852	20,548	21,202	4,213	25,414	71,551	8,452	80,003			
70423	Uvuvi na Uwindaji	9,943	0	9,943	8,151	7,401	15,552	7,647	9,873	17,520			
70431	Makaa ya Mawe na Nishati nyingine	6,266	900	7,166	6,777	12,660	19,437	5,137	13,360	18,497			
70432	Petrol na Gesi Asilia	15,740	387,456	403,195	48,972	495,386	544,358	22,609	1,031,755	1,054,364			
70433	Nishati ya Nyukilia	0	0	0	0	0	0	0	0	0			
70434	Nishati nyingine	0	0	0	0	0	0	0	0	0			
70435	Umeme	950	0	950	659	349,873	350,532	500	0	500			
70436	Nishati isiyo ya umeme	12,027	0	12,027	12,219	0	12,219	6,030	0	6,030			
70441	Uchimbaji Madini yasiyo Nishati	39,596	7,750	47,346	59,612	6,697	66,308	32,038	19,156	51,195			
70442	Uzalishaji Viwandani	3,460	63,576	67,036	4,587	10,780	15,367	3,658	17,000	20,658			
70443	Ujenzi	76,925	20,716	97,640	98,351	88,499	186,850	40,660	63,253	103,913			
70451	Usafiri wa Barabara	111,551	955,459	1,067,009	131,670	957,594	1,089,264	109,102	2,706,205	2,815,306			
70452	Usafiri wa Majini	0	0	0	0	0	0	0	0	0			
70453	Usafiri wa Reli	0	0	0	0	0	0	0	0	0			
70454	Usafiri wa Anga	235	30,847	31,082	458	182,763	183,221	160	1,937,814	1,937,974			
70455	Usafirishaji kwa njia ya Bomba na njia nyingine za usafiri	1,707	625	2,332	2,992	15,070	18,061	1,268	0	1,268			
70460	Mawasiliano	4,490	339	4,829	8,967	2,097	11,065	7,633	92,390	100,023			
70471	Huduma za Biashara na Utunzaji Mizigo	2,177	160	2,336	3,636	3,459	7,095	13,349	18,200	31,549			
70472	Hoteli na Migahawa	0	0	0	0	0	0	0	0	0			
70473	Utalii	11,171	0	11,171	14,443	400	14,843	13,810	1,000	14,810			
70474	Miradi ya Maendeleo	4,007	9,693	13,699	5,806	51,829	57,634	40,669	58,428	99,097			
70481	Utafiti katika shughuli za Kiuchumi, Biashara na Kazi	172	50	222	235	933	1,168	160	250	410			
70482	Utafiti na Maendeleo ya Kilimo, Misitu, Uvuvi na Uwindaji	0	0	0	0	0	0	0	0	0			
70483	Utafiti na Maendeleo ya Mafuta na Nishati	0	0	0	0	0	0	0	0	0			
70484	Utafiti na Maendeleo ya Uchimbaji Madini, Uzalishaji Viwandani na Ujenzi	0	0	0	0	0	0	0	0	0			
70485	Utafiti na Maendeleo ya Usafiri	0	0	0	0	0	0	0	0	0			
70486	Utafiti na Maendeleo ya Mawasiliano	0	0	0	0	0	0	0	0	0			
70487	Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Vingine	0	0	0	0	0	0	0	0	0			
70490	Shughuli nyingine za Kiuchumi zisizotajwa hapo juu	8,068	1,749	9,816	11,325	10,053	21,378	7,497	30,585	38,082			
	<i>Jedwali linaendelea ukurasa unaofuata</i>												

Fungu	Maelezo	2014/2015 (Halisi)			2015/2016 (Bajeti)			2016/2017 (Makadirio)		
		Matumizi ya kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla	Matumizi ya kawaida	Matumizi ya	Jumla	Matumizi ya kawaida	Matumizi ya	Jumla
705	Hifadhi ya Mazingira	22,271	10,558	32,829	32,309	21,357	53,665	35,719	41,542	77,261
70510	Hifadhi ya Taka	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70520	Hifadhi ya Maji Taka	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70530	Kupunguza Uharibifu wa Mazingira	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70540	Hifadhi ya Viumbwani na Mazingira	13,870	222	14,092	21,561	2,370	23,931	25,573	8,295	33,867
70550	Utafiti na Maendeleo ya Hifadhi ya Mazingira	390	0	390	422	1,571	1,993	308	5,000	5,308
70560	Huduma nyingine za Hifadhi ya Mazingira zisizotajwa hapo juu	8,011	10,336	18,347	10,325	17,416	27,741	9,839	28,248	38,086
706	Nyumba na Huduma za Jamii	34,917	137,403	172,320	72,542	495,842	568,384	51,097	909,972	961,069
70610	Maendeleo ya Nyumba	9,397	18,335	27,732	21,848	17,998	39,845	16,925	7,800	24,725
70620	Maendeleo ya Jamii	9,031	782	9,814	29,384	4,704	34,088	15,867	2,942	18,808
70630	Usambazaji Maji	15,975	116,024	131,999	20,620	470,342	490,962	17,720	896,231	913,951
70640	Taa za Barabarani	514	2,262	2,776	691	2,799	3,490	585	3,000	3,585
70650	Utafiti wa Nyumba na Maendeleo ya Jamii	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70660	Nyumba na Huduma za Jamii zisizotajwa hapo juu	0	0	0	0	0	0	0	0	0
707	Afya	418,425	265,583	684,008	514,134	456,894	971,028	459,416	536,547	995,963
70711	Madawa	0	0	0	31,355	0	31,355	221	251,500	251,721
70712	Bidhaa nyingine za madawa	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70713	Huduma za Tiba na Vifaa vya Tiba	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70721	Huduma za Tiba za Jumla	226,705	15,497	242,201	229,401	62,379	291,780	209,870	52,240	262,110
70722	Huduma Maalumu za Tiba	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70723	Huduma za Meno	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70724	Huduma za Wakunga Wasaidizi	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70731	Huduma za Hospitali	22,234	1,783	24,017	30,486	2,867	33,353	27,431	3,581	31,012
70732	Huduma za Hospitali Maalumu	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70733	Huduma za Vifaa vya Kujifungulia Wajawazito	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70734	Huduma za Wakunga na Wakunga wa Jadi	0	0	0	422	0	422	325	0	325
70740	Huduma za Afya	42,570	184,668	227,238	51,912	348,889	400,802	53,458	165,925	219,383
70750	Utafiti na Maendeleo ya Huduma za Afya	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70760	Huduma za Afya zisizotajwa hapo juu	126,916	63,636	190,552	170,558	42,758	213,316	168,112	63,302	231,414
708	Burudani, Utamaduni na Dini	14,036	9,000	23,036	18,014	2,150	20,164	14,470	2,200	16,670
70810	Huduma za Burudani na Michezo	2,380	4,000	6,380	2,744	100	2,844	1,416	100	1,516
70820	Huduma za Utamaduni	3,906	2,000	5,906	5,552	1,000	6,552	4,656	0	4,656
70830	Huduma za Utangazaji na Uchapishaji	7,362	3,000	10,362	9,424	1,050	10,474	7,692	1,100	8,792
70840	Dini na Huduma nyingine za Kijamii	0	0	0	0	0	0	438	1,000	1,438
70850	Utafiti na Maendeleo katika Burudani, Utamaduni na Dini	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70860	Huduma nyingine za Burudani, Utamaduni na Dini zisizotajwa hapo juu	387	0	387	294	0	294	267	0	267
709	Elimu	560,418	439,722	1,000,141	754,571	505,209	1,259,780	722,822	954,150	1,676,972
70911	Elimu ya Awali	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70912	Elimu ya Msingi	16,013	44,928	60,941	24,066	45,804	69,870	21,470	21,373	42,842
70921	Elimu ya Sekondari (Kidato cha I - IV)	364	10,782	11,146	467	9,921	10,388	289	7,000	7,289
70922	Elimu ya Sekondari (Kidato cha V - VI)	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70930	Elimu baada ya Sekondari isiyo ya Chuo Kikuu	419	635	1,055	526	0	526	398	100	498
70941	Daraja la Awali Elimu ya Chuo Kikuu	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70942	Daraja linalofuata Elimu ya Chuo Kikuu	0	0	0	6,625	1,000	7,625	2,157	6,000	8,157
70950	Elimu isiyopambanuliwa	194,559	29,214	223,773	221,002	5,418	226,420	211,263	50,192	261,455
70960	Huduma za Ziada kwa Elimu	317,387	354,163	671,550	486,500	443,065	929,565	470,695	867,985	1,338,680
70970	Utafiti na Maendeleo ya Elimu	0	0	0	0	0	0	10,048	0	10,048
70980	Huduma za Elimu zisizotajwa hapo juu	31,677	0	31,677	15,386	0	15,386	6,502	1,500	8,002
710	Kinga ya Jamii	264,100	16,658	280,758	292,061	26,262	318,323	333,944	53,967	387,911
71011	Ugonjwa	0	0	0	0	0	0	0	0	0
71012	Ulemavu	0	0	0	0	0	0	0	0	0
71020	Wazee	0	0	0	0	0	0	0	0	0
71030	Waathirika	0	0	0	0	0	0	0	0	0
71040	Familia na Watoto	123,678	14,339	138,017	150,556	22,006	172,562	158,989	49,584	208,573
71050	Ukosefu wa Ajira	0	0	0	0	0	0	0	0	0
71060	Nyumba	0	0	0	0	0	0	0	0	0
71070	Huduma za Jamii zisizotajwa hapo juu	521	1,041	1,561	560	750	1,310	608	0	608
71080	Utafiti na Maendeleo ya Kinga ya Jamii	0	0	0	0	0	0	0	0	0
71090	Huduma za Kinga ya Jamii zisizotajwa hapo juu	139,902	1,278	141,180	140,946	3,505	144,451	174,347	4,383	178,730
Jumla Kuu		13,618,980	3,341,462	16,960,442	16,586,439	5,909,051	22,495,490	17,719,100	11,820,503	29,539,603
	Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu									
	CS: Huduma za umma zinazotolewa na serikali na wanufaika ni watu wote									
	IS: Huduma za umma zinazotolewa na serikali na wanufaika ni wanakaya									

SURA YA 5

FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA

Ujazi wa Fedha na Karadha

106. Mwaka 2016, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kutekeleza sera ya fedha iliyolenga kudhibiti ujazi wa fedha ili uendane na mahitaji halisi ya uchumi kwa lengo la kuzuia ongezeko la mfumuko wa bei. Katika kipindi hicho, ujazi wa fedha kwa tafsiri finyu (M1) uliongezeka kutoka shilingi bilioni 9,575.7 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 9,986.7, sawa na ongezeko la asilimia 4.3. Aidha, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) uliongezeka kwa asilimia 4.7, kutoka shilingi bilioni 15,780.1 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 16,523.2 mwaka 2016. Kwa upande mwingine, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka na kufikia shilingi bilioni 22,760.4 kutoka shilingi bilioni 22,115.3 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 2.9. Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) na kwa tafsiri pana zaidi (M3) kwa mwaka 2016 ulikuwa chini ya kiwango cha ukuaji wa asilimia 13.4. na asilimia 18.8 mwaka 2015, kwa mtiririko huo. Mwenendo huu ulitokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa rasilimali katika fedha za kigeni kwenye mabanki na mikopo kwa sekta binafsi na Serikali kuu. Kupungua kwa mikopo kwa Serikali kuu kulitokana na kuongezeka kwa mapato ya serikali pamoja na kuimarika kwa usimamizi wa matumizi ya serikali. Aidha, kupungua kwa kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kumechangiwa na tahadhari zinazoendelea kuchukuliwa na mabanki katika kutoa mikopo kufuatia ongezeko la mikopo chechefu.

Mwenendo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi

107. Mwaka 2016, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 7.2 na kufikia shilingi bilioni 16,608.9 kutoka shilingi bilioni 15,492.7 mwaka 2015. Ukuaji huu ulikuwa chini ya ukuaji wa mwaka 2015 wa asilimia 24.7. Aidha, mikopo kwa sekta binafsi ilikuwa sawa na wastani wa asilimia 15.4 ya Pato la Taifa, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 16.6 mwaka 2015. Ukuaji wa mikopo kwenye shughuli za uzalishaji katika kilimo, uchukuzi na mawasiliano, viwanda, huduma za kifedha, umeme, majengo na ujenzi ulipungua ikilinganishwa na mwaka 2015. Vile vile, mikopo katika shughuli za madini na uchimbaji mawe, biashara, utalii, hoteli na migahawa na watu binafsi iliimarika japo kwa kasi ndogo ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Hata hivyo, sehemu

kubwa ya mikopo hiyo ilielekezwa katika shughuli za biashara ambazo zilipata wastani wa asilimia 20.9 ya mikopo yote ikifuatiwa na shughuli za watu binafsi asilimia 18.6 na shughuli za viwanda asilimia 10.2.

Amana Katika Benki za Biashara

108. Mwaka 2016, amana katika benki za biashara ziliongezeka kwa asilimia 2.3 na kufikia shilingi bilioni 19,729.5 kutoka shilingi bilioni 19,293.7 mwaka 2015. Kati ya amana hizo, sekta binafsi ilichangia asilimia 97.1 ikilinganishwa na asilimia 95.6 mwaka 2015. Aidha, uwiano wa amana za fedha za kigeni katika amana zote ulipungua na kufikia asilimia 31.6 mwaka 2016 kutoka asilimia 32.8 mwaka 2015. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa kiwango cha ukuaji wa amana za kigeni.

Mwenendo wa Viwango vya Riba

109. Mwaka 2016, viwango vya riba za amana na za mikopo vilipungua ikilinganishwa na viwango hivyo mwaka uliotangulia. Riba za amana za muda maalum kwa ujumla zilipungua kutoka wastani wa asilimia 9.30 hadi wastani wa asilimia 8.78. Aidha, viwango vya riba za amana za mwaka mmoja vilipungua kutoka wastani wa asilimia 11.16 mwaka 2015 hadi wastani wa asilimia 11.03 mwaka 2016. Vile vile, viwango vya riba za mikopo hadi mwaka mmoja vilipungua kutoka wastani wa asilimia 14.22 hadi wastani wa asilimia 12.87 mwaka 2016. Mwenendo huu ulitokana na mikakati ya mabanki kuhamasisha uwekaji wa amana na kuvutia ukopaji kwa riba na masharti nafuu. Kulingana na hali hiyo, tofauti kati ya riba za amana za mwaka mmoja na riba za mikopo za mwaka mmoja ilipungua na kufikia nukta za asilimia 1.83 mwaka 2016 kutoka nukta za asilimia 3.06 mwaka 2016. Riba katika soko la fedha baina ya mabanki iliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 13.49 mwezi Desemba 2016, kutoka wastani wa asilimia 7.29 mwezi Desemba 2015, kutokana na kupungua kwa hali ya ukwasi hususan katika kipindi cha pili cha mwaka 2016. Aidha, riba kwenye soko la dhamana za serikali zilipungua hadi kufikia wastani wa asilimia 15.12 mwezi Desemba 2016 kutoka wastani wa asilimia 18.25 mwezi Desemba 2015.

Maendeleo katika Sekta ya Fedha

110. Mwaka 2016, sekta ya fedha iliendelea kuimarika katika nyanja tofauti ikiwemo ongezeko la idadi ya taasisi na maboresho katika utoaji wa huduma za fedha. Hadi Desemba 2016, idadi ya taasisi za fedha zilizokuwa zinasimamiwa

na Benki Kuu ya Tanzania ilikuwa 67 (benki 59 na taasisi nyingine 8) ikilinganishwa na taasisi 63 (benki 56 na taasisi nyingine 7) mwaka 2015. Taasisi zilizoongezeka zilijumuisha benki 3 ambazo ni: *Mwalimu Commercial Bank Plc*, *Canara Bank (Tanzania) Limited* na *Hakika Microfinance Bank Tanzania*; pamoja na taasisi nyingine moja ambayo ni *Bank of China – Representative Office*. Katika kurahisisha upatikanaji wa huduma, benki ziliendelea kuongeza idadi ya matawi kutoka 728 Desemba 2015 hadi 795 Desemba 2016. Hata hivyo, sekta hii ilikabiliwa na hali ya upungufu wa ukwasi japokuwa viashiria vingi bado vilikuwa juu ya ukomo unaokubalika kisheria. Miongoni mwa viashiria hivyo ni uwiano kati ya mali inayoweza kubadilishwa kuwa fedha taslim na amana zinazoweza kuhitajika kwa muda mfupi (Liquid assets to Demand Liabilities) ambao ulipungua kufikia asilimia 35.1 mwezi Desemba 2016 kutoka asilimia 37.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2015 ukilinganisha na uwiano wa chini unaohitajika kisheria wa asilimia 20. Aidha, katika kipindi hicho hicho uwiano wa mtaji wa msingi na rasilimali za benki uliongezeka kufikia asilimia 17.8 kutoka asilimia 16.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 10.

111. Mwaka 2016, utekelezaji wa Mpango wa Huduma za Fedha Jumuishi nchini uliendelea kuwa na mafanikio makubwa ambapo huduma hizo ziliendelea kupatikana kwa wingi mijini na vijijini, zikichangiwa kwa sehemu kubwa na matumizi ya simu za mikononi pamoja na Wakala wa Benki. Hadi Desemba 2016, idadi ya benki zilizoruhusiwa kutoa huduma za benki kwa njia ya uwakala ilikuwa 18 ikilinganishwa na benki 10 Desemba 2015, sawa na ongezeko la asilimia 80.0. Aidha, idadi ya mawakala iliongezeka kwa asilimia 72.1 kutoka mawakala 3,298 Desemba 2015 hadi mawakala 5,676 Desemba 2016.

112. Miamala ya kuweka amana kupitia huduma za benki kwa njia ya uwakala ilikuwa 4,869,842 Desemba 2016 ikilinganishwa na miamala 1,758,098 Desemba 2015, sawa na ongezeko la asilimia 177.0. Fedha taslimu zilizowekwa kwa kipindi kilichoishia Desemba 2016 zilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 1,883.29 ikilinganishwa na shilingi bilioni 874.25 Desemba 2015. Vile vile, idadi ya miamala ya kutoa fedha ilikuwa 1,657,092 Desemba 2016 ikilinganishwa na miamala 675,651 Desemba 2015. Fedha taslimu zilizotolewa kwa kipindi kilichoishia Desemba 2016 zilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 427.13 ikilinganishwa na shilingi bilioni 185.23 mwaka 2015.

113. Kwa upande wa malipo kupitia simu za viganjani, thamani ya miamala iliyofanywa na Kampuni ya Vodacom Tanzania kupitia huduma ya M-Pesa ilikuwa ni asilimia 58.1 ya miamala yote ikifuatiwa na Tigo-Pesa (asilimia 31.15), Airtel Money (asilimia 10.4), Ezy-Pesa (asilimia 0.29) na Halopesa (asilimia 0.1). Katika kipindi hicho, idadi ya mawakala waliosajiliwa iliongezeka na kufikia 371,132 ikilinganishwa na mawakala 267,047 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 39.0. Kati ya hao, mawakala waliosajiliwa na Kampuni ya Vodacom walikuwa 157,731 ambao ni sawa na asilimia 42.5 ya mawakala wote; Airtel ilikuwa na mawakala 72,593 (asilimia 19.6); Tigo ilikuwa na mawakala 65,913 (asilimia 17.8); Halotel ilikuwa na mawakala 56,932 (asilimia 15.3); na Zantel ilikuwa na mawakala 17,963 (asilimia 4.8). Fedha taslimu zilizowekwa kwenye akaunti ya dhamana ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 561.2 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 665.7 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 18.6.

Maendeleo ya Masoko la Mitaji na Dhamana

114. Mwaka 2016, idadi ya kampuni zilizo rodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam iliongezeka kutoka 22 mwaka 2015 hadi 25, sawa na ongezeko la asilimia 13.6. Kati ya hizo, kampuni za ndani zilikuwa 18 na kampuni za nje (kutoka masoko ya hisa ya Nairobi na London) zilikuwa saba. Ongezeko hili lilitokana na kuorodheshwa kwa kampuni tatu ambazo ni: *YETU Microfinance Bank*, Benki ya Wananchi Mufindi (MUCOBA) na Kampuni ya Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE Plc). Aidha, hadi Desemba 2016, kampuni zilizo rodheshwa kwenye soko la kukuza ujasiriamali zilikuwa tano ikilinganishwa na kampuni nne katika kipindi kilichoishia Desemba 2015. Katika kipindi hicho, idadi ya wawekezaji kwenye soko la hisa iliongezeka kutoka 435,000 mwaka 2015 hadi wawekezaji 454,214, sawa na ongezeko la asilimia 4.4. Ongezeko la idadi ya wawekezaji kwa kiasi kikubwa lilichangiwa na matumizi ya simu za mikononi katika uwekezaji.

115. Kwa upande wa uuzaji na ununuzi wa dhamana, katika kipindi cha mwaka 2016, hisa 194,479,350 zenye thamani ya shilingi milioni 420 ziliuzwa na kununuliwa katika soko la hisa la Dar es Salaam, ikilinganishwa na hisa 268,115,487 kwa mwaka 2015 zilizokuwa na thamani ya shilingi trilioni 1.07. Aidha, hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 429 zilinunuliwa na kuuzwa

katika soko la pili (*secondary market*) kwa mwaka 2016 ikilinganishwa na hatifungani za shilingi bilioni 327 mwaka 2015. Vile vile, katika kipindi husika, Soko limeweza kuorodhesha hatifungani za serikali 25 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.53 na hatifungani za kampuni moja yenye thamani ya shilingi bilioni 41, ikilinganishwa na hatifungani za serikali 24 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.05 na hatifungani za kampuni mbili, zenye thamani ya shilingi bilioni 47.6 ziliorodheshwa mwaka 2015.

116. Kufuatia idhini ya kuuzwa kwa hatifungani kwa wawekezaji wadogo wadogo katika masoko ya mitaji ya Afrika ya Mashariki, Benki ya Exim ilipata mafanikio makubwa kwa kuvuka lengo la kukusanya shilingi bilioni 10 kwa kupata shilingi bilioni 19.97 kutoka kwa wawekezaji 512. Vile vile, benki ya NMB ilikusanya shilingi bilioni 41.40 kwa kuvuka lengo la kukusanya shilingi bilioni 8.68 kutoka kwa wawekezaji 4,570. Hii inaonesha uhitaji uliokuwepo kwa wawekezaji wadogo wadogo katika fursa zinazopatikana katika uwekezaji kwenye hatifungani.

117. Mwaka 2016, thamani ya skimu za uwekezaji wa pamoja ilipungua na kufikia shilingi bilioni 238,188.63 kutoka shilingi bilioni 246,579.36 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 3.4. Upungufu huu ulichangiwa na kushuka kwa uwekezaji kwenye Mfuko wa Umoja na Mfuko wa Jikimu ambayo inachukua sehemu kwenye skimu ya uwekezaji wa pamoja (asilimia 84.3 na asilimia 9.8 kwa mtiririko huo).

Jedwali Na. 5.1: Mwenendo wa Skimu za Uwekezaji wa Pamoja (TZS Bilioni)

Aina ya Uwekezaji	2015	2016	Ukuaji (%)
Mfuko wa Umoja	213,313.31	200,894.17	(5.8)
Mfuko wa Jikimu	26,296.00	23,379.00	(11.1)
Mfuko wa Wekeza Maisha	3,455.38	3,460.11	0.1
Mfuko wa Watoto	2,805.19	3,115.52	11.1
Mfuko wa Ukwasi	709.48	7,339.83	934.5
Jumla	246,579.36	238,188.63	(3.4)

Chanzo: Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana

Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA)

118. Mwaka 2015/16, wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii waliongezeka kwa asilimia 4.3 na kufikia 2,234,246 kutoka wanachama 2,142,350 mwaka 2014/15. Ongezeko hilo ni dogo ikilinganishwa na ukuaji wa mwaka 2014/15 ambao ulikuwa asilimia 9.8. Kwa upande mwingine, michango kutoka kwa wanachama ilipungua kutoka shilingi trilioni 2.27 mwaka 2014/15 hadi shilingi trilioni 2.15 mwaka 2015/16, sawa na upungufu wa asilimia 5.5.

119. Mwaka 2015/16, jumla ya mafao yaliyolipwa kwa wanachama yaliongezeka hadi shilingi trilioni 2.93 kutoka shilingi trilioni 1.53 mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 90.1. Ongezeko hili lilitokana na malipo ya malimbikizo ya mafao yaliyofanywa na PSPF. Katika kipindi hicho, uwekezaji uliofanywa na Skimu za Hifadhi za Jamii uliongezeka kwa asilimia 19.0 kutoka shilingi trilioni 7.8 mwaka 2014/15 hadi shilingi trilioni 9.3 mwaka 2015/16. Aidha, thamani ya vitega uchumi katika Sekta ya Hifadhi ya Jamii ilikuwa shilingi trilioni 10.28.

Jedwali Na.5.2 : Taarifa ya Hali ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Mwaka	Idadi ya Wanachama	Michango Sh.bilioni	Mafao Sh.bilioni	Uwekezaji Sh.bilioni
2007/08	1,198,298	508	272	1,789
2008/09	1,275,993	750	308	2,432
2009/10	1,432,950	842	455	3,147
2010/11	1,599,208	1,178	575	3,757
2011/12	1,676,715	1,376	733	4,827
2012/13	1,856,245	1,631	1,068	5,649
2013/14	1,951,751	1,976	1,411	6,667
2014/15	2,142,350	2,273	1,543	7,807
2015/16	2,234,246	2,148	2,934	9,289

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii

Mfuko wa Mafao ya Kustaafu (GEPP)

120. Mwaka 2015/16, Mfuko ulikuwa na wanachama 114,005 ikilinganishwa na wanachama 91,157 Juni 2015, sawa na ongezeko la wanachama wapya 22,848. Idadi hii ilijumuisha wanachama 8,419 waliosajiliwa kupitia mfumo wa pensheni wa lazima na wanachama 14,429 walisajiliwa kupitia mpango wa hiari.

Michango iliyokusanywa kutoka kwa wanachama ilifikia shilingi milioni 69,430.13 mwaka 2015/16 ikilinganishwa na shilingi milioni 53,930.17 zilizokusanywa mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 28.74.

121. Mwaka 2015/16 Mfuko ulilipa pensheni kwa wastaafu jumla ya shilingi milioni 18,858.02 ikilinganishwa na shilingi milioni 12,226.08 mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 35.0. Sababu za kuongezeka kwa malipo hayo ni pamoja na: kuachishwa kazi kwa baadhi ya wafanyakazi katika taasisi za Serikali na kumalizika kwa miradi iliyokuwa ikifadhiliwa na washirika wa maendeleo; ulipaji wa mafao ya wanachama kutoka Polisi na Magereza waliopaswa kuhamishwa kipindi cha nyuma kwenda kwenye Mfuko wa PSPF; na kujitoa kwa baadhi ya wanachama wanaochangia kwenye Mpango wa Kujiwekea kwa Hiari na hasa wanachama waliokuwa wakichangia moja kwa moja kwa kukatwa kwenye mishahara.

122. Mwaka 2015/16, Mfuko uliendelea kuwekeza katika vitega uchumi mbalimbali ambavyo ni rasilimali zenye uhakika wa faida, hisa za kampuni, majengo na mfuko wa uwekezaji wa pamoja. Rasilimali zenye uhakika wa faida zinajumuisha amana za benki, dhamana za serikali, dhamana za kampuni na mikopo. Hadi Juni 2016, Mfuko ulikuwa umewekeza jumla ya shilingi milioni 403,322.50 ikilinganishwa na shilingi milioni 324,823.11 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 24.2. Aidha, Mfuko uliwekeza jumla ya shilingi milioni 34,909.60 kwenye hisa za kampuni zilizo rodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam ikilinganishwa na shilingi milioni 28,965.36 Juni 2015, sawa na ongezeko la asilimia 20.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya hisa za kampuni katika soko la mitaji. Vile vile, uwekezaji katika majengo na viwanja uliongezeka na kufikia jumla ya shilingi milioni 28,269.04 Juni 2016 ikilinganishwa na shilingi milioni 25,786.24 Juni 2015 sawa na ongezeko la asilimia 9.6.

123. Mwaka 2015/16, makusanyo ya mapato yanayotokana na uwekezaji yalipungua na kufikia shilingi milioni 36,441.94 kutoka shilingi milioni 44,079.97 mwaka 2014/15, sawa na upungufu wa asilimia 20.94. Kupungua kwa makusanyo hayo kulitokana na kushuka kwa bei ya hisa kwenye soko la mitaji. Hadi kufikia Juni 2016, Mfuko ulikuwa na thamani ya shilingi milioni

427,795.25 ikilinganishwa na shilingi milioni 342,110.28 Juni 2015, sawa na ongezeko la asilimia 25.0.

Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF)

124. Mwaka Mwaka 2015/16, wanachama wapya waliosajiliwa na Mfuko wa Pensheni wa LAPF walikuwa 16,001. Usajili huu ulifanya idadi ya wanachama wa Mfuko kuongezeka kwa asilimia 10.6 kutoka wanachama 150,835 mwaka 2014/15 hadi wanachama 166,836. Aidha, Mfuko ulikusanya michango kutoka kwa wanachama yenye thamani ya shilingi bilioni 279.68 mwaka 2015/16 ikilinganishwa na shilingi bilioni 210.07 mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 33.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa usajili wa wanachama wapya na mabadiliko ya mishahara. Vile vile, mafao yaliyolipwa kwa wanachama mwaka 2015/16 yaliongezeka kwa asilimia 21.0 kutoka shilingi bilioni 88.60 mwaka 2014/15 hadi shilingi bilioni 107.25.

125. Thamani ya uwekezaji katika vitega-uchumi iliongezeka kutoka shilingi bilioni 883.62 mwaka 2014/15 hadi shilingi bilioni 1,098.37 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 24.30. Thamani ya uwekezaji katika dhamana za serikali iliongezeka kutoka shilingi bilioni 304.82 mwaka 2014/15 hadi shilingi bilioni 474.83 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 55.8.

126. Katika kipindi husika, mapato kutokana na uwekezaji katika vitega-uchumi yaliongezeka kwa asilimia 30.3 kutoka shilingi bilioni 72.07 mwaka 2014/15 hadi shilingi bilioni 93.88. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa shughuli za uwekezaji katika amana za muda maalumu, dhamana za serikali na kampuni, mitaji mbalimbali ikiwemo mali zisizohamishika na mikopo ya muda mrefu. Aidha, thamani halisi ya mali za Mfuko ilikua na kufikia shilingi bilioni 1,169.06 mwaka 2015/16, ikilinganishwa na shilingi 939.35 bilioni mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 24.5.

Mfuko wa Pensheni wa PSPF

127. Mwaka 2016, Mfuko wa Pensheni wa PSPF ulisajili wanachama 47,238 ikijumuisha wanachama 8,116 katika mfumo wa pensheni wa lazima na wanachama 39,122 katika mpango wa hiari ukilinganisha na wanachama 40,525 waliosajiliwa kwa mwaka 2015, ambapo wanachama 26,447 waliokuwa katika mfumo wa pensioni wa lazima na wanachama 14,078 katika mpango wa hiari. Kuongezeka kwa usajili wa wanachamakulitokana na kuongezeka kwa ari ya

wananchi kujiunga na mpango wa uchangiaji wa hiari ambapo waliongezeka kwa asilimia 177 ukilinganisha na mwaka 2015. Usajili huu wa mwaka 2016, ulifanya jumla ya idadi ya wanachama wa Mfuko kuongezeka na kufikia 404,972 ikilinganishwa na wanachama 366,865 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 10.4.

128. Michango kutoka kwa wanachama iliongezeka hadi shilingi bilioni 784.76 mwaka 2016 kutoka shilingi bilioni 661.8 mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 18.6. Ongezeko hili lilitokana na usajili wa wanachama kutoka kwenye mfumo wa pensheni wa lazima. Aidha, katika kipindi hicho, mafao yaliyolipwa kwa wanachama 7,416 yaliongezeka kwa asilimia 39.5 na kufikia shilingi bilioni 786.36 ikilinganishwa na shilingi bilioni 563.82 zilizolipwa kwa wanachama 7,937 mwaka 2015. Mchanganuo wa malipo ya mafao haya ni kama yanavyoonekana katika **Jedwali Na.5.3**

Jedwali Na.5.3: Malipo ya Mafao kwa Wanachama wa Mfuko (Shs. Biln)

Aina ya Mafao	2015	2016	Ongezeko (%)
Malipo ya Kustaafu kwa Umri (Kiinua Mgongo)	354.6	497.0	40.2
Mafao ya Kifo/Mirathi	57.92	70.33	21.4
Msaada wa Mazishi	0.42	0.52	23.8
Mafao ya Kujitoa	1.61	2.62	62.7
Pensheni kwa Wastaafu	119.25	161.6	35.5
Pensheni ya Wategemezi	29.99	54.29	81.0
Jumla	563.8	786.4	39.5

Chanzo: Mfuko wa Pensheni wa PSPF

129. Mwaka 2016, mapato ya uwekezaji wa Mfuko yalishuka kwa asilimia 57.6 kufikia shilingi bilioni 75.59 kutoka shilingi bilioni 178.2 mwaka 2015. Vile vile, mapato mengineyo yalipungua hadi shilingi bilioni 2.8 mwaka 2016 kutoka shilingi bilioni 5.1 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 45.1. Kushuka kwa mapato kulitokana na kupungua kwa fedha kwa ajili ya uwekezaji na kuongezeka kwa malipo ya mafao zaidi kuliko michango.

130. Hadi kufikia Desemba 2016, thamani ya rasilimali za uwekezaji wa Mfuko ilipungua hadi shilingi trilioni 1.38 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.46 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 5.5. Hali hii ilitokana na kutokuwepo kwa uwiano kati ya mafao yanayolipwa na michango inayopokelewa ambapo Mfuko unalipa mafao mengi ukilinganisha na michango inayopokelewa. Aidha, katika kipindi hicho, tafiti zilionesha kuwa asilimia 65 ya wanachama waliridhishwa na huduma zinazotolewa na Mfuko ikilinganishwa na asilimia 78 iliyoripotiwa mwaka 2015 kutokana na ucheleweshwaji katika ulipaji wa mafao kwa wanachama.

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)

131. Mwaka 2015/16, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ulikuwa na jumla ya wanachama 1,003,563 ikilinganishwa na wanachama 941,482 mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 6.6. Aidha, Mfuko ulikusanya michango kutoka kwa wanachama yenye thamani ya shilingi milioni 631,031.54 mwaka 2015/16 ikilinganishwa na shilingi milioni 605,090.41 mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 4.3. Ongezeko hili lilitokana na usajili wa wanachama wapya 138,917 na waajiri wapya 3,575 ambao waliwasilisha michango kwa wakati.

132. Mwaka 2015/16, mafao yaliyolipwa kwa wanachama yalikuwa shilingi milioni 378,282.58 ikilinganishwa na shilingi milioni 357,673.79 zilizolipwa mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 5.8. Wanachama waliolipwa mafao hayo walikuwa 94,103 ikilinganishwa na wanachama 89,693 waliolipwa mwaka 2014/15, sawa na upungufu wa asilimia 4.9. Aidha, jumla ya semina 4,412 ziliendeshwa nchi nzima kwa lengo la kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa hifadhi ya jamii, ikilinganishwa na semina 4,078 zilizoendeshwa mwaka 2014/15.

133. Katika kipindi hicho, thamani ya uwekezaji katika vitega-uchumi iliongezeka hadi shilingi milioni 2,817,676.37 kutoka shilingi milioni 2,726,013.46 mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 3.4. Kwa upande mwingine, thamani ya uwekezaji katika dhamana za serikali ilipungua na kufikia shilingi milioni 254,932.88 mwaka 2015/16, kutoka shilingi milioni 315,927.85 mwaka 2014/15, sawa na upungufu wa asilimia 19.3. Mapato kutokana na uwekezaji katika vitega-uchumi yaliongezeka hadi shilingi milioni 215,999.90

mwaka 2015/16 kutoka shilingi milioni 209,687.40 mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 3.0.

134. Mwaka 2015/16, thamani ya Mfuko iliongezeka kwa asilimia 1.6 kutoka shilingi milioni 3,130,993.65 mwaka 2014/15 hadi shilingi milioni 3,181,266.61. Aidha, rasilimali halisi za Mfuko zilikuwa na thamani ya shilingi milioni 3,008,439.12 mwaka 2015/16 ikilinganishwa na shilingi milioni 2,933,972.03 mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 2.54. Hivyo, ongezeko halisi la rasilimali baada ya kodi kwa mwaka 2015/16 lilikuwa shilingi milioni 74,467.10 ikilinganishwa na shilingi milioni 351,051.27 mwaka 2014/215, sawa na upungufu wa asilimia 78.8. Upungufu huu ulisababishwa na kuongezeka kwa madeni yenye mashaka/yaliyochelewa kulipwa yenye thamani ya shilingi milioni 192,993.27 mwaka 2015/16 kutoka shilingi milioni 39,625.88 mwaka 2014/15; kupungua kwa thamani ya hisa za kampuni zilizosajiliwa katika Soko la Mitaji la Dar es Salaam kutoka shilingi milioni 17,668.88 mwaka 2014/15 hadi shilingi milioni 11,420.64 mwaka 2015/16; na kukosekana kwa faida kutokana na kutokuwepo kwa mauzo ya hisa kwa mwaka 2015/16 ikilinganishwa na faida ya shilingi milioni 18,781.29 iliyopatikana kwa mauzo ya hisa mwaka 2014/15.

Mfuko wa Pensheni wa PPF

135. Idadi Idadi ya wanachama wapya walioandikishwa katika Mfuko wa Pensheni wa PPF mwaka 2015/16 walikuwa 70,942 ikilinganishwa na wanachama 99,043 walioandikishwa mwaka 2014/15. Hii ilifanya idadi ya wanachama kufikia 222,543 ikilinganishwa na wanachama 242,530 mwaka 2014/15, sawa na upungufu wa asilimia 8.2. Upungufu huu ulitokana na kuwepo wa wanachama walioondoka katika ajira na kulipwa mafao yao pamoja na wanachama ambao wameondolewa katika orodha wakati wa zoezi linaloendelea la kuboresha kumbukumbu za wanachama.

136. Mwaka 2015/16, Mfuko ulikusanya michango ya wanachama yenye thamani ya shilingi bilioni 378.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 503.6 zilizokusanywa mwaka 2014/15, sawa na upungufu wa asilimia 24.9. Hii ilitokana na kupungua kwa idadi ya wanachama walioandikishwa katika kipindi hicho. Aidha, mafao yaliyolipwa na Mfuko kwa wanachama wanaostahili yalikuwa shilingi bilioni 214.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 267.8

zilizolipwa mwaka 2014/15, sawa na upungufu wa asilimia 19.9. Hadi kufikia Juni 2016, idadi ya wastaafu waliomo katika daftari la wastaafu la Mfuko wa Pensheni wa PPF ilikuwa 31,133 ambao walilipwa pensheni yao ya mwaka iliyokuwa na thamani ya shilingi bilioni 66.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 78.5 zilizolipwa kwa wastaafu 28,363 mwaka 2014/15. Vile vile, mwaka 2015/16 Mfuko ulilipa mafao ya elimu (ada na gharama nyingine za masomo) kwa watoto wa wanachama waliofariki wakiwa kazini yenye thamani ya shilingi bilioni 1.1 kwa watoto 1,112 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1.9 kwa watoto 1,259 zilizolipwa mwaka 2014/15 sawa na upungufu wa asilimia 42.1 na asilimia 11.7 kwa mtiririko huo. Aidha, Mfuko pia katika kipindi kusika ulilipa mafao ya uzazi yenye thamani ya shilingi milioni 827.

137. Mwaka 2015/16, jumla ya shilingi trilioni 2.0 ziliwekezwa katika vitegachumi mbalimbali vya Mfuko ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.9 zilizowekezwa mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 5.3. Mapato yatoanayo na uwekezaji mwaka 2015/16 yalikuwa shilingi bilioni 154.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 506.7 mwaka 2014/15, sawa na upungufu wa asilimia 69.5. Hii ilitokana na kushuka kwa bei za hisa za kampuni ambazo Mfuko umewekeza. Thamani ya Mfuko iliongezeka na kufikia shilingi trilioni 2.3 mwaka 2015/16, kutoka shilingi trilioni 2.08 mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 10.5.

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)

138. Mwaka Mwaka 2016, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi uliendelea na taratibu za usajili wa waajiri wote waliopo katika sekta ya umma na binafsi Tanzania Bara. Hadi Desemba 2016, waajiri waliopewa namba za usajili na ambao wanachangia kwenye Mfuko walifikia 6,448 ikilinganishwa na waajiri 1,525 kwa kupindi kilichoishia Desemba 2015. Viwango vya uchangiaji vya Mfuko ni asilimia 0.5 ya mapato ya mfanyakazi kwa waajiri wa sekta ya umma na asilimia 1.0 kwa waajiri wa sekta binafsi. Hadi kufikia Desemba 2016, Mfuko ulikusanya kiasi cha shilingi bilioni 37.41 ambayo ilijumuisha shilingi bilioni 26.31 kutoka kwa waajiri wa sekta binafsi na mashirika ya umma na kiasi cha shilingi bilioni 11.10 kutoka serikalini. Makusanyo haya ni sawa na asilimia 87.82 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 42.6.

139. Mwaka 2016, Mfuko uliwekeza katika vitega-uchumi mbalimbali ikiwa ni pamoja na: hatifungani za serikali, amana za benki na hisa za makampuni. Katika kipindi hicho, Mfuko uliwekeza kiasi cha shilingi bilioni 41.55 ikiwa ni chini ya lengo la kuwekeza shilingi bilioni 47.68 kwa kipindi kilichoishia Desemba 2016. Mchanganuo wa uwekezaji wa Mfuko kuanzia Julai – Desemba 2016 ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na.5.4**

Jedwali Na.5.4: Uwekezaji wa Mfuko hadi kufikia Desemba 2016 (TZS Biln)

Maeneo ya Uwekezaji	Makadirio ya Uwekezaji	Uwekezaji Halisi	Utekelezaji wa Makadirio (%)
Hatifungani za Serikali (muda mrefu)	31.0	25.94	83.7
Hatifungani za Serikali (muda mfupi)	4.0	8.93	223.3
Amana za mabenki	6.0	0	0.0
Uwekezaji unaoiva	6.68	6.68	100.0
Jumla	47.7	41.55	87.1

Chanzo: Mfuko wa Fidia ya Wafanyakazi Tanzania

140. Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ulianza kupokea rasmi madai ya fidia tarehe 1 Julai 2016. Hadi Desemba 2016, Mfuko ulipokea madai ya malipo ya fidia 37, ambapo Mfuko ulilipa madai 13 yenye jumla ya thamani ya shilingi milioni 2.43. Madai matano yalikuwa kwenye hatua za malipo, madai matatu yalifungwa kwa kutokuwa na vigezo vya kulipwa na madai 16 yalikuwa hayajakamilika kwa sababu ya kukosa viambatisho. Madai yote yaliyokuwa na kasoro yamerudishwa kwa waajiri ili kukamilisha vielelezo.

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

141. Mwaka 2015/16, idadi ya wanachama wachangiaji kwenye Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya iliongezeka na kufikia 702,598 kutoka wanachama 640,341 mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 9.7. Ongezeko hilo kwa kiasi kikubwa lilichangiwa na uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya juu. Vile vile, katika kipindi hicho, Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) uliandikisha jumla ya kaya 1,452,855 kwa wanachama ikilinganishwa na kaya 1,112,874 zilizoandikishwa mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 30.5.

142. Hadi kufikia Juni 2016, Mfuko ulikuwa unahudumia jumla ya wanufaika 12,094,153 ambao ni sawa na asilimia 24.1 ya idadi ya watu wote Tanzania ikilinganishwa na asilimia 20.9 mwaka 2014/15. Kati ya hao, idadi ya wanufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ilikuwa 3,377,023 (sawa na asilimia 6.7 ya watanzania) na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ulikuwa na jumla ya wanufaika 8,717,130 (sawa na asilimia 17.4 ya watanzania).

143. Mwaka 2015/16, Mfuko ulilipa kiasi cha shilingi milioni 220,088.33 kwa watoa huduma, sawa na asilimia 96.0 ya madai ya shilingi milioni 229,258.67 yaliyowasilishwa. Tofauti ya madai yaliyowasilishwa na yaliyolipwa ilitokana na baadhi ya watoa huduma kutozingatia miongozo ya matibabu ya Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, mpangilio wa bei za Mfuko (NHIF), uandaaji usiofaa wa madai na kughushi madai.

144. Mapato ya Mfuko yaliongezeka kwa asilimia 22.5 kufikia shilingi milioni 453,997.10 mwaka 2015/16 kutoka shilingi milioni 370,476.06 mwaka 2014/15. Kati ya mapato hayo, michango ya wanachama iliongezeka kutoka shilingi milioni 286,702.26 mwaka 2014/15 hadi shilingi milioni 352,762.80 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 23.0. Aidha, michango ya wanachama ilichangia asilimia 77.7 ya mapato yote ya Mfuko ikifuatiwa na mapato yatokanayo na vitega-uchumi asilimia 21.9, na mapato mengineyo asilimia 0.4. Mwaka 2015/16, rasilimali halisi za Mfuko zilifikia shilingi 1,188,197,873,000 ikilinganishwa na shilingi 1,020,877,380,000 mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 16.4.

145. Mwaka 2015/16, vituo vya afya vilivyosajiliwa na Mfuko vilifikia 6,439 ikilinganishwa na vituo 6,185 vilivyosajiliwa mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 4.1. Kati ya hivyo, vituo 5,091 (asilimia 79) vinamilikiwa na Serikali na vituo 776 (asilimia 12) vinamilikiwa na sekta binafsi wakati vituo 572 (asilimia 10) vinamilikiwa na Madhehebu ya Dini. Mchanganuo wa vituo hivyo ni kama inavyoonekana kwenye **jedwali Na.5.5**.

Jedwali Na.5.5: Jumla ya Vituo vya Afya Vilivyosajiliwa na Mfuko hadi kufikia 2015/16

Aina ya Vituo	2014/15				2015/16				Ukuaji (%)
	Serikali	Mashirika ya Dini	Binafsi	Jumla	Serikali	Mashirika ya Dini	Binafsi	Jumla	
Hospitali	126	106	22	254	131	106	25	262	3.1
Vituo vya Afya	461	132	21	614	449	142	37	628	2.3
Zahanati	4,332	349	63	4,744	4,509	319	103	4,931	3.9
Maduka ya dawa	0	5	558	563	2	5	586	593	5.3
Kliniki maalum	0		8	8	-	-	21	21	162.5
Vituo vya uchunguzi wa Magonjwa	0	0	2	2	-	-	4	4	100
Jumla	4,919	592	674	6,185	5,091	572	776	6,439	4

Chanzo: Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania (TIRA)

146. Mwaka 2016, idadi ya kampuni zilizosajiliwa kufanya biashara ya bima zilikuwa 31 ikilinganishwa na kampuni 30 mwaka 2015. Kampuni hizo zinajumuisha kampuni 25 zilizosajiliwa kufanya biashara ya bima za kawaida pekee; kampuni nne (4) bima za maisha pekee; kampuni moja (1) bima za kawaida na za maisha; na kampuni moja (1) bima mtawanyo.

147. Mauzo ya soko la Bima katika mwaka 2016 yalikuwa kwa asilimia 8.4 kufikia shilingi bilioni 670.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 618.9 mwaka 2015. Bima za kawaida zilichangia asilimia 89.0 kwa mwaka 2016, wakati bima za maisha zilichangia asilimia 11.0 ya mauzo hayo. Mauzo ya bima za kawaida yalikuwa kwa asilimia 8.5 kufikia shilingi bilioni 596.9, ikilinganishwa na shilingi bilioni 550.2 mwaka 2015. Wakati huo huo, mauzo ya bima za maisha yalikuwa kwa asilimia 7.8 kufikia shilingi bilioni 74.1, ikilinganishwa na shilingi bilioni 68.7 mwaka 2015. Idadi ya hati za bima zilizotolewa na makampuni ya bima ziliongezeka kwa asilimia 34.1 kufikia 2,316,867 mwaka 2016 ikilinganishwa na hati 1,727,342 mwaka 2015.

Jedwali Na.5.6: Mauzo ya Bima kwa Mwaka 2014 – 2016 (Shs. Milioni)

Mauzo	2014	2015	2016
Bima za Kawaida	493,981	550,168	596,859
Ukuaji (%)	18.27	11.37	8.50
Mchango kwa Jumla (%)	89.10	88.90	89.00
Bima za Maisha	60,420	68,691	74,074
Ukuaji (%)	7.10	13.70	7.80
Mchango kwa Jumla (%)	10.90	11.10	11.00
Jumla ya Mauzo	554,401	618,859	670,932
Ukuaji (%)	16.90	11.60	8.40

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania

148. Kwa upande wa mapato, kampuni za bima za kawaida zilipata faida ya shilingi bilioni 27.9 hadi kufikia Desemba mwaka 2016, ikiwa ni pungufu kwa asilimia 16.4 ikilinganishwa na faida ya shilingi bilioni 33.3 iliyopatikana mwaka 2015. Upungufu huu wa faida umetokana na kupungua kwa mapato yatokanayo na uwekezaji.

149. Thamani ya mali za kampuni za bima iliongezeka kufikia shilingi bilioni 788.7 mwaka 2016 kutoka shilingi bilioni 729.3 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 8.1. Madeni ya kampuni za bima yalifikia shilingi bilioni 506.7 mwaka 2016 ikilinganishwa na shilingi bilioni 483.9 mwaka 2015. Hivyo, tofauti kati ya mali na madeni ya kampuni hizo ilikuwa shilingi bilioni 282.0 mwaka 2016 ikilinganishwa na shilingi bilioni 245.5 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 14.9.

Jedwali Na.5.7: Thamani ya Mali na Madeni ya Kampuni za Bima (Shs. Miln)

Mali Na Madeni	2013	2014	2015	2016
Jumla ya Mali	518,984	619,979	729,326	788,746
Ukuaji (%)	15.20	19.50	17.60	8.10
Jumla ya Madeni	343,718	401,665	483,869	506,718
Ukuaji (%)	8.20	16.90	20.50	4.70
Ziada ya Mali	175,266	218,314	245,457	282,028
Ukuaji (%)	32.10	24.60	12.40	14.90

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania.

Mwenendo wa Soko la Mikopo ya Nyumba Tanzania

150. Mwaka 2016, jumla ya mikopo ya nyumba za kuishi iliyotolewa ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 416.94 ikilinganishwa na shilingi bilioni 359.4 zilizotolewa mwaka 2015, sawa na ukuaji wa asilimia 16.0. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa ushindani uliosababishwa na kuingia kwa taasisi mpya na kuongezeka kwa ufahamu juu ya mikopo ya nyumba miongoni mwa wakopaji. Taasisi mpya zilizoingia sokoni ni *Diamond Trust Bank* na *Standard Chartered Bank* na hivyo kufanya idadi ya taasisi hizo kufika 28 ikilinganishwa na taasisi 26 mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 7.7. **Jedwali Na.5.8** linaonesha taasisi za fedha zilizo kwenye soko na umiliki wao kwenye soko la mikopo ya nyumba.

Jedwali Na.5.8: Taarifa ya Soko la Nyumba nchini hadi Desemba 2016

Mkopeshaji	Idadi ya Wateja	Kiasi cha Mikopo (Bilioni)	Miliki ya Soko (%)
Equity Bank Tanzania Limited	73	97.75	23.4
Stanbic Bank (T) Ltd	159	58.3	14
Bank M Tanzania Public Limited Company	28	54.53	13.1
Azania Bank Limited	629	40.4	9.7
CRDB Bank Plc	285	34.82	8.4
Commercial Bank of Africa (T) Limited	175	25.84	6.2
KCB Bank Tanzania Limited	62	10.31	2.5
First National Bank Tanzania Limited	99	9.8	2.4
NIC Bank Tanzania Limited	18	9.61	2.3
Bank of Africa Tanzania Limited	85	9.47	2.3
DCB Commercial Bank Plc	844	8.56	2.1
I & M Bank Tanzania Limited	41	8.54	2
Barclays Bank (T) Limited	62	7.76	1.9
National Microfinance Bank (T) Plc.	36	5.16	1.2
African Banking Corporation (T) Ltd	32	5.14	1.2
Exim Bank Tanzania Limited	29	4.11	1
Standard Chartered Bank (T) Ltd	17	3.97	1
Akiba Commercial Bank Ltd	547	3.93	0.9
EFC Tanzania M.F.B Limited	209	3.59	0.9
Diamond Trust Bank (T) Ltd.	4	2.58	0.6
NBC Limited	25	2.51	0.6
TIB Corporate Bank Limited	15	2.26	0.5
Citibank Tanzania Limited	14	2.24	0.5
International Commercial Bank (T) Ltd.	4	2.04	0.5
China Commercial Bank Limited	1	1.57	0.4
TIB Development Bank Limited	9	1.02	0.2
Peoples Bank of Zanzibar	13	0.63	0.2
Amana Bank Limited	4	0.5	0.1
Jumla	3,519	416.94	100


Chanzo: Soko la Mikopo ya Nyumba Tanzania

151. Mwaka 2016, Serikali iliongeza jitihada na kuhakikisha riba inayotozwa na wakopeshaji wa mikopo ya nyumba za makazi inapungua. Jitihada hizo zilishusha kiwango cha riba kufikia wastani wa asilimia 16 hadi 19 ikilinganishwa na asilimia 19 hadi 21 mwaka 2015. Aidha, kipindi cha ulipaji wa mikopo kiliongezeka kutoka miaka 7 mwaka 2010 hadi miaka 20 mwaka 2016. Vile vile, wastani wa mikopo ya nyumba ilikuwa shilingi milioni 118 mwaka 2016 ikilinganishwa na shilingi milioni 106 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 11.3. Wastani huu unatofautiana miongoni mwa benki kutokana na mikakati na aina ya wateja waliolengwa.

152. Mpango wa Mradi wa Fedha za Nyumba unaotekelezwa na Kampuni ya Mikopo ya Nyumba Tanzania (*Tanzania Mortgage Refinance Company Limited –TMRC*) ulianzisha Mfuko wa Mikopo Midogo ya Nyumba kwa lengo la kutoa mikopo ya muda mrefu kwa wafanyakazi wa kipato cha chini kwa ajili ya kukarabati na kujenga nyumba mpya. Mfuko huu ulianza rasmi shughuli zake Julai 2015 kwa kutoa mkopo wa shilingi bilioni moja kwa *DCB Commercial Bank Plc*. Hadi Desemba 2016, mikopo ya jumla ya shilingi bilioni sita ilitolewa kwa *EFC*, shilingi bilioni nne kwa *Tanzania Microfinance Bank Ltd* na shilingi bilioni mbili kwa *Yetu Microfinance Bank Plc*

153. Hadi Desemba 2016, Kampuni ya TMRC ilitoa mikopo ya shilingi bilioni 59.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 43.9 iliyotolewa hadi kipindi kama hicho mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 35.8. Aidha, mikopo ya nyumba iliyotolewa na TMRC ilikuwa ni sawa na asilimia 14 ya jumla ya mikopo yote ya nyumba nchini. Kwa upande mwingine, uwiano wa mikopo ya nyumba kwa Pato la Taifa uliendelea kuwa asilimia 0.45 kama ilivyokuwa mwaka 2015. Uwiano huu ni mdogo ukilinganisha na nchi za Afrika ya Mashariki kama inavyoonekana kwenye Kielelzo Na 5.1

Kielelezo Na.5.1: Uwiano wa Mikopo ya Nyumba kwa Pato la Taifa



Chanzo: Soko la Mikopo ya Nyumba Tanzania

Benki ya Wanawake Tanzania

154. Hadi Desemba 2016, idadi ya wateja wa benki waliongezeka na kufikia 65,735 ikilinganishwa na wateja 62,301 waliokuwepo hadi Desemba 2015, sawa na ongezeko la asilimia 5.5. Ongezeko hili lilitokana na uhamasishaji wa wananchi hususan, wanawake kufungua akaunti. Hata hivyo, amana za wateja wa benki zilipungua kwa asilimia 21.6 kutoka shilingi bilioni 25.1 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 19.7 mwaka 2016, kutokana na wateja wengi kuwa na kiwango kidogo cha amana.

155. Mwaka 2016, benki ilitoa mikopo ya shilingi bilioni 19.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 21.2 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 9.4. Upungufu huo ulitokana na sababu mbalimbali ikiwemo uwepo wa mikopo chechefu. Aidha, kiwango cha mikopo chechefu hadi Desemba 2016 ilikuwa asilimia 43.0 ikilinganishwa na asilimia 26.0 mwaka 2015. **Jedwali Na. 5.9** linaonesha taarifa ya mikopo ya benki kwa mwaka 2015 na 2016.

Jedwali Na.5.9: Thamani ya Mikopo ya Benki ya Wanawake

Aina ya Mikopo	2015			2016		
	Wateja	Kiasi cha Mikopo	NPL(%)	Wateja	Kiasi cha Mikopo	NPL (%)
Vikundi	12,042	7,727,176,159	26	10,509	6,628,374,995	40
Mikopo Binafsi	427	3,363,040,483	26	397	3,531,599,356	40
Mikopo ya Biashara	57	1,588,680,141	25	56	1,400,862,396	18
Mikopo ya Wafanyakazi	766	2,729,830,080	18	564	1,870,064,463	41
SACCOS	3	681,713,106	46	1	778,668,447	82
Wafanyakazi wa Ndani	108	1,080,654,530	-	124	1,184,487,737	-
Mikopo ya Akaunti ya Hundi	13	798,779,724	11	6	882,464,877	82
Maendeleo	2,638	2,974,467,724	27	2,458	2,353,071,737	71
Viwanja	119	259,015,410	20	145	574,652,194	30
Jumla	16,173	21,203,357,357	26	14,260	19,204,246,202	43

Chanzo: Benki ya Wanawake Tanzania

156. Mwaka 2016, mapato ya Benki ya Wanawake yalipungua kwa asilimia 24.3 kutoka shilingi bilioni 8.5 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 6.4 mwaka 2016. Hii ilitokana na kupungua kwa kiwango cha mikopo na baadhi ya mikopo kutolipika kama ilivyotegemewa. Vile vile, thamani ya uwekezaji katika kipindi hicho ilipungua kutoka shilingi bilioni 9.6 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 5.8 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 39.0. Hii ilitokana na kupungua kwa amana.

Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania

157. Mwaka 2016, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilitoa mikopo ya shilingi bilioni 6.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni moja iliyotolewa mwaka 2015. Mikopo hiyo ilitolewa kwa miradi ya kilimo cha mazao ya mahindi, mchele, maua na miwa kwa wakulima wa mikoa ya Iringa, Tanga na Morogoro. Aidha, jumla ya vikundi 8 vya wakulima 857 wa mahindi katika mkoa wa Iringa na vikundi vya wakulima 11 vyenye wanachama 1,384 katika mikoa ya Morogoro, Tanga na Iringa vilinufaika na mikopo hiyo. Kwa upande wa miradi ya kilimo cha umwagiliaji, benki ilitoa mikopo ya shilingi bilioni 2.2 kwa vikundi sita vya wakulima vyenye wanachama 1,216 vinavyojishughulisha na kilimo cha mahindi, mchele na kilimo cha mbogamboga katika wilaya za Mufindi, Kilombero, Iringa Vijijini na Korogwe.

158. Mwaka 2016, benki ilipata faida ya shilingi bilioni 2.26 ikiwa ni mwaka wa kwanza wa uendeshaji wa shughuli zake. Aidha, katika kutafuta vyanzo

vingine vya mapato, benki ilipokea mkopo wa shilingi bilioni 204 kutoka Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) kwa ajili kugharamia miradi ya kilimo. Vile vile, benki ilipata shilingi milioni 578.3 kutoka programu ya MIVARF kwa ajili ya kugharamia uendeshaji wa *loan guarantee scheme*.

159. Mwaka 2016, benki ilitoa mafunzo kwa vikundi 336 vya wakulima vilivyokuwa na wanachama 44,000 katika mikoa ya Iringa, Morogoro na Tanga. Kati ya hivyo, vikundi 19 vilitimiza vigezo vya kukopa na kupatiwa mikopo, wakati vikundi vingine viliendelea kupewa mafunzo husika.

Benki ya Posta

160. Mwaka Mwaka 2016, Benki ya Posta Tanzania iliendelea kutoa huduma zake kwa kutumia matawi 30, ikilinganishwa na matawi 29 mwaka 2015. Aidha, benki ilikuwa na matawi madogo 24 ya kutoa huduma zake kama ilivyokuwa mwaka 2015. Katika kipindi hicho, jumla ya akaunti 298,874 zilifunguliwa kupitia mpango wa *TPB popote* ikiwa ni ongezeko la asilimia 26.1 ikilinganishwa na akaunti 236,981 zilizofunguliwa mwaka 2015. Mwaka 2016, benki iliendelea kutoa huduma kwa wateja kwa kutumia mashine 200 za ATM za Umoja Switch ambazo kati ya hizo, mashine 44 zilikuwa ni mali ya benki ikilinganishwa na mashine 196 za Umoja Switch zilizojumuisha mashine 38 za Benki ya Posta mwaka 2015.

161. Mwaka 2016, amana za wateja katika Benki ya Posta zilikuwa shilingi milioni 292,200 ikilinganishwa na shilingi milioni 302,181 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 3.3. Kushuka kwa kiwango cha amana kulisababishwa na ongezeko la ushindani miongoni mwa benki nchini, hususan katika kukusanya amana kutoka kwa wateja wale wale pamoja na ukuaji wa taasisi za huduma ndogo za fedha zinazohamasisha wateja wake kutoka katika kundi kubwa la watu wa kipato cha chini.

162. Kwa upande wa huduma za vikundi, hadi Desemba 2016, benki ilikuwa na wateja 5,077 wa vikundi vya kuweka na kukopa vijijini wenye amana zenye thamani ya shilingi milioni 927; wateja 33,146 wa VICOBA wenye amana zenye thamani ya shilingi bilioni 3.1; wateja 2,482 wa vikundi visivyo rasmi waliokuwa na amana zenye thamani ya shilingi bilioni 2.3; na akaunti maalum kwa mashabiki wa mpira wa miguu wa timu za Simba, Yanga na Mbeya City

zilikwa na wateja 17,857 na amana zenye thamani ya shilingi bilioni 1.3. Aidha, benki ilitoa mikopo iliyokuwa na thamani ya shilingi milioni 298,057 mwaka 2016 ikilinganishwa na shilingi milioni 254,358 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 17.2.

Jedwali Na.5.10: Mchanganuo wa Thamani ya Mikopo ya Benki ya Posta (Shs. Miln)

Aina ya Mkopo	2013	2014	2015	2016
Mikopo ya Biashara	10,534	24,393	34,794	33,800
Mikopo ya Watumishi	94,760	124,965	135,164	141,400
Mikopo ya Wastaafu		18,540	43,319	76,000
Mikopo midogo midogo	7,471	18,536	22,867	23,929
Mikopo ya Uwezeshaji	1,920	196	187	36
Mikopo ya Vikundi		2,297	5,831	4,600
PSL Loans			2,010	4,000
Mikopo ya VICOBA			225	705
Mikopo ya Wafanyakazi	5,049	7,078	9,961	13,500
Jumla	119,734	196,005	254,358	298,057
Badiliko (%)	24.8	63.7	29.8	17.2

Chanzo: Benki ya Posta Tanzania

163. Mwaka 2016, thamani ya uwekezaji uliofanywa na benki katika dhamana za Serikali ulipungua kwa asilimia 33.8 kufikia shilingi milioni 42,452 kutoka shilingi milioni 64,101 mwaka 2015. Kushuka kwa uwekezaji katika dhamana za Serikali kulitokana na ongezeko la mahitaji ya mikopo kwa wateja. Kwa upande mwingine, mapato ya benki yaliongezeka kwa asilimia 23.5 kutoka shilingi milioni 74,485 mwaka 2015 hadi shilingi milioni 92,000 mwaka 2016. Aidha, faida kabla ya kodi iliongezeka na kufikia shilingi milioni 16,100 kutoka shilingi milioni 12,025 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 33.9.

Jedwali Na.5.11: Thamani ya Rasilimali katika Dhamana (Shs. Milioni)

Kitega Uchumi	2013	2014	2015	2016
Dhamana za Serikali za muda mfupi	15,894	16,434	36,880	24,269
Dhamana za Serikali	29,404	26,225	27,221	18,183
Dhamana binafsi	437	263	0	0
Jumla ya dhamana	45,735	42,922	64,101	42,452
Badiliko (%)	19.9	-6.2	49.3	-33.8

Chanzo: Benki ya Posta Tanzania

Mfuko wa SELF

164. Mwaka 2016, Mfuko wa SELF uliendelea kutoa huduma kwa wananchi ambapo mikopo iliyotolewa ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 11.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 8.6 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 33.7. Mikopo hiyo ilitolewa kwa Asasi za fedha 75 ikilinganishwa na Asasi 87 zilizokopeshwa mwaka 2015. Kati ya hizo, SACCOS zilikuwa 44, Kampuni za Fedha 28 na Benki za Jamii tatu (3). Vile vile, mikopo hiyo iliweza kuwafikia wajasiriamali wadogo 5,130 ikilinganishwa na wajasiriamali 2,686 walionufaika na mikopo mwaka 2015.

165. Mwaka 2016, Mfuko ulikuwa na mtaji wenye thamani ya shilingi bilioni 57.09 ikilinganishwa na shilingi bilioni 55.5, mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 2.9. Mchanganuo wa uwekezaji wa Mfuko ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali Na.5.12.

Jedwali Na.5.12: Mchanganuo wa Mtaji wa Mfuko wa SELF (TZS Bilioni)

Eneo la Uwekezaji	Desemba 2015	Desemba 2016	Ukuaji (%)
Fedha Taslimu Benki	6.18	2.30	(62.8)
Kasma ya mikopo	7.93	11.09	39.8
Uwekezaji katika Amana za Serikali	41.40	43.70	5.6
Jumla	55.51	57.09	2.8

Chanzo: Mfuko wa SELF

166. Mwaka 2016, Mfuko ulipata mapato kutoka kwenye vyanzo vikuu vitatu ambavyo ni: mikopo, uwekezaji katika dhamana za serikali na mapato

mengineyo. Hadi Desemba 2016, Mfuko ulikuwa na mapato ya shilingi bilioni 7.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 4.6 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 62.8. Ongezeko hilo kwa kiasi kikubwa lilitokana na uwekezaji katika dhamana za Serikali ambao ulikuwa asilimia 80.5. Mchanganuo wa vyanzo vya mapato ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali Na.5.13.

Jedwali Na.5.13: Vyanzo vya Mapato ya Mfuko wa SELF hadi Desemba 2016

Vyanzo vya Mapato	2015	2016	Ukuaji (%)
Mikopo	1,075,570,710.3	1,258,417,731.0	17.0
Uwekezaji katika Amana za Serikali	3,309,964,320.4	5,991,035,420.0	81.0
Mapato mengineyo	182,855,501.0	188,341,166.0	3.0
Ruzuku kutoka Serikalini	-	-	0.0
Jumla	4,568,390,531.7	7,437,794,317.0	62.8

Chanzo: Mfuko wa SELF

MWENENDO WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA

Jedwali Na. 27

Sh. Bilioni

	Kipindi kinachoishia mwezi Desemba						Badiliko 2015/16	
	2011	2012	2013	2014	2015	2016	Kiasi	%
Fedha ya msingi (M0)	2,235.8	2,414.8	2,764.0	3,244.7	3,678.5	3,608.7	-69.8	-1.9
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)	5,572.0	6,538.6	7,218.1	8,284.2	9,575.7	9,986.7	411.0	4.3
Amana za Akiba na za muda maalum	3,676.0	4,186.0	4,672.4	5,632.9	6,204.4	6,536.5	332.1	5.4
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)	9,247.9	10,724.5	11,890.6	13,917.0	15,780.1	16,523.2	743.1	4.7
Amana za fedha za kigeni	3,773.4	3,922.6	4,216.2	4,697.1	6,335.2	6,237.2	-98.0	-1.5
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)	13,021.3	14,647.1	16,106.8	18,614.2	22,115.3	22,760.4	645.1	2.9
Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye benki (Net foreign assets)	6,273.6	6,396.0	6,576.3	6,551.5	8,244.0	8,209.0	-35.0	-0.4
Rasilimali halisi katika fedha za ndani kwenye benki (Net domestic assets)	6,747.7	8,251.1	9,530.4	12,062.6	13,871.3	14,551.4	680.1	4.9
Karadha Nchini	10,958.1	13,719.0	16,293.0	18,863.7	22,505.5	23,775.8	1,270.3	5.6
Madai halisi kwa serikali kuu	1,471.3	2,019.4	2,554.6	3,651.6	4,881.6	4,282.0	-599.7	-12.3
Mikopo kwa serikali kuu	3,335.7	4,708.6	5,900.4	6,451.5	7,012.8	7,166.9	154.1	2.2
Mikopo kwa sekta isiyo serikali	7,622.3	9,010.4	10,392.7	12,412.3	15,492.7	16,608.9	1,116.2	7.2
Rasilimali nyinginezo (Other Items Net)	-2,345.9	-2,778.7	-3,416.8	-4,001.3	-6,503.1	-6,339.5	163.6	-2.5

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

VIWANGO VYA UKUAJI WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA

Jedwali Na. 28

	Kipindi kinachoishia mwezi Desemba					
	2011	2012	2013	2014	2015	2016
Fedha ya msingi (M0)	17.9%	8.0%	14.5%	17.4%	13.4%	-1.9%
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)	23.2%	17.3%	10.4%	14.8%	15.6%	4.3%
Amana za Akiba na za muda maalum	4.4%	13.9%	11.6%	20.6%	10.1%	5.4%
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)	15.0%	16.0%	10.9%	17.0%	13.4%	4.7%
Amana za fedha za kigeni	27.0%	4.0%	7.5%	11.4%	34.9%	-1.5%
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)	18.2%	12.5%	10.0%	15.6%	18.8%	2.9%
Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye benki (Net foreign assets)	2.4%	2.0%	2.8%	-0.4%	25.8%	-0.4%
Rasilimali halisi katika fedha za ndani kwenye benki (Net domestic assets)	38.1%	22.3%	15.5%	26.6%	15.0%	4.9%
Karadha Nchini	15.1%	25.2%	18.8%	15.8%	19.3%	5.6%
Madai halisi kwa serikali kuu	82.4%	37.3%	26.5%	42.9%	33.7%	-12.3%
Mikopo kwa serikali kuu	-5.5%	41.2%	25.3%	9.3%	8.7%	2.2%
Mikopo kwa sekta isiyo serikali	27.2%	18.2%	15.3%	19.4%	24.8%	7.2%
Rasilimali nyinginezo (Other Items Net)	22.7%	18.5%	23.0%	17.1%	62.5%	-2.5%

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

MWENENDO WA VIWANGO VYA UBADILISHAJI KATI YA SHILINGI NA DOLA YA MAREKANI

Jedwali Na.29

	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016
Shs/Dola mwisho wa mwaka	1,313.29	1,453.54	1,605.35	1,578.41	1603.2067	1,723.69	2,148.52	2,172.62
Badiliko la thamani ya shilingi (%)	-2.5	-9.6	-9.5	1.7	-1.5	-7.0	-19.8	-1.1
Shs/Dola wastani wa mwaka	1,307.23	1,401.79	1,557.43	1,571.71	1598.66	1,652.51	1985.39	2,177.09
Badiliko la wastani wa thamani ya shilingi (%)	-7.7	7.2	-10.0	-0.9	-1.7	-3.3	-16.8	-8.8

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

MIKOPO YA BENKI ZA BIASHARA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI

Jedwali Na. 30

Aina ya Shughuli	Kipindi kinachoishia mwezi Desemba (Sh. Milioni)						Ukuaji (%)	Mchangano (%)
	2011	2012	2013	2014	2015	2016		
Uzalishaji katika Kilimo	912331.8	938915.0	965140.6	1057347.9	1174242.9	1107645.3	-5.7	6.9
Huduma za Kifedha	177691.8	231269.4	251255.0	310711.6	404605.8	388745.2	-3.9	2.4
Madini na Uchimbaji Mawe	39175.7	55158.0	96739.0	166275.2	275233.3	328620.4	19.4	2.1
Viwanda	928746.6	991795.9	1160593.7	1386236.9	1695767.4	1627766.0	-4.0	10.2
Majengo na Ujenzi	320938.2	410748.0	514408.4	660147.8	741401.0	740726.8	-0.1	4.6
Uchukuzi na Mawasiliano	545243.5	610053.9	727538.0	925723.9	1231805.7	1180904.6	-4.1	7.4
Biashara	1523962.2	1843242.7	2162191.4	2652057.0	3077683.0	3349328.7	8.8	20.9
Utalii	49730.4	60152.3	113394.5	129478.1	176626.3	198482.0	12.4	1.2
Mahoteli na Migahawa	361039.7	363033.4	371008.5	436101.1	514642.0	526390.2	2.3	3.3
Umeme	166672.8	338035.1	403022.7	440936.5	439801.0	429919.2	-2.2	2.7
Watu Binafsi	1557495.5	1778743.2	1744954.0	2104496.5	2731740.4	2981134.8	9.1	18.6
Sekta Nyinginezo	815729.5	1101473.5	1643118.0	1842250.1	2641095.5	3144834.3	19.1	19.6
Jumla	7398757.6	8722620.4	10153363.7	12111762.6	15104644.3	16004497.5	6.0	100.0

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

MWENENDO WA AMANA KATIKA BENKI ZA BIASHARA

Jedwali Na.31

Sh. Bilioni

	Kipindi Kinachoishia mwezi Desemba							Badiliko 2015/16 (%)
	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	
Amana za Sekta Binafsi								
Amana za Hundi/Zinazaohamishika	2,624.3	3,336.2	4,123.8	4,454.2	5,039.4	5,897.2	6,378.0	8.2
Amana za Akiba na za Muda Maalum	3,520.7	3,676.0	4,186.0	4,672.4	5,632.9	6,204.4	6,536.5	5.4
Amana za fedha za kigeni	2,926.4	3,722.0	3,882.4	4,216.0	4,697.1	6,335.2	6,237.2	-1.5
Jumla	9,071.5	10,734.2	12,192.2	13,342.6	15,369.4	18,436.8	19,151.7	3.9
Amana za Serikali	699.3	626.6	736.8	791.8	808.4	856.9	577.8	-32.6
Jumla za Amana zote	9,770.8	11,360.8	12,929.0	14,134.4	16,177.8	19,293.7	19,729.5	2.3

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

VIWANGO VYA WASTANI WA RIBA

Jedwali Na. 32

Asilimia

Aina ya Riba	Kipindi Kinachoishia Mwezi Desemba				
	2012	2013	2014	2015	2016
Riba ya Benki Kuu (Bank rate)	12.00	16.00	16.00	16.00	16.00
Riba za Amana					
Amana za akiba	2.94	3.11	3.12	3.42	3.08
Amana za muda maalum	8.82	8.87	8.76	9.30	8.78
Riba za mikopo					
Mikopo ya muda mfupi hadi mwaka mmoja	14.09	13.84	14.80	14.22	12.87
Mikopo ya muda wa kati na mrefu	15.68	16.13	15.75	16.39	15.66
Riba za Hawala za Hazina					
Siku 91	11.89	13.62	13.20	9.28	7.09
Siku 182	12.96	15.46	15.22	17.15	14.54
Siku 364	13.69	15.63	16.23	18.72	15.80

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

SURA YA 6

RASILIMALI WATU

Idadi ya Watu

167. Idadi ya watu Tanzania ilikadiriwa kuwa 50,144,175 mwaka 2016 ikilinganishwa na watu 48,776,405 mwaka 2015. Katika mwaka 2016, Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na watu 48,676,698, sawa na asilimia 97.1 ya watu wote na Tanzania Zanzibar watu 1,467,477, sawa na asilimia 2.9. Aidha, mchanganuo wa watu kwa jinsia unaonesha kuwa wanawake walikadiriwa kuwa 25,731,286 sawa na asilimia 51.3 ya watu wote na wanaume 24,412,889 sawa na asilimia 48.7. Makadirio haya yalitokana na matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 ambayo yalionesha ukuaji wa idadi ya watu unaongezeka kwa wastani wa asilimia 2.7 kwa mwaka.

Mgawanyiko wa Watu Kimkoa

168. Mwaka 2016, mkoa wa Dar es salaam ulikuwa na watu wengi zaidi, ukiwa na watu takribani 5,465,420 ambao ni sawa na asilimia 11.2 ya watu wote Tanzania Bara ikilinganishwa na watu 5,166,570, sawa na asilimia 10.9 mwaka 2015. Mkoa wa Mwanza ulifuatia kwa kuwa na watu takribani 3,122,992 (asilimia 6.4); na Kagera watu 2,789,577 (asilimia 5.7). Idadi kubwa ya watu katika mkoa wa Dar es salaam ilitokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu wanaohamia kutoka mikoa mingine hususan vijana katika harakati za kujikimu kimaisha, kupata huduma za kijamii na za kiuchumi. Aidha, mkoa wa Katavi ulikuwa na idadi ndogo zaidi ya watu ikilinganishwa na mikoa mingine ya Tanzania Bara, ukiwa na watu takribani 642,567 (asilimia 1.3). Kwa upande wa Zanzibar, mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na watu wengi zaidi ikilinganishwa na mikoa mingine, ukiwa na watu takribani 702,283, sawa na asilimia 47.9 ya watu wote Tanzania Zanzibar na mkoa uliokuwa na idadi ndogo zaidi ya watu ni Kusini Unguja uliokuwa na watu 125,215, sawa na asilimia 8.5.

169. Msongamano wa watu kwa kila kilometa moja ya mraba kwa Tanzania ulikuwa na wastani wa watu 57 kwa mwaka 2016. Aidha, kwa upande wa Tanzania Bara msongamano ulikuwa wastani wa watu 55 kwa kila kilometa moja ya mraba. Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na msongamano mkubwa zaidi wa watu kwa upande wa Tanzania Bara, ukiwa na watu 3,923 kwa kila kilometa

moja ya mraba ukifuatiwa na Mwanza (330), Kilimanjaro (133) na Kagera (110). Mkoa ya Lindi na katavi ilikuwa na idadi ndogo zaidi ya watu kwa kila kilometa moja ya mraba ikiwa na wastani wa watu 14 ikifuatiwa na mkoa wa Ruvuma uliokuwa na wastani wa watu 24 kwa kila kilometa moja ya mraba. Kwa upande wa Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na msongamano mkubwa wa wastani wa watu waliokadiriwa kuwa 3,053 kwa kila kilometa moja ya mraba wakati Mkoa wa Kusini Unguja ulikuwa na wastani wa watu 147 kwa kila kilometa moja ya mraba.

170. Mchanganuo wa watu kwa makundi ya umri ulionyesha kuwa asilimia 16 ya idadi ya watu Tanzania mwaka 2016 ilihusisha watoto wa umri wa chini ya miaka mitano, ambao ni sawa na watoto 8,104,714. Idadi ya watu wenye umri kuanzia miaka mitano (5) hadi 14 ilikuwa ni 13,847,638, sawa na asilimia 28 ya watu wote Tanzania. Mchanganuo unaonesha kuwa watu wenye umri wa miaka 15 – 24 ni asilimia 19 ya watu wote Tanzania. Vile vile, idadi ya watu wenye umri kuanzia miaka 25 hadi 64 ilikuwa ni 16,680,855 sawa na asilimia 33 ya watu wote Tanzania. Hata hivyo, idadi ya watu wenye umri kuanzia miaka 15-35 ni 18,482,345, sawa na asilimia 34.9 ya watu wote ikiwa ndio nguvu kazi ya vijana. Wazee wenye umri zaidi ya miaka 64 walikuwa ni 1,917,996 sawa na asilimia 4. Aidha, idadi ya watu wenye umri wa miaka 15 hadi 64 ambayo ni nguvukazi ya taifa ilikuwa ni 26,273,828, sawa na asilimia 52.4 ya watu wote Tanzania.

Jedwali Na: 6.1 Mchanganuo wa Idadi ya Watu kwa Makundi ya Umri na Jinsi kwa mwaka 2016

Umri	Jinsi			Asilimia
	ME	KE	Jumla	
5<	4,053,609	4,051,105	8,104,714	16.2
5 - 14	6,922,419	6,925,218	13,847,638	27.6
15 - 24	4,511,359	5,081,613	9,592,973	19.1
25 - 35	3,690,798	4,198,575	7,889,373	15.7
36 - 64	4,328,383	4,463,100	8,791,483	17.5
65+	906,322	1,011,674	1,917,996	3.8
Jumla	24,412,890	25,731,286	50,144,175	

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Afya ya Uzazi na Mtoto

171. Kwa mujibu wa Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Tanzania 2015/16, wanawake wanazaa wastani wa watoto 5.2 kwa kila mwanamke ikiwa umepungua kutoka wastani wa watoto 5.4 kwa kila mwanamke mwaka 2010. Wanawake wanaoishi maeneo ya vijijini Tanzania Bara wanazaa wastani wa watoto 6.0 ikilinganishwa na wastani wa watoto 3.8 kwa wanawake wanaoishi maeneo ya mijini. Uzazi pia unatofautiana kulingana na viwango vya elimu na uwezo wa kiuchumi. Wanawake wasio na elimu wanazaa wastani wa watoto 6.6 ikilinganishwa na wastani wa watoto 3.6 kwa wanawake wenye elimu ya sekondari au zaidi. Aidha wanawake wanaoishi kaya maskini wanazaa wastani wa watoto 7.5 ikilinganishwa na wastani wa watoto 3.1 kwa wanawake wanaoishi kaya tajiri. Vile vile, vifo vya watoto wachanga chini ya mwaka mmoja vilipungua kutoka 51 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2010 hadi 43 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2015/16. Aidha, vifo vya watoto chini ya miaka mitano vilipungua kutoka 81 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2010 hadi 67 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2015/16.

Nguvu kazi na Ajira

172. Taarifa ya matokeo ya Utafiti wa Ajira na Mapato wa Mwaka 2015 (Employment and Earning Survey of 2015) katika sekta rasmi ilionesha kuwa ajira katika sekta rasmi ziliongezeka na kufikia 2,334,969 mwaka 2015 ikilinganishwa na ajira 2,141,351 mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 9.0. Matokeo ya utafiti huo yalibainisha kuwa ajira za masharti ya muda mrefu pia ziliongezeka kwa asilimia 15.6 kufikia ajira 2,060,013 kutoka ajira 1,781,900 mwaka 2014. Ajira za muda mfupi zilipungua kwa asilimia 23.5 kutoka ajira 359,451 mwaka 2014 hadi kufikia ajira 274,956 mwaka 2015. Ajira za muda mfupi hazina mazingira mazuri ya ufanyaji kazi hivyo kupungua kwa ajira hizo kunaashiria matokeo chanya ya sera mbalimbali zinazosaidia kupungua kwa ajira hizo.

173. Ajira za kudumu zilichangia asilimia 88.2 ya ajira zote wakati ajira za muda mfupi zilichangia asilimia 11.8 ya ajira zote nchini. Aidha, mwaka 2015, sekta binafsi ilitoa ajira 1,568,165 (asilimia 67.1) ikilinganishwa na ajira 766,803 zilizotolewa katika sekta ya umma (asilimia 32.9). Vile vile, mwaka 2015, uwiano wa ajira kwa jinsia kwa wanawake ulibaki kuwa asilimia 37.0 ya

ajira zote katika sekta rasmi na wanaume ulikuwa asilimia 63.0 kama ilivyokuwa mwaka 2014.

174. Matokeo ya utafiti yalibainisha kuwa, vijana wenye umri wa miaka 15-35 walioajiriwa ajira za muda mrefu walikuwa asilimia 31.3 wakati wenye umri wa miaka 36 na kuendelea walikuwa asilimia 68.7. Sekta binafsi ilitoa nafasi nyingi za ajira za muda mfupi (asilimia 95.8) ikilinganishwa na sekta ya umma iliyotoa asilimia 4.2. Mwaka 2015, idadi ya waajiriwa wenye ulemavu walikuwa 3,977 ikilinganishwa na waajiriwa 3,547 mwaka 2014, sawa na ongezeko la asilimia 12.1. Miongoni mwao, asilimia 58.5 walijajiriwa katika sekta binafsi na asilimia 41.5 walijajiriwa katika sekta ya umma. Aidha, kati ya hao, asilimia 60.2 walikuwa wanaume na asilimia 39.8 walikuwa wanawake

Jedwali Na: 6.2 Mchanganuo wa Jumla ya Ajira kwa Aina za Ajira na Sekta

Aina za Ajira	2014				2015			
	Umma	Binafsi	Jumla	%	Umma	Binafsi	Jumla	%
Ajira za Kudumu	1,088,542	693,358	1,781,900	83.2	1,304,653	755,360	2,060,013	88.2
Ajira za Muda Mfupi	344,443	15,008	359,451	16.8	263,512	11,444	274,956	11.8
Jumla	1,432,985	708,366	2,141,351	100	1,568,165	766,804	2,334,969	100

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

175. Mchanganuo wa mchango wa sekta mbalimbali katika kutoa ajira ulibainisha kuwa sekta ya elimu ilitoa mchango mkubwa zaidi katika ajira ambapo uliongezeka hadi kufikia asilimia 19.6 mwaka 2015 kutoka asilimia 17.1 mwaka 2014. Sekta ya viwanda ilifuatia kwa kuchangia asilimia 18.1 ya ajira zote mwaka 2015 kutoka asilimia 19.8 mwaka 2014; wakati sekta ya upangishaji majengo ilitoa mchango mdogo zaidi wa asilimia 0.2 ya ajira zote.

176. Matokeo ya utafiti huo yaliendelea kubainisha kuwa Mkoa wa Dar es Salaam uliongoza kwa kuchangia asilimia 30.6 ya waajiriwa wote mwaka 2015, ikilinganishwa na asilimia 33.6 mwaka 2014, Mkoa uliofuatia ni Morogoro kwa asilimia 11.5; Arusha (asilimia 7.1); na Mwanza (asilimia 6.2). Mikoa ya Katavi na Njombe ilijiri watu wachache zaidi kuliko mikoa mingine yote ambapo kila mkoa ulitoa ajira kwa kiwango kisichozidi asilimia moja ya waajiriwa wote.

Mgawanyo huo wa ajira unategemea mahitaji ya huduma yanayotokana na idadi ya watu katika mikoa hiyo pamoja na shughuli za kiuchumi.

177. Matokeo ya utafiti huo yaliendelea kubainisha kuwa Mkoa wa Dar es Salaam uliongoza kwa kuchangia asilimia 30.6 ya waajiriwa wote mwaka 2015, ikilinganishwa na asilimia 33.6 mwaka 2014, Mkoa uliofuatia ni Morogoro kwa asilimia 11.5; Arusha (asilimia 7.1); na Mwanza (asilimia 6.2). Mikoa ya Katavi na Njombe iliajiri watu wachache zaidi kuliko mikoa mingine yote ambapo kila mkoa ulitoa ajira kwa kiwango kisichozidi asilimia moja ya waajiriwa wote.

Jedwali Na. 6.3: Mchanganuo wa Ajira Kimkoa na Kisekta (%)

Mkoa	Binafsi		Umma		Jumla	
	2014	2015	2014	2015	2014	2015
Dodoma	0.7	1.0	1.7	1.7	2.5	2.7
Arusha	5.1	5.9	1.2	1.1	6.3	7.1
Kilimanjaro	3.1	3.8	1.7	1.7	4.8	5.5
Tanga	2.6	3.1	1.7	1.6	4.3	4.7
Morogoro	8.8	8.3	3.4	3.2	12.1	11.5
Pwani	0.9	0.9	1.4	1.2	2.3	2.1
DSM	29.3	26.3	4.3	4.3	33.6	30.6
Lindi	0.2	0.3	1.1	1.0	1.3	1.2
Mtwara	0.6	0.5	0.7	0.7	1.3	1.2
Ruvuma	1.1	1.0	1.0	1.0	2.0	2.0
Iringa	1.5	1.5	1.2	1.2	2.7	2.7
Mbeya	2.5	2.8	2.3	2.3	4.8	5.1
Singida	0.5	0.7	1.0	1.0	1.5	1.6
Tabora	0.4	0.6	1.1	1.0	1.5	1.6
Rukwa	0.3	0.4	0.6	0.7	0.9	1.1
Kigoma	0.5	0.6	1.1	1.1	1.6	1.8
Shinyanga	1.3	1.1	1.3	1.2	2.5	2.3
Kagera	0.7	0.9	1.0	1.2	1.7	2.0
Mwanza	4.2	4.4	1.7	1.7	5.9	6.2
Mara	0.6	0.8	1.3	1.2	2.0	2.0
Manyara	0.6	0.7	0.7	0.7	1.3	1.4
Njombe	0.3	0.4	0.5	0.5	0.8	0.80
Katavi	0.0	0.0	0.2	0.3	0.2	0.3
Simiyu	0.1	0.2	0.8	0.7	0.9	1.0
Geita	0.8	1.1	0.4	0.4	1.2	1.5
Jumla	66.9	67.2	33.1	32.8	100.0	100.0

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

178. Matokeo ya utafiti huo pia yalionesha kuwa ajira mpya mwaka 2014/15 zilipungua hadi 102,672 kutoka ajira mpya 281,698 mwaka 2013/14. Kati ya ajira hizo mpya, wanaume walikuwa 56,988 na wanawake 45,684. Aidha, utafiti ulibaini kuwa mwaka 2014/15 kulikuwa na ajira mpya 56,072 katika sekta ya umma ikilinganishwa na ajira mpya 46,601 katika sekta binafsi. Kati ya idadi ya ajira mpya zilizotolewa kada za mafundi na wataalam washiriki ilitoa waajiriwa wengi ambao walikuwa 48,377 ikifuatiwa na wataalam, waajiriwa 21,400 na wahudumu na wafanyakazi wa madukani, waajiriwa 11,374.

179. Mwaka 2016, Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA) ulisajili na kutoa ushauri wa jinsi ya kuchagua fani na kazi stahiki kulingana na sifa zao na mahitaji ya soko la ajira ili kuwajengea uwezo wa kuajiriwa na kuajirika. Katika kipindi hicho, jumla ya watafutakazi 1,516 walisajiliwa ikilinganishwa na watafutakazi 1,249 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 21.4. Kati ya waliosajiliwa, wanaume walikuwa 942, sawa na asilimia 62.1 na wanawake 574. Ongezeko hilo, lilitokana na Wakala kuendelea kujitangaza, kutembelea taasisi za elimu ya juu, kuwaunganisha watafutakazi na waajiri na kutoa mafunzo elekezi kwa watafuta kazi yanayowajengea uwezo wa kushindania fursa za ajira ndani na nje ya nchi.

180. Mwaka 2016, watafutakazi 624 waliunganishwa na waajiri wenye fursa za ajira ndani ya nchi. Kati yao, wanaume walikuwa 456, sawa na asilimia 73.1 na wanawake walikuwa 168, sawa na asilimia 26.9. Idadi hiyo iliongezeka kwa asilimia 24.1 ikilinganishwa na mwaka 2015 ambapo watafutakazi 503 waliunganishwa kwa waajiri wenye fursa za ajira. Aidha, Wakala uliendelea kutekeleza utaratibu wa kuwasiliana na waajiri kwa kuwatembelea au kwa njia za mawasiliano ya simu na barua pepe kwa lengo la kupata fursa za ajira, ambapo jumla ya waajiri 108 walifikwa na kusajili nafasi za kazi 79 zenye fursa za ajira 389.

181. Mwaka 2016, Wakala kwa kushirikiana na taasisi binafsi za ajira na Balozi za Tanzania katika nchi husika ulipitia na kuridhia mikataba ya watanzania 914 waliopata ajira katika nchi za Oman (wanaume 22, wanawake 764), Dubai (wanaume 4, wanawake 20), Qatar (wanaume 73), Japan (wanaume 4) na Saudi Arabia (wanaume 27). Wakala pia ulihakikisha mikataba ya ajira ya

watanzania hao inazingatia sheria za nchi na miongozo ya Shirika la Kazi Duniani(ILO) ili kukabiliana na aina yoyote ya unyanyasaji na ubaguzi.

182. Mwaka 2016, Wakala ulitoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kushindania fursa za ajira ndani na nje ya nchi kwa watafutakazi 629 ikilinganishwa na watafutakazi 584 waliopewa mafunzo mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 7.7. Kati yao, wanaume walikuwa 332, sawa na asilimia 52.8 na wanawake walikuwa 297, sawa na asilimia 47.2 ya watafutakazi wote waliopewa mafunzo mwaka 2016. Mafunzo hayo yalilenga jinsi ya kubaini vyanzo vya taarifa za soko la ajira, uandishi wa wasifu binafsi na barua za maombi ya kazi, namna ya kufanya vyema kwenye usaili na dondoo muhimu za kujibu vyema maswali ya usaili. Vile vile, Wakala ulitoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kushindania fursa za ajira ndani na nje ya nchi kwa wanafunzi 1,255 wa vyuo mwaka 2016 ikilinganishwa na wanafunzi 665 waliopatiwa mafunzo hayo mwaka 2015. Kati yao, wanaume walikuwa 630, sawa na asilimia 50.2 na wanawake walikuwa 625, sawa na asilimia 49.8.

IDADI YA WATU NCHINI TANZANIA KIMKOA: 2007-2016

Jedwali 33

Mkoa	2007	2008	2009	2010	2011	2012**	2013	2014	2015	2016
Dodoma	1951071	2004544	2058630	2111764	2163817	2083588	2127416	2172165	2217856	2264508
Arusha	1522975	1570394	1617728	1664780	1711624	1694310	1741396	1789791	1839531	1890653
Kilimanjaro	1535975	1569212	1602530	1635870	1669174	1640087	1669051	1698526	1728522	1759048
Tanga	1837661	1880389	1923468	1966908	2010480	2045205	2091341	2138517	2186757	2236086
Morogoro	1975160	2021713	2068426	2115275	2162197	2218492	2271310	2325386	2380750	2437431
Pwani	991586	1014968	1038654	1062574	1086658	1098668	1122685	1147227	1172306	1197933
Dar es Salaam	2881548	2961150	3040118	3118132	3194903	4364541	4617000	4884061	5166570	5465420
Lindi	869522	887434	905480	923607	941884	864652	872758	880939	889197	897533
Mtwara	1246089	1271912	1297751	1323568	1349235	1270854	1286501	1302340	1318374	1334606
Ruvuma	1268738	1303330	1338800	1375017	1412084	1376891	1406411	1436563	1467362	1498821
Iringa	1649200	1679828	1709225	1737382	1764285	941238	951964	962813	973784	984882
Mbeya	2423635	2502258	2581792	2662156	2743084	2707410	2781971	2858585	2937310	1883024
Singida	1258545	1294584	1330931	1367481	1404065	1370637	1402820	1435758	1469469	1503972
Tabora	2086048	2170926	2258664	2349374	2443049	2291623	2359642	2429679	2501796	2576053
Rukwa	1349579	1398866	1450118	1503184	1558200	1004539	1037259	1071044	1105931	1141953
Kigoma	1601020	1669078	1740111	1814158	1891173	2127930	2179598	2232520	2286727	2342250
Shinyanga	3411023	3549342	3692941	3841787	3998664	1534808	1566734	1599325	1632593	1666554
Kagera	2293093	2379637	2469904	2563870	2661671	2458023	2537021	2618558	2702715	2789577
Mwanza	3265729	3364378	3464566	3566263	3669380	2772509	2856258	2942537	3031422	3122992
Mara	1631031	1692449	1756442	1822866	1891907	1743830	1787279	1831810	1877451	1924230
Manyara	1241994	1288280	1337015	1388295	1441771	1425131	1471083	1518516	1567479	1618020
Njombe	-	-	-	-	-	702097	707698	713345	719036	724772
Katavi	-	-	-	-	-	564604	583160	602325	622121	642567
Simiyu	-	-	-	-	-	1584157	1613580	1643549	1674075	1705168
Geita	-	-	-	-	-	1739530	1785824	1833350	1882141	1932230
Songwe	-	-	-	-	-	-	-	-	-	1136415
Tanzania Bara	38291222	39474672	40683294	41914311	43169305	43625354	44827757	#####	#####	#####
Kaskazini Ungu	160175	165544	171150	177095	183209	187455	193551	199844	206343	213053
Kusini Unguja	105456	107811	110183	112612	115035	115588	117923	120305	122736	125215
Mjini Magharibi	447716	459502	471341	483205	495054	593678	619144	645701	673398	702283
Kaskazini Pemb	224951	234142	243759	253999	264677	211732	214502	217309	220153	223033
Kusini Pemba	216479	226055	236072	246601	257577	195116	197274	199456	201662	203893
Zanzibar	1154777	1193054	1232505	1273512	1315552	1303569	1342394	1382616	1424292	1467477
Tanzania	39445999	40667726	41915799	43187823	44484857	44928923	46170151	#####	#####	#####

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Takwimu za matokeo ya sensa mwaka 2012

- Takwimu Hazipo, Mikoa Mipya

SEHEMU YA PILI

UENDELEZAJI SEKTA BINAFSI

SURA YA 7

UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI

Uwekezaji Vitega Uchumi Nchini

183. Mwaka 2016, Kituo cha Taifa cha Uwekezaji kilisajili jumla ya miradi 345 ikilinganishwa na miradi 466 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 25. Upungufu huo ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na matatizo ya kiuchumi duniani. Kati ya Miradi iliyosajiliwa, miradi 103 ilikuwa ya wazawa, 143 ya wageni na 105 ya ubia kati ya wazawa na wageni. Thamani ya miradi iliyosajiliwa mwaka 2016 ilikuwa thamani ya dola za Marekani bilioni 5.92 ikilinganishwa na dola bilioni 5.89 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 0.5. Miradi hiyo ilikuwa na fursa za ajira 49,711 ikilinganishwa na fursa za ajira 46,250 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 7.5.

Mgawanyiko wa Miradi Kisekta

184. Mwaka 2016, sekta ya nishati ilisajili miradi yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 2.46 ikifuatiwa na majengo ya biashara dola za Marekani bilioni 1.13, uzalishaji viwandani dola za Marekani bilioni 0.62, kilimo dola za Marekani bilioni 0.5, usafirishaji mizigo dola za Marekani bilioni 0.38, mawasiliano dola za Marekani bilioni 0.28, na Maliasili dola za Marekani bilioni 0.26. Aidha, sekta ya uzalishaji viwandani iliongoza kwa kuvutia wawekezaji wengi, ambapo mwaka 2016 ilisajili miradi 178, ikifuatiwa na majengo ya biashara iliyosajili miradi 48, utalii miradi 33 na kilimo miradi 24.

Mgawanyiko wa Miradi Kimkoa

185. Mwaka 2016, mkoa wa Dar es Salaam uliendelea kupata wawekezaji wengi kwa sekta zote isipokuwa sekta ya kilimo na nishati. Hii ilitokana na mkoa huo kuwa na mazingira mazuri ya uwekezaji hususan miundombinu ikilinganishwa na mikoa mingine. Mwaka 2016 mkoa wa Dar es Saam ulipata miradi ya uwekezaji 173 ikifuatiwa na mkoa wa Arusha uliopata miradi 36, Pwani miradi 34 na Mwanza miradi 16. Mikoa ya Katavi, Rukwa, Manyara na Kigoma haikupata mradi hata mmoja.

Jedwali Na. 1: Mtawanyiko wa Miradi ya Uwekezaji Kimkoa Iliyosajiriwa na Kituo Cha Uwekezaji Tanzania katika mwaka 2016

Sekta	Arusha	Pwani	DSM	Dodoma	Geita	Iringa	Kaera	Katavi	Kigoma	Kiliman	Lindi	Manyar	Mbeva	Morogo	Mtwara	Mwanza	Niombe	Mara	Ruvuma	Shinyan	Simiyu	Singida	Tabora	Tanga	Jumla	
Kilimo		5	2			1				4			1	5		1	1		1			1				24
Utangazaji																										
Kompyuta			1																							1
Majengo ya Biashara	6	1	33								1				1	2								4	48	
Miundombinu																										
Nishati	2		2			2							1											1	8	
Taasisi za Kifedha			4																							4
Rasilimali watu	2		6																							8
Uzalishaji Viwandani	11	27	90	5	7	4	2			2	2		6	2	1	7	1	1		5		1	1	3	178	
Maliasili			1											1												2
Huduma	2		12							1						1										16
Mawasiliano			2																							2
Utalii	8		8	1						1	3					4		4						3	33	
Usafirishaji	5	1	12		1	1										1					1				21	
Jumla	36	34	173	6	8	8	2			8	6		8	8	2	16	2	5	1	5	1	2	1	11	345	

Chanzo: Kituo cha Uwekezaji Tanzania

Urahisi wa Kufanya Biashara Nchini

186. Mwaka 2016, serikali iliendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, ikiwa ni pamoja na kuimarisha utulivu wa uchumi jumla, kupunguza urasimu, kuharakisha maamuzi, kuimarisha ulinzi na usalama, na kuhakikisha upatikanaji wa miundombinu imara (kama vile barabara, reli) na huduma bora zikiwemo upatikanaji wa umeme wa uhakika. Katika eneo hili la kuboresha mazingira ya biashara, serikali ilifanya vizuri kulingana na taarifa ya Benki ya Dunia ya mwaka 2017 iliyoonesha kuwa Tanzania ilikuwa nchi ya 132 kwa urahisi wa kufanya biashara ikiwa imepiga hatua kwa nafasi 12 kutoka nafasi ya 144 mwaka 2016.

Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

187. Mwaka 2016, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi liliendelea kusimamia, kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya

Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2004. Katika kipindi hicho, Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi unaosimamiwa na Baraza ulitoa dhamana ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 11.4 kwa wajasiriamali 11,457 (Wanaume 7,086; Wanawake 4,371). Fedha hizo zilitolewa na Benki ya Posta (TPB), Benki ya Maendeleo ya Rasilimali Tanzania (TIB) na Benki ya CRDB.

Maendeleo ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

188. Mwaka 2016, Serikali iliendelea kuibua na kuendeleza miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi pamoja na kutoa mafunzo, ushauri na maelekezo ya namna ya kutekeleza miradi ya ubia katika wizara, tawala za mikoa na serikali za mitaa, taasisi na mashirika ya umma. Katika kipindi hicho, Serikali ilipokea maandiko ya miradi iliyokusudiwa kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia yaliyohusu ujenzi wa gati mbili mpya katika bonde la Gerezani, ujenzi wa bandari za Mtwara na Mwambani (Tanga), na Kasanga (Rukwa). Aidha, maandiko hayo yalikusisha ujenzi wa reli ya kati kwa viwango vya kimataifa kutoka Dar-es Salaam hadi Keza (Tanzania) kuunganisha hadi Kigali (Rwanda) na Musongati (Burundi); mradi wa kukagua na kusajili magari kwa njia ya kielektroniki na mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi wa Somanga-Fungu. Vile vile, Serikali iliendelea kusimamia miradi inayotekelezwa kwa utaratibu wa ubia ambayo ni pamoja na: mradi wa mabasi yaendayo haraka jijini Dar Es Salaam; mradi wa kufua umeme kwa kutumia gesi wa Kinyerezi III; mradi wa barabara ya tozo ya Dar es Salaam hadi Chalinze; mradi wa kuzalisha madawa muhimu na vifaa tiba wa Bohari Kuu ya Dawa.

KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC): MIRADI YA UWEKEZAJI ILIYOSAJILIWA

Jedwali Na.34

Sekta	2015								2016							
	A	B	C	D	E	F	G	H	A	B	C	D	E	F	G	H
Kilimo	33	33	0	14	10	9	3036	124.2	24	24	0	7	8	9	25547	496.1
Maliasili	3	3	0	1	1	1	195	4.2	2	2	0	0	0	2	235	264.9
Utafiti	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Uzalishaji Viwandani	184	180	4	57	92	35	16958	782.4	178	178	0	48	86	44	12455	615.1
Bidhaa za petroli na madini	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Majengo ya biashara	65	65	0	33	24	8	4756	1129.8	48	48	0	16	16	16	4812	1133.7
Usafirishaji Mizigo	84	84	0	58	17	9	7907	837.9	21	21	0	12	9	6	2605	384.9
Huduma	9	9	0	2	3	4	1517	939.4	16	16	0	1	6	9	670	48.0
Komputa	-	-	-	-	-	-	-	-	1	1	0	1	0	0	37	0.1
Asasi za fedha	3	3	0	1	2	0	213	28.6	4	4	0	0	1	3	140	9.0
Mawasiliano	1	1	0	1	0	0	47	1.3	2	2	0	1	0	1	58	282.3
Nishati	8	8	0	2	2	4	4548	1373.0	8	8	0	3	3	2	627	2457.7
Rasilimali watu	10	10	0	5	0	5	1801	73.9	8	8	0	3	1	4	362	33.3
Utalii	62	61	1	26	20	16	4637	281.2	33	33	0	11	13	9	2163	194.4
miundombinu	1	1	0	0	0	1	570	304.0	0	0	0	0	0	0	0	0
Utangazaji	3	3	0	3	0	0	65	11.8	0	0	0	0	0	0	0	0
Jumla	466	461	5	203	171	92	46250	5891.7	345	345	0	103	143	105	49711	5919.4

Chanzo: Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)

- A Jumla ya Miradi Iliyosajiliwa
- B Miradi Mipya
- C Miradi ya Upanuzi
- D Miradi ya Wazawa
- E Miradi ya Wageni
- F Miradi ya Ubia
- G Jumla ya Ajira
- H Jumla ya Thamani ya Uwekezaji (USD. Milioni)
- Takwimu Hazikupatikana

SURA YA 8

MASUALA MTAMBUKA

UKIMWI

189. Mwaka 2016, Serikali kupitia Tume ya kudhibiti UKIMWI iliandaa miongozo minne ya Taifa ya kudhibiti UKIMWI ambayo ni: Mkakati wa Kondomu; Mkakati wa Uwekezaji; Mpango Kazi wa Kinga; na Mpango Jinsia na UKIMWI. Miongozo hii itasaidia wadau katika kupanga mipango ya kudhibiti maambukizi ya VVU kwa kutumia takwimu rasmi. Aidha, mwaka 2016 Serikali ilianza zoezi la kufanya utafiti wa nne (Tanzania HIV Impact Survey – 2016 THIS) ili kubaini viwango vya maambukizi ya VVU na hali ya UKIMWI nchini. Utafiti huo utatoa taarifa juu ya ushamiri wa VVU kwa watu wazima, vijana na watoto ikiwemo mienendo na tabia hatarishi ya kuambukizwa VVU na utumiaji wa huduma zinazohusiana na VVU.

190. Mwaka 2016, Serikali iliridhia miongozo kutoka Shirika la Afya Duniani iliyohusu upimaji na utoaji wa dawa kwa watu watakapo gundulika kuwa na VVU bila kuangalia kiwango cha CD4. Aidha, Serikali iliendelea na uhamasishaji wa upatikanaji rasilimali fedha na watu ili kufikia lengo la 90-90-90 kama ilivyoainishwa na Shirika la Afya Duniani ambalo linamaanisha kufikia mwaka 2020 asilimia 90 ya watu wanaoishi na VVU watajua hali zao ya maambukizi; asilimia 90 ya watu wanaoishi na VVU wanapata huduma endelevu za tiba; na asilimia 90 ya watu wanaopata huduma endelevu za tiba virusi vimefubazwa.

191. Mwaka 2016, Serikali kupitia Tume ya kudhibiti UKIMWI ilianzisha Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI kwa lengo la kupunguza utegemezi wa fedha za UKIMWI kutoka kwa wadau wa maendeleo kwa asilimia 30 ifikapo 2018. Hatua hizo zilifuatiwa na kuanzishwa kwa Bodi ya Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI ambayo iliandaa mpango wa utekelezaji kwa nchi nzima.

Mwaka 2016, Serikali kupitia Tume ya Kudhibiti UKIMWI ilianzisha mchakato wa kufanya tathmini ya muda wa kati wa utekelezaji wa Mkakati wa Tatu wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI 2013/14 – 2017/18. Mkakati huonalenga kupunguza maambukizi mapya kwa asilimia 50, kupunguza vifo vitokanavyo na UKIMWI na kuondoa unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI ifikapo 2018. Mapendekezo kutokana na tathmini hii yatasaidia kuboresha utekelezaji wa afua zote za UKIMWI nchini.

192. Kutokana na utafiti wa *Spectrum 2015*, inakadiriwa kuwa wataanzania milioni 1.3 wanaishi na Virusi vya Ukimwi ambapo wanawake ni 780,000, sawa na asilimia 60 na wanaume 520,000. Aidha, idadi ya watoto wenye umri wa miaka 0 – 14 wanaoishi na VVU ni 91,000. Vile vile, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Matunzo na Matibabu ambapo jumla ya Watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (WAVIU) ilikuwa 839,574, sawa na asilimia 63 ya WAVIU wote walikuwa wanapata dawa za ARV na jumla ya watoto 55,670 walikuwa wanapata matibabu ya ART sawa na asilimia 66 ya watoto wenye VVU. Aidha, lengo la kimataifa ni kufikia kiwango cha asilimia 90 cha WAVIU wote ifikapo mwaka 2020.

Mazingira

193. Mwaka 2016, Serikali katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira iliendelea kuhimiza wananchi kupanda na kutunza miti ili kuhifadhi mazingira, ambapo kila halmashauri ya Wilaya ilitakiwa kupanda na kutunza miti isiyopungua milioni 1.5. Katika kipindi hicho, jumla ya miti 264,177,045 ilipandwa na kati ya hiyo miti 211,204,160 ilitawi sawa na asilimia 80, ikilinganishwa na miti 217,301,650 iliyopandwa mwaka 2015 ambapo miti 181,301,650 ilitawi sawa na asilimia 83.4. Vile vile, Serikali iliandaa Mkakati wa Taifa wa Upandaji na Utunzaji Miti wa miaka mitano (2016 - 2021) ili kuboresha kampeni ya upandaji miti. Mkakati huu unalenga kupanda miti milioni 280 kwa mwaka ili kupunguza vichochezi vinavyochangia uharibifu wa mazingira na upoteaji wa misitu, bioanuai na kurejesha uoto wa asili kwa kuhusisha jamii na wadau wote nchini.

194. Mwaka 2016, katika kuhakikisha maendeleo endelevu katika uwekezaji, Serikali iliendelea kuwahimiza wawekezaji kuzingatia sheria ya usimamizi wa mazingira ya uwekezaji kwa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kabla ya kutekeleza miradi yao. Katika kipindi hicho, miradi 1,058 ilisajiliwa kwa ajili ya kuandaa TAM ikilinganishwa na miradi 1,574 iliyosajiliwa mwaka 2015. Kati ya miradi iliyofanyiwa tathmini mwaka 2016, miradi 475 sawa na asilimia 44.9 ilipata hati za kukidhi vigezo vya TAM ikilinganishwa na miradi 628 sawa na asilimia 39.9mwaka 2015. Aidha, ili kuboresha uwezo wa ukaguzi wa mazingira, Serikali ilisajili wataalam binafsi 139 na kampuni 26 kwa ajili ya kufanya TAM na ukaguzi wa mazingira. Idadi hii, ilifanya kuwa na jumla ya wataalam elekezi wa mazingira 1000 na kampuni 210 zilizosajiliwa mwaka 2016.

195. Mwaka 2016, kwa kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Serikali ilifanya ukaguzi wa miradi 782 ambayo inajumuisha viwanda, migodi, majengo, mabwawa ya majitaka, machinjio, hospitali na vituo vya afya, masoko, mashamba, mifumo ya majitaka, mifumo ya maji ya mvua, vituo vya mafuta, hoteli, vyanzo vya maji na makambi ya wakimbizi. Katika ukaguzi huo, hatua stahiki za kisheria zilichukuliwa kwa miradi 237 iliyokiuka Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ikiwemo kulipa faini. Vile vile, Serikali iliendelea kusimamia na kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaotokana na taka za plastiki kwa kupiga marufuku uzalishaji, uingizaji na matumizi ya vifungashio vya plastiki kwa ajili ya pombe kali. Halikadhalika, Serikali iliendelea kuelimisha umma kupitia njia mbalimbali zikiwemo vipindi vya redio na televisheni, matangazo na hotuba za viongozi kuhusu hatua hii na kuhamasisha matumizi na mifuko mbadala.

196. Mwaka 2016, Serikali iliendelea kutekeleza mradi wa kujenga uwezo wa jamii za Pwani kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Mradi huo unatekelezwa katika maeneo ya Pemba na Unguja, Jiji la Dar es Salaam na wilaya za Pangani, Rufiji na Bagamoyo. Kazi zilizofanyika kupitia mradi huo zilikuwa: kupanda mikoko pandwa katika eneo la hekta 792 la delta ya kaskazini ya Rufiji ili kurudisha uoto wa asili na kupunguza mmomonyoko wa fukwe za eneo hilo; kutoa mafunzo juu ya tathmini ya athari za mabadiliko ya tabianchi kwa maafisa 80 kutoka maeneo ya mradi na kujenga upya kuta za pembeni ya bahari za Pangani (mita 950), Kisiwa Panza-Pemba (mita 40) na Kilimani-Unguja (mita 200). Aidha, katika Jiji la Dar es Salaam mradi unatekelezwa katika maeneo ya ufukwe wa Barabara ya Barack Obama (mita 820) na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (mita 380). Vile vile, mitaro ya maji ya mvua ya Bungoni-Ilala na Mtoni-Temeke ilisafishwa na kukarabatiwa katika eneo la jumla ya mita 2300. Halikadhalika, mradi umesambaza majiko sanifu 3000 kwa manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke ili kuhamasisha jamii kutumia majiko hayo kwa lengo kupunguza matumizi ya kuni na mkaa ambavyo huchangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa misitu.

Usalama wa Raia

197. Mwaka 2015/16, hali ya ulinzi na usalama iliendelea kuwa tulivu licha ya kuwepo kwa baadhi ya matukio ya mauaji, unyang'anyi, uharibifu wa mali na ajali zilizojitokeza. Katika kipindi hicho, jumla ya makosa ya jinai 70,925 yaliripotiwa ikilinganishwa na makosa 63,844 yaliyoripotiwa mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 11.1. Makosa ya kugombania mali yalikuwa 40,386 ikilinganishwa na makosa 37,672 yaliyoripotiwa mwaka 2014/15, sawa

na ongezeko la asilimia 7.2. Aidha, makosa yaliyoripotiwa dhidi ya binadamu mwaka 2015/16 yalikuwa 10,999 ikilinganishwa na makosa 11,311 yaliyoripotiwa mwaka 2014/15, sawa na upungufu wa asilimia 2.8. Vile vile, makosa dhidi ya maadili ya jamii yaliyoripotiwa yaliongezeka kwa asilimia 31.5 kufikia makosa 19,540 ikilinganishwa na makosa 14,861 yaliyoripotiwa mwaka 2014/15. Makosa yaliyokuwa na ongezeko kubwa kwa idadi yalikuwa ni kupatikana na pombe haramu ya gongo, bangi, mazao ya misitu na madawa ya kulevyo.

198. Mwaka 2015/16, matukio ya ajali za barabarani yalipungua kufikia 8,418 kutoka matukio 11,067 mwaka 2014/15, sawa na upungufu wa asilimia 23.9. Upungufu huo ulitokana na kuzingatia sheria za barabarani. Aidha, ajali zilizosababisha vifo zilipungua kutoka 3,637 mwaka 2014/15 hadi ajali 2,419 mwaka 2015/16, sawa na upungufu wa asilimia 33.5. Vile vile, vifo vilivyotokana na ajali hizo vilipungua kutoka 3,879 mwaka 2014/15 hadi vifo 3,363 mwaka 2015/16, sawa na upungufu wa asilimia 13.3. Idadi ya majeruhi waliotokana na ajali mwaka 2015/16 ilikuwa 9,827 ikilinganishwa na majeruhi 11,992 mwaka 2014/15, ikiwa ni upungufu wa asilimia 18.1.

199. Mwaka 2015/16, hali ya ulinzi na usalama wa magereza yote nchini ilikuwa tulivu. Hata hivyo, huduma kwa wafungwa na mahabusu ziliendelea kutolewa licha ya kuwepo changamoto mbalimbali zikiwemo uchakavu wa magereza na uhaba wa vitendea kazi. Katika kipindi hicho, magereza yote yalikuwa na jumla ya wafungwa na mahabusu 32,297 ikilinganishwa na uwezo wa magereza hayo wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu 29,552. Idadi hii inaonesha uwepo wa wafungwa na mahabusu 2,745 zaidi ya uwezo wa magereza. Idadi ya wafungwa ilikuwa 17,518 na mahabusu 14,779 mwaka 2016 ikilinganishwa na wafungwa 15,234 na mahabusu 16,877 waliokuwa na kesi mahakamani mwaka 2015.

200. Mwaka 2015/16, Serikali iliendelea kuchukua hatua zakupunguza msongamano magerezani, ambazo nipamoja na: kutumia vikao vya Bodi ya Parole (vifungo vya nje); na misamaha ya Mheshimiwa Rais. Mwaka 2015/16 vikao vitatu vya Parole vilifanyika ambapo jumla ya majalada 244 ya wafungwa yalijadiliwa na kupendekezwa kuingizwa kwenye mpango wa Parole ikilinganishwa na majalada 266 yaliyojadiliwa mwaka 2015. Aidha, wafungwa 239 waliachiwa kutoka gereza kwa wa parole mwaka 2015/16 ikilinganishwa na wafungwa 259 walioachiwa mwaka 2014/15. Vile vile, wafungwa 735

walitolewa magerezani kwenda kutumikia kifungo cha nje ikilinganishwa na wafungwa 667 mwaka 2014/15. Idadi hii ilifanya jumla ya wafungwa walioachiwa kwenda kutumikia kifungo nje kufikia wafungwa 974 mwaka 2015/16 ikilinganishwa na wafungwa 926 mwaka 2014/15

201. Mwaka 2015/16, jeshi la zimamoto na uokoaji liliendelea kukabiliana na majanga ya moto pamoja na majanga mengine kwa lengo la kuokoa maisha na mali za watu. Katika kipindi hicho, jumla ya miito 607 ya matukio ya moto ilipokelewa ikilinganishwa na miito 2,761 mwaka 2014/15. Kupungua kwa miito kwa kiasi kikubwa kulitokana na jitihada za Jeshi kutoa elimu kwa umma pamoja na ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto kwenye maeneo mbalimbali. Jumla ya maeneo 53,399 yalikaguliwa mwaka 2015/16 ikilinganishwa na maeneo 50,957 yaliyokaguliwa mwaka 2014/15. Vile vile, Jeshi lilifanya uokoaji katika matukio 264 ikilinganishwa na matukio 156 mwaka 2014/15.

202. Mwaka 2015/16, jumla ya wageni 1,117,707 waliingia na wageni 1,161,931 walitoka nchini kwa vibali halali ikilinganishwa na wageni 1,341,223 walioingia na wageni 1,179,048 waliotoka mwaka 2014/15. Aidha, jumla ya hati za ukaazi 34,014 zilitolewa mwaka 2015/16 ikilinganishwa na hati za ukaazi 22,631 zilizotolewa mwaka 2014/15, kati ya hati zilizotolewa, hati 2,798 zilikuwa za daraja "A"; 20,016 daraja "B"; 8,568 daraja "C"; 1064 za mfuasi; na 1,568 za msamaha. Vile vile, jumla ya hati za kusafiria 97,786 zilitolewa kwa watanzania ikilinganishwa na hati za kusafiria 74,651 zilizotolewa mwaka uliotangulia. Kati ya hati zilizotolewa mwaka 2015/16, hati za kawaida zilikuwa 96,509, za kibalozi 425, za watumishi 199 na za Afrika Mashariki 653. Halikadhalika, doria na misako ilifanyika na kuwakamata wahamiaji haramu 9,989 mwaka 2015/16 ikilinganishwa na wahamiaji haramu 3,188 waliokamatwa mwaka 2014/15.

203. Mwaka 2015/16, Serikali iliendelea kuhifadhi wakimbizi 241,498 kutoka mataifa ya Burundi (176,317), Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (964,803), Somalia (150) na wakimbizi 228 kutoka mataifa mengine (Rwanda, Uganda, Sudan ya Kusini na Ethiopia). Wakimbizi hao walihifadhiwa katika kambi na makazi yaliyoko mikoa ya Kigoma, Katavi, Tabora na Tanga, na wengine wenye uwezo wa kujitegemea waliruhusiwa kuishi nje ya kambi za wakimbizi. Aidha, wakimbizi 3,910 walihamishiwa katika nchi za Marekani, Australia, Ireland na Canada.

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa

204. Mwaka 2015/16, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa iliendelea na zoezi la usajili na utambuzi kwa wananchi wa mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar. Katika kipindi hicho, Mamlaka ilikuwa imesajili jumla ya wananchi 4,668,481 na kati ya hao, jumla ya wananchi 2,774,412 walipatiwa vitambulisho. Aidha, Mamlaka ilikabidhiwa vifaa vya usajili (BVR) 5000 kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili kuongeza kasi ya usajili na utambuzi. Sambamba na hilo, Mamlaka ilipeleka watumishi 96 katika Wilaya 48 nchini kwa lengo la kuboresha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake. Mamlaka iliunganisha mfumo wa mawasiliano kati ya makao makuu na ofisi za wilaya sita (6) kwa upande wa Zanzibar na vituo kumi (10) kwa upande wa Tanzania Bara. Vile vile, Mamlaka iliunganisha mfumo wa utambuzi na taasisi 20 kwa lengo la kurahisisha utambuzi wa wananchi na wageni wakaazi katika utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii.

Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini

205. Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini uliendelea na shughuli za usajili na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa, vifo, ndoa, talaka pamoja na kuasili watoto. Mwaka 2015/16, Wakala ulisajili jumla ya vizazi 980,012, vifo 24,061, ndoa 18,339, talaka 110 na watoto wa kuasili 24 ikilinganishwa na vizazi 537,060, vifo 63,441, ndoa 17,044, talaka 143 na watoto wa kuasili 34 mwaka 2015.

206. Mwaka 2016, Wakala ulisajili watoto 365,433 ikilinganishwa na watoto 204,137 waliosajiliwa mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 79.0. Ongezeko hilo lilitokana na kusimikwa kwa mfumo wa usajili wa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano katika mikoa ya Iringa na Njombe pamoja na uhamasishaji wa usajili wa watoto chini ya rika hilo katika mikoa ya Mbeya na Songwe. Aidha, Wakala ulisajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto 14,721 walioko mashuleni ambao hawakuwa na vyeti ikilinganishwa na watoto 15,000 mwaka 2015.

207. Kwa upande wa udhamini, mwaka 2016 Wakala ulisajili na kutoa hati 155 za miunganisho ya wadhamini. Katika kipindi hicho, Wakala ulisimamia jumla ya mashauri 141 ya masuala ya mirathina uliendelea kushirikiana na warithi katika kusimamia mirathi kwa kuwaelimisha umuhimu wa kufunga mirathi mapema ili kuepusha mali kupotea au kuvamiwa. Aidha, jumla ya wosia 49 ziliandikwa na kuhifadhiwa mwaka 2016 ikilinganishwa na wosia 57 mwaka 2015. Vile vile, Wakala uliendelea kutoa elimu kwa umma kupitia radio, luninga

na makala katika magazeti juu ya umuhimu wa kuandika na kuhifadhi wosia ili kuepusha migogoro ya wanafamilia pindi mwenye mali anapofariki.

208. Kwa upande wa ufilisi, mwaka 2016 Wakala katika kutekeleza “Road Map” ya masuala ya mazingira ya biashara, ulipitia na kuandaa taarifa ya mapendekezo ya kutunga Sheria ya Ufilisi ili kuwa na sheria moja ya ufilisi na kupunguza muda wa kufunga biashara.

SURA YA 9

HALI YA UMASKINI NA MAENDELEO YA WATU

UTANGULIZI

209. Mwaka 2016, Serikali kupitia Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21) imeendelea na juhudi za kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kupambana na umaskini. Mpango huo umezingatia uhusiano asili uliopo kati ya maendeleo ya viwanda na rasilimali watu, ambao ndio uliokuwa kielelezo cha sifa ya malengo ya MKUKUTA II na Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Aidha, lengo kuu la Mpango huo ni kujenga msingi thabiti wa mabadiliko ya muundo wa uchumi na kuhakikisha maendeleo jumuiishi ya jamii.

HALI YA UMASKINI

210. Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano unalenga kupunguza uwiano wa idadi ya watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji muhimu kutoka asilimia 28.2 ya mwaka 2012 hadi asilimia 16.7 mwaka 2020/21 na asilimia 12.7 mwaka 2025/26.

Umaskini wa Mikoa na Wilaya

211. Mwaka 2016, Serikali ilitoa tathmini ya umaskini katika ngazi ya mikoa na wilaya. Tathmini hiyo ilitumia taarifa za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 pamoja na Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi (Household Budget Survey) wa mwaka 2011/12. Katika kupima hali ya umaskini, tathmini ilizingatia mahitaji ya msingi kwa kila mwanakaya ambayo ni pamoja na elimu, afya, maji na chakula.

212. Kwa mujibu wa tathmini hiyo mkoa wa Kigoma ulikuwa na kiwango kikubwa cha watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini cha asilimia 48.9 ikilinganishwa na mkoa wa Dar es Salaam uliokuwa na asilimia 5.2. Kiwango kidogo cha umaskini Dar es Salaam kimetokana na kuwepo kwa shughuli nyingi za uzalishaji na biashara kutokana na kuimarika kwa miundombinu ya barabara, maji na umeme ambavyo ni vichocheo vya kuinua kipato cha wananchi hasa maskini ukilinganishwa na mikoa mingine. Kwa upande mwingine, mkoa wa Kigoma umekuwa na kiwango kikubwa cha umaskini japokuwa ni mhimili wa uzalishaji wa chakula Kanda ya Magharibi kutokana na changamoto ya miundombinu ya usafiri inayofanya bidhaa zisifike kwa urahisi sokoni na hivyo

kusababisha uwepo wa fursa chache za kiuchumi. Aidha, ukosefu wa umeme wa uhakika katika mkoa huo umechangia kuwepo kwa shughuli chache za kiuchumi. Jedwali Na.9.1 linaonyesha mchanganuo wa viwango vya umaskini kwa mikoa

Jedwali Na. 9.1: Hali ya Umaskini kwa Mikoa

Nafasi	Mkoa	Kiwango Cha Umaskini (%)
1	Kigoma	48.9
2	Geita	43.7
3	Kagera	39.3
4	Singida	38.2
5	Mwanza	35.3
6	Ruvuma	34.9
7	Shinyanga	34.2
8	Mtwara	33.9
9	Tanga	32.7
10	Tabora	32.6
11	Lindi	30.0
12	Simiyu	28.8
13	Dodoma	27.1
14	Rukwa	27.1
15	Iringa	26.7
16	Mara	26.2
17	Njombe	25.7
18	Mbeya ¹	24.3
19	Katavi	23.9
20	Morogoro	23.1
21	Manyara	18.3
22	Arusha	14.7
23	Pwani	14.7
24	Kilimanjaro	14.3
25	Dar es Salaam	5.2

Chanzo: Taarifa ya Hali ya Umaskini Kimkoa na Kiwilaya

213. Kwa upande wa hali ya umaskini kwa wilaya, Wilaya ya Kakonko (Kigoma) ilikuwa na kiwango kikubwa cha umaskini ambapo asilimia 63 ya

¹ Taarifa hizi zinajumuisha mkoa wa Songwe ambao wakati wa utafiti ulikuwa ni sehemu ya mkoa wa Mbeya.

watu walikuwa chini ya mstari wa umaskini ikifuatiwa na Wilaya za Biharamulo (Kagera) na Kibondo (Kigoma) zenye viwango sawa vya asilimia 58 kila moja. Kwa upande mwingine, Wilaya tatu zilizoonekana kuwa na viwango vidogo vya umaskini ni Ilala iliyokuwa na asilimia 4.8, Kinondoni asilimia 4.9 na Temeke asilimia 6 zote za mkoa wa Dar es salaam. Tathmini hiyo pia ilionesha hali ya tofauti ya kipato miongoni mwa wananchi kimkoa na kiwilaya. Tofauti hiyo hupimwa kwa kipimo kijulikanacho kama *Gini coefficient* ambacho kina wigo wa kuanzia sifuri hadi moja (0 - 1). Kadri uwiano unavyokaribia moja inamaanisha tofauti ya kipato inakuwa kubwa na kadri inavyokaribia 0 inamaanisha tofauti ya kipato inakuwa ndogo. Kwa kipimo hicho, mkoa wa Kigoma ulikuwa na uwiano mdogo zaidi wa tofauti ya kipato wa 0.28 ikiwa ni chini ya uwiano wa Taifa wa 0.34 ikilinganishwa na mkoa wa Kilimanjaro uliokuwa na uwiano mkubwa zaidi wa 0.35. Kwa upande wa wilaya, Manispaa ya Mtwara ilikuwa na uwiano mkubwa wa tofauti ya kipato wa 0.43 na wilaya ya Buhigwe ilikuwa na uwiano mdogo zaidi wa 0.25. Aidha, kwa mujibu wa tafiti za mapato na matumizi ya kaya za mwaka 2007 na 2011/12, tofauti ya kipato miongoni mwa wananchi kitaifa ilipungua kidogo kutoka 0.35 mwaka 2007 hadi 0.34 mwaka 2011/12.

214. Tathmini hiyo ilitumiwa na Serikali katika maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao pamoja na mambo mengine unalenga kukabiliana na changamoto za umaskini

MAENDELEO YA WATU

215. Serikali kupitia Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano imeendelea kuongeza upatikanaji na ubora wa huduma zinazohitajika na jamii ili kuboresha hali ya maisha. Katika kutathmini maendeleo ya watu vigezo vikuu vinavyotumika ni elimu na afya.

216. Mwaka 2016, Serikali iliongeza uwekezaji kwenye elimu na mafunzo kwa lengo la kuongeza ujuzi na kujenga uwezo wa watu ili kuboresha mchango wa mtaji wa watu katika maendeleo ya Taifa. Uwekezaji huo ulihusisha ugharamiaji wa elimu msingi bila malipo na utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ambao ulisaidia kuongezeka upatikanaji wa fursa za elimu na mafunzo katika fani mbalimbali. Aidha, Serikali iliendelea kuimarisha na kuboresha mfumo wa uthibiti na uthibiti wa shule na vyuo, mafunzo ya ualimu, mazingira ya kufundishia na kujifunzia pamoja na huduma za maktaba kwa lengo la kuinua ubora wa elimu katika ngazi zote.

217. Serikali inatambua kwamba, afya bora ni nguzo na rasilimali muhimu katika kuchangia maendeleo ya mtu binafsi, familia na nchi hususan katika kuleta maisha bora na kupunguza umaskini. Kutokana na hilo, Mwaka 2016, Serikali iliendelea kuboresha huduma za afya kwa kuendeleza ujenzi, upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya; kuboresha upatikanaji wa dawa muhimu, vifaa tiba; na kuboresha afya ya uzazi, mama na mtoto. Aidha, serikali iliendelea kuhamasisha wananchi kujiunga na bima za afya kwa lengo la kuwa na uhakika wa huduma za matibabu.

218. Mwaka 2016, Serikali iliendelea kuimarisha huduma za lishe na upatikanaji wake hususan kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano ili kuwajengea misingi imara ya ukuaji na afya ya akili. Kama mtoto hatapata lishe ya kutosha, uwezo wake kiakili unapungua, anakuwa kwenye hatari ya kukumbwa na magojwa hatarishi, anaweza kuwa na matokeo yasiyoridhisha shuleni na hatimaye kusababisha taifa kukosa nguvu kazi yenye tija na ufanisi.

219. Upatikanaji wa maji safi na salama ni muhimu katika kufikia maendeleo endelevu ya watu. Katika kufikia lengo hilo, mwaka 2016 Serikali iliendelea na juhudi za kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama karibu na makazi ya watu ili watumie muda mwingi katika shughuli za kiuchumi badala ya kwenda umbali mrefu kutafuta maji.

220. Mwaka 2016, Serikali iliendelea kupambana na vitendo vya rushwa na kuboresha ufanisi katika matumizi ya rasilimali za umma. Mojawapo ya hatua zilizochukulia na Serikali katika kipindi hicho ni uanzishwaji wa Mahakama ya Mafisadi ili kupambana na vitendo vya rushwa nchini. Rushwa huathiri mapato ya Serikali na kupunguza uwezo wake kuwekeza katika maeneo mbalimbali na kupunguza umaskini. Aidha, kwa mujibu wa taarifa ya taasisi ya *Transparency International* (TI)” ya mwaka 2016, Tanzania ilipata alama 32 katika masuala ya kupambana na rushwa ikilinganishwa na alama 30 mwaka 2015, ikimaanisha mapambano dhidi ya rushwa yaliimarika mwaka 2016. Kulingana na fahirisi za TI, rushwa hupimwa kati ya alama 0-100 ambapo alama sifuri (0) inamaanisha rushwa iliyokithiri na alama mia (100) inamaanisha kutokuwepo kwa rushwa.

SEHEMU YA TATU

SUALA MAALUMU KIMAENDELEO

SURA YA 10

UJENZI WA UCHUMI WA VIWANDA

Utangulizi

221. Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ina lengo la kuiwezesha Tanzania kufikia hadhi ya nchi zenye uchumi wa kipato cha kati unaoongozwa na uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025. Malengo mengine ni pamoja na kufikia pato la wastani kwa kila mtu la dola za Marekani 3,000 na uchumi kukua kwa wastani wa asilimia 8 - 10. Hili litawezekana ikiwa Tanzania itajielekeza katika kuongeza uzalishaji na mauzo ya bidhaa zilizoongezewa thamani tofauti na uuzaji wa mazao ghafi. Ili kuongeza mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) umeweka msisitizo katika kujenga uchumi wa viwanda kwa lengo la kuchochea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu. Kufanikisha hilo jitihada za makusudi zinahitajika katika kujenga uwezo wa ndani wa uzalishaji sanjari na kuweka mazingira rafiki kwa uendeshaji biashara na uwekezaji ili kuvutia ushiriki wa sekta binafsi. Aidha, maendeleo ya viwanda yanayokusudiwa, pamoja na mambo mengine, hayana budi kujikita katika kutumia fursa asili (natural endowment) zilizopo nchini.

222. Sekta ya viwanda ni mhimili katika utoaji wa ajira zenye staha, kuongeza thamani ya bidhaa na kukuza uchumi. Hata hivyo, ukuaji wa sekta ya viwanda siyo wa kuridhisha kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo miundombinu isiyokidhi mahitaji hususan nishati ya umeme na ushindani usio wa usawa wa bidhaa kutoka nje. Kufuatia jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali hususan katika kuimarisha miundombinu na upatikanaji wa umeme wa uhakika, uwekezaji umeanza kuongezeka na hivyo kuongeza uzalishaji viwandani. Hata hivyo, ipo haja ya kuongeza na kuboresha kasi ya uwekezaji sanjari na kuhakikisha mwelekeo sahihi wa mageuzi tarajiwa, ambapo sekta binafsi inapewa hatamu za uendeshaji.

Hali ya Sekta ya Viwanda kwa Sasa

223. Tanzania ni moja ya nchi za Afrika zenye viwango vya juu vya ukuaji wa uchumi ambapo kwa kipindi cha muongo mmoja (2007 – 2016), uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 6.7. Katika kipindi hicho, sekta ya viwanda ilikua kwa wastani wa asilimia 7.5 na kuchangia wastani wa asilimia 6.5 katika Pato la Taifa. Hata hivyo, mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa ni

mdogo ikilinganishwa na lengo la asilimia 15 linalohitajika ili kuiwezesha Tanzania kuwa nchi ya viwanda. Sekta hii inaajiri wastani wa asilimia 3.1 ya nguvu kazi na kuna fursa za kuweza kuongeza ajira zenye staha, kupunguza umaskini, kuongeza mapato ya mauzo nje na kukuza uchumi. Mchango wa mapato ya mauzo ya bidhaa za viwandani nje uliongezeka kutoka asilimia 15.3 mwaka 2007 hadi asilimia 21.1 mwaka 2016. Kwa mujibu wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 ilionekana kuwa Tanzania ina viwanda vidogo, vya kati na vikubwa vinavyojihusisha na uzalishaji wa bidhaa vipatavyo 47,922 ambavyo viliajiri jumla ya watu 231,099.

224. Hadi kufikia Desemba 2016, jumla ya kampuni 140 zilikuwa zimepatiwa leseni za uanzishwaji wa viwanda katika ukanda wa mauzo nje (EPZ). Aidha, yapo maeneo maalum ya uwekezaji (SEZ) nane (8) yaliyotengwa kwa ajili ya viwanda na huduma za biashara na kwa sehemu kubwa yana miundombinu msingi. Katika kuhakikisha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji, mikoa yote Tanzania bara ilielekezwa kutenga maeneo kwa ajili hiyo na tayari mikoa tisa (9) imeshatekeleza agizo hilo. Vile vile, mwaka 2016, kituo cha uwekezaji kilisajili jumla ya miradi 178 ya uzalishaji viwandani.

Historia ya Mageuzi ya Viwanda Nchini

225. Ajenda ya kuendeleza viwanda nchini imeendelea kuwa ya kipaumbele katika mipango ya maendeleo ya Tanzania tangu uhuru. Hata hivyo, mfumo wa utekelezaji wa ajenda hii umekuwa ukibadilika kwa kuzingatia mabadiliko ya sera za kiuchumi na kijamii za kipindi husika. Zipo awamu kuu tano katika hatua za mageuzi ya viwanda nchini. Awamu ya kwanza ilikuwa kipindi cha baada ya uhuru (1961 – 1966) iliyolenga kuchakata mazao ghafi na kuanzisha viwanda vya kuzalisha bidhaa zilizokuwa zikihitajika na watawala na wakazi wachache wa mijini badala ya kuagiza kutoka nje, awamu ya pili ilikuwa kipindi cha Azimio la Arusha (1967 – 1975) ambayo ililenga kuongeza ushiriki wa wazawa katika umiliki wa nyenzo kuu na muhimu za uchumi chini ya Sera ya Ujamaa na Kujitegemea, awamu ya tatu ililenga kuanzisha mkakati mahsusi wa kuchochea mabadiliko mfumo wa uchumi na maendeleo ya viwanda (BIS, 1975-1995), awamu ya nne, ilikuwa kipindi cha kutekeleza sera za maboresho na mageuzi ya uchumi (Economic Recovery Programme - ERP I mwaka 1986 na ERP II mwaka 1989) na awamu ya tano ilihusisha kuchochea maendeleo endelevu ya viwanda.

226. Ubinafsishaji wa mashirika ya umma ilikuwa ni moja ya ajenda ya kuishirikisha sekta binafsi. Kufuatia utekelezaji wa sera ya ubinafsishaji iliyotekelezwa kuanzia katikati ya miaka ya 1990, Serikali ilibinafsisha jumla ya taasisi 337, na kati ya hizo, viwanda vilivyobinafsishwa vilikuwa 142. Kati ya hivyo, viwanda 34 vina ufanisi katika uzalishaji, vikiendeshwa kwa faida na kuchangia katika mapato ya kodi na viwanda 39 vimesimamisha uzalishaji. Tathmini iliyofanyika mwaka 2015/16 kwa viwanda 80 vilivyobinafsishwa inonesha kuwa viwanda 65 vinafanya kazi na viwanda 15 vimefungwa kutokana na sababu mbalimbali.

Umuhimu wa Uchumi wa Viwanda

227. Serikali ya awamu ya tano iliamua kuweka msisitizo wa kuendeleza sekta ya viwanda kutokana na sababu kuu nne zifuatazo:

a) Uwezo wa kuongeza ajira zenye staha

228. Inakadiriwa kuwa zaidi ya watanzania 800,000 wanaingia katika soko la ajira kila mwaka baada ya kuhitimu masomo, na wengi wao ni vijana. Hata hivyo, uwezo wa uchumi wa Tanzania ni kuajiri watu 40,000 tu kwa mwaka. Uchumi wa Tanzania hauna haujaweza kutoa fursa nyingi za ajira zenye staha. Kwa mujibu wa taarifa ya utafiti wa nguvukazi na ajira wa mwaka 2014, idadi ya watanzania wasiokuwa na ajira wenye umri wa miaka 15 na zaidi ni takribani milioni 2.3, sawa na asilimia 10.3 ya nguvukazi (watu wenye uwezo wa kufanya kazi). Theluthi mbili ya hao (karibia watu milioni 1.5) ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35. Hili ni kundi kubwa linalohitaji kuwezesha kiuchumi kwani liko katika mazingira hatarishi japo lina nguvu na ujuzi wa kutosha. Sekta ya viwanda ikiimarishwa inaweza kuwa mkombozi katika kutoa ajira zenye staha hususan kwa vijana.

b) Maendeleo Endelevu ya Uchumi

229. Tanzania ni moja ya nchi zilizojaliwa kuwa na rasilimali asili kama mafuta, gesi na madini. Kwa upande wa madini, hivi karibuni iligunduliwa gesi asilia yenye ujazo wa futi za mraba trilioni 57 (57 TCF) na kuna matarajio ya kugundua gesi zaidi kwani utafiti bado unaendelea sehemu mbalimbali nchini. Tofauti na viwanda, rasilimali asili zina tabia/sifa za kipekee ambazo pia zinahitaji usimamizi wa kipekee. Mojawapo ya sifa hizo ni kwamba upatikanaji wa rasilimali asili una ukomo. Hivyo, kama rasilimali hizo hazitatumika kwa namna ambayo ni endelevu, uchumi wa nchi unaweza kuporomoka mara upatikanaji wa rasilimali hizo utakapofikia ukomo. Aidha, iwapo mapato

yatokanayo na rasilimali hizo yatawekezwa kimkakati hususan katika ujenzi wa viwanda, yatawezesha kuongeza uzalishaji, ajira na mapato ya kigeni na hivyo kuwa na ukuaji endelevu wa uchumi hata pale rasilimali hizi zitakapofikia ukomo. Hivyo, ni muhimu kubadili mfumo wa uchumi unaotegemea rasilimali asili ambazo zina ukomo kwa kupanua wigo wa shughuli za kiuchumi ikiwemo kutumia fursa hiyo ya kuwa na rasilimali kuanzisha na kuendeleza viwanda.

c) Kupunguza Umaskini

230. Matokeo ya tafiti za hali ya kipato na matumizi katika kaya (Household Budget Survey – HBS) na utafiti wa nguvukazi na ajira (Integrated Labor Force Survey – ILFS) zilizofanyika kwa nyakati tofauti yalionesha kuwa watazania maskini wengi wanajishughulisha na shughuli za kilimo. Aidha, kufuatia juhudi zilizokuwa zikichukuliwa na Serikali katika harakati za kufanya mageuzi ya kiuchumi, kiwango cha umaskini kimekuwa kikipungua kadiri nguvukazi inavyopungua katika sekta ya kilimo. Vile vile, takriban asilimia 86.1 ya nguvukazi ilikuwa inajihusisha na kilimo mwaka 2000 ambako umaskini ulikuwa asilimia 35.6. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa nguvukazi na ajira, kiwango cha watazania wanaojihusisha na kilimo kilipungua kufikia asilimia 73.4 mwaka 2010 na kupungua zaidi hadi asilimia 66.3 mwaka 2014, ambapo umaskini ulipungua kutoka asilimia 34.4 (HBS 2007) hadi asilimia 28.2 (HBS 2012). Kutokana na mwenendo huo, ni dhahiri kuwa sera za kupunguza umaskini zililenga kupunguza nguvukazi iliyoko katika sekta ya kilimo kwenda kwenye viwanda na shughuli nyingine za kiuchumi nje ya kilimo. Hivyo, mageuzi ya viwanda ni nyenzo muhimu ya kupunguza umaskini endapo vitajengwa viwanda vya kuongeza thamani kwenye mazao ya kilimo.

d) Fursa za Kipekee kwa Tanzania

231. Tanzania imejaliwa kuwa na fursa za kipekee ambazo zikitumika kimkakati zinaweza kuwa chachu ya maendeleo ya viwanda na uchumi kwa ujumla. Moja ya fursa hizo ni wingi wa rasilimali asili kama vile ardhi yenye rutuba inayofaa kwa kilimo, misitu, gesi asilia, madini, pamoja na maziwa makubwa na bahari ambayo yanaweza kutumika kama vyanzo vya maji ya umwagiliaji na uvuvi. Fursa nyingine ni nafasi ya nchi kijiografia ambayo imezungukwa na nchi sita zisizokuwa na mlango bahari ambapo nchi hizo zinaweza kufikia masoko ya nje (kununua na kuuza bidhaa) kupitia Tanzania. Kutokana na fursa hizo, Serikali imedhamiria kujenga uchumi wa viwanda ili kuongeza mnyororo wa thamani na hivyo kupunguza au kuacha kabisa kuuza bidhaa zisizosindikwa na wakati huo huo kutumia nafasi yake ya kijiografia

kufikia masoko ya nje kwa bidhaa zilizozalishwa viwandani badala ya kuhudumia nchi majirani tu.

Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Viwanda

232. Kutokana na umuhimu wa sekta ya viwanda, Serikali ya awamu ya tano imeazimia kufanya mageuzi ya viwanda kwa lengo la kuinua uchumi wa Tanzania kwa kutumia fursa zilizopo. Serikali inatekeleza ajenda hii kupitia Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) wenye kaulimbiu ya *“Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu”*. Serikali kupitia Mpango huu inahamasisha ushiriki wa sekta binafsi kwa kuhakikisha uwepo wa mazingira rafiki ya uwekezaji ili waweze kuwekeza kwa faida, kustawi na kuimarika. Serikali imedhamiria kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na kutoa vivutio mbalimbali vya kodi na visivyo vya kodi ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi hususan katika kutumia kikamilifu fursa zilizopo nchini kuinua uchumi kupitia viwanda. Aidha, Mpango huu umeainisha maeneo manne ya utekezaji wa kimkakati ambayo yataweka msingi wa ujenzi wa uchumi wa viwanda utakaohanikiza ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Maeneo hayo ni:

- a. Ukuaji wa uchumi na maendeleo ya viwanda (mfano ujenzi wa maeneo maalum ya kiuchumi na kutenga maeneo ya viwanda);
- b. Kuchochea maendeleo ya watu na mageuzi ya kijamii (elimu, ujuzi maalum na huduma za afya);
- c. Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji (utulivu wa viashiria vya kiuchumi, amani, ulinzi na usalama, miundombinu na huduma bora, na gharama za kufanya biashara); na
- d. Kuimarisha usimamizi wa utekezaji wa Mpango (ugharamiaji, mfumo thabiti wa ufuatiliaji na tathmini) .

233. Msisitizo katika mkakati huu wa mageuzi ya viwanda ni kujenga viwanda vitakavyoweza kuongeza fursa za ajira, vitakavyotumia rasilimali zilizoko nchini (hususan za kilimo na madini), vitakavyoweza kuzalisha kukidhi mahitaji ya soko la ndani na ziada kwa ajili ya mauzo nje. Vile vile, Serikali inakamilisha Mkakati wa kuharakisha mageuzi ya viwanda (Strategy for Fast-Tracking Industrialization in Tanzania 2016 – 2020). Mkakati huu umeainisha maeneo mbalimbali ya kimkakati yatakayozingatiwa katika kufikia malengo makuu ya mageuzi ya viwanda ikiwemo kufufua viwanda vilivyobinafsishwa

ambavyo vimesimamisha uzalishaji na ujenzi wa viwanda vinavyotumia malighafi zilizoko nchini.

Uendelezaji wa Sekta na Maeneo Shirikishi

234. Mageuzi ya viwanda hayawezi kupatikana bila kuendeleza na kushirikisha sekta nyingine. Hivyo, ili kuweza kupiga hatua katika azma ya kuleta mageuzi katika uchumi wa viwanda, Serikali kupitia Mpango wa Pili wa Maendeleo imejielekeza katika kutekeleza yafuatayo:

- a. Kujenga misingi ya kilimo cha kisasa;
- b. Kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika;
- c. Kuimarisha miundombinu ya usafirishaji;
- d. Kuimarisha Viashiria vya Uchumi Mkuu;
- e. Kujenga mazingira wezeshi ikiwemo misingi ya kisheria na kikanuni na taasisi ili kuvutia wawekezaji; na
- f. Kuwekeza katika maendeleo ya watu.

235. Sekta ya **kilimo** ni kitovu cha maendeleo ya viwanda kwa kutoa masoko ya bidhaa za viwandani na malighafi za viwanda. Sekta ya kilimo inaajiri asilimia 66.3 ya watanzania, inachangia asilimia 29 ya Pato la Taifa, asilimia 30 ya mapato ya mauzo nje, na pia huchangia asilimia 65 ya malighafi za viwandani. Pamoja na mchango huo mkubwa, sekta hii imekuwa na maendeleo ya kutoridhisha na inaathiriwa na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, eneo linalotumika kwa ajili ya umwagiliaji Tanzania ni chini ya asilimia 10 ya eneo linaloweza kutumika kwa kilimo cha umwagiliaji. Serikali kupitia Mpango wa Pili wa Maendeleo imeainisha mpango mkakati wa kuimarisha kilimo cha umwagiliaji ikiwemo kuongeza uwekezaji kwenye miundombinu ya umwagiliaji. Vilevile, sehemu kubwa ya mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi ni ghafi kutokana na uwepo wa viwanda vichache vya kuongeza thamani. Hii ni miongoni mwa sababu za serikali kuweka mkakati wa kuanzisha viwanda vinavyotumia malighafi ya hapa nchini. Mikakati mingine iliyowekwa na serikali ni kuhamasisha kilimo cha kisasa na chenye tija kupitia uendelezaji wa Ukanda wa Ukuzaji Kilimo Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) ambao unalenga kuboresha kilimo cha kibiashara kwa kuanzisha mashamba makubwa na miradi endelevu ya kilimo.

236. Kwa upande wa upatikanaji wa umeme wa uhakika na wa gharama nafuu, jitihada kubwa zimeendelea kuchukuliwa na serikali ikiwemo kuimarisha

miundombinu ya ufuaji, usafirishaji na usambazaji. Changamoto kubwa iliyokuwepo ni gharama kubwa za ufuaji wa umeme wa nguvu za mafuta pamoja na kukatika kwa umeme kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kupungua kwa kina cha maji na uchakavu wa mitambo. Hata hivyo, kufuatia kugunduliwa kwa gesi asilia yenye ujazo wa futi za mraba trilioni 57, ni dhahiri kwamba upatikanaji wa umeme viwandani utaongezeka sambamba na kupungua kwa gharama zake. Aidha, Serikali inaendelea na mchakato wa ujenzi wa kiwanda cha kubadilisha gesi asilia iwe katika hali ya kimiminika (LNG plant) pamoja na miundombinu yake. Mchakato huu ukikamilika utaongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika utokanao na gesi asilia pamoja na kuongeza mauzo ya gesi (LNG) nje.

237. Miundombinu ya usafirishaji pia imeendelea kuimarishwa ikiwemo ujenzi na ukarabati wa barabara zinazofungua fursa za kiuchumi na zinazounganisha maeneo ya uzalishaji na masoko ya ndani na nchi jirani pamoja na ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa cha “standard gauge”. Aidha, serikali inaendelea na mkakati wa kuimarisha usafiri wa anga ambapo tayari imeshanunua ndege mpya mbili na kulipa malipo ya awali kwa ajili ya ndege nyingine nne. Hatua zote hizi zinalenga kurahisisha usafirishaji wa malighafi na bidhaa za viwandani.

238. Katika kuboresha **mazingira ya biashara** na uwekezaji, Serikali inaendelea na: jitihada za kuimarisha utulivu wa uchumi jumla; kuwa na sera za fedha na za bajeti zinazotabirika (zisizobadilika mara kwa mara); kuhakikisha nidhamu na uwazi katika taratibu za serikali; kuimarisha ulinzi na usalama; na kuhakikisha uwepo wa miundombinu imara (kama vile barabara, reli) na huduma bora zikiwemo umeme wa uhakika na mikopo kwa sekta binafsi. Katika eneo hili la kuboresha mazingira ya biashara, Tanzania ilifanya vizuri kulingana na taarifa ya Benki ya Dunia ya mwaka 2017 iliyoonesha kuwa Tanzania ilikuwa nchi ya 132 mwaka 2016 kwa urahisi wa kufanya biashara ikiwa imepiga hatua kwa nafasi 12 kutoka nafasi ya 144 mwaka 2015.

239. Maendeleo ya watu na maendeleo ya viwanda ni vitu ambavyo vinategemeana. Viwanda hutoa nafasi ya kipekee katika kusukuma maendeleo na kukuza ujuzi ambao unahitajika katika uendeshaji wa viwanda. Kwa upande mwingine, ujuzi husukuma maendeleo ya viwanda katika kuchochea ukuaji wa teknolojia. Hivyo, maendeleo ya rasilimali watu na kuinua kiwango cha ujuzi katika nchi ni muhimu sana kwa maendeleo ya viwanda. Rasilimali watu yenye

ujuzi wa juu ikiendana na nidhamu ya kazi inawezesha nchi kuharakisha mageuzi ya uchumi na hatimaye kuchochea mageuzi ya kijamii na maendeleo ya watu. Kwa upande wa elimu, msisitizo umewekwa kwenye ubora wa elimu inayolenga kukidhi mahitaji ya jamii sambamba na ushindani katika soko la ajira la ndani, kikanda na kimataifa. Elimu ya ujuzi maalum unaohitajika katika sekta mbalimbali pia imezingatiwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo. Vile vile, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za afya ili kuhakikisha watu wote wanakuwa na afya nzuri za kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na viwanda.

Ugharamiaji wa Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda

240. Utekelezaji madhubuti wa mpango wowote hutegemea uwezo wa kutafuta rasilimali fedha kutoka vyanzo vya ndani na nje pamoja na uwezo wa kuzitumia fedha hizo kwa ufanisi. Vyanzo vikuu vya mapato ya serikali ni pamoja na mapato ya ndani ya kodi na yasiyo ya kodi; mikopo yenye masharti ya kibiashara ya ndani na nje; na misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo. Aidha, soko la fedha la ndani halina uwezo wa kugharamia kikamilifu mahitaji ya soko na pia serikali ina ukomo wa kukopa katika soko la ndani. Misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo inazidi kupungua mwaka hadi mwaka na mikopo ya kibiashara kutoka nje ina masharti magumu ikiwemo riba kubwa, muda mfupi wa marejesho na baadhi ya mikopo kufungamanishwa na miradi (tied projects).

241. Kutokana na hali hiyo, Serikali imeweka nguvu zaidi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani; kuimarisha soko la fedha la ndani ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa benki mahsusi ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Kilimo na Benki ya Maendeleo ya TIB; na kuboresha mazingira ya biashara ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi hususan katika ugharamiaji wa mpango wa pili wa maendeleo. Ugharamiaji wa Mpango kupitia ushiriki wa sekta binafsi ni wa muhimu kwa kuwa uchumi wa viwanda hautaweza kujengwa kwa kutegemea bajeti ya serikali pekee. Hivyo, Serikali inaendelea kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi kwa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Vile vile, katika kupunguza utegemezi wa bajeti katika kugharamia miradi ya maendeleo, Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi. Aidha, Serikali inakamilisha mkakati wa ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo ambao utainisha vyanzo mbalimbali vya mapato ya kugharamia Mpango ambao unajumuisha uendelezaji wa viwanda.

Hatua ya Utekelezaji Iliyofikiwa

242. Katika kutekeleza azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda, miradi ya viwanda mbalimbali imeanzishwa kutokana na mchango wa Serikali na sekta binafsi. Aidha, mkoa wa Pwani unaongoza, ukiwa na jumla ya miradi mipya ya viwanda 82 iliyoanzishwa na sekta binafsi. Serikali imekuwa na mchango mkubwa katika uanzishwaji wa miradi hiyo, ikiwa ni pamoja na kusaidia upatikanaji wa ardhi, kuweka miundombinu inayohitajika, na kutoa vibali vya ujenzi.

243. Serikali kupitia mashirika yake imeanza kuwekeza katika ujenzi wa viwanda ambapo mifuko ya hifadhi ya jamii ikiwemo PPF na NSSF inashirikiana kuwekeza katika kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari katika eneo la Mkulazi na Mbigiri (Morogoro); LAPF wanajenga machinjio ya kisasa ya nyama (kwa Makunganya – Morogoro); na mifuko mingine inashiriki katika miradi mbalimbali. Vile vile, Shirika la Taifa la Maendeleo linashirikiana na sekta binafsi kuwekeza katika eneo la viwanda la TAMCO – Kibaha kwa lengo la kuendeleza viwanda vya nguo na uunganishaji wa magari pamoja na matrekta, ambapo kiwanda cha kuunganisha matrekta kimefikia hatua ya kuanza majaribio.

244. Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuimarisha na kuboresha miundombinu na huduma za uchumi wa viwanda. Miongoni mwa miradi hii ni: ujenzi wa msingi kwa ajili ya mtambo wa kufua umeme wa Kinyerezi II (MW 240); ukarabati wa njia ya reli ya kati na kuanza kwa taratibu za ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge); ununuzi wa ndege; ujenzi na ukarabati wa barabara zikiwemo barabara za juu za TAZARA na Ubungo.

245. Kwa upande wa kufungamanisha ukuaji wa viwanda na maendeleo ya watu, Serikali inaendelea kutekeleza sera ya elimu msingi bila malipo, kuboresha miundombinu na huduma za ufundishaji na kufundishia, ujenzi wa mabweni katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; na kutoa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Aidha, Serikali imekamilisha ujenzi wa Hospitali ya Taaluma na Tiba ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Kampasi ya Mloganzila.

Hitimisho

246. Serikali ya awamu ya tano imedhamiria kuleta mageuzi ya uchumi wa viwanda kufikia nchi ya kipato cha kati kwa kuendeleza viwanda vyenye kutoa fursa za ajira na kuimarisha tija katika kilimo. Ili kufikia malengo hayo, serikali itaendelea kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu muhimu, kuhakikisha uwepo wa mazingira tulivu ya uwekezaji, usimamizi wa sheria, kanuni na taratibu za nchi pamoja na kushirikisha sekta binafsi katika mageuzi ya viwanda.

SEHEMU YA NNE

MAENDELEO KATIKA SEKTA MBALIMBALI

SURA YA 11 KILIMO NA USHIRIKA

Kiwango cha Ukuaji

247. Mwaka 2016, kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi za kilimo kilipungua na kuwa asilimia 2.1 ikilinganishwa na asilimia 2.3 mwaka 2015. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kulitokana na kutokuwa na mvua za kutosha na za wakati katika msimu wa kilimo wa mwaka 2015/16. Hali hiyo iliathiri uzalishaji wa mazao na pia upatikanaji wa maji na malisho ya kutosha kwa ajili ya mifugo. Shughuli ndogo za uzalishaji mazao ndizo zilizoathirika zaidi ambapo kiwango cha ukuaji kilipungua na kuwa asilimia 1.4 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 2.2 mwaka 2015. Hata hivyo, shughuli nyingine ndogo za kilimo zilikuwa na ongezeko la ukuaji kama ifuatavyo: uvuvi; misitu na uwindaji; na mifugo zilikuwa kwa asilimia 4.2; 3.4; na 2.6 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 2.5; 2.6; na 2.4 mwaka 2015 kwa mtiririko huo. Shughuli za kiuchumi za kilimo zilichangia asilimia 29.1 ya Pato la Taifa mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 29.0 mwaka 2015.

Uzalishaji wa Mazao ya Chakula

248. Mwaka 2016, uzalishaji wa mazao makuu ya chakula hususan mahindi, mchele, muhogo, maharage na mazao mengine ya jamii ya kunde uliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2015. Ongezeko hili lilitokana na kuwepo kwa hali nzuri ya hewa katika maeneo yanayozalisha mazao hayo. Mwenendo wa uzalishaji wa mazao ya chakula ni kama unavyoonekana katika Jedwali Na. 11.1.

Jedwali Na. 11.1: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula (Tani 000)

Zao	2011	2012	2013	2014	2015	2016	Badiliko (%) 2015/16
Mahindi	4341	5104	5174	6734	5903	6149	4.2
Mchele	1461	1170	1307	1681	1937	2229	15.1
Ngano	113	109	92	167	72	76	5.4
Mtama/Ulezi	1119	1052	1041	1246	1007	1003	-0.4
Mihogo	1549	1821	1943	1664	1962	2205	12.4
Maharage/Mikunde	1632	1827	1641	1697	1808	1959	8.3
Ndizi	1048	842	1307	1064	1195	1061	-11.2
Viazi vitamu	1710	1418	1259	1167	1090	1044	-4.2

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi

Uzalishaji wa Mazao ya Biashara

249. Mwaka 2016, uzalishaji wa kahawa na mkonge uliongezeka kwa asilimia 48.3 na asilimia 9.2 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 0.8 na asilimia 21.9 kwa mtiririko huo mwaka 2015. Kuongezeka kwa uzalishaji wa kahawa kulitokana na kuwa ni msimu wa mzunguko wa juu wa uzalishaji na pia kulikuwa na hali nzuri ya hewa kwenye maeneo yanayozalisha kahawa kwa wingi. Kwa upande mwingine, ongezeko la uzalishaji wa mkonge lilitokana na kuendelea kuongezeka kwa mahitaji ya singa za mkonge na hivyo kusababisha bei kupanda na kuvutia uzalishaji zaidi. Hata hivyo, uzalishaji wa mazao ya pamba, tumbaku, sukari, chai, pareto na korosho ulishuka mwaka 2016 ikilinganishwa na mwaka 2015. Kushuka huko kulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo: upungufu wa mvua za kutosha katika maeneo yanayozalisha mazao hayo; na baadhi ya wakulima kuacha kulima mazao hayo kutokana na kushuka kwa bei ya mazao hayo katika soko la dunia. Jedwali Na. 11.2 linaonesha hali ya uzalishaji wa mazao ya biashara kwa kipindi cha mwaka 2009 – 2016.

Jedwali Na. 11.2: Uzalishaji wa Mazao ya Biashara (Tani)

Zao	2011	2012	2013	2014	2015	2016	Badiliko (%) 2015/16
Pamba	225938	225938	357130	246767	203312	149455	-25.8
Tumbaku	126624	126624	86359	100000	87737	60691	-30.8
Sukari	260055	262880	296697	294421	304007	293075	-3.6
Chai	33000	32810	33700	33000	35750	32629	-8.7
Pareto	5700	5700	6100	7090	6050	2011	-66.6
Kahawa	33219	33219	71200	47301	41674	60921	48.3
Mkonge	33406	25690	34875	37571	39204	42314	9.2
Korosho	160000	160000	127947	123449	197933	155416	-21.5

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi

Uzalishaji wa Mazao ya Mafuta

250. Mwaka 2016, uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta ukijumuisha alizeti, karanga, ufuta, mawese na soya uliongezeka hadi tani 6,301,147 ikilinganishwa na tani 5,936,527 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 6.1. Ongezeko hilo lilitokana na uwepo wa soko la uhakika, ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji katika viwanda vidogo na vya kati na hivyo kuongeza hamasa kwa wakulima kuongeza uzalishaji. Jedwali Na.11.3 linaonesha uzalishaji wa mazao hayo katika kipindi cha mwaka 2010 - 2016.

Jedwali Na. 11.3: Uzalishaji wa Mazao ya Mafuta (Tani)

Zao	2011	2012	2013	2014	2015	2016	Badiliko (%) 2015/16
Alizeti	786902	1125000	2625000	2755000	2878500	2995500	4.1
Karanga	651397	810000	1425000	1635735	1835933	2025595	10.3
Ufuta	357162	456000	1050000	1113892	1174589	1232092	4.9
Mawese	17000	24880	40500	41000	41475	41925	1.1
Soya	2500	5620	5830	6025	6030	6035	0.1

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi

Uzalishaji wa Mazao ya Bustani

251. Mwaka 2016, uzalishaji wa mazao ya bustani ya matunda, mboga, maua na viungo ulikuwa tani 5,931,900 ikilinganishwa na tani 5,635,364 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 5.3. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa usindikaji wa mazao haya pamoja na hamasa ya ulaji wa matunda na mboga kwa wingi. Jedwali Na. 11.4 linaonesha mwenendo wa uzalishaji wa mazao bustani katika kipindi cha mwaka 2012 – 2016.

Jedwali Na.11. 4: Uzalishaji wa mazao ya Bustani (Tani)

Zao	2012	2013	2014	2015	2016	Badiliko (%) 2015/16
Matunda	3938730	4096280	4416690	4574240	4711000	3.0
Mboga	901680	937750	1005305	1041375	1189000	14.2
Maua	9850	10200	10790	11140	11500	3.2
Viungo	7370	8125	8377	8609	20400	137.0

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi

Uwekezaji katika Shughuli za Kiuchumi za Kilimo

252. Mwaka 2016, sekta binafsi ilinunua matrekta makubwa mapya 900 na madogo 260 kutoka nje ikilinganishwa na matrekta makubwa 939 na madogo 354 mwaka 2015. Katika kipindi hicho, zana za kilimo zenye thamani ya shilingi bilioni 3.1 zilikopeshwa kwa wakulima katika sehemu mbali mbali nchini. Zana hizo ni: matrekta makubwa 66, matrekta madogo ya mkono mawili (2), zana za umwagiliaji tano (5) na mashine ya kuvuna mpunga (combine harvester) moja (1). Vile vile, mwaka 2016, Serikali kupitia Mradi wa Sera ya Maendeleo ya

Rasilimali Watu ilinunua na kusambaza mashine za kukoboa mpunga katika skimu zilizo ndani ya Mradi huo. Kati ya skimu 14 zilizolengwa, skimu tisa (9) zilifungiwa mashine hizo kwa kuwa zilikamilisha ujenzi wa jengo na kuweka umeme.

Huduma za Ugani

253. Mwaka 2016, wakulima wawezeshaji 100 na maafisa ugani 20 walipata mafunzo ya uzalishaji wa mpunga kwa kutumia teknolojia ya kilimo shadidi. Aidha, katika kuimarisha taaluma ya ugani, Serikali ilifadhili na kufundisha wanafunzi 2,000 katika mafunzo ya kilimo ngazi ya astashahada na stashahada katika vyuo mbalimbali nchini ikilinganishwa na wanafunzi 3,047 mwaka 2015. Kozi wanazosomea ni; kilimo, umwagiliaji, matumizi bora ya ardhi, uzalishaji chakula na lishe, matumizi ya zana katika kilimo, uzalishaji wa mazao, mboga, maua na matunda.

Utafiti

254. Mwaka 2016, aina 29 za mbegu bora zilizalishwa katika vituo vya utafiti vya umma na binafsi. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya tani 8.2 za mbegu mama za mazao mbalimbali pamoja na vipando/vikonyo mama 919,700 vya mazao ya muhogo na viazi vitamu zilizalishwa. Vile vile, sampuli 7,313 za udongo kutoka kanda za mashariki, kaskazini na kanda ya ziwa zilipimwa na kuainisha virutubisho vilivyomo. Matokeo ya tathmini hiyo yatasaidia kuainisha maeneo na aina ya mazao yanayofaa kwa uwekezaji katika kilimo pamoja na kuandaa ramani za aina mbalimbali za udongo na kutoa ushauri kwa wakulima.

Mwenendo wa bei na Masoko ya Mazao ya Kilimo

255. Serikali kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko iliendelea kuimarisha soko la mazao ya kilimo ili kuwanufaisha wakulima wadogo. Mwaka 2016 Bodi ilinunua tani 3,300.04 za mahindi kutoka kwa wakulima wa mikoa ya Iringa, Njombe na Ruvuma. Aidha, Bodi iliongeza thamani ya mazao kwa kusaga tani 1,047.8 za mahindi na kuzalisha tani 896.8 za unga na tani 145.2 za pumba.

256. Mwaka 2016, wastani wa bei ya sukari kiwandani ulikuwa kati ya shilingi 1,850 na 1,920 kwa kilo. Aidha, wastani wa bei ya jumla kwa wafanyabiashara ilikuwa kati ya shilingi 2,050 na 2,117 kwa kilo na bei ya rejareja ni kati ya shilingi 2,250 na 2,400 kwa kilo katika maeneo mengi ya makao makuu ya miji ya mikoa na wilaya. Hata hivyo, katika mikoa ya

pembezeni bei ya rejareja ilifikia hadi wastani wa shilingi 2,500 kwa kilo. Bei ya pamba nyuzi katika soko la dunia ilipungua kufikia shilingi 932 kwa kilo mwaka 2015/16 ikilinganishwa na shilingi 1,010 mwaka 2014/15. Aidha, bei ya pamba nyuzi katika soko la ndani iliongezeka kwa asilimia 20 kutoka wastani wa shilingi 833.3 kwa kilo mwaka 2014/15 hadi kufikia shilingi 1,000 kwa kilo mwaka 2015/16 kutokana na kuongezeka kwa mahitaji katika soko la ndani.

257. Mwaka 2016, bei ya kahawa ilipanda kwa asilimia 26.2 kwa kahawa ya arabika laini na asilimia 7.8 kwa kahawa ya robusta katika soko la mnada la ndani pia ilipanda kwa wastani wa asilimia 12.2 kwa kahawa ya arabika laini na asilimia 8.4 kwa kahawa ya robusta katika soko la moja kwa moja. Hali hii ilisababisha kuongezeka kwa bei ya mkulima kutoka shilingi 2,500 hadi shilingi 4,700 kwa kilo (Ongezeko la asilimia 88) kwa kahawa ya arabika na shilingi 1,100 hadi shilingi 1,400 kwa kilo (ongezeko la asilimia 27.2) kwa kahawa ya robusta.

Ruzuku ya Pembejeo

258. Mwaka 2016, Serikali iliendelea na utaratibu wa kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa kutumia vocha zikiwemo mbolea na mbegu bora za mahindi na mpunga. Jumla ya kaya 999,926 za wakulima zilinufaika kwa kupata tani 99,993 za mbolea na tani 10,270.86 za mbegu bora za mahindi na mpunga. Matumizi ya pembejeo yamechangia kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao ya mahindi na mpunga ambapo uzalishaji wa mahindi uliongezeka kutoka wastani wa gunia tano (5) hadi wastani wa gunia 15 kwa ekari na mpunga kutoka wastani wa gunia nne (4) hadi wastani wa gunia 20 kwa ekari. Aidha, jumla ya miche bora 2,106,510 ya kahawa na miche bora 1,600,000 ya korosho ilizalishwa kutokana na mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo. Vile vile, viuatilifu tani 8,011 na ekapaki 1,244,075 kwa zao la korosho na kahawa zilitolewa kwa wakulima kwa utaratibu wa ruzuku.

Mfuko wa Pembejeo

259. Mwaka 2015/16, Mfuko wa Pembejeo ulitoa mikopo 65 ya matrekta makubwa ikilinganishwa na matrekta 74 mwaka 2014/15, sawa na upungufu wa asilimia 12.2. Vilevile, mikopo 30 ilitolewa kwa ajili ya pembejeo mchanganyiko zikiwemo mbolea za viwandani, mbegu bora na madawa ya mifugo ikilinganishwa na mikopo 32 iliyotolewa mwaka 2014/15, sawa na upungufu wa asilimia 6.3. Mfuko ulitoa mikopo 6 ya zana za umwagiliaji ikilinganishwa na mikopo 5 mwaka 2014/15. Aidha, Mfuko ulitoa mikopo

mmoja wa mashine ya kuvuna na mmoja wa ununuzi wa vifaa vya ukarabati wa trekta mwaka 2015/16.

Maendeleo ya Ushirika

260. Mwaka 2016, idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika iliongezeka na kufikia 2,234,016 kutoka 1,432,978 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 55.9. Ongezeko hilo lilitokana na uhamasishaji wananchi kuanzisha na kujiunga na vyama vya ushirika. Kutokana na uhamasishaji huo, vyama vipya 161 vilianzishwa na hivyo kufikia jumla ya vyama vya ushirika 10,522. Vyama vipya vilivyoanzishwa vinajumuisha vyama 125 vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS), vyama 29 vya Ushirika wa Masoko ya Mazao ya Kilimo na vyama vingine saba (7) vya ushirika.

261. Mwaka 2016, Ushirika wa Akiba na Mikopo uliendelea kutoa huduma za kifedha ambapo thamani ya hisa, akiba na amana ziliongezeka kwa asilimia 0.2 kutoka shilingi bilioni 377.67 mwaka 2015 na kufikia shilingi bilioni 378.34. Aidha, thamani ya mikopo iliyotolewa kwa wanachama kwa mwaka 2016 ilikuwa shilingi bilioni 854.34 kama ilivyokuwa mwaka 2015. Vile vile, mikopo iliyotolewa kwa wanachama na wananchi kwa ujumla kupitia benki za ushirika ilikuwa shilingi bilioni 6.4 kama ilivyokuwa mwaka 2015.

262. Mwaka 2016, Vyama vya Ushirika wa Mazao – AMCOS viliendelea kutoa huduma za ugani, usambazaji wa pembejeo, ukusanyaji na uuzaji wa mazao ya wakulima. Kufuatia matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani, bei ya korosho ilipanda kutoka wastani wa shilingi 1,800 msimu wa mwaka 2015/16, hadi kufikia shilingi 4,000 kwa kilo msimu wa mwaka 2016/17. Mfumo huo umesaidia kupanda kwa bei ya korosho katika mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani. Kwa upande mwingine, uzalishaji wa maziwa katika vyama vya ushirika wa wafugaji ulipungua kutoka lita milioni 12.2 mwaka 2015 hadi lita milioni 11.9 mwaka 2016, sawa upungufu wa asilimia 2.1 uliotokana na uhaba wa malisho. Hata hivyo, bei ya maziwa iliendelea kuwa ya wastani wa shilingi 1,000 kwa lita

MIFUGO

Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake

263. Mwaka 2016, idadi ya mifugo ilifikia ng'ombe milioni 25.8, mbuzi milioni 17.1 na kondoo milioni 9.2 ikilinganishwa na ng'ombe milioni 22.8, mbuzi milioni 15.6 na kondoo milioni 7.0 mwaka 2015. Aidha, mwaka 2016 kulikuwa na kuku wa asili milioni 42.0 na wa kisasa milioni 34.5 na nguruwe

milioni 2.67 ikilinganishwa na kuku wa asili milioni 37.4 na nguruwe milioni 2.01 mwaka 2015.

264. Mwaka 2016, uzalishaji wa nyama uliongezeka kutoka tani 597,757 mwaka 2015 hadi tani 648,810, sawa na ongezeko la asilimia 8.5. Kati ya hizo, uzalishaji wa nyama ya ng'ombe ulikuwa tani 323,775, mbuzi na kondoo tani 129,292, kuku tani 104,292 na nguruwe tani 91,451, ikilinganishwa na ng'ombe tani 319,112; mbuzi/kondoo tani 124,745; kuku tani 99,540 na nguruwe tani 54,360 mwaka 2015. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyama katika soko maalum la ndani hususan migodi, maduka makubwa na hoteli za kitalii. Kwa upande wa mauzo ya nyama nje, jumla ya tani 23.4 za nyama ya ng'ombe; tani 1,388.9 za nyama ya mbuzi na tani 36.7 za nyama ya kondoo zenye thamani ya shilingi bilioni 52.1 ziliuzwa katika nchi za Msumbiji, Vietnam, Oman, Qatar na Falme za Kiarabu. Aidha, jumla ya tani 735 za nyama ya ng'ombe, tani 804 za nyama ya nguruwe na tani 16.5 za nyama ya kondoo ziliingizwa nchini.

265. Uzalishaji wa maziwa nchini uliongezeka kwa asilimia 3.4 kutoka lita bilioni 2.058 mwaka 2015 hadi lita bilioni 2.127 mwaka 2016. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa ukusanyaji wa maziwa kutoka kwenye kundi la ng'ombe wa asili. Kati ya kiasi kilichozalishwa, lita milioni 704 zilitokana na ng'ombe wa kisasa na lita milioni 1,423.3 kwa ng'ombe wa asili. Usindikaji wa maziwa kwa siku uliongezeka kwa asilimia 19.9. kutoka lita 139,800 kwa siku mwaka 2015 na kufikia lita 167,620 kwa siku mwaka 2016. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa idadi ya viwanda vya kusindika maziwa kutoka 74 mwaka 2015 na kufikia 82 mwaka 2016. Pamoja na kuongezeka kwa usindikaji, viwanda vilivyoko bado havijaweza kutumika kikamilifu kwani kiasi kilichosindikwa ni asilimia 26.2 tu ya uwezo wa viwanda hivyo ambavyo kwa pamoja vina uwezo wa kusindika lita 640,800 kwa siku.

Jedwali Na. 11.5: Uzalishaji wa Mazao yatokanayo na Mifugo

Aina ya Zao	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016
Uzalishaji wa Maziwa ('000' lita)							
Ng'ombe wa Asili	997,261	1,135,422	1,255,938	1,297,775	1,339,613	1,381,451	1,423,288
Ng'ombe wa Kisasa	652,596	608,800	597,161	623,865	650,570	677,275	703,979
Jumla	1,649,857	1,744,222	1,853,099	1,921,640	1,990,183	2,058,726	2,127,267
Uzalishaji wa Nyama (Tani)							
Ng'ombe	243,943	262,606	289,835	299,581	309,086	319,112	323,775
Mbuzi/Kondoo	86,634	103,709	111,106	115,652	120,199	124,745	129,292
Nguruwe	38,180	43,647	47,246	50,814	74,174	54,360	91,451
Kuku	80,916	93,534	84,524	87,408	95,292	99,540	104,292
Jumla	449,673	503,496	532,711	553,455	598,751	597,757	648,810
Uzalishaji wa Mayai ('000')							
Mayai	2,917,875	3,339,566	3,494,584	3,725,200	3,899,569	4,153,800	4,353,182

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi

266. Mwaka 2016, uzalishaji wa mayai uliongezeka hadi mayai bilioni 4.35 kutoka mayai bilioni 4.15 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 4.8. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa mahitaji ya ulaji wa mayai. Aidha, uzalishaji wa vifaranga wa mayai na wa nyama uliongezeka kutoka vifaranga milioni 63.6 vilivyozalishwa mwaka 2015 na kufikia vifaranga milioni 68.28 mwaka 2016.

267. Kiwango cha ulaji wa mazao ya mifugo kulingana na viwango vya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO, 2011) ni kilo 50 za nyama, lita 200 za maziwa na mayai 300 kwa mtu mmoja kwa mwaka. Kwa upande wa Tanzania, viwango vya ulaji wa mazao hayo haujafikia hata nusu ya viwango hivyo vilivyopendekezwa, vikiwa na wastani wa kilo 15 za nyama, lita 47 za maziwa na mayai 106 kwa mtu kwa mwaka.

Uzalishaji na Usindikaji wa Malisho ya Mifugo

268. Mwaka 2016, tani 49.96 za mbegu bora za aina mbalimbali za malisho zilizalishwa ikilinganishwa na tani 48.5 za mbegu zilizozalishwa mwaka 2015. Aidha, jumla ya marobota 1,140,266 ya majani ya hei yalizalishwa mwaka 2016 ikilinganishwa na marobota 1,098,311 yaliyozalishwa mwaka 2015. Kati ya kiasi hicho, marobota 456,016 yalizalishwa katika mashamba ya Serikali na

marobota 684,250 yalizalishwa katika mashamba ya sekta binafsi na kuuzwa kwa wafugaji wadogo. Kuongezeka kwa uzalishaji kulitokana na uboreshaji wa miundombinu ya mashamba ya Serikali na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa malisho na mbegu bora za malisho kama shughuli za kibiashara.

269. Mwaka 2016, Serikali iliendelea kuratibu usindikaji na kusimamia ubora wa vyakula vya mifugo vinavyozalishwa na sekta binafsi ambayo imezalisha jumla ya tani 1,903 za vyakula vya mifugo ikilinganishwa na tani 1,200 zilizozalishwa mwaka 2015. Ongezeko hili la usindikaji wa vyakula limetokana na kuongezeka kwa viwanda vya usindikaji kutoka viwanda 65 mwaka 2015 hadi viwanda 80 mwaka 2016, sambamba na mahitaji ya vyakula vya mifugo. Aidha, jumla ya ng'ombe 213,000 walinenepeshwa mwaka 2016 ikilinganishwa na ng'ombe 175,000 mwaka 2015.

Biashara ya Mifugo na Mazao Yake

270. Mwaka 2016, Serikali iliendelea kuratibu biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi. Katika kipindi hicho, jumla ya ng'ombe hai 1,337,095; mbuzi 1,056,218 na kondoo 230,221 wenye thamani ya shilingi bilioni 1,027.4 waliuzwa katika minada ya ndani ikilinganishwa na ng'ombe hai 1,215,541, mbuzi 960,199 na kondoo 209,292 wenye thamani ya shilingi bilioni 989.3 waliouzwa mwaka 2015. Aidha, idadi ya mifugo hai iliyouzwa nje ya nchi iliongezeka kutoka ng'ombe 1,123 mwaka 2015, hadi ng'ombe 2,139 wenye thamani ya shilingi bilioni 34 mwaka 2016. Ongezeko la biashara ya mifugo hai ndani na nje ya nchi lilitokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya masoko ikiwemo kukarabati na kusimika mizani katika minada, hususan katika minada ya upili na ya mipakani.

271. Mwaka 2016, ngozi za ng'ombe zilizosindikwa ziliongezeka kufikia vipande 1,575,139 kutoka vipande 1,388,139 mwaka 2015 na vipande vya ngozi ya mbuzi na kondoo viliongezeka kutoka vipande 1,020,000 mwaka 2015 hadi kufikia vipande 1,124,000 mwaka 2016. Thamani ya vipande vyote (vya ng'ombe, mbuzi na kondoo) kwa mwaka 2016 ilikuwa shilingi bilioni 52.5. Ongezeko hili lilitokana na ukuaji wa usindikaji katika kiwanda cha SAK International Ltd – Arusha na kuanza usindikaji katika viwanda vipya vya ngozi vya Meru Tannery-Arusha na Xing Hua Investment Tannery-Shinyanga.

Jedwali Na. 11.6: Ukusanyaji na Uuzaji wa Ngozi Ndani na Nje ya Nchi

A. UKUSANYAJI WA NGOZI			
Mwaka	Ngozi za Ng'ombe	Ngozi za Mbuzi/Kondoo	Thamani Shilingi. '000'
2002	1,400,000	1,050,000	4,500,000
2003	1,400,000	1,260,000	5,500,000
2004	1,600,000	1,850,000	6,500,000
2005	1,600,000	2,250,160	5,500,000
2006	1,660,000	2,350,000	6,800,000
2007	1,980,000	2,720,000	8,700,000
2008	2,500,000	3,400,000	13,500,000
2009	1,650,000	4,240,000	10,900,000
2010	1,500,000	3,050,000	8,500,000
2011	2,500,000	2,600,000	16,100,000
2012	2,800,000	4,050,000	32,988,000
2013	2,900,000	4,300,000	34,673,500
2014	3,100,000	3,350,000	32,000,000
2015	4,050,000	4,640,000	85,165,000
2016	4,620,000	4,220,000	22,962,000
B. UZAJI NGOZI NJE			
Mwaka	Ngozi za Ng'ombe	Ngozi za Mbuzi/Kondoo	Thamani Sh. '000
2002	1,200,000	676,700	4,000,000
2003	1,300,000	900,000	4,600,000
2004	1,774,000	1,919,000	5,712,000
2005	1,400,000	1,797,155	4,025,400
2006	1,363,721	2,078,510	7,500,000
2007	1,700,000	1,980,530	16,200,000
2008	2,300,000	2,700,000	21,500,000
2009	982,668	3,469,936	12,800,000
2010	739,315	2,088,582	8,191,803
2011	1,719,506	1,561,000	17,400,000
2012	2,000,000	3,600,000	17,500,000
2013	1,269,060	2,582,525	63,600,000
2014	1,263,472	2,716,436	76,300,000
2015	1,388,139	1,020,000	39,200,000
2016	1,575,139	1,124,000	52,500,000

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi

Jedwali Na. 11.7: Mwenendo wa Mauzo ya Ngozi Nje 2007 – 2016

Mwaka	Ngozi ghafi		Ngozi zilizoongezwa thamani		Jumla ya Thamani (Shilingi milioni)	Ngozi zilizoongezwa thamani (%)
	Kiasi kg ('000')	Thamani (Shilingi Milioni.)	Kiasi kg ('000')	Thamani (Shilingi Milioni.)		
2007	10,569	8,571	5,566	16,036	24,607	65.2
2008	5,482	5,107	6,749	12,093	17,200	70.3
2009	1,666	1,433	5,026	6,797	8,230	82.6
2010	3,241	2,438	7,217	8,672	11,110	78.1
2011	8,141	6,831	7,904	17,005	23,836	71.3
2012	2,887	3,445	5,011	17,375	20,820	83.5
2013	2	3	7,061	22,686	22,689	99.9
2014	1,559	2,231	11,186	33,372	35,603	93.7
2015	372	1,185	6,594	20,878	22,063	94.6
2016	1,758	2,397	2,592	5,097	7,494	68.0

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania, 2016

Maendeleo ya Ushirika

272. Mwaka 2016, Serikali ilieendelea kuimarisha ushirika katika sekta mbalimbali zikiwemo kilimo, ufugaji, uvuvi, madini, viwanda, nyumba na ushirika wa kifedha yaani ushirika wa akiba na mikopo (SACCOS) na benki za ushirika. Aidha, ushirika wa akiba na mikopo uliendelea kutoa huduma za kifedha ambapo thamani ya hisa, akiba na amana ziliongezeka hadi shilingi bilioni 378.34 kutoka shilingi bilioni 377.67 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 0.18. Vile vile, thamani ya mikopo iliyotolewa kwa wanachama kwa mwaka 2016 iliongezeka kidogo kufika shilingi bilioni 854.40 kutoka shilingi bilioni 854.34 mwaka 2015.

273. Mwaka 2016, idadi ya wanachama iliongezeka kufikia 2,234,016 kutoka 1,432,978 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 55.9. Aidha, jumla vyama vya ushirika 161 vilianzishwa ambavyo vinajumuisha vyama 125 vya ushirika wa akiba na mikopo, 29 vyama vya ushirika wa mazao (AMCOS) na 7 vya ushirika wa aina nyingine na kufanya jumla ya vyama vya ushirika kufikia 10,522 mwaka 2016. Huduma za fedha kupitia benki za ushirika ambapo mikopo hutolewa kwa wanachama na wananchi ilikuwa shilingi bilioni 6.3

mwaka 2016 ikilinganishwa na shilingi bilioni 6.4 mwaka 2015. Mikopo hiyo ilitumika kuendeleza uwekezaji hususan katika sekta ya kilimo, uvuvi, ufugaji, biashara pamoja na shughuli za maendeleo ya kijamii.

274. Mwaka 2016, vyama vya ushirika wa mazao viliendelea kutoa huduma za ugani, usambazaji wa pembejeo, ukusanyaji na uuzaji wa mazao ya wakulima. Aidha, uzalishaji wa maziwa katika vyama vya ushirika wa wafugaji ulipungua kutoka lita milioni 12.15 mwaka 2015 hadi lita milioni 11.89, sawa na upungufu wa asilimia 2.1. Aidha, katika kipindi hicho, bei ya maziwa iliendelea kuwa ya wastani wa shilingi 1,000 kwa lita moja ya maziwa.

275. Mwaka 2016, wananchi kupitia vyama vya ushirika waliendelea kuhamasishwa kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kupitia “Wakulima Scheme”. Jumla ya wanachama 90,047 walijiunga na mfuko wa NSSF kutoka wanachama 78,747 mwaka 2015.

UZALISHAJI WA MIWA NA SUKARI NCHINI

Jedwali Na. 35

Msimu ¹	Miwa				Sukari		
	Wakulima		Jumla (000 Tani)	Bei ² (Sh./Tani)	Iliyozalishwa Tani	iliyotumika ³	
	Umma (000 Tani)	Binafsi (000 Tani)				Jumla Tani	Kilo kwa kila mtu ⁴
1990/91	1068	116	1184	2525.90	118560	212585	5.93
1991/92	967	114	1081	3476.85	108480	202478	6.07
1992/93	1098	273	1371	5267.67	121414	204126	6.11
1993/94	1105	362	1467	6200.00	123949	139829	5.38
1994/95	914	370	1284	8600.00	104624	238424	5.38
1995/96	997	372	1369	8900.00	116810	268910	..
1996/97	951	347	1298	9500.00	116100	275700	5.54
1997/98	808	176	984	10500.00	116100	271790	5.70
1998/99	948	320	1268	12500.00	113622	101272	5.87
1999/00	907	341	1248	12500.00	116927	100127	6.70
2000/01	1050	284	1334	14000.00	135534	122534	10.00
2001/02	1134	389	1523	14700.00	164498	142398	10.10
2002/03	1402	411	1813	15000.00	190120	167300	10.42
2003/04	1672	670	2342	16800.00	223839	290711	10.90
2004/05	1594	752	2346	20568.00	229617	328005	10.90
2005/06	1545	956	2501	22383.00	263317	343292	12.00
2006/07	1430	611	2041	29000.00	192095	366708	12.00
2007/08	1967	799	2766	32767.00	265434	382518	13.00
2008/09	2056	693	2749	32770.51	279850	396113	13.40
2009/10	1972	598	2570	42046.00	263461	398070	13.68
2010/11	2357	661	3018	43865.00	304135	410259	12.00
2011/12	2036	680	2716	48833.00	262879	439307	12.00
2012/13	2242	711	2953	52167.00	296698	468000	12.00
2013/14	2198	602	2800	50500.00	294300	434782	12.00
2014/15	2466	697	3163	51333.33	304007	511680	12.00
2015/16	2270	569	2839	59706.67	293075	525784	12.00
Badiliko (%)							
2014/15-2015/16	-0.08	-0.18	-0.10	0.16	-0.04	0.03	0.00
Ongezeko (%)							
1990/91-2015/16	1.1	3.9	1.4	22.6	1.5	1.5	1.0

Chanzo: Bodi ya Sukari Tanzania

- 1 Msimu ni Kati ya Julai na Juni
 - 2 Bei ya Mimea ni ile iliyo na asilimia 10 za Sucrose
 - 3 Ni pamoja na Sukari iliyopelekwa Zanzibar
 - 4 Ni kwa Tanzania bara
- * Sukari yote huzalishwa na wakulima/mashirika binafsi

PAMBA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

Jedwali Na. 36

Msimu ¹	Pamba yenye mbegu						Pamba iliyoondolewa mbegu					
	Uzalishaji Kiasi (tani)			Bei ya wastani (Shs/Kilo)			Kiasi (tani)			Mauzo nchini		
										Kiasi (tani)	Bei ya wastani (Shs/tani)	
	AR	BR	Jumla	AR	BR		AR	BR	Jumla	Jumla ²	AR	BR
1990/91	148124	1017	149141	41.00	14.00	48880	341	49221	300000	300000	240000	
1991/92	26841	32	26873	70.00	28.00	90706	11	90717	14301	325000	255000	
1992/93	281984	22000	303984	60.00	28.00	85784	..	85784	4405	542916	..	
1993/94	125434	0	125434	120.00	..	42695	..	42695	
1994/95	125434	0	125434	120.00	..	42695	..	42695	
1995/96	221148	0	221148	207.00	..	84782	..	84782	
1996/97	251751	74	251825	170.00	..	85162	25	85187	
1997/98	202217	0	202217	180.00	..	67780	..	67780	
1998/99	105853	0	105853	185.00	..	35480	..	35480	
1999/00	100500	0	100500	123.00	..	33686	..	33686	
2000/01	123558	0	123558	180.00	..	41415	..	41415	
2001/02	148180	0	148180	165.00	..	49668	..	49415	
2002/03	187908	781	188689	180.00	50	62983	262	63245	
2003/04	139756	213	139969	280.00	100	46843	72	46915	
2004/05	341589	0	341589	250.00	0	114496	..	114496	
2005/06	376591	0	376591	220.00	0	126228	..	126228	
2006/07	130585	0	130585	350.00	0	43770	..	43770	
2007/08	200662	0	200662	450.00	..	70773	..	70773	37488	
2008/09	368697	0	368697	480.00	0	123582	0	123582	66554	
2009/10	267644	0	267644	480.00	0	54851	0	54851	
2010/11	163518	0	163518	900.00	0	54809	0	54809	
2011/12	225938	0	225938	1000.00	..	75731	..	75731	
2012/13	351156	0	351156	660.00	..	117702	..	117702	
2013/14	245815	0	245815	700.00	0	82394	0	82394	
2014/15	202312	0	202312	750.00	0	67812	0	67812	
2015/16	149765	0	149765	800.00	0	50199	0	50199	
Badiliko (%)												
2014/15-2015/16	-0.26		-0.26	0.07		-0.26		-0.26	
Ongezeko (%)												
1990/91-2015/16	0.01		0.00	18.51		0.03		0.02	

Chanzo: Bodi ya Mauzo ya Pamba

¹ Msimu ni kati ya Juni na Mei

² Ni jumla ya AR na BR

.. Takwimu hazikupatikana

ENEO LILILOPANDWA MICHAI NA MAJANI MABICHI YALIYOPATIKANA

Jedwali Na. 37

Msimu ¹	Eneo lililopandwa (hekta): mashamba			Majani Mabichi yaliyopatikana (tani)						Bei kwa mkulima (Shs/Kilo)	Mauzo ² Nchini (tani)
				Kiumilikaji: mashamba			Kikanda: mashamba				
	Makubwa	Madogo	Jumla	Makubwa	Madogo	Jumla	Kaskazini	Kusini	Jumla		
1990/91	9699	9177	18876	70442	22434	92876	23531	69345	92876	17.00	3491
1991/92	9699	9177	18876	62994	20229	83223	19296	63927	83223	28.00	2750
1992/93	9699	9197	18896	80896	19934	100830	32218	68412	100630	45.00	3278
1993/94	10029	9197	19226	81159	21231	102390	32148	70242	102390	45.00	11124
1994/95	10149	9197	19346	93608	22641	116249	36825	79424	116249	50.00	..
302. Mwaka 2016, uzalishaji wa vito vya thamani ulikuwa kilo 2,554,932.41 ikilinganishwa na kilo 1,872,914.64 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 36.4. Ongezeko hilo lilitokana na kuimarika kwa uchimbaji wa madini ya vito na kuimarika kwa soko la vito vya thamani kwenye minada na maonesho ya vito Arusha. Aidha, thamani ya mauzo ya vito vya thamani nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 31.2 mwaka 2016 hadi kufikia dola za Marekani milioni 60.5 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 46.1 mwaka 2015. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha uzalishaji wa madini ya vito.

Makaa ya Mawe

303. Mwaka 2016, uzalishaji wa makaa ya mawe ulikuwa tani 276,030 ikilinganishwa na tani 257,321 zilizoalishwa mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 7.3. Ongezeko hilo lilitokana na kuimarika kwa uzalishaji wa makaa ya mawe katika mgodi wa TANCOAL na ongezeko la wanunuzi wa makaa ya mawe baada ya zuiro la kununua makaa ya mawe nje ya nchi. Aidha, thamani ya mauzo ya makaa ya mawe ilipungua kwa asilimia 11.0 hadi kufikia dola za Marekani milioni 11.58 mwaka 2016, kutoka dola za Marekani milioni 13.01 mwaka 2015, kutokana na kushuka kwa bei ya makaa ya mawe.

Madini Mengine

304. Mwaka 2016, uzalishaji wa chumvi ulikuwa tani 145,718 ikilinganishwa na tani 72,158.45 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 101.9. Thamani ya mauzo ya chumvi ilikuwa dola za Marekani milioni 5.99 mwaka 2016 ikilinganishwa na dola milioni 5.16 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 16.1. Ongezeko hilo lilitokana na kuimarika kwa uzalishaji na kupanuka kwa soko la madini ya chumvi katika nchi za Rwanda, Burundi na DRC. Aidha, uzalishaji wa chokaa ulikuwa tani 4,170,056.87 ikilinganishwa na tani 2,944,535.28 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 41.6. Thamani ya mauzo ya chokaa yalikuwa dola za Marekani milioni 22.71 mwaka 2016 ikilinganishwa na dola milioni 13.5 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 68.2. Ongezeko hili lilitokana na kuanzishwa kwa viwanda vipya vya saruji.

305. Mwaka 2016, uzalishaji wa kaolin ulipungua hadi kufikia tani 656.31 kutoka tani 1,952.59 zilizozalishwa mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 66.4. Vile vile, mauzo ya kaolin yalipungua kwa asilimia 49.3 hadi dola za Marekani 30,400.89 mwaka 2016 ikilinganishwa na dola za Marekani 59,999.2 mwaka 2015. Aidha, uzalishaji wa jasi ulikuwa tani 213,743.57 mwaka 2016 ikilinganishwa na tani 239,301.89 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 10.7. Mauzo ya jasi yalikuwa dola za Marekani milioni 6.28 mwaka 2016 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 4.44 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 41.4. Uzalishaji wa madini ya bati ulikuwa tani 138.22 ikilinganishwa na tani 191.54 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 27.8. Mauzo ya bati yalikuwa dola za Marekani milioni 1.5 mwaka 2016 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1.51 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 0.7.

Uhifadhi wa Mazingira katika uchenjaji wa Madini

306. Mwaka 2016, Kitengo cha Usimamizi wa Mazingira kilifanya ukaguzi wa mazingira katika mikoa minne (4) ambapo jumla ya maeneo 47 ya migodi midogo na uchenjaji wa madini (vat leaching process) yalidikaguliwa. Mikoa iliyodikaguliwa ilijumuisha Tanga (maeneo 5), Geita (maeneo 10) na Shinyanga (maeneo 5). Vile vile, maeneo 14 ya uchenjaji wa madini yalidikaguliwa ambayo ni Mara (maeneo 13) na maeneo ya Kihara na Mongo yaliyopo ndani ya msitu wa hifadhi wa Amani katika wilaya ya Muheza. Halikadhalika, jumla ya ripoti 11 za tathmini ya athari kwa mazingira katika miradi ya madini

zilipokelewa kutoka Baraza la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa lengo la kufanyiwa uhakiki ili kutoa au kutotoa cheti cha mazingira kwa miradi husika.

Uongezaji Thamani Madini

307. Mwaka 2016, Serikali iliendelea kutilia mkazo kwa wafanyabiashara wa madini ya vito watanzania (*Gemstone Dealers*) kuwa na mashine za ukataji (*lapidary*) zisizopungua tano (5) na wale wenye ubia na wawekezaji wa nje kuwa na mashine zisizopungua 30 kama Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 inavyowataka ili kukuza shughuli za uongezaji thamani madini nchini. Hii ilisabababisha kuwa na jumla ya wafanyabiashara 180 wa madini ya vito waliosajiliwa kuweza kuwekeza mashine 500 zilizokaguliwa za kukata, kusanifu na kung'arisha madini ya vito. Aidha, Kituo cha Uongezaji Thamani Madini Arusha (*Tanzania Gemological Centre*) kiliendelea kutoa mafunzo ya usanifu wa madini ya vito ambapo wanafunzi 36 walidahiliwa mwaka 2016 na hivyo kufanya wahitimu katika Kituo hicho kufikia 65 tangu kuanzishwa kwa mafunzo hayo mwaka 2014. Vile vile, Serikali iliendelea kuhamasisha vyuo na taasisi nyingine kutoa mafunzo ya ukataji, ung'arishaji, usonara na usanifu wa madini vito kwa watanzania wengi zaidi ili kuwezesha uwekezaji wa viwanda vya uongezaji thamani madini hapa nchini. Taasisi/vyuo hivyo ni kama *Arusha Technical College*, *VETA-Shinyanga* na *African Minerals and Geosciences Centre (AMGC)*.

UCHIMBAJI WA MADINI: KIASI KILICHOPATIKANA

Jedwali Na.56

MADINI	Kipimo	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016*
Almasi	Carat	237676	181874	80498	28378	127174	179633	252875	216491	237685
Dhahabu	Kg	36434	39112	39448	37085	39012	42534	40481	43293	45155
Gemstones	Kg	1858287	1068481	2646109	1241581	1237625	1692436	3083765	1872915	2554932
Chumvi	Tani	25897	27393	34455	32297	34016	36032	54757	92158	145718
Phosphate	Tani	28684	752	17180	848512	570626	397020	738000	222800	23658
Limestone	000 Tani	1282	1284	1437	202	1224	35529	873	2945	4170
Tin Ore	Tani	-	-	3	-	-	2	79	179	138
Gypsum	Tani	55730	8105	26918	9288	91610	171567	200179	239302	213744
Makaa ya mawe	Tani	15242	1	179	80710	78672	84772	246128	257321	276030
Pozolana	Tani	260403	61501	60320	113489	75193	79452	68925	342628	230045
Kaolin	Tani	13926	18624	58	178	1422	907	3809	1953	605
Madini ya fedha	Kg	10388	8231	12470	10399	11227	12159	14493	15569	17984
Shaba	Pound	6288503	4451697	11741898	7531164	12426025	12749548	14027008	14252341	15762430
Bauxite	Tani	20601	122920	39326000	29520000	28433930	39977300	25641201	204956	72779

Chanzo: Wizara ya Nishati na Madini, Idara ya Madini

- Takwimu hazikupatikana

Carat = 0.205 gm

* Takwimu za awali

MADINI YALIYOUZWA NCHI ZA NJE 2011 - 2016

Jedwali Na. 57

Aina ya madini	Kipimo	Kiasi kilichouzwa						Thamani ('000 US \$)					
		2011	2012	2013	2014	2015	2016*	2011	2012	2013	2014	2015	2016*
Almasi (Rough)	'000 Carats	80	127174	179633	252875	216491	239305	7480	33827	46013	82053	56003	85090
Almasi (iliyokatwa)	'000 Carats	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Almasi (Construct goods)	'000 Carats	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Dhahabu	'000 Gramu	37085	39012	42534	40481	43358	45155	1879622	2161520	1735708	1640072	1609392	1824815
Mawe ya thamani	'000 Gramu	1058580	-	1086532	3083765	1872915	2944107	6309	32570	62453	49146	46067	60483
Chumvi	Tani	32298	32004	33210	54757	92158	145718	3699	3408	3785	5275	5071	4806
Phosphate	Tani	848512	570626	397020	738000	222800	23658	425	277	225	140	126	721
Bati	Tani	-	48	-	79	179	138	-	732	-	907	959	1499
Jasi	Tani	11820	71610	-	200179	235920	213744	99	215	231	2518	4445	23792
Grafiti	Tani	-	-	-	25	30	1180	-	-	-	3	5	2132
Fedha	000Grams	10399	11227	11013	14493	15569	17984	11615	12682	17214	10283	7626	9901
Shaba	0001b	7531	12426	12654045	14027008	14252	16247	30202	44816	42134	43675	35658	35421
Madini ya viwandani	Tani	-	-	-	98	151297	4769577	-	-	-	9	3254	78473
Bauxite	Tani	37700000	28433930	39977300	25641201	204956	74660	1385	12479	35827	20014	325	1242
Jumla ('000 US \$)								1940836	2302526	1943590	1854095	1768930	2128372

Chanzo: Wizara ya Nishati na Madini, Idara ya Madini

- Takwimu hazikupatikana

* Takwimu za awali

SURA YA 14

VIWANDA NA BIASHARA

Kiwango cha Ukuaji

308. Mwaka 2016, shughuli za kiuchumi za uzalishaji bidhaa za viwandani zilikua kwa asilimia 7.8 ikilinganishwa na asilimia 6.5 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 1.3 Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa zikiwemo bidhaa za vyakula, saruji, vinywaji, tumbaku na nguo. Aidha, mchango wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani katika Pato la Taifa ulipungua na kuwa asilimia 5.1 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 5.2 mwaka 2015.

Viwanda Vidogo

309. Katika uendelezaji wa viwanda vidogo, mwaka 2016 Programu ya Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini (MUVI) na NEDF ilitoa mafunzo kwa wajasiriamali 39,319 ikilinganishwa na wajasiriamali 26,887 waliopatiwa mafunzo mwaka 2015. Mafunzo hayo yalihusu kilimo bora, kuzalisha mizinga ya nyuki ya kisasa, kubuni mavazi na ushonaji, usindikaji wa vyakula, utengenezaji wa mitambo na mashine za aina mbalimbali, matumizi ya mbegu bora, ukamuaji wa mafuta na utengenezaji wa bidhaa mbalimbali. Vile vile, programu ya MUVI ilitoa mafunzo ya kuongeza thamani katika mazao ya alizeti na mhogo na kuweza kuzalisha mikate, keki, biskuti, mafuta, chakula cha mifugo, dawa za mbu na dawa za viatu kwa wajasiriamali 5,307 mwaka 2016 ikilinganishwa na wajasiriamali 32,129 mwaka 2015. Aidha, Serikali kupitia taasisi zake iliendelea kuboresha na kuanzisha mitaala mipya ya mafunzo kuweza kuendana na kasi ya wananchi katika sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo.

310. Mwaka 2016, Serikali kupitia TanTrade ilitoa mafunzo kwa vijana 50 ya utengenezaji wa bidhaa za ngozi katika mikoa ya kanda ya ziwa ambayo ni Mwanza, Mara, Shinyanga, Simiyu na Geita. Mafunzo haya yalilenga kuwapa fursa vijana kutumia malighafi ya ngozi kujijaji lakini pia kuongeza wigo wa matumizi ya ngozi ambayo inapatikana kwa wingi hapa nchini. Mafunzo hayo yalitolewa kwa ushirikiano kati ya TanTrade na Chuo cha Ufundi Dar es Salaam kituo cha Mwanza ambacho ni maalum kwa teknolojia ya Ngozi. Vile vile, iliratibu mafunzo yaliyolenga kuwajengea uwezo wazalishaji asali na

wafungashaji wa asali, ili kujenga uelewa wa biashara ya asali kwa kuzingatia mahitaji ya soko na kuwezesha bidhaa wanazozalisha kuwa na ushindani katika soko la ndani na nje. Mafunzo haya yalihudhuriwa na jumla ya washiriki 197 kati yao 84 walitoka katika wilaya saba za mkoa wa Singida na 113 walitoka mikoa ya Tabora na Katavi. Mafunzo haya yalitolewa na TanTrade kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania, Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) na taasisi ya kusimamia Msimbo Miria (GS1).

311. Mwaka 2016, Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 39,679.2 kwa wajasiriamali 66,253 ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 49,073.8 kwa wajasiriamali 75,469 mwaka 2015. Kwa upande mwingine, teknolojia 252 zilibunuliwa na mashine mpya 659 zilitengenezwa kwa kupitia vituo saba vya kukuza teknolojia ikilinganishwa na teknolojia 186 na mashine 416 zilizotengenezwa mwaka 2015. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya teknolojia mpya na mashine mpya.

Uzalishaji katika Baadhi ya Viwanda Nchini

312. Mwaka Mwaka 2016, uzalishaji wa bidhaa za viwandani kwa ujumla uliongezeka. Bidhaa zilizokuwa na ongezeko katika uzalishaji ni pamoja na chibuku asilimia 15.1; sigara asilimia 3.2; kamba za katani asilimia 4.1; nyavu za uvuvi asilimia 0.3; dawa za pareto asilimia 6.8; saruji asilimia 45.9 na chuma asilimia 4.9. Kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa hizo kulitokana na ongezeko la mahitaji ya bidhaa za viwandani katika soko la ndani na nje. Hata hivyo, uzalishaji ulipungua kwa bidhaa za biskuti na tambi asilimia 17.3; unga wa ngano asilimia 6.4; konyagi asilimia 2.5; bia asilimia 0.8; nguo asilimia 4.6; tabaka za mbao asilimia 3.8; rangi asilimia 8.5; betri asilimia 20.7 na sukari asilimia 3.6.

313. Mwaka 2016, kwa ujumla gharama za uzalishaji bidhaa ziliongezeka hadi kufikia shilingi milioni 4,305,293 kutoka shilingi milioni 4,100,280 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 5. Ongezeko hilo lilitokana na kubadilika kwa thamani ya shilingi ya Tanzania, hususani pale malighafi za viwandani zinaponunuliwa kutoka nje ya nchi na gharama za wafanyakazi kuongezeka.

Mwenendo wa Biashara ya Tanzania Kimataifa

314. Biashara kati ya Tanzania na nchi mbalimbali imekuwa ya kuridhisha katika miaka ya hivi karibuni kwa kuonesha tofauti ndogo katika urari wa biashara ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Hii imechangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa nje na kupungua kwa uagizwaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi. Vile vile, utofauti huu ulitokana na kuwepo kwa masoko ya upendeleo ya mpango wa AGOA kutoka Marekani; *Quota Free Duty Free* (QFDF) kutoka Japan, India na China; Jumuiya ya Umoja wa Ulaya; pamoja na masoko ya kikanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika na masoko mengine ya kimataifa kupitia Shirika la Biashara la Dunia. Kwa ujumla nakisi katika urari ya biashara baina ya Tanzania na nchi nyingine duniani ilipungua kwa asilimia 49.2 mwaka 2016 kufikia dola za Marekani milioni 2,774.9 kutoka dola milioni 4,440.7 mwaka 2011. Mwenendo wa biashara ya bidhaa baina ya Tanzania na nchi/Jumuiya mbalimbali duniani umeoneshwa katika Sura ya 3.

Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa

315. Mwaka Mwaka 2016, Serikali kupitia TanTrade iliratibu na kuendesha maonesho ya 40 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yaliyofanyika katika Uwanja wa Maonesho wa Mwl. Julius K. Nyerere ambapo jumla ya kampuni 2,500 zilishiriki ikilinganishwa na kampuni 2,302 zilizoshiriki mwaka 2015, ikiwa ni ongezeko la asilimia 8.6. Kati ya kampuni zilizoshiriki, 501 zilitoka nje ya nchi na 1,999 zilikuwa za ndani. Aidha, jumla ya nchi 30 zilishiriki maonesho hayo ikilinganishwa na nchi 25 zilizoshirika mwaka 2015. Nchi zilizoshiriki katika maonyesho hayoni pamoja na:- Afrika ya Kusini, Australia, Bulgaria, Brazil, China, Ghana, Ufaransa, India, Indonesia, Italia, Iran, Japan, Kenya, Korea ya Kusini, Malawi, Mauritius, Misri, Msumbiji, Pakistani, Singapore, Syria, Uganda, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Bulgaria, Rwanda, Sudani ya Kusini, Urusi na Vietnam.

316. Mwaka 2016, Serikali iliandaa maonesho ya kwanza ya viwanda vya ndani yenye kaulimbiu "*Tanzania tunajenga viwanda*" ambayo yalilenga kuongeza uelewa wa wananchi juu ya falsafa na dhima ya ujenzi wa uchumi wa viwanda. Katika maonesho hayo, jumla ya viwanda 441, taasisi 13 za serikali na taasisi 5 za fedha zilishiriki. Aidha, Serikali iliandaa maonesho yaliyoambatana na mkutano wa wananchi wa Tanzania wanaoishi nchi za nje (Diaspora) katika

viwanja vya Maisara-Unguja. Maonesho hayo yalilenga kuwapa fursa watanzania wanaoishi nchi za nje kubaini bidhaa zinazozalishwa nchini ili wasaidie kuzitangaza. Kadhalika, mwaka 2016, Tanzania ilishiriki katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Rwanda yaliyofanyika Kigali ambapo kampuni 9 kutoka Tanzania zilishiriki. Vile vile, Tanzania ilishiriki katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Swaziland yalifanyika mjini Manzini ambapo wajasiriamali 8 waliweza kushiriki na Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Nairobi yaliyofanyika Uwanja wa maonesho wa Jamhuri Park, ambapo jumla ya kampuni 3 za uzalishaji pamoja na wajasiriamali 19 walishiriki. Maonesho yote ya Kimataifa yalilenga kutafuta fursa za masoko ya bidhaa za Tanzania katika nchi husika.

Bei ya Soko kwa Bidhaa za Mazao

317. Mwaka 2016, wastani wa bei za mazao makuu ya chakula zilipanda ambapo wastani wa bei ya mahindi uliongezeka na kufikia shilingi 64,228 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 51,235 kwa gunia la kilo mia moja mwaka 2015. Ongezeko hilo lilitokana na kushuka kwa ugavi katika soko la ndani kufuatia kuongezeka kwa mahitaji na bei katika masoko ya nchi jirani ambazo hazikuwa na uzalishaji wa kutosha kukidhi mahitaji yao. Aidha, bei ya mchele kwa gunia la kilo mia moja ilishuka kutoka wastani wa shilingi 161,487 mwaka 2015 hadi wastani wa shilingi 158,510 mwaka 2016. Kushuka kwa bei ya mchele kulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mchele.

MATUMIZI YA SARUJI NCHINI

Jedwali Na. 58

Mwaka	Kutoka Nje	Uuzaji nje	Uzalishaji wa Ndani	Tani	
				Matumizi Tani	Badiliko, %
2000	7281	30497	833092	809876	-0.6%
2001	56395	53517	900430	903308	11.5%
2002	149079	37203	1026082	1137958	26.0%
2003	166446	34396	1186434	1318484	15.9%
2004	125007	37655	1280851	1368203	3.8%
2005	120200	40430	1375222	1454992	6.3%
2006	92711	98	1421460	1514073	4.1%
2007	101827	52170	1629890	1679547	10.9%
2008	356468	99688	1755862	2012642	19.8%
2009	516182	57569	1940845	2399458	19.2%
2010	566828	189321	2312055	2689562	12.1%
2011	768343	217944	2408765	2959164	10.0%
2012	1013986	145793	2557798	3425991	15.8%
2013	1218453	154481	2369819	3433791	0.2%
2014	1428995	142001	2795687	4082681	18.9%
2015	1257578	126391	3273000	4404187	7.9%
2016	1306732	194338	4916400	6028794	36.9%

Chanzo: Ofisi ya Taifa Takwimu

* Takwimu za Awali

UZALISHAJI WA BAADHI YA BIDHAA VIWANDANI

Jedwali Na.59

Aina ya Bidhaa	Kipimo											Badiliko(%)
		2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2015/16
Biskuti & tambi	Tani	11273	15435	15200	7435	12053	16423	17440	18225	19204	15890	-17.3
Unga wa ngano	Tani	406336	287925	368885	444242	439926	442345	516778	529797	533257	498940	-6.4
Konyagi	000 Lita	5622	4049	10201	11186	15432	16229	20680	31963	29491	28754	-2.5
Bia	000 Lita	310194	291178	284906	242689	323393	338041	374238	379913	386310	383251	-0.8
Chibuku	000 Lita	10320	10235	16141	21037	23474	22359	19935	20301	23028	26513	15.1
Sigara	Milioni	5821	6101	5831	6181	6630	7723	7710	8028	7837	8091	3.2
Nguo	000 M ²	139000	140531	91501	103177	101820	81437	97522	119458	100491	76436	-23.9
Kamba za katani	Tani	7012	7783	7913	6872	6976	7927	7542	7871	8851	9216	4.1
Nyavu za uvuvi	Tani	156	-	64	247	164	272	297	279	311	312	0.2
Mazulia	000 M ²	-	-	37152	-	-	-	-	-	0	0	-
Tabaka za mbao	M ²	45147	44547	266	-	30589	38871	36935	38913	36317	34983	-3.7
Dawa za pareto	Tani	33	73	-	49	53	70	83	136	118	126	6.5
Mbolea	Tani	-	-	25762	-	11200	-	-	-	0	0	-
Rangi	000 Lita	17451	24857	-	28201	31211	35025	36623	38308	38372	35096	-8.5
Bidhaa za petrol	000 Tani	-	-	1941	-	-	-	-	-	0	0	-
Saruji	000 Tani	1630	1756	34793	2313	2409	2558	2369	2795	3135	4572	45.8
Chuma	Tani	52163	39969	34793	33384	39955	46690	48500	56752	62612	65686	4.9
Bati	Tani	36492	31743	50664	71276	76912	81427	85314	86825	91385	91421	0.0
Aluminium	Tani	110	105	58	59	33	23	37	27	32	14	-56.3
Radio	000 namba	-	-	-	-	-	-	-	-	0	0	-
Betri	Milioni	75	53	78	93	89	68	75	93	87	69	-20.7

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Wizara ya Viwanda na Biashara

- Hakuna uzalishaji

VIWANDA - IDADI YA WATU WALIOAJIRIWA

Jedwali Na. 60

ISIC (Rev 3)	Shughuli	Walioajiriwa					Wengine					Jumla				
		2012	2013	2014	2015	2016	2012	2013	2014	2015	2016	2012	2013	2014	2015	2016
151-4	Vyakula	48,913	51,358	53,926	56,622	59,453	353	371	390	410	432	49266	51729	54316	57033	59885
155	Vinywaji	6,520	6,846	7,188	7,548	7,925	58	61	64	67	71	6578	6907	7252	7615	7996
160	Tumbaku na Sigara	7,588	7,968	8,366	8,785	9,224	-	-	-	-	-	7588	7968	8366	8785	9224
171-2, 181	Ufumaji na Ushonaji	13,217	13,878	14,572	15,300	16,065	273	287	302	318	334	13490	14165	14874	15618	16399
191	Ngozi, bidhaa za ngozi	714	750	788	827	868	5	5	5	6	6	719	755	793	832	874
192	Viatu	903	948	995	1,045	1,097	6	6	6	7	7	909	954	1002	1052	1104
201-202	Mbao, Bidhaa za Mbao	849	892	937	983	1,033	28	30	32	33	35	877	922	968	1017	1068
210-221- 222	Karatasi, Uchapishaji	6,149	6,456	6,779	7,118	7,474	106	112	118	124	130	6255	6568	6897	7242	7604
241-2	Utengenezaji wa Kemikali	3,246	3,408	3,578	3,757	3,945	34	36	38	40	42	3280	3444	3616	3797	3987
251	Bidhaa za mpira	1,353	1,421	1,492	1,567	1,645	14	15	16	17	17	1367	1436	1508	1583	1662
252	Bidhaa za Plastiki	4,625	4,856	5,099	5,354	5,621	15	16	17	18	19	4640	4872	5116	5371	5640
261-9	Bidhaa za Madini yasiyo Chuma	2,768	2,906	3,051	3,204	3,364	34	36	38	40	42	2802	2942	3089	3244	3406
271-369	Nyinginezo	22,601	23,731	24,918	26,163	27,471	468	491	516	543	571	23069	24222	25434	26707	28043
	Jumla	119,446	125,418	131,689	138,273	145,186	1,394	1,466	1,542	1,622	1,706	120,840	126,884	133,231	139,895	146,892

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu ziimerekebishwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013

VIWANDA - GHARAMA ZA KAZI

Jedwali Na. 61

(Sh.milioni)

ISIC(Rev 3)	Shughuli	Mishahara					Malipo Mengine					Jumla				
		2012	2013	2014	2015	2016	2012	2013	2014	2015	2016	2012	2013	2014	2015	2016
151-4	Vyakula	59,257	62,220	65,330	68,596	72,025	25,743	27,030	28,382	29,801	31,292	85000	89250	93712	98397	103317
155	Vinywaji	40,797	42,836	44,977	47,226	49,586	23,210	24,370	25,589	26,869	28,212	64007	67206	70566	74094	77799
160	Tumbaku na Sigara	19,541	20,518	21,544	22,621	23,751	10,729	11,266	11,829	12,421	13,042	30270	31784	33373	35042	36794
171-2, 181	Ufumaji na Ushonaji	11,542	12,119	12,725	13,361	14,029	4,460	4,683	4,917	5,163	5,421	16002	16802	17642	18524	19450
191	Ngozi, Bidhaa za ngozi	538	565	593	623	654	124	131	138	144	152	662	696	731	767	806
192	Viatu	1,161	1,219	1,280	1,344	1,411	446	468	491	516	542	1607	1687	1771	1860	1953
201-202	Mbao, Bidhaa za Mbao	855	897	942	989	1,038	245	257	270	283	298	1100	1154	1212	1272	1336
210-221-222	Karatasi, Uchapishaji	20,020	21,021	22,072	23,175	24,334	6,457	6,780	7,119	7,475	7,849	26477	27801	29191	30650	32183
241-2	Utengenezaji wa Kemikali	8,215	8,626	9,057	9,510	9,985	4,760	4,998	5,248	5,510	5,786	12975	13624	14305	15020	15771
251	Bidhaa za Mpira	6,393	6,712	7,048	7,400	7,770	1,594	1,674	1,758	1,846	1,938	7987	8386	8805	9245	9708
252	Bidhaa za Plastiki	7,054	7,406	7,776	8,165	8,573	5,895	6,190	6,500	6,825	7,166	12949	13596	14276	14990	15739
261-9	Bidhaa za Madini yasiyo Chuma	84,917	89,162	93,619	98,299	103,213	9,550	10,028	10,530	11,056	11,609	94467	99190	104149	109355	114822
271-369	Nyinginezo	49,463	51,936	54,532	57,258	60,120	36,615	38,446	40,369	42,388	44,508	86078	90382	94901	99646	104628
	Jumla	309753	325237	341495	358566	376490	129828	136321	143139	150298	157815	439581	461558	484634	508864	534305

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu ziimerekebishwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013

VIWANDA - MUHTASARI WA MATOKEO

Jedwali Na. 62																	(Tshs. Millions)			
ISIC(Rev 3)	Shughuli	PATO				GHARAMA				Thamani Iliyoongezeka (Value Added)				Uchakavu wa Mitambo (Depreciation)						
		2013	2014	2015	2016	2013	2014	2015	2016	2013	2014	2015	2016	2013	2014	2015	2016			
151-4	Vyakula	1416291	1487106	1561461	1639533	804640	844872	887115	931471	611651	642234	674346	708063	39270	41233	43295	45459			
155	Vinywaji	1075129	1128885	1185330	1244596	685236	719498	755472	793246	389893	409388	429857	451350	51580	54159	56866	59709			
160	Tumbaku na Sigara	334539	351266	368829	387271	208258	218671	229604	241084	126281	132595	139225	146186	25182	26441	27763	29151			
171-2, 181	Ufumaji na Ushonaji	242096	254201	266911	280256	138761	145699	152984	160633	103335	108502	113927	119623	26487	27811	29202	30661			
191	Ngozi, bidhaa za ngozi	11195	11755	12342	12960	7592	7972	8370	8789	3603	3783	3972	4171	354	372	390	410			
192	Viatu	10381	10900	11445	12017	6320	6636	6968	7316	4061	4264	4477	4701	770	808	849	891			
201-202	Mbao, Bidhaa za Mbao	15414	16185	16994	17844	7881	8275	8689	9123	7533	7910	8305	8720	572	601	631	662			
210-221-222	Karatasi, Uchapishaji	232228	243839	256031	268833	130613	137144	144001	151201	101615	106696	112031	117632	10297	10812	11352	11920			
241-2	Utengenezaji wa Kemikali	335334	352101	369706	388191	194607	204337	214554	225282	140727	147763	155152	162909	9178	9637	10119	10624			
251	Bidhaa za mpira	190365	199883	209877	220371	99060	104013	109214	114674	91305	95870	100664	105697	2761	2899	3044	3196			
252	Bidhaa za Plastiki	546215	573526	602202	632312	379193	398153	418060	438963	167022	175373	184142	193349	11414	11985	12584	13213			
261-9	Bidhaa za Madini yasiyo Chuma	439340	461307	484372	508591	282029	296130	310937	326484	157311	165177	173435	182107	36498	38323	40239	42250			
271-369	Nyinginezo	1164516	1222742	1283879	1348072	774887	813631	854312	897028	389629	409111	429566	451045	40795	42834	44976	47224			
	Jumla	6013043	6313695	6629379	6960847	3719077	3905030	4100280	4305293	2293966	2408665	2529099	2655554	255158	267914	281308	295371			
Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu																				
* Takwimu ziimerekebishwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013																				

VIWANDA - MUHTASARI WA MATOKEO KIMKOA *

Jedwali Na. 63

Jina la mkoa	Idadi ya Wafanyakazi				Idadi ya Waajiriwa				Mishahara (TShs. Milioni)				Thamani Iliyoongezeka (TShs. Milioni)			
	2013	2014	2015	2016	2013	2014	2015	2016	2013	2014	2015	2016	2013	2014	2015	2016
Dodoma	238	286	300	315	229	284	299	313	598	710	746	783	10157	10407	10928	11474
Arusha, Manyara	15787	18977	19926	20923	15169	18834	19776	20765	22844	27141	28497	29922	423301	433728	455415	478186
Kilimanjaro	11919	14327	15044	15796	11453	14220	14931	15678	12592	14960	15708	16493	162864	166876	175220	183981
Tanga	10377	12474	13098	13753	9970	12379	12998	13648	12507	14859	15602	16382	281198	288125	302531	317658
Morogoro	8384	10078	10582	11111	8056	10003	10503	11028	21947	26075	27378	28747	342668	351109	368665	387098
Pwani,	63	76	80	83	60	74	78	82	81	96	101	106	516	529	555	583
Dar es Salaam	24930	29967	31466	33040	23519	29202	30662	32195	136306	161943	170039	178538	740740	758987	796937	836784
Lindi	119	143	150	158	114	142	149	156	1547	1838	1930	2026	4911	5032	5284	5548
Mtwara	1009	1213	1274	1337	969	1203	1263	1326	546	649	681	715	8903	9122	9578	10057
Ruvuma	9392	11290	11854	12447	9024	11205	11765	12353	16960	20150	21157	22215	38726	39680	41664	43747
Iringa	2977	3579	3758	3945	2860	3551	3729	3915	6468	7685	8069	8472	26324	26972	28321	29737
Mbeya	246	296	310	326	236	293	308	323	545	648	680	714	2743	2811	2951	3099
Singida	833	1001	1051	1104	800	993	1043	1095	1360	1616	1697	1781	5275	5405	5675	5959
Tabora	132	159	167	175	127	158	166	174	1061	1261	1324	1390	1614	1654	1736	1823
Rukwa	700	841	884	928	673	836	877	921	1611	1914	2010	2110	6316	6472	6795	7135
Kigoma	2265	2723	2859	3002	2177	2703	2838	2980	10321	12262	12875	13519	22706	23265	24429	25650
Shinyanga	9816	11799	12390	13009	9432	11711	12297	12911	9982	11859	12452	13075	39077	40040	42042	44144
Kagera	7412	8910	9355	9823	7122	8843	9285	9749	14046	16688	17522	18398	121105	124088	130293	136807
Mwanza	3556	4275	4488	4713	3417	4243	4455	4678	10284	12218	12829	13470	97730	100137	105144	110402
Mara	681	819	860	903	654	812	853	895	5827	6923	7269	7632	13883	14225	14936	15683
Jumla	110836	133231	139895	146892	106061	131689	138273	145186	287433	341495	358566	376490	2350757	2408665	2529099	2655554

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu ziimerekebishwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013

Viwanda rasmi vyenye wafanyakazi 10 na zaidi

VICEZO VYA UFANISI KATIKA SEKTA YA VIWANDA (%)

Jedwali Na. 65

Mwaka	Mchango katika Pato la Taifa (Bei za miaka husika)	Ukuaji wa Sekta (Bei za 2007)	Mchango katika mauzo nje	Mchango katika mauzo nje yasiyo asilia	Ongezeko la mauzo nje ya bidhaa za viwanda
2005	7.29		9.3	11.81	
2006	7.50	8.4	11.2	13.81	25.4
2007	7.02	11.5	15.3	18.14	57.9
2008	6.97	11.4	20.7	28.48	139.9
2009	6.88	4.7	15.4	21.35	-31.7
2010	6.89	8.9	22.3	30.34	90.3
2011	7.64	6.9	16.9	22.99	-10.6
2012	7.49	4.1	17.6	24.91	20.4
2013	6.45	6.5	20.4	28.95	3.3
2014	5.58	6.8	23.3	32.63	15.6
2015	5.25	6.5	25.3	33.14	10.1
2016	5.11	7.8	19.2	25.48	-20.0

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

SURA YA 15

UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI

UJENZI

Kiwango cha Ukuaji

318. Shughuli za ujenzi zilikuwa kwa asilimia 13.0 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 16.8 mwaka 2015. Kasi ya ukuaji ilipungua sambamba na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa za kukuza mitaji kutokana na kukamilika kwa miradi mikubwa ya ujenzi wa kiwanda cha saruji, mitambo ya kufua umeme na bomba la gesi kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam. Aidha, ukuaji wa mwaka 2016 ulitokana na kuwepo kwa shughuli za ujenzi wa nyumba za makazi na biashara na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara, madaraja na viwanja vya ndege. Mchango wa shughuli za kiuchumi za ujenzi katika Pato la Taifa uliongezeka na kufikia asilimia 14.0 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 13.6 mwaka 2015.

Mtandao wa Barabara

319. Mtandao wa barabara nchini una urefu wa kilometa 87,581. Mtandao huo unajumuisha kilometa 12,786 za barabara kuu zinazounganisha mikoa na nchi jirani, kilometa 22,214 za barabara za mikoa zinazounganisha wilaya na miji mikuu na kilometa 52,581 ni barabara zinazounganisha wilaya na vijiji.

320. Mwaka 2016, barabara kuu na za mikoa za kiwango cha lami na changarawe zilikuwa na urefu wa kilometa 30,265 ikilinganishwa na kilometa 31,366 mwaka 2015, sawa na pungufu ya asilimia 3.5. Upungufu huo ulitokana na kazi za ujenzi na ukarabati wa barabara kwa kiwango cha lami zinazoendelea. Kuhusu hali ya barabara, kati ya kilometa 30,265 kilometa 12,388 za barabara kuu sawa na asilimia 41 zilikuwa katika hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 11,330 mwaka 2015. Aidha, kilometa 13,642 sawa na asilimia 45 zilikuwa katika kiwango cha wastani ikilinganishwa na kilometa 15,627 mwaka 2015 na kilometa 4,235 sawa na asilimia 14 zilikuwa na hali mbaya ikilinganishwa na kilometa 4,408 mwaka 2015.

321. Kati ya kilometa 12,786 za barabara kuu, jumla ya kilometa 9,953 zilikuwa na kiwango cha lami na changarawe ikilinganishwa na kilometa 9,870 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 0.8. Kati ya hizo: kilometa 6,672 sawa na asilimia 60 zilikuwa katika hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 5,543 mwaka 2015; kilometa 2,386, sawa na asilimia 30 zilikuwa na hali ya wastani ikilinganishwa na kilometa 3,386 mwaka 2015; na kilometa 896, sawa na asilimia 10 zilikuwa na hali mbaya ikilinganishwa na kilometa 941 mwaka 2015.

Aidha, kati ya kilometa 22,214 za barabara za mikoa, barabara zilizokuwa na kiwango cha lami na changarawe zilikuwa na urefu wa kilometa 20,312 ikilinganishwa na kilometa 21,496 mwaka 2015. Kati ya hizo: kilometa 5,716 zilikuwa na hali nzuri; kilometa 11,256 zilikuwa katika hali ya wastani; na kilometa 3,339 zilikuwa na hali mbaya ikilinganishwa na kilometa 5,787, kilometa 12,242 na kilometa 3,467 mwaka 2015 kwa mtiririko huo. **Jedwali Na.15.1** linaonesha mchanganuo wa mtandao wa barabara kuu na za mikoa kwa kiwango cha lami na changarawe.

Jedwali Na.15.1: Hali ya Mtandao wa Barabara Hadi Desemba 2016

Aina ya Barabara	Hali ya Mtandao wa Barabara						Jumla Kuu
	Nzuri		Wastani		Mbaya		
	Km	%	Km	%	Km	%	
Barabara Kuu za Lami	5,408	80	910	13	481	7	6,798
Barabara Kuu za Changarawe / Udongo	1,264	40	1,476	47	415	13	3,155
Jumla Ndogo-Barabara Kuu	6,672	67	2,386	24	896	9	9,953
Barabara za Mikoa za Lami	544	50	300	28	239	22	1,084
Barabara za Mikoa za Changarawe / Udongo	5,172	27	10,956	57	3,100	16	19,228
Jumla Ndogo-Barabara za Mikoa	5,716	28	11,256	7	3,339	16	20,312
Jumla Kuu	12,388	41	13,642	45	4,235	14	30,265

Chanzo: Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

Matengenezo ya Barabara, Magari, Madaraja na Vivuko

322. Mwaka 2016, jumla ya kilometa 33,058.01 za barabara kuu na za mikoa zilifanyiwa matengenezo ikilinganishwa na kilometa 24,601 zilizofanyiwa matengenezo mwaka 2015. Aidha, madaraja 2,934 yalifanyiwa matengenezo ikilinganishwa na madaraja 1,710 mwaka 2015. Ongezeko hilo la barabara na madaraja yaliyofanyiwa matengenezo lilitokana na fedha za utekelezaji wa miradi hiyo kupatikana kwa wakati. Vile vile, mwaka 2016, Serikali ilifanya ukarabati na matengenezo ya vivuko 23 kati ya 29 inavyovisimamia. Halikadhalika, Serikali imekamilisha ujenzi wa kivuko kipya cha Mto Pangani chenye uwezo wa kubeba tani 50 na ujenzi wa kivuko kipya cha MV Kazi kitakachotoa huduma katika kituo cha Magogoni-Kigamboni (Dar es Salaam) ulifikia asilimia 90.

Bodi ya Mfuko wa Barabara

323. Mwaka 2016, mapato yaliyokusanywa na Mfuko wa Barabara yaliongezeka kufikia shilingi milioni 819,680.75 kutoka shilingi milioni

676,037.66 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 21.2. Ongezeko hilo lilitokana na usimamizi mzuri wa makusanyo ikiwemo matumizi ya mifumo ya kielektroniki na ongezeko la kiasi cha mafuta ya petroli kilichoagizwa kutoka nje pamoja na kuongezeka kwa magari yanayosafirisha mizigo kwenda nchi jirani. Aidha, Bodi ilifanya ukaguzi wa miradi ya barabara 692 ikilinganishwa na miradi 670 iliyokaguliwa mwaka 2015. Idadi ya miradi iliyokaguliwa iliongezeka kutokana na ongezeko la mikoa na halmashauri ambazo ni watumiaji wa fedha za Mfuko.

Wakala wa Nyumba na Majengo ya Serikali

324. Mwaka 2016, Serikali iliendelea kutekeleza miradi 110 ya ujenzi na ukarabati wa nyumba ikilinganishwa na miradi 119 mwaka 2015. Katika kipindi hicho, jumla ya miradi 63 ya ukarabati wa nyumba na majengo ilisimamiwa ikilinganishwa na miradi 103 mwaka 2015. Kupungua kwa ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali kulitokana na miradi mingi kukamilika. Aidha, idadi ya nyumba za makazi na biashara zilizopangishwa kwa watumishi wa serikali na watu mbalimbali zilikuwa 2,518 ikilinganishwa na nyumba 1,159 mwaka 2015. Vile vile, mikataba ya pango kwa nyumba 94 ilisitishwa kutokana na wapangaji kutolipa kodi ya pango kwa wakati.

Bodi ya Usajili wa Wakandarasi

325. Mwaka 2016, Bodi ya Wakandarasi ilisajili jumla ya wakandarasi 774 ikilinganishwa na wakandarasi 903 mwaka 2015. Usajili huu unafanya jumla ya wakandarasi waliosajiliwa hadi Desemba 2016 kufikia 8,418 ikilinganishwa na wakandarasi 8,839 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Kupungua kwa wakandarasi waliosajiliwa kulitokana na kupungua kwa miradi ya maendeleo. Aidha, wakandarasi 7 walifutiwa usajili mwaka 2016 ikilinganishwa na wakandarasi 245 mwaka 2015 kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kushindwa kulipa ada ya mwaka na kutozingatia taratibu za kazi na taaluma zao. Vile vile, Bodi ilisajili miradi ya ujenzi 3,556 ikilinganishwa na miradi 2,967 mwaka 2015, ambapo kati ya hiyo, miradi 2,934 ilifanyiwa ukaguzi ikilinganishwa na miradi 2,735 mwaka 2015. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa ofisi za ukaguzi ikiwemo kufunguliwa kwa ofisi mpya kanda ya Dodoma.

Bodi ya Usajili ya Wahandisi

326. Bodi ya Usajili wa Wahandisi ilisajili wahandisi 1,892 wa fani mbalimbali mwaka 2016 ikilinganishwa na wahandisi 1,467 waliosajiliwa mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 29.0. Kati ya hao, wahandisi 1,775 walikuwa watanzania na wahandisi 117 walikuwa wageni. Aidha, Bodi ilisajili kampuni za ushauri 14 ambapo kampuni 8 zilikuwa za kitanzania na 6 za kigeni

ikilinganishwa na kampuni 9 zilizosajiliwa mwaka 2015, ambapo kampuni 7 zilikuwa za kitanzania na 2 za kigeni. Vile vile, jumla ya wahandisi 459 walipata mafunzo ikilinganishwa na wahandisi 393 mwaka 2015. Bodi pia ilisajili miradi ya ujenzi 829 na kukagua miradi 178 ikilinganishwa na usajili wa miradi 821 na ukaguzi wa miradi 180 mwaka 2015. Usajili wa miradi uliongezeka kutokana na wadau kujitokeza na kujua umuhimu wa kusajili miradi.

Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi

327. Mwaka 2016, Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilisajili jumla ya wataalam 830 ikilinganishwa na wataalam 747 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilinia 11.1. Ongezeko hilo lilitokana na wahitimu wengi kujitokeza kufanya mitihani ya Bodi kwa mwaka husika. Aidha, katika kipindi hicho, kampuni mpya 22 za wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi zilisajiliwa na hivyo kuwa na jumla ya kampuni 346 ikilinganishwa na kampuni mpya 19 mwaka 2015. Ongezeko hili lilitokana na juhudi za Bodi kuendelea kuwahamasisha waendelezaji wa majengo kutumia huduma za wataalamu waliosajiliwa.

328. Mwaka 2016, Bodi ilikagua miradi 2,153 ikilinganishwa na miradi 2,101 iliyokaguliwa mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 2.5. Aidha, katika kipindi hicho, miradi 780 ya ujenzi ilisajiliwa ikilinganishwa na miradi 799 iliyosajiliwa mwaka 2015. Vile vile, ili kuongeza ufanisi katika fani ya ubunifu na ukadiriaji majenzi, jumla ya wahitimu 104 walipatiwa mafunzo kwa vitendo ikilinganishwa na wahitimu 60 mwaka 2015.

Baraza la Taifa la Ujenzi

329. Mwaka 2016, Baraza la Taifa la Ujenzi lilitoa mafunzo kwa wadau 119 wa sekta ya ujenzi ikilinganishwa na wadau 149 waliopatiwa mafunzo mwaka 2015. Kati ya hao, wadau 61 walipata mafunzo ya usimamizi wa mikataba ya ujenzi na wadau 53 mafunzo ya usuluhishi wa migogoro. Aidha, Baraza lilifanya ukaguzi wa kiufundi katika miradi 151 mwaka 2016 ikilinganishwa na miradi 85 mwaka 2015. Vile vile, Baraza lilifanya usuluhishi wa migogoro ya ujenzi 23 ikilinganishwa na migogoro 19 mwaka 2015.

MAENDELEO YA ARDHI

Utayarishaji wa Hatimiliki, Ukaguzi, na Uhakiki Milki

330. Mwaka 2016, jumla ya milki 32,230 zilikaguliwa, kuhakikiwa na kuandaliwa hatimiliki katika kanda nane za ardhi ikilinganishwa na milki 42,642 zilizohakikiwa na kuandaliwa mwaka 2015. Aidha, ilani za ubatisho 5,016 zilitumwa kwa wapangaji waliokiuka masharti ya upangaji ardhi ikilinganishwa

na ilani 4,313 mwaka 2015. Vile vile, jumla ya migogoro ya ardhi 820 ilitatuliwa kiutawala mwaka 2016 ikilinganishwa na migogoro 1,211 iliyotatuliwa mwaka 2015. Kwa upande wa utoaji wa vyeti vya ardhi ya vijiji na hati za hatimiliki za kimila jumla ya hatimiliki za kimila 7,833 zilitolewa ikilinganishwa na hatimiliki za kimila 18,325 mwaka 2015.

Usajili wa Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria

331. Mwaka 2016, jumla ya hatimiliki na nyaraka za kisheria 91,187 zilisajiliwa ikilinganishwa na hatimiliki na nyaraka za kisheria 77,464 zilizosajiliwa mwaka 2015. Kati ya hizo, hati za kumiliki ardhi zilikuwa 33,257; hati za umiliki wa sehemu ya jengo/eneo zilikuwa 1,410; na nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura ya 334) zilikuwa 34,682. Vile vile, nyaraka 20,525 zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka (Sura ya 117) na jumla ya rehani 1,313 zinazohamishika zilisajiliwa mwaka 2016.

Jedwali Na.15.2: Usajili wa Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria

Hati na Nyaraka zilizosajiliwa	2014	2015	2016
Hati za kumiliki Ardhi zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Hati	29,951	31,254	33,257
Hati ya sehemu ya jengo/eneo zilizosajiliwa chini ya Sheria ya usajili wa Hati 'Unit Title Act No. 17/2008'.	1,027	1,541	1,410
Nyaraka za kisheria zilizosajiliwa chini ya Sheria ya usajili wa Hati Sura Na. 334	39,540	29,546	34,682
Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka Sura Na. 117	13,403	13,041	20,525
Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya mali zinazohamishika Sura na. 210	3,100	2,082	1,313
Jumla	87,021	77,464	91,187

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Uthamini wa Mali kwa Madhumuni Mbalimbali na ya Ulipaji Fidia

332. Mwaka 2016, jumla ya taarifa za uthamini 9,047 ziliidhinishwa ikilinganishwa na taarifa 15,294 zilizoidhinishwa mwaka 2015. Idadi hii inajumuisha taarifa zilizopokelewa kutoka katika mamlaka za Serikali za itaa, kampuni binafsi za uthamini pamoja na zilizofanywa na wizara husika. Aidha, Serikali ilihakiki na kuidhinisha taarifa 192 za uthamini wa fidia zenye wafidiwa 4,984 kwa ajili ya kulipwa fidia ili kupisha miradi mbalimbali ya maendeleo kwa manufaa ya umma. Hii ilihusisha miradi ya uwekezaji kwenye

eneo la nishati, ujenzi wa barabara, kilimo, upanuzi wa bandari, mabwawa ya maji safi na upimaji wa viwanja.

Upimaji wa Mashamba na Viwanja

333. Mwaka 2016, Serikali iliidhinisha milki za ramani zenye viwanja 123,727 na mashamba 391 katika mikoa 26 ya Tanzania Bara ikilinganishwa na viwanja 135,433 na mashamba 636 yaliyoidhinishwa mwaka 2015.

Jedwali Na. 15.3: Upimaji wa Viwanja na Mashamba

Mikoa	Miliki zilizoidhinishwa mwaka 2014		Miliki zilizoidhinishwa mwaka 2015		Miliki zilizoidhinishwa mwaka 2016	
	Viwanja	Mashamba	Viwanja	Mashamba	Viwanja	Mashamba
Arusha	2,818	43	1,209	58	1,769	19
Pwani	21,141	229	20,227	241	21,539	190
DSM	9,336	0	22,178	0	29,985	1
Dodoma	2,298	0	2,512	0	1,653	0
Geita	3,945	0	2,688	0	1,808	0
Iringa	2,020	22	2,606	9	1,893	38
Kagera	1,728	37	804	14	1,211	9
Kigoma	2,812	0	3,120	0	4,773	0
Kilimanj	5,992	32	833	144	1284	0
Katavi	1,464	0	5,936	0	767	58
Lindi	6,599	1	2,786	0	3,000	4
Manyara	16,333	18	192	7	1,198	14
Mara	423	1	4,983	17	4,998	0
Mbeya	1,896	10	2,735	11	2,093	15
Morogor	4,017	71	4,877	80	6,538	4
Njombe	1,913	12	1,955	3	1829	11
Mtwara	3,440	2	1,825	2	4847	2
Mwanza	10,302	5	7,369	4	6042	0
Rukwa	695	0	659	0	248	8
Ruvuma	5,961	2	1,700	0	2,368	0
Shinyang	3,651	0	9,230	1	4,690	0
Songwe	0	0	0	0	1022	0
Singida	3,674	0	9,282	1	4,101	1
Simiyu	927	3	1,232	0	832	0
Tabora	1,008	4	16,248	0	11,524	0
Tanga	4,406	42	8,247	44	1,715	17
Jumla	118,799	534	135,433	636	123,727	391

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Mipango ya Matumizi ya Ardhi

334. Mwaka 2016, mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya tatu (3) za Ulanga, Kilombero na Malinyi iliandaliwa. Aidha, mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 79 iliandaliwa katika wilaya 25 nchini ikilinganishwa na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 91 iliyoandaliwa mwaka 2015. Lengo la mipango

hii ni kuepusha migogoro ya ardhi na kuhakikisha uwepo wa matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya kilimo, ufugaji na matumizi mengine.

Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya

335. Jumla ya mabaraza matatu (3) ya Kilindi, Kiteto na Lushoto yaliundwa mwaka 2016 ikilinganishwa na Baraza moja (1) lililoundwa mwaka 2015. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya mashauri 18,546 yalifunguliwa katika mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya na kufanya jumla ya mashauri kufikia 44,859. Kati ya hayo, mashauri 20,667 yaliamuliwa na mashauri 24,192 yaliendelea kusikilizwa ikilinganishwa na mashauri 12,163 yaliyoamuliwa mwaka 2015.

MAENDELEO YA MAKAZI

Ujenzi wa Nyumba za Makazi na Biashara

336. Mwaka 2016, Shirika la Nyumba la Taifa lilijenga nyumba za biashara na makazi 2,033 ikilinganishwa na nyumba za biashara na makazi 3,831 mwaka 2015.

Jedwali Na.15.4: Nyumba zilizojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa

Mikoa	2015				2016				
	Aina ya Nyumba			Jumla	Aina ya Nyumba				Jumla
	Makazi/Ghar		Biashara		Makazi/Ghar		Biashara	Matumizi Mengineyo	
	Nafuu	Kati & Juu		Nafuu	Kati & Juu				
Arusha	40	100	0	140	20	100	0	0	120
Pwani	0	0	0	0	0	0	0	0	0
D'Salaam	0	1,280	2,299	3,579	0	630	276	0	906
Dodoma	44	153	0	197	44	155	0	0	199
Geita	68	0	0	68	48	0	0	0	48
Iringa	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Kagera	20	0	45	65	20	0	0	0	20
Katavi	100	0	59	159	70	0	0	0	70
Kigoma	36	0	0	36	36	0	0	0	36
K' Njaro	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Lindi	30	0	0	30	30	0	0	0	30
Manyara	40	0	0	40	40	0	0	0	40
Mara	52	0	59	111	0	0	40	0	40
Mbeya	35	0	13	48	14	0	26	0	40
Morogoro	42	0	58	100	42	0	0	0	42
Mtwara	55	30	236	321	0	33	0	281	314
Mwanza	62	0	0	62	0	0	0	0	0
Njombe	52	0	0	52	0	0	0	0	0
Ruvuma	18	0	0	18	18	0	0	0	18
Rukwa	20	0	0	20	0	0	0	0	0
Simiyu	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Singida	20	0	57	77	20	0	0	0	20
Songwe	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Shinyanga	51	0	0	51	0	0	0	0	0
Tabora	81	0	0	81	50	0	0	0	50
Tanga	40	0	0	40	40	0	0	0	40
Jumla	906	1,563	2,826	5,295	492	918	342	281	2,033

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

SURA YA 16

MAWASILIANO NA UCHUKUZI

Kiwango cha Ukuaji

337. Mwaka 2016, shughuli za kiuchumi za habari na mawasiliano zilikuwa kwa kiwango cha asilimia 13.0 ikilinganishwa na asilimia 12.1 mwaka 2015. Ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa matumizi ya huduma za simu za viganjani, muda wa maongezi, utangazaji na huduma ya intaneti nchini. Kwa upande mwingine, shughuli za uchumi za usafirishaji na uhifadhi mizigo zilikuwa kwa asilimia 11.8 ikilinganishwa na asilimia 7.9 mwaka 2015. Ukuaji huo ulitokana na: kuongezeka kwa shehena ya mizigo iliyohudumiwa katika bandari; kuongezeka kwa abiria na shehena ya mizigo iliyosafirishwa kwa njia ya barabara, reli na anga; na kuongezeka kwa ufanisi katika huduma za upakiaji na upakuaji wa mizigo bandarini. Mchango wa huduma za usafirishaji na uhifadhi mizigo katika Pato la Taifa uliendelea kuwa asilimia 4.3 mwaka 2016 kama ilivyokuwa mwaka 2015. Aidha, mchango wa shughuli za huduma za habari na mawasiliano katika Pato la Taifa mwaka 2016 ulikuwa asilimia 2.0, sawa na ilivyokuwa mwaka 2015.

UCHUKUZI

Usafiri wa Barabara

338. Mwaka 2016, jumla ya leseni 146,974 za usafirishaji zilitolewa ikilinganishwa na leseni 135,072 zilizotolewa mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 8.8. Kati ya leseni zote zilizotolewa, leseni 46,691 zilitolewa kwa basi ya abiria kwa ajili ya masafa marefu na mijini, leseni 87,383 zilitolewa kwa magari ya mizigo yenye uwezo wa kubeba shehena kuanzia tani tatu na kuendelea na leseni 12,900 zilitolewa kwa pikipiki zilizojihusisha na ubebaji wa abiria kibiashara.

Jedwali Na. 6.1: Leseni za usafirishaji Zilizotolewa

Leseni	2015	2016
Mabasi ya Abiria	47,451	46,691
Magari ya Mizigo	81,567	87,383
Bajaj/Pikipiki	6,054	12,900
Jumla	135,072	146,974
Ratiba za mabasi	6,077	6,637

Chanzo: SUMATRA

Kampuni ya Reli Tanzania (TRL)

339. Mwaka 2016, Kampuni ya reli ilisafirisha shehena tani 209,203 kwa umbali wa kilometa 230,203,929 ikilinganishwa na tani 211,016 zilizosafirishwa kwa umbali wa kilometa 230,865,230 mwaka 2015, sawa na upungufu wa shehena kwa asilimia 0.86. Kupungua kwa shehenailiyosafirishwa kulitokana na kusitishwa kwa safari za treni kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe mwezi Februari hadi Aprili 2016 kulikosababishwa na mafuriko. Aidha, abiria 517,358 walisafirishwa mwaka 2016, ikilinganishwa na abiria 405,360 waliosafirishwa mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 27.6. Ongezeko hilo lilitokana na kuanzishwa kwa treni maalumu (Delux Train) iendayo Kigoma na Mwanza, pia kuanza kwa huduma ya treni ya kawaida ya abiria.

Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)


340. Mwaka 2016, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia ilisafirisha shehena tani 128,105 ikilinganishwa na tani 87,860 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 45.8. Aidha, jumla ya abiria 414,746 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 455,117 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 8.9.

Usafiri wa Anga

Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA)


341. Mwaka 2016, jumla ya kampuni 61 za usafiri wa ndege zilikuwa zinatoa huduma ya usafiri wa anga ikilinganishwa na kampuni 47 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 29.8. Hadi Desemba 2016, mashirika ya ndege ya kimataifa (ya ndani na nje) yaliyokuwa yanatoa huduma kwa utaratibu wa *Bilateral Aviation Safety Agreement (BASA)*, yalikuwa 29 sawa na ilivyokuwa mwaka 2015. Aidha, idadi ya abiria waliowasili na kuondoka katika viwanja vya ndege nchini iliongezeka kutoka abiria 4,850,017 mwaka 2015 hadi abiria 4,912,186 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 1.3. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa miruko ya ndege kwa wiki kwa watoa huduma wafuatao: Kenya airways, Qatar, ATCL, Precision Air na Rwanda Air.

Kielelezo Na. 16.1: Idadi ya Abiria Waliowasili na Kuondoka Nchini




342. Mwaka 2016, safari za ndege ziliongezeka hadi 233,260 kutoka 225,103 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 3.6. Ongezeko hilo lilitokana na kuanza kutolewa kwa huduma za mashirika ya ndege ya Air Mauritius na Air Zimbabwe. Katika kipindi hicho, mizigo iliyosafirishwa ilipungua kutoka tani 30,023 hadi tani 27,362 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 8.9. Upungufu huu ulitokana na kupungua kwa usafirishaji wa maua na mbogamboga kwenda nje ya nchi.

Kielelezo Na. 16.2: Idadi ya Safari za Ndege



Kielelezo Na.16.3: Tani za Mizigo Zilizosafirishwa



Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

343. Mwaka 2015/16, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ilihudumia shehena tani milioni 15.293 ikilinganishwa na tani milioni 16.001 zilizohudumiwa mwaka 2014/15, sawa na upungufu wa asilimia 4.4. Aidha, katika kipindi hicho, shehena iliongezeka katika bandari za Tanga, Kilwa, Lindi na Mafia pamoja na Kigoma wakati bandari za, Dar es Salaam, Mwanza na Kyela shehena ilipungua. Upungufu huo ulitokana na uchache wa meli za kubeba mabehewa katika Ziwa Victoria, kuharibika mara kwa mara meli ya kubeba shehena ya mbolea katika bandari ya Kyela kwenda Malawi, ambapo kwa sasa shehena hii inasafirishwa kwa njia ya barabara na kuendelea kutumika kwa magati binafsi kwa bandari za Ziwa.

Jedwali Na. 16.2: Shehena Zilizosafirishwa (Tani, Milioni)

Kituo (Bandari)	2014/2015	2015/16	Badiliko (%)
Bandari Kuu za Mwambao			
Dar es Salaam	14.803	14.033	3.1
Tanga	0.645	0.677	74.2
Mtwara	0.2966	0.273	-16.8
Jumla ndogo	15.745	14.983	4.4
Bandari ndogo na Bandari za Maziwa Makuu			
Kilwa, Lindi na Mafia	0.026	0.046	0.046
Mwanza	0.129	0.123	0.123
Kigoma	0.099	0.139	0.139
Kyela	0.002	0.0004	0.0004
Jumla ndogo	0.231	0.264	0.264
Jumla Kuu	16.001	15.293	15.293

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

344. Mwaka 2015/16, idadi ya kontena iliyohudumiwa na kitengo cha mizigo ya kawaida kinachosimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ilipungua kutoka kontena (TEUs) 213,115 mwaka 2014/15 hadi kontena (TEUs) 130,893, sawa upungufu wa asilimia 38.6. Aidha, katika kipindi hicho, kitengo cha kontena cha TICTS kilihudumia kontena 202,463 ikilinganishwa na kontena 126,663 mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 59.8 Vile vile, kitengo cha kontena cha TICTS kilihudumia kontena (TEUs) 497,769 ikilinganishwa na kontena (TEUs) 465,851 zilizohudumiwa mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 6.9.

Jedwali Na. 16.3: Shehena ya Kontena (TEUs) Katika Bandari ya Dar es Salaam

	2014/2015	2015/2016
TICTS	465,851	497,769
General Cargo	213,115	130,893
Jumla ndogo	678,966	628,662
Tanga	10,207	8,118
Mtwara	12,982	14,337
Jumla ndogo	23,189	22,455
JUMLA KUU	702,155	651,117

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

345. Mwaka 2015/16, Mamlaka ilihudumia jumla ya abiria 1,827,666 ikilinganishwa na abiria 1,963,468 waliohudumiwa mwaka 2014/15, sawa na upungufu wa asilimia 6.9. Upungufu huo ulitokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya barabara.

Jedwali Na.16.4: Idadi ya Abiria Waliohudumiwa

Bandari	2009/10	2010/11	2011/12	2012/13	2013/14	2014/15	2015/16
DSM	892,465	1,008,731	1,342,875	1,373,146	1,412,357	1,569,053	1,614,831
Tanga	16,670	23,287	12,747	23,287	12,747	-	-
Mwanza	819,730	593,342	524,457	395,808	735,794	340,125	206,763
Kigoma	19,626	21,033	25,066	20,063	15,239	38,749	4,700
Kyela	12,607	9,913	8,334	13,756	12,325	15,541	1,372
Jumla	1,761,098	1,656,306	1,913,479	1,826,060	2,188,462	1,963,468	1,827,666

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)

Muda wa Meli kukaa Bandarini

346. Mwaka 2015/16, muda wa meli kukaa bandarini kwa kitengo cha kontena ulipungua na kufikia siku 2.0 kutoka siku 2.5 mwaka 2014/15. Aidha, kwa upande wa mizigo ya kawaida muda wa meli kukaa bandarini ulipungua na kufikia siku 2.5 kutoka siku 3.1 mwaka 2014/15. Hii ilitokana na bandari kufanya kazi saa 24 kwa siku saba za wiki. Aidha, katika kitengo cha mafuta muda uliongezeka na kufikia siku 3.2 kutoka siku 3.1 mwaka 2014/15. Kwa mizigo ya kontena, muda wa kukaa bandarini baada ya kupakuliwa kutoka melini na kabla ya mteja kuchukua uliendelea kuwa wastani wa siku 10.2 kama ilivyokuwa mwaka 2014/15.

Shehena za Nchi Jirani

347. Mwaka 2015/16 jumla ya tani 4,839,467 za mizigo ya kwenda nchi jirani zilihudumiwa katika bandari ya Dar es Salaam ikilinganishwa na tani 5,013,452 zilizohudumiwa mwaka 2014/15, sawa na upungufu wa asilimia 3.5. Upungufu huo ulitokana na bandari shindani za nchi jirani.

Jedwali Na.16.5 : Shehena za Nchi Jirani

Nchi	2009/10	2010/11	2011/12	2012/13	2013/14	2014/15	2015/16
Zambia	1,112,283	1,500,459	1,627,537	1,858,718	1,818,141	1,737,650	1,819,069
DR Congo	568,275	800,986	965,639	965,377	1,352,457	1,677,527	1,464,847
Burundi	327,468	384,648	336,410	308,180	346,159	332,263	351,044
Rwanda	261,068	301,778	436,029	636,998	670,634	724,683	839,826
Malawi	131,532	136,375	92,869	93,411	141,536	94,294	106,883
Uganda	32,612	45,453	74,670	190,876	122,318	127,737	156,105
Nyinginezo	8,319	303,571	360,059	70,148	118,206	319,298	101,693
JUMLA	2,441,557	3,473,270	3,893,213	4,123,708	4,569,451	5,013,452	4,839,467

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

Uchukuzi kwenye Maziwa

Kampuni ya Huduma za Meli

348. Mwaka 2016, jumla ya abiria 101,103 walisafirishwa na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) ikilinganishwa na abiria 122,769 waliosafirishwa mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 17.7. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya tani za mizigo 18,419 zilisafirishwa ikilinganishwa na tani za mizigo 42,178 zilizosafirishwa mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 56.3.

Kampuni ya meli ya China na Tanzania (SINOTASHIP)

349. Mwaka 2016, Kampuni ya Meli ya China na Tanzania ilisafirisha shehena tani 390,000 ikilinganishwa tani 380,000 zilizosafirishwa mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 2.6. Ongezo hilo lilitokana na Meli kufanya jumla ya safari 11 ambazo nyingi zilikuwa za masafa mafupi. Aidha, makasha 8,800 yalihudumiwa na kampuni katika bandari ya Da-es Salaam ikilinganishwa na makasha 4,320 ya mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 103.7. Ongezeko hilo lilitokana na kampuni kupanua biashara ya uwakala na kuhudumia meli nyingi zaidi.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

350. Mwaka 2016, idadi ya meli na boti zilizopatiwa huduma za hali ya hewa katika Bahari ya Hindi ilifikia meli na boti 2,586 ikilinganishwa na meli na boti 2,651 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 2.5. Kupungua kwa idadi ya meli zilizopewa huduma za hali ya hewa kulitokana na kusitisha huduma kwa baadhi ya kampuni zinazotoa huduma ya usafiri ikiwa ni pamoja na Royal, Spider, Kilimanjaro II, Seabus I & II na Buraq. Aidha, katika kipindi hicho, huduma za hali ya hewa kwa sekta za nishati, utalii, ujenzi, kilimo na elimu zilitolewa ambapo jumla ya maombi 268 ya taarifa za hali ya hewa yalifanyiwa kazi ikilinganishwa na maombi 193 mwaka 2015.

Huduma za Mawasiliano

Huduma za Posta

351. Mwaka 2016, Shirika la Posta Tanzania lilisafirisha barua 24,445,425 ndani ya nchi ikilinganishwa na barua 16,904,137 zilizosafirishwa mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 44.61. Ongezeko hilo limetokana na juhudi za kuwapata wateja wa barua za jumla (bulk post). Aidha, barua zilizotumwa nje ya nchi mwaka 2016 zilikuwa 3,405,317 ikilinganishwa na barua 8,189,193 zilizotumwa mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 58.4. Upungufu huo ulitokana na kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia na mitandao ya kijamii.

352. Mwaka 2016, idadi ya vifurushi vilivyosafirishwa ndani ya nchi ilikuwa 86,902 ikilinganishwa na vifurushi 37,459 vilivyosafirishwa mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 131. Ongezeko hilo lilitokana na kupatikana kwa aina mbalimbali za usafirishaji na kuendelea kukua kwa biashara. Aidha, vifurushi vilivyotumwa nje ya nchi mwaka 2016 vilikuwa 4,242 ikilinganishwa na vifurushi 8,468 vilivyotumwa mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 49.9.

353. Mwaka 2016, jumla ya rejesta 578,731 zilisafirishwa nchini ikilinganishwa na rejesta 608,185 zilizosafirishwa mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 4.8. Upungufu huo ulitokana na kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia na mitandao ya kijamii. Aidha, rejesta zilizotumwa nje ya nchi mwaka 2016 zilikuwa 46,069 ikilinganishwa na rejesta 42,975 zilizotumwa mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 7.2. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kuimarika kwa mtandao unaomwezesha mteja kufuatilia na kutafuta mzigo wake (track and trace).

354. Mwaka 2016, nyaraka na vipeto vilivyotumwa kwa njia ya haraka (EMS) nchini vilikuwa 825,479 ikilinganishwa na nyaraka na vipeto 625,372 vilivyotumwa mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 32.0. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa wateja wanaohusiana na Bodi ya Mikopo ya

Wanafunzi wa Elimu ya Juu na uwekezaji katika vifaa vya usambazaji na rasilimali watu. Aidha, idadi ya nyaraka na vipeto vilivyotumwa nje ya nchi kwa njia ya haraka mwaka 2016 vilikuwa 24,981 ikilinganishwa na nyaraka na vipeto 43,009 vilivyotumwa mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 41.9. Vile vile, mwaka 2016 barua na nyaraka 72,327 zilipokelewa na kusambazwa kwa njia ya huduma ya usambazaji wa barua za haraka ndani ya miji ikilinganishwa na barua na nyaraka 56,467 zilizopokelewa na kusambazwa mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 28.1. Ongezeko hili lilitokana na utangazaji na uboreshaji wa huduma za usambazaji wa barua na nyaraka.

355. Mwaka 2016, jumla ya miamala ya fedha 516 ilihaulishwa kwa njia ya kielektroniki (Electronic Money Transfer) ikilinganishwa na miamala 284 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 81.7. Aidha mwaka 2016, miamala ya fedha 7,039 ilitumwa kupitia mfumo wa Kimataifa wa Utumaji Fedha ikilinganishwa na miamala 10,343 iliyotumwa mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 31.9. Katika kipindi hicho, wateja 168,867 walihudumiwa kwa kupitia huduma ya kufanya malipo kwa uwakala ya Post Giro ndani ya nchi ikilinganishwa na wateja 177,645 waliohudumiwa mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 5.0.

Huduma za Simu

356. Hadi kufikia Desemba 2016, mitandao ya simu za viganjani ilikuwa na jumla ya kadi za simu 40,044,186 ikilinganishwa na kadi 39,808,419 katika kipindi kama hicho mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 0.6. Ongezeko hili lilitokana na kukua na kuimarika kwa huduma zitolewazo na mitandao ya simu za viganjani na kuongezeka kwa ushindani. Kati ya kadi hizo za simu kwa mwaka 2016 zilizosajjiwa rasmi ni 39,229,918 sawa na asilimia 98.0 ya kadi zote. Aidha, kati ya kadi zote, kampuni ya simu ya Vodacom ilikuwa na asilimia 31.0 ya kadi zote na kampuni ya Tigo (asilimia 29.2); Airtel (asilimia 26.1); Zantel (asilimia 2.7); Smart (asilimia 2.0) Halotel (asilimia 8.6) na TTCL (asilimia 0.4). Aidha, watumiaji wa simu za mezani walipungua kutoka watumiaji 142,819 mwaka 2015 hadi watumiaji 129,597 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 6.6.

Jedwali Na.16.6: Idadi ya Wanaotumia Simu za Mezani na Viganjani

Kampuni za Simu	Idadi ya Kadi za Simu			Badiliko (%)
	2014	2015	2016	
Vodacom Mobile	11,810,064	12,714,297	12,419,425	(2.32)
Tigo Mobile	8,624,638	11,115,991	11,677,344	5.05
Airtel Mobile	9,551,977	11,047,505	10,456,117	(5.35)
Zantel Mobile	1,719,222	1,839,391	1,083,157	(41.11)
TTCL Mobile	156,227	304,214	166,383	(45.31)
Halotel		1,226,678	3,438,509	180.31
Smart		1,560,343	803,251	(48.52)
Jumla Simu za Kiganjani	31,862,128	39,808,419	40,044,186	0.59
Simu za Mezani	Idadi ya Wateja			
TTCL Fixed	140,391	138,754	127,112	(8.39)
Zantel Fixed	10,883	4,065	2,485	(38.87)
Jumla ya Simu za mezani	151,274	142,819	129,597	(9.26)

Chanzo: Mamlaka ya Mawasiliano

Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

357. Mwaka 2016, jumla ya kilometa 18,192 za miundombinu ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano zilijengwa, ambapo kilometa 12,532 zilijengwa chini ya ardhi na kilometa 5,660 juu ya ardhi katika wilaya zote nchini. Hadi Desemba, 2016 mawasiliano yalifika katika vijiji 2,889, halmashauri za wilaya 123, hospitali za wilaya 74, vituo vya Polisi vya wilaya 131 pamoja na ofisi za Posta 68. Vile vile, miundombinu ya mtandao wa intaneti ilijengwa kwenye shule 417.

Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

Uendelezaji wa Rasilimali Watu

358. Mwaka 2016, Serikali ilindelea na juhudi za kuongeza rasilimali watu katika teknolojia na tasnia ya ubunifu nchini. Katika kuhakikisha hilo, jumla ya wanafunzi 3,982 walidahilwa katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ikilinganishwa na wanafunzi 3,743 waliidahiliwa mwaka 2015. Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Dar es Salaam ilidahili wanachuo wapya 2,298 ikilinganishwa na wanachuo 1,386 waliidahiliwa mwaka 2015. Kati ya hao, wanafunzi 1,577, walijiunga katika ngazi ya Stashahada, 670 Shahada na 51 Shahada ya Uzamili. Vile vile, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela ilidahili wanachuo 198 ambapo wanachuo 135 walikuwa ngazi ya Shahada ya Uzamili na 63 Shahada ya Uzamivu.

Udhibiti wa Mionzi

359. Mwaka 2016, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ilipokea na kutathmini jumla ya maombi 273 yahasuyo vifaa na matumizi ya mionzi ikilinganishwa na maombi 281 yaliyopokelewa mwaka 2015. Kati ya hayo, maombi 29 yalihusu leseni za kuanzisha vituo vipya vinavyotumia na kumiliki vyanzo vya mionzi na maombi 244 yalihusu umiliki na utumiaji wa vyanzo vya mionzi. Katika maombi ya umiliki na utumiaji wa vyanzo vya mionzi, maombi 216 yalihusu leseni ya kutumia mionzi, maombi 15 yalihusu leseni ya uingizaji vyanzo vya mionzi nchini, maombi 9 yalihusu usafirishaji wa vyanzo vya mionzi nchini na maombi 4 yalihusu usafirishaji wa vyanzo vya mionzi nje ya nchi. Aidha, Tume ilitathmini vigezo vya ubora na kubaini kwamba maombi hayo yalilikidhi mahitaji ya sheria ya Nguvu za Atomiki na kupatiwa leseni. Vile vile, Tume ilifanya ukaguzi wa vituo 131 vinavyotumia mionzi ili kujiridhisha kama vinakidhi vigezo vilivyoainishwa kwenye Sheria ya Nguvu za Atomiki na kutoa ushauri kwa lengo la kuhakikisha usalama kwa watumiaji, raia na mazingira. Kati ya vituo hivyo, 102 vilikidhi vigezo, viwili (2) vilifungiwa hadi virekebishe kasoro kubwa zilizooneka, 26 vilipewa muda wa kurekebisha kasoro ndogo ndogo zilizobainishwa na kimoja (1) kilikutwa hakifanyi kazi.

HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Sekta ya Habari

360. Mwaka 2016, kulikuwa na jumla ya magazeti 428 yaliyosajiliwa ikilinganishwa na magazeti 875 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 51.1. Upungufu huu ulitokana na magazeti 473 kufutiwa usajili kwa kutochapisha kwa miaka mitatu mfululizo kinyume na taratibu za usajili. Aidha, katika kipindi hicho, vyombo vya habari ambavyo ni magazeti na majarida 26, redio 23 na televisheni 6 vilisajiliwa.

Jedwali 16.7: Idadi ya Vituo vya Radio na Televisheni Vilivyosajiliwa

Mwaka	Idadi ya Magazeti	Idadi ya Redio	Idadi ya vituo vya Televisheni
2010	8	14	1
2011	41	12	0
2012	29	12	0
2013	36	4	0
2014	23	8	3
2015	39	22	1
2016	26	23	6

Chanzo: Idara ya Habari - MAELEZO, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

Sekta ya Maendeleo ya Sanaa

361. Mwaka 2015/2016, Serikali kupitia Bodi ya Filamu Tanzania ilitoa vibali 168 vya utengenezaji wa filamu, makala za filamu na picha jongevu kwa kampuni za utengenezaji kutoka ndani na nje ya nchi ikilinganishwa na vibali 169 vilivyotolewa mwaka 2014/2015.

Jedwali 16.8: Idadi ya Vibali vya Kutengeneza Filamu Vilivyotolewa Nchini

Mwaka	Vibali kwa Wageni	Vibali kwa Watanzania	Jumla
2011/12	84	21	105
2012/13	123	30	153
2013/14	125	33	158
2014/15	133	36	169
2015/16	137	31	168
Jumla	602	151	753

Chanzo: Bodi ya Filamu Tanzania

Sekta ya Maendeleo ya Michezo

362. Mwaka 2016, kulikuwa na jumla ya vilabu vya michezo 331 vilivyosajiliwa ikilinganishwa na vilabu 224 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 47.8. Ongezeko hilo lilitokana wananchi kuzingatia sheria zinazohimiza usajili vilabu. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya vyama vya michezo 9 vilisajiliwa ikilinganishwa na vyama 15 vilivyosajiliwa mwaka 2015. Vile vile, katika kipindi hicho, jumla ya vituo 15 vya michezo vilisajiliwa ikilinganishwa na vituo 12 mwaka 2015.

Jedwali 16.9: Idadi ya Vilabu, Vyama na Vituo vya Michezo Vilivyosajiliwa

Mwaka	Vilabu vya Michezo	Vyama vya Michezo	Vituo vya Michezo
2010	272	9	9
2011	168	5	2
2012	339	26	5
2013	285	37	12
2014	464	17	7
2015	224	15	12
2016	331	9	15

Chanzo: Idara ya Maendeleo ya Michezo

SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jedwali Na. 67

Maelezo	Kipimo	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016
Urefu wa Reli	KM	2707	2707	2707	2707	2707	2707	2707	2707	2707	2707
Magari ya Moshi:	Namba	84	45	43	25	22	20	45	45	30	25
Mvuke	Namba	1	1	1	0	0	0	0	0	0	0
Dizeli	Namba	83	45	0	0	0	0	0	0	0	0
Mainlain		62	5	5	21	19	16	38	38	21	40
Shunting		21	40	38	4	3	4	7	7	9	4
Jumla ya mabehewa:	Namba	1912	1648	1357	1071	1326	1162	1200	1214	1155	426
Abiria	Namba	102	45	68	50	53	36	91	91	56	56
Mizigo ya kawaida	Namba	1369	1190	1093	648	658	635	681	590	561	22
Mafuta	Namba	208	244	178	179	335	208	178	203	196	123
Mifugo	Namba	76	18	39	88	88	80	39	64	64	27
Mengineyo	Namba	157	151	105	106	192	203	211	266	278	198
Uchukuzi	Namba										
Abiria	000	524	392	285	284	227	339	373	170	196	1707
Mizigo	Tani'000	714	429	237	265	138	154	185	127	283	102

Chanzo: Shirika la Reli Tanzania

RELI YA UHURU - TAZARA

Jedwali Na. 68

Maelezo	Kipimo	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016
Urefu wa Reli Kuu	Km	1860	1860	1860	1860	1860	1860	1860	1860	1860	1860
Magari ya Moshi	Namba	19	10	16	15	13	13	15	16	17	21
Reli Kuu	Namba	14	8	11	10	9	9	11	13	12	14
Ya kujongeza	Namba	5	2	5	5	4	5	4	3	6	7
Mabehewa ya abiria	Namba	71	62	53	36	36	35	52	50	51	56
Abiria	Namba	59	53	44	31	30	30	45	44	43	48
Chakula	Namba	8	4	3	2	3	2	3	3	3	4
Vifurushi	Namba	4	5	6	3	3	3	4	3	5	4
Mabehewa ya mizigo	Namba	1458	1371	1412	1620	930	858	1391	1101	1142	1221
Mizigo ya kawaida	Namba	1295	1217	1174	1381	795	765	1229	966	1007	1077
Mifugo	Namba	6	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Mafuta	Namba	81	114	196	197	93	59	104	82	82	89
Barafu	Namba	10	4	7	7	7	0	5	5	5	5
Mengineyo	Namba	2	2	2	2	2	1	1	1	1	1
Breki	Namba	46	17	16	16	16	16	35	30	30	32
Ballast	Namba	18	17	17	17	17	17	17	17	17	17
Uchukuzi mizigo (Tani)	000	569	525	333	540	248	259	245	33	81	96
Abiria	000	1000	1177	923	758	414	678	654	287	327	440

Chanzo: Mamlaka ya Reli ya Uhuru

+ Urefu ni km. 1860.54, km 974.814 zikiwa nchini Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

USAFIRISHAJI KWA MELI: DAR ES SALAAM

Jedwali Na. 69

Maelezo	Kipimo	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016
Jumla ya meli	Namba	3038	697	1842	1274	1232	1600	742	1426	4028	1600
Uwezo wa kubeba mizigo	000	16588	7260	17472	18721	24240	24496	13359	23278	24506	31212
Jumla ya abiria	000	714	310	141	228	312	375	347	1000	1023	1748
Jumla ya bidhaa zote	000wt	5703	2316	4946	4954	5432	10122	5547	9082	9369	10814
Bidhaa zilizopakuliwa	000wt	4932	2136	4382	4559	4816	9018	3899	7998	5556	10043
Za kawaida	000wt	2762	1053	2430	2159	2474	5021	2682	4495	2951	4791
Saruji	000wt	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Mafuta	000wt	2054	1013	1852	2400	2342	3997	1217	3489	2605	5223
Mengineyo ¹	000wt	116	70	100	0	0	0	0	14	0	29
Bidhaa zilizopakiwa	000wt	761	181	497	466	616	1105	414	808	780	789
Za kawaida	000wt	713	153	466	419	557	1033	391	763	738	674
Mafuta	000wt	48	28	24	47	59	72	23	45	42	87
Mengineyo ¹	000wt	0	0	7	0	0	0	0	0	0	28
Mabadilishano	000wt	126	-	68	0.1	32	15	0	275	49	20

Chanzo: Mamlaka ya Bandari

1 Kama vile mbolea, mollasses, tallow fats n.k

- Takwimu hazikupatikana

USAFIRISHAJI KWA MELI: TANGA

Jedwali Na. 69 (linaendelea)

Maelezo	Kipimo	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016
Jumla ya meli	Namba	242	95	144	215	201	232	92	64	63	87
Uwezo wa kubeba mizigo	000	551	133	671	1059	1005	1378	700	990	620	945
Jumla ya abiria	000	7.1	8.3	0	228	312	2865	0	0	0	0
Jumla ya bidhaa zote	000wt	542	178	359	529	508	608	271	536	475	500
Bidhaa zilizopakuliwa	000wt	330	836	213	357	373	1051	5357	437	308	469
Za kawaida	000wt	242	817	147	313	365	436	3171	437	308	338
Mafuta	000wt	88	19	66	44	8	615	2186	0	0	131
Bidhaa zilizopakwiwa	000wt	212	66	145	171	507	166	912	100	64	75
Za kawaida	000wt	212	66	145	171	507	166	912	100	64	75
Mafuta	000wt	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Mabadilishano	000wt	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

USAFIRISHAJI KWA MELI: MTWARA

Jedwali Na. 69 (linaendelea)

Maelezo	Kipimo	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016
Jumla ya meli	Namba	99	36	32	58	129	498	339	428	166	113
Uwezo wa kubeba mizigo	000	251	131	31	455	307	1557	1245	1343	475	778
Jumla ya abiria	000	10	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Jumla ya bidhaa zote	000	112	82	95	107	112	178	144	248	125	379
Bidhaa zilizopakuliwa	000wt	53	26	23	39	44	309	894	149	57	151
Za kawaida	000wt	47	22	23	36	35	55	274	140	56	151
Mafuta	000wt	6	4	0	3	9	254	620	9	1	0
Bidhaa zilizopakiwa	000wt	59	56	72	68	71	123	70	100.3	67	6
Za kawaida	000wt	59	56	72	68	71	113	70	100	67	6
Mafuta	000wt	-	-	-	-	-	10	0	0.3	0	0
Mabadilishano	000wt	-	-	-	-	-	0	0	0	0	0

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

HUDUMA ZA POSTA

Jedwali Na. 70

Maelezo	Kipimo	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016
Ofisi Ndogo Posta	Namba	162	167	202	171	105	65	74	74	65	65
Franchised Post Offices	Namba	86	113	81	81	151	112	89	89	90	90
Ofisi Kubwa	Namba	113	172	170	170	163	147	160	160	158	158
Jumla	Namba	361	452	453	422	419	324	323	323	313	313
Masanduku Binafsi	000	173	174	117		146	162	173	142	160	160
Masanduku Yaliokodishwa	000	150	130	87	120	130	140	148	128	138	138
Maombi Yasiotimizwa	000	0	5	4	0	21	28	25	18	4	1
Mifuko Pekee Iliyokodishwa	Namba	217	182	62	183	361	278	212	260	180	180
Barua Zilizotumwa bila Vifurushi	Mill.	24	15	14	29	27	15	26	15	10	4
Regista na Barua za Amana	000	41	307	377	480	347	397	568	455	402	297
Vifurushi Nchini	000	29	18	9	15	10	15	29	12	17	36
Vifurushi Nje	000	12	6	2	7	11	12	9	5	9	2
Leseni za kuuza stamp	Namba	6324	6242	6256	25145	28257	33311	2637	3715	0	0
Huduma za Haraka, barua na vifurushi	"										
Ndani ya Nchi	"	262381	216762	493709	283711	501635	404453	620478	406732	416007	452827
Nje ya Nchi	"	12289	14650	4012	18766	16965	24347	17130	20564	308288	6364
EMS Money Fax	"	379084	366382	23165	82002	36357	2940	550	745	748	272
EMS Fax (Fax message received)	"	14659	121901	103558	31594	1595	876187	544	1194	3844	2518
Overnight Mail Services	"						9963	115126	0	0	0
Mifuko ya Barua Iliyosafirishwa	"	75900	85595	68912	76983	115403	50082	87051	46652	53639	57605
Vifurushi vya magazeti vilivyosafirishwa	"	20314	12754	13934	2752	12040	10652	18784	8700	9130	113448
Huduma za gari ndogo											
Idadi ya Mifuko ya Barua Iliyosafirishwa	"	6542	4328	268	0	193	24095	849	714	9576	-
Amana za Haraka Zilizotolewa	"	214558	0	20057	8169	4717	3087	2034	845	58423	272
Amana za Haraka Zilizolipwa	"	132030	93508	23069	11881	17397	516	555	0	0	0
Amana za Haraka za Nje ya Nchi											
Zilizotumwa	"	1519	1354	1030	1027	998	369	478	325	221	220
Zilizopokelewa	"	686	671	150	150	217	77	83	227	283	116
Amana za Posta zilizouzwa	"	9152	8062	8831	1924	633	414	684	261	251	107
Amana za Posta Zilizolipwa	"	4615	5709	5490	3262	1662	252	166	67	25	18
Benki ya Akiba (Transaction)											
Uwekaji Amana (Deposit)	"	25382	24574	9535	18863	13438	6260	21491	12732	21541	261423
Uchukuaaji Amana (Withdrawal)	"	19534	21122	11663	23025	72358	17527	37556	12807	18098	45449

Chanzo: Shirika la Posta

IDADI YA WANAOTUMIA SIMU ZA MEZANI NA VIGANJANI

Jedwali Na. 71

Kampuni	2006	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016
A. Simu za Kiganjani											
Mobitel/Tigo	760874	1191678	2084878	4178089	4477510	5450766	6370796	6297288	8624638	10639610	11677344
Vodacom	2975580	3870843	5269761	6883661	8670536	11625775	9357672	10288972	11810064	12520645	12419425
Airtel	2148336	2505546	3866906	4910359	6021091	6993418	8356095	8995824	9551977	10887742	10456117
Zantel	355993	684214	1087713	1378595	1715985	1524601	3083889	1814444	1730105	1563503	1083157
Benson	0	3300	3000	3101	2396	1558	725	528	528	528	803251
TTCL Mobile	6390	72729	105804	115681	246019	225578	221663	210766	296618	165460	166383
Sasatel					24827	5824	4810	0	0	0	0
Hallotel										0	3438509
Jumla Ndogo	6247173	8328310	12418062	17469486	21158364	25827520	27395650	27607822	32013930	35777488	40044186
B. Simu za Mezani											
TTCL	150897	157816	116265	157321	159054	159364	166148	158935	140391	140391	127112
Zantel	747	5453	7544	15601	15457	1699	10219	6064	10833	10833	24585
Jumla Ndogo	151644	163269	123809	172922	174511	161063	176367	164999	151224	151224	151697
Jumla Kuu	6398817	8491579	12541871	17642408	21332875	25988583	27572017	27772821	32165154	35928712	40195883

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

P - Takwimu za Awali

SHIRIKA LA NDEGE TANZANIA (ATCL)⁺

Jedwali Na.73

Maelezo	Kipimo	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016
Tani-Kilometa:											
Zilizokuwepo	000	32533	-	5313	9482	1662	1932	6154	3052	60042	3937
Zilizotumika	000	18480	-	1508	2888	268	815	2503	117	30889	1756
Matumizi	%	56.7	-	28.4	30.5	16.0	42.0	40.7	3.8	54.4	46.9
Viti-kilometa:											
Vilivyokuwepo	000	306461	469426	41396	59724	7140	15131	54665	3680	21693	37877
Vilivyotumika	000	190006	129000	16469	30527	2946	10209	27279	946	11472	20692
Matumizi	%	62.0	27.5	39.8	51.1	41.0	67.0	50.0	25.7	52.8	56.0
Abiria ⁺⁺	000	190	188	27	41	9	11	35	56	31	28
Mizigo ya ziada	Tani	103	30	9	8	2	0	45	0	53	1
Mizigo mingine	Tani	1123	1044	54	145	4	5	35	45	42	7
Shehena za Posta	Tani	241	162	11	30	0	0	25	405	4	-

Chanzo: Shirika la Ndege Tanzania

- + Zinahusu "scheduled traffic" tu
- ++ Abiria waliolipa nauli kamili
- Takwimu hazikupatikana

SURA YA 17

NISHATI

Kiwango cha Ukuaji

363. Mwaka 2016, shughuli za kiuchumi za usambazaji umeme zilikua kwa asilimia 8.5 ikilinganishwa na ukuaji halisi wa asilimia 5.8 mwaka 2015. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa ufuaji wa wa umeme na kasi ya usambazaji wa umeme vijijini. Aidha, mchango wa shughuli za usambazaji umeme katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 0.9 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 1.0 mwaka 2015.

Ufuaji wa Umeme

364. Mwaka 2016, uwezo wa uzalishaji wa umeme ulipungua kwa asilimia 10.6 hadi kufikia MW 1,469.39 kutoka MW 1,643.50 mwaka 2015. Kati ya hizo, jumla ya MW 1,366.01 zilitokana na mitambo iliyounganishwa katika gridi ya Taifa, MW 84.38 kutokana na mitambo iliyo nje ya gridi na MW 19 ziliingizwa kwenye gridi kutoka nje ya nchi (Kenya, Uganda na Zambia). Katika kipindi hicho, umeme uliozalishwa kutoka vyanzo mbalimbali uliongezeka kwa asilimia 9.8 kufikia saa za gigawati 7,092.13 ikilinganishwa na saa za gigawati 6,457.37 zilizozalishwa mwaka 2015. Kati ya hizo, saa za gigawati 6,788.96 zilizalishwa kwenye gridi ya Taifa na saa za gigawati 303.17 zilizalishwa kwenye vituo nje ya gridi ya Taifa. Aidha, mahitaji ya juu ya umeme yalifikia MW 1,051.27 ikilinganishwa na MW 988.27 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 6.4.

365. Mchanganuo wa umeme uliozalishwa mwaka 2016 unaonesha kuwa umeme wa mitambo ya nguvu za maji ulikuwa saa za gigawati 2,365.82; gesi saa za gigawati 4,097.03 na mafuta mazito na dizeli saa za gigawati 629.2. Aidha, umeme uliofuliwa kutokana na mitambo inayomilikiwa na TANESCO ilikuwa saa za gigawati 5,153.07 ikilinganishwa na saa za gigawati 3,829.13 zilizozalishwa mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 34.6. Vile vile, wazalishaji binafsi wa kampuni za Songas, IPTL na Aggreko kwa pamoja walifua saa za gigawati 1,795.46, sawa na upungufu wa asilimia 29.7 ikilinganishwa na saa za gigawati 2,553.15 zilizozalishwa mwaka 2015. Kwa upande mwingine, umeme ulionunuliwa kutoka nchi jirani za Kenya, Uganda na

Zambia ulikuwa saa za gigawati 101.54 mwaka 2016 ikilinganishwa na saa za gigawati 75.09 mwaka 2015, sawa na asilimia 1.4 ya umeme wote uliozalishwa.

366. Mwaka 2016, umeme uliouzwa kwa watumiaji mbalimbali ulikuwa saa za gigawati 5,871.47 ikilinganishwa na saa za gigawati 5,297.09 zilizouzwa mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 10.8. Aidha, umeme uliopotea kutokana na uchakavu wa mitambo ya kusafirisha na kusambaza umeme ulikuwa saa za gigawati 1,220.66 sawa na asilimia 17.2 ya umeme uliozalishwa ikilinganishwa saa za gigawati 1,119.74 sawa na asilimia 17.3 ya umeme uliozalishwa mwaka 2015.

**UWEZO WA MITAMBO YA UMEME NA KIASI CHA UMEME
ULIOTENGENEZWA KWA VITUO KATIKA MWAKA 2016**

Jedwali Na. 74

Kituo	Uwezo MW	Uliotengenezwa GWH
GRIDI YA TAIFA		
Kidatu	204.00	962.76
Mtera	80.00	323.42
Hale	21.00	44.08
New Pangani Falls	68.00	189.52
Nyumba ya Mungu	8.00	25.27
Kihansi	180.00	794.05
Mwenga Min Hydro	4.00	19.27
Other stations	2.11	7.46
Jumla Hydro	567.11	2,365.82
Ubungo II Gas Plant (UGP 2)	129	643.91
Ubungo I Gas Plant	102	628.17
Tegeta Gas Plant -Watsila	45	317.76
Dodoma (Zuzu)	7.4	3.65
Nyakato Mwanza	63	130.60
Kinyerezi I	150	903.59
Jumla Thermal	496.40	2,627.67
IPTL	103	154.63
Songas Gas Plant	189	1,349.43
Aggreko Ubungo	-	12.43
Aggreko Tegeta (Gas)	-	3.54
Symbion Ubungo (Gas)	-	254.18
Import from SPPs	10.50	21.25
Jumla Wazalishaji Binafsi	302.50	1,795.46
Jumla Grid	1,366.01	6,788.96
MATAWI MENGINE - ISOLATED STATIONS		
Bukoba	2.56	0.31
Kigoma	11.94	26.22
Namtumbo	0.34	1.07
Mafia	2.13	4.45
Mtwara	18	86.65
Songea	8.33	10.82
Sumbawanga	5	1.26
Mpanda	2.98	10.06
Tunduru	2.07	5.09
Liwale	0.85	2.33
Ngara	0.95	4.79
Biharamulo	1.5	1.51
Mbinga	2.26	4.49
Ludewa	1.27	1.30
Somanga	7.5	12.73
Kasulu	2.5	6.08
Kibondo	2.5	3.77
Loliondo	5	1.13
Umeme kutoka nchi jirani	19	101.54
Umeme kutoka IPPS	6.70	17.57
Jumla ya Matawi Mengine	103.38	303.17
JUMLA YA UMEME-NCHI NZ	1,469.39	7,092.13

Chanzo: Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

MW Megawatt

GWH GigaWatt-Hour (Saa za GigaWatt) = Million KWH

* Za Awali (Provisional)

MAUZO YA UMEME KWA WATUMIAJI MBALIMBALI

Jedwali Na. 75

GWH

Mwaka	Tanzania Bara			Zanzibar	Jumla	Umeme uliopotea	Jumla ya umeme uliotengenezwa
	Wateja wadogo (D1)	Wateja wa Kati (T1)	Wateja Wakubwa (T2, T3 & T8)	T5			
2011	328.8	1270.8	2118.0	277.2	3994.7	1158.7	5153.4
2012	320.8	1480.1	2301.8	298.6	4401.4	1048.3	5449.7
2013	280.6	1747.0	2560.4	218.7	4806.7	1139.5	5997.4
2014	217.0	1891.0	2595.0	348.5	5051.5	1135.3	6285.0
2015	148.8	2082.7	2721.1	344.6	5297.1	1119.7	6457.6
2016	345.3	2263.4	2887.2	375.6	5871.5	1220.7	7092.1

Chanzo: Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)

MAUZO YA UMEME KWA MIKOA

Jedwali Na. 76

Mkoa	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016
Dodoma	59	68	79	83	86	94	105	111	116	137
Arusha	223	296	236	269	240	286	316	326	311	357
Manyara		14	17	19	20	23	24	25	26	29
Kilimanjaro	110	109	88	124	118	138	144	154	151	182
Tanga	165	169	166	209	219	245	264	266	300	322
Morogoro	119	136	121	179	163	207	221	232	212	240
Coast		104	94	106	116	142	171	199	220	260
Dar-es-Salaam	1343	1412	1014	1615	1387	1548	1932	2118	2229	2398
Lindi	12	11	11	13	14	15	18	23	22	24
Mtwara	29	23	29	27	30	34	35	9	51	49
Ruvuma	14	15	15	21	21	24	27	28	31	34
Iringa	79	79	85	101	92	102	105	107	112	107
Mbeya	109	115	125	139	132	150	153	170	164	177
Singida	28	18	26	26	23	29	32	35	47	43
Tabora	37	98	84	97	95	103	109	60	52	57
Rukwa	12	11	12	17	19	19	20	22	23	28
Kigoma	10	12	12	16	18	21	23	25	28	29
Shinyanga	195	196	253	313	310	279	280	359	417	428
Kagera	36	37	33	44	29	55	53	54	60	72
Mwanza	151	173	192	215	200	224	231	241	236	262
Mara	95	44	52	110	109	108	125	134	135	142
Njombe										69
Katavi										4
Geita										34
Simyu										8
Isiyobainishwa Kimkoa								6.4	11.4	5
Jumla Tanzania Bara	2826.0	3140.0	2744.0	3743.0	3440.5	3845.5	4388.0	4702.8	4952.6	5496.9
Zanzibar	231.0	229.0	186.0	174.0	277.2	298.6	218.7	348.5	344.6	375.6
JUMLA	3057.0	3369.0	2930.0	3917.0	3717.8	4144.1	4606.7	5051.3	5297.1	5872.5

Chanzo: Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

MW Megawatt

GWH GigaWatt-Hour (Saa za GigaWatt) = Million KWH

Utafutaji Mafuta na Gesi

Gesi Asilia

367. Mwaka 2016, kazi ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia iliendelea katika kina kirefu cha bahari na nchi kavu ambapo jumla ya futi za ujazo zilizogundulika nchini hadi kufikia Desemba ni trillion 57.25. Aidha uzalishaji wa gesi asilia uliendelea ambapo uzalishaji katika visima viwili vya Songosongo na Mnazi Bay uliongezeka kwa asilimia 23.05 kufikia futi za ujazo bilioni 48.32 kutoka futi za ujazo bilioni 37.18 mwaka 2015. Kati ya hizo, jumla ya futi bilioni 36.7 zilitumika kuzalisha umeme, na zilizobaki zilitumika kama nishati viwandanina majumbani. Mapato yaliyopatikana kutokana na mauzo ya gesi asilia katika mwaka 2016 yalifikia dola za Marekani 51,991,433 ikilinganishwa na dola za Marekani 45,776,201 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 1.2.

368. Mwaka 2016, Serikali ilikamilisha maandalizi ya kanuni zinazotoa mwongozo wa ukokotoaji wa bei ya gesi asilia na kutangazwa katika Gazeti la Serikali (GN 285) ili kuhakikisha usimamizi thabiti wa sekta ndogo ya gesi. Vile vile, kanuni za ushiriki wa watanzania katika sekta ya gesi na mafuta ziliendelea kuandaliwa, ambapo kanuni hizi zitatoa mwongozo wa namna watanzania wanavyoweza kushiriki katika mnyororo wa thamani wa sekta hiyo. Aidha, Serikali iliendelea kuandaa Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia Nchini, ambao utawezesha usimamizi madhubuti wa matumizi ya gesi asilia nchini kwa kuzingatia vipaumbele vya Taifa hususan viwanda na miradi mingine itakayoainishwa katika Mpango huo pamoja na usambazaji wa gesi asilia kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na katika magari na mradi wa kusindika gesi asilia.

Jedwali Na. 17.1: Uzalishaji wa Gesi Asilia Songo Songo na Mnazi Bay

Mwaka	Futi za Ujazo (SCF)			
	Songo Songo	Mnazi Bay	Kiliwani North	Jumla
2016	29,747,400,000	15,792,127,458	2,783,497,464	48,323,024,922
2015	31,384,100,000	5,792,141,976		37,176,241,976
2014	33,061,500,000	783,595,488		33,845,095,488
2013	35,217,410,596	715,942,883		35,933,353,479
2012	36,233,010,000	673,870,408		36,906,880,408
2011	30,970,500,000	664,980,487		31,635,480,487
2010	27,633,000,000	454,123,320		28,087,123,320
2009	23,593,000,000	323,686,310		23,916,686,310
2008	20,084,000,000	321,239,550		20,405,239,550
2007	19,705,000,000	258,186,803		19,963,186,803
2006	17,907,000,000	-		17,907,000,000
2005	14,704,000,000	-		14,704,000,000
2004	4,659,000,000	-		4,659,000,000
Jumla Kuu	324,898,920,596	25,779,894,683	2,783,497,464	353,462,312,743

Chanzo: Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

Jedwali Na. 17.2: Mapato yaliyotokana na Mauzo ya Gesi ya Songo Songo na Mnazi Bay (Dola za Marekani)

Mwaka	Songo Songo	Mnazi Bay	Jumla
2016	38,172,718	13,818,715	51,991,433
2015	43,854,236	1,921,965	45,776,201
2014	58,761,119	1,762,977	60,524,096
2013	50,582,385	1,592,879	52,175,264
2012	35,026,145	1,525,251	36,551,396
2011	38,337,903	1,444,856	39,782,759
2010	25,607,621	1,080,131	26,687,753
2009	21,403,804	396,109	21,799,913
2008	19,521,646	388,449	19,910,095
2007	16,861,492	305,236	17,166,727
2006	14,966,409	-	14,966,409
2005	9,019,384	-	9,019,384
2004	2,411,281	-	2,411,281
Jumla	374,526,143	24,236,568	398,762,711

Chanzo: Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania – TPDC

Uagizaji na Mwenendo wa Bei za Mafuta

369. Mwaka 2016, mafuta yaliyoingizwa nchini yalifikia lita za ujazo milioni 5,414.4 kutoka lita za ujazo milioni 4,929.5 kwa mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 9.8. Sehemu kubwa ikiwa ni ongezeko la mafuta yaliyokuwa yakisafirishwa kwenda nchi jirani. Kati ya hizo, lita za ujazo milioni 2,874.4 sawa na asilimia 53.1 ya mafuta yaliyoingizwa nchini yalisafirishwa kwenda nchi jirani na lita milioni 2,539.9 yalikuwa kwa ajili ya matumizi ya ndani. Mwaka 2016, jumla ya kiasi cha mafuta yaliyosafirishwa kwenda nchi jirani yaliongezeka kwa asilimia 55.8 kutoka lita za ujazo milioni 1,845.1 mwaka 2015 wakati mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi yalipungua kwa asilimia 17.7 kutoka lita za ujazo milioni 3,084.5 mwaka 2015.

370. Mwaka 2016, bei za mafuta katika soko la dunia zilibadilika kulingana na nguvu ya soko wakati kiwango cha juu cha wastani wa bei ya mafuta ya, kilikuwa mwezi Desemba ambapo bei kwa pipa ilikuwa petroli dola za Marekani 532, dizeli 461, na na mafuta ya taa 498 kwa mtiririko huo. Bei za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa kwa ujumla zilishuka hadi kufikia wastani wa dola za Marekani 416 mwaka 2016 ikilinganishwa na wastani wa dola za Marekani 513 mwaka 2015, sawa na upungufu wa bei kwa asilimia 18.9. Kushuka kwa bei za mafuta katika soko la dunia kulitokana na kuendelea kuongezeka kwa uzalishaji wa mafuta katika nchi zinazozalisha mafuta kwa wingi duniani. Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa mwaka 2016 hadi kufikia dola za Marekani 462 kwa mafuta ya petroli; dola 380 kwa mafuta ya dizeli na dola 407 kwa mafuta ya taa kwa pipa kutoka dola za Marekani 478; 558; na 502 kwa pipa mwaka 2015 kwa mtiririko huo. Sawa na upungufu wa asilimia 3.3 kwa mafuta ya petroli; asilimia 31.9 kwa mafuta ya dizeli; na asilimia 18.9 kwa mafuta ya taa.

**Jedwali Na. 17.3: Bei za Mafuta kwenye Soko la Dunia (FOB) –
Dola za Marekani kwa Mita za Ujazo (FoB)**

Aina ya Mafuta	Petroli			Dizeli			Mafuta ya Taa		
	2014	2015	2016	2014	2015	2016	2014	2015	2016
Mwezi/Mwaka									
Januari	939	449	398	877	468	258	876	495	284
Februari	970	539	357	888	573	280	883	576	312
Machi	976	509	431	874	593	333	861	540	361
Aprili	1008	529	467	886	622	352	867	553	381
Mei	995	594	497	879	669	401	860	597	425
Juni	1021	562	498	871	689	429	867	577	451
Julai	1004	495	440	855	643	397	853	509	419
Agosti	938	442	464	836	539	389	834	457	411
Septemba	906	449	478	802	503	399	804	467	425
Oktoba	809	433	512	716	485	449	724	455	473
Novemba	732	407	471	669	469	417	686	435	440
Disemba	564	329	532	550	438	461	555	363	498
Wastani wa Bei	905	478	462	809	558	380	806	502	407
(USD/MT)									
Wastani wa ongezeko kwa mwaka (%)		-47	-3.3		-31	-32		-37.7	-19

Chanzo: EWURA

371. Kufuatia kushuka kwa wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia, bei za mafuta katika soko la ndani zilishuka zaidi kwa mwaka 2016 ikilinganishwa na mwaka 2015. Wastani wa bei za ukomo za mafuta katika soko la ndani mwaka 2016 ulipungua na kuwa shilingi 1,845 kwa lita moja ya petroli; shilingi 1,673 mafuta ya dizeli; na shilingi 1,644 kwa mafuta ya taa ikilinganishwa na shilingi 1,973 kwa lita moja ya petroli; shilingi 1,808 mafuta ya dizeli; na shilingi 1,739 mafuta ya taa mwaka 2015. Hii ni sawa na upungufu wa bei kwa asilimia 6.5, 7.5 na 5.5 kwa mafuta ya petroli, dizeli, na mafuta ya taa kwa mtiririko huo.

Jedwali Na.17.4 Mwenendo wa Bei za Mafuta kwa Dar es Salaam

Mwezi	Petroli (TSh/Lita)	Dizeli (TSh/Lita)	Mafuta ya Taa (TSh/Lita)	Mwezi	Petroli (Tsh/Lita)	Dizeli (Tsh/Lita)	Mafuta ya Taa (TSh/Lita)
Januari-15	1,955	1,846	1,833	Januari-16	1,898	1,747	1,699
Februari-15	1,768	1,708	1,657	Februari-16	1,842	1,600	1,699
Machi-15	1,652	1,563	1,523	Machi-16	1,811	1,486	1,465
15-Apr	1,755	1,672	1,655	16-Apr	1,728	1,516	1,501
Mei-15	1,866	1,695	1,624	Mei-16	1,785	1,602	1,578
Juni-15	1,966	1,782	1,624	Juni-16	1,867	1,633	1,607
Julai 15	2,198	2,043	1,993	Julai-16	1,888	1,720	1,687
Agosti-15	2,290	2,026	1,964	Agosti-16	1,905	1,811	1,759
Septemba-15	2,153	1,832	1,770	Septemba-16	1,840	1,747	1,673
Oktoba-15	2,086	1,828	1,733	Oktoba-16	1,827	1,699	1,658
Novemba-15	2,004	1,879	1,733	Novemba-16	1,860	1,720	1,669
Desemba-15	1,977	1,823	1,765	Desemba-16	1,890	1,798	1,737
Wastani Mwaka 2015	1,973	1,808	1,739	Wastani Mwaka 2016	1,845	1,673	1,644
Wastani Mwaka 2014	2,186	2,082	2,030	Wastani Mwaka 2015	1,973	1,808	1,739
Mabadiliko (%)	-10%	-13%	-14%	Mabadiliko (%)	-6.50%	-7.50%	-5.50%

Chanzo: EWURA

Nishati Jadidifu

Jotoardhi

372. Mwaka 2016, Serikali kupitia Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Nchini kwa kushirikiana na wahisani mbalimbali, waliendelea na tafiti za jotoardhi ikiwemo kubainisha maeneo yenye viashiria vya uwepo wa jotoardhi nchini ambapo hadi sasa zaidi ya maeneo 50 yanakadiriwa kuwa na uwezo wa kuzalisha umeme utokanao na jotoardhi na pia matumizi mengine ya moja kwa moja kutokana na mvuke wa jotoardhi. Aidha, utafiti wa kina wa kijiolojia, kijiokemia na kijiofizikia ulifanyika kwenye maeneo ya Kisaki mkoani Morogoro, Mlima Meru (Arusha), Luhoi (Pwani), ziwa Ngozi (Mbeya) na Songwe (Songwe) ili kuweza kuona uwezekano wa upatikanaji wa mvuke kwa ajili ya uzalishaji wa umeme na matumizi mengine.

Maporomoko Madogo ya Maji

373. Mwaka 2016, jumla ya megawati 36.74 zilizalishwa kutokana na maporomoko madogo ya maji. Kati ya hizo, megawati 25 ziliingizwa kwenye gridi ya Taifa na MW 11.74 zilitumika katika maeneo ambayo uzalishaji huwa unafanyika kwa ajili ya jamii zinazozunguka mitambo ya uzalishaji kwa ajili ya shughuli za kijamii na kiuchumi za maeneo husika. Aidha, mwaka 2016, jumla ya wateja 4,088 waliunganishiwa nishati ya umeme unaotokana na maporomoko madogo ya maji katika vyanzo vya Mawengi wateja 1,243; Mwenga (2,000); Andoya (143); Ikondo (699); Ngombeni (1); Yovi (1); na Tulia (1) na hivyo wastani wa jumla ya wanaonufaika wa nishati hiyo ulifikia watu 20,425. Aidha, kiasi cha MW 11.8 kilizalishwa na kusambazwa katika maeneo tajwa hapo juu. Vilevile, Wakala wa Nishati Vijijini waliendelea kuwajengea uwezo waendelezaji wa nishati ya maporomoko ya maji kuwawezesha kuandaa miradi ambayo itasaidia upatikanaji wa fedha za miradi hiyo.

Nishati ya Upepo

374. Mwaka 2016, tafiti zilizofanyika, zilionesha kuwa, maeneo ya Singida na Makambako ndiyo yenye kasi kubwa na endelevu ya upepo, hivyo kuwezesha uzalishaji wa umeme mzuri ikilinganishwa na maeneo mengine. Hadi sasa, kampuni tano za Wind Power East Africa, Geo wind Power Ltd, Upepo Energy, Miombo wind na Sino-Tan Renewable Energy Limited zipo katika hatua mbalimbali za uwekezaji katika mikoa ya Singida na Njombe (Makambako).

Tungamotaka, Bayogesi na LPG

375. Mwaka 2016, uzalishaji wa umeme kutokana na mabaki ya malighafi kutoka viwanda vya sukari na mazao ya misitu ulifikia MW 38.0, kati ya hizo megawati 10.5 ziliingizwa katika gridi ya Taifa na megawati 27.5 zilitumika kwa matumizi ya viwanda vya sukari na mazao ya misitu. Aidha, Serikali iliendelea na uhamasishaji wa ujenzi na matumizi ya nishati ya bayogesi kwa ajili ya kupikia ambapo zaidi ya mitambo 28,000 ya bayogesi ilijengwa mwaka 2016 ikilinganishwa na mitambo 24,000 iliyojengwa mwaka 2015. Hali kadhalika, matumizi ya gesi ya mitungi kwa ajili ya kupikia majumbani (LPG) yaliongezeka hasa katika maeneo ya mijini ambapo mwaka 2016 ilikadiriwa zaidi ya asilimia 50 ya kaya za mijini zinatumia nishati hii kwa ajili ya kupikia badala ya kuni na mkaa.

Nishati ya Mionzi ya Jua

376. Mwaka 2016, Serikali ilifanya ukaguzi wa maendeleo ya miradi ya uzalishaji wa umeme wa jua kupitia mifumo ya gridi ndogo (*Solar Min Grid*) ambapo makampuni ya Jumeme na *REX Solar investment* yako katika hatua mbalimbali za uzalishaji wa umeme katika visiwa vya Ziwa Victoria ambavyo havitafikiwa na umeme wa gridi. Aidha, jumla ya kW 300 zilizalishwa katika visiwa vya Ukara kupitia Kampuni ya Jumeme na katika kisiwa cha Ghana, Kampuni ya *REX Solar Energy* ilikamilisha usimikaji wa nguzo na utandazaji wa nyanya za umeme. Upatikanaji wa umeme katika visiwa hivi umechochea ukuaji wa uchumi kwa wananchi ambao shughuli zao kuu ni uvuvi ambapo thamani ya samaki na mazao yake iliongezwa.

SURA YA 18

MAJI

Kiwango cha Ukuaji

377. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za usambazaji maji na udhibiti maji taka kilikuwa asilimia 4.3 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 0.1 mwaka 2015. Ongezeko hilo lilitokana na uboreshaji wa miundombinu ya usambazaji maji mijini na vijijini na kuongezeka kwa idadi ya wateja waliounganishiwa maji. Aidha, mchango wa shughuli za usambazaji maji katika Pato la Taifa umeendelea kuwa asilimia 0.4 mwaka 2016 kama ilivyokuwa mwaka 2015.

Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

378. Mwaka 2016, Serikali iliendelea kusimamia rasilimali za maji, kufanya utafiti wa vyanzo vipya na ufuatiliaji wa vyanzo vilivyokuwepo ili kuhakiksha inaendelea kuvilinda visiharibiwe na shughuli za kibinadamu. Aidha, katika utafiti huo vyanzo 269 vilitambuliwa kuwa vipo katika hatari ya kuharibiwa na kuathiriwa kutokana na uharibifu wa mazingira uliosababishwa na ongezeko la shughuli za kibinadamu. Katika kulinda vyanzo hivyo, Serikali ilichukua hatua mbali mbali ikiwemo kuweka mipaka katika vyanzo 59 vya maji na kuanzisha mchakato wa kuvitangaza kuwa maeneo tengefu kwa lengo la kuvihifadhi na kuvilinda dhidi ya uharibifu wa mazingira. Maeneo hayo tengefu ni pamoja na vyanzo vya maji chini ya ardhi yaliyoko Chokaa, Kidole, Kiswaga, Matundasi A, Matundasi B, Mkola na Bwawa la Milala katika Bonde la Ziwa Rukwa; Bwawa la Mtera katika Bonde la Rufiji; Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini vyanzo vya maji vya chemichemi za Mbwinji, Ndanda, Mwena na Liputu kwenye miteremko ya milima ya Makonde na Mitema-Kitangari.

379. Hadi mwaka 2016, kulikuwa na jumla ya vituo 694 vya kupima wingi na ubora wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi ili kuboresha upatikanaji wa takwimu na taarifa sahihi na kwa wakati. Katika mwaka 2016, jumla ya vituo vipya 54 vilijengwa na vituo 78 vilikarabatiwa katika kuhakikisha upatikanaji wa takwimu sahihi za hali ya maji.

380. Mwaka 2016, jumla ya vibali vipya 800 vya matumizi ya maji vilitolewa na Bodi za Maji za Mabonde kwa watumiaji wa maji ikilinganishwa na vibali 618 vilivyotolewa mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 29.4. Aidha, vibali tisa (9) vya kutiririsha majitaka vilitolewa kwa taasisi mbalimbali za uzalishaji viwandani. Hadi kufikia mwaka 2016 jumla ya vibali 13,565 vya

matumizi ya maji, uchimbaji visima na utiririshaji wa majitaka vilikuwa vimetolewa na Bodi za Maji za Mabonde. Vile vile, utayarishaji wa Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika mabonde yote tisa (9) uliendelea ambapo hadi mwezi Desemba 2016, jumla ya mipango 6 ilikamilika.

381. Mwaka 2016, Serikali iliendelea na shughuli ya ukusanyaji na uchunguzi wa sampuli za maji ili kuangalia kama zinakidhi ubora na vigezo vinavyokubalika. Aidha, jumla ya sampuli 1,980 zilikusanywa kutoka kwenye vyanzo vya maji, viwanda, migodi, na mifumo ya utoaji maji taka ya viwandani na kupimwa maabara ikilinganishwa na sampuli 6,487 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 69.5. Kati ya sampuli zilizokusanywa na kupimwa mwaka 2016 asilimia 70 ya sampuli zilionekana kukidhi viwango vya kumwagwa katika mazingira bila kuleta athari zozote. Aidha, sampuli 151 kutoka mifumo ya utoaji majitaka zilichukuliwa na kupimwa mwaka 2016 ikilinganishwa na sampuli 854 mwaka 2015 ambapo asilimia 77 ya sampuli hizo zilioneka kuwa na viwango vinavyokubalika.

Huduma ya Maji Vijijini

382. Mwaka 2016, miradi ya maji vijijini iliendelea kutekelezwa chini ya Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Hadi Desemba, 2016 idadi ya miradi 1,301 ya maji vijijini ilikuwa imekamilika na miradi 509 ilikuwa imefikia hatua mbalimbali za utekelezaji. Utekelezaji wa miradi hiyo umewezesha vituo vya maji kufikia 98,298 na kuongeza idadi ya watu wanaopata huduma ya maji vijijini kufikia 22,816,624 sawa na asilimia 72.15 ya wakazi wa vijijini ukilinganisha na vituo 94,013 vilivyokuwa vinahudumia watu 21,910,562 sawa na asilimia 68.9 ya wakazi wa vijijini mwaka 2015.

Huduma za Maji Mijini na Usafi wa Mazingira

383. Mwaka 2016, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika miji mikuu ya mikoa zilitoa huduma ya maji kwa wastani wa kiwango cha asilimia 86 sawa na wakazi takribani milioni 4.5. Uzalishaji wa maji katika Miji Mikuu ya Mikoa uliongezeka kwa asilimia 4.3 kutoka mita za ujazo milioni 140.98 mwaka 2015 hadi kufikia mita za ujazo milioni 147.11 mwaka 2016. Aidha, idadi ya wateja wanaopata huduma ya maji iliongezeka kutoka wateja 400,093 mwaka 2015 hadi kufikia wateja 428,435 mwaka 2016. sawa na ongezeko la asilimia 7.1. Hali hiyo ilichangia kuongezeka kwa makusanyo yaliyofikia

shilingi bilioni 110.68 mwaka 2016 ikilinganishwa na shilingi bilioni 91.93 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 20.4.

384. Serikali iliendelea kuzijengea uwezo mamlaka za maji katika ngazi ya Wilaya na Miji Midogo ambazo zipo daraja ‘C’ ili ziweze kufikia madaraja ya B’ na ‘A’, yenye uwezo wa kujiendesha yenyewe ilikupunguza gharama za uendeshaji kwa Serikali. Utoaji wa huduma ya maji katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na maeneo yanayohudumiwa na Miradi ya Kitaifa kwa sasa ni wastani wa asilimia 60 ya wakazi wanaopata maji. Uzalishaji wa maji uliongezeka kutoka mita za ujazo milioni 50 mwaka 2015 hadi mita za ujazo milioni 59 mwaka 2016. Idadi ya wateja wanaopata huduma ya maji iliongezeka kutoka wateja 134,692 mwaka 2015 hadi kufikia wateja 147,163 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 9.

385. Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam, wastani wa asilimia 72 ya idadi ya wakazi walipata huduma ya maji safi na salama mwaka 2016 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 68 mwaka 2015. Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji pamoja na maeneo ya miji ya Kibaha na Bagamoyo, iliimarika kutokana na kukamilika kwa mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini ambapo uzalishaji wa maji uliongezeka kutoka mita za ujazo 300,000 hadi mita za ujazo 504,000 kwa siku. Aidha, mahitaji ya maji katika Jiji yaliongezeka kutoka wastani wa mita za ujazo 450,000 kwa siku mwaka 2015 hadi wastani wa mita za ujazo 544,000 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 20.9. Vile vile, wateja wanaopata huduma ya maji waliongezeka kutoka wateja 148,000 mwaka 2015 hadi wateja 171,784 mwaka 2016, hali hii iliwezesha kuongezeka kwa makusanyo kutoka shilingi bilioni 52.04 hadi shilingi billioni 86.87 mwaka 2016.

Hali ya sekta ya umwagiliaji

386. Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji iliendelea kusimamia sekta ya umwagiliaji kwa lengo la kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 461,326 hadi kufikia hekta 1,000,000 katika skimu za wakulima wadogo, wa kati na wakubwa ifikapo mwaka 2020. Aidha, jumla ya hekta 468,338 zilikuwa zinamwagiliwa mwaka 2016 ikilinganishwa hekta 461,326 zilizokuwa zinamwagiliwa mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 1.5.

UZALISHAJI WA MAJI NA MAPATO YATOKANAYO NA MAJI MIJINI

Jedwali Na. 77

Mamlaka	Uzalishaji wa Maji (Mita za ujazo)	Mapato (TShs)	Uzalishaji wa Maji (Mita za ujazo)	Mapato (TShs)	Uzalishaji wa Maji (mita za ujazo)	Mapato (TShs)	Wastani wa Upatikanji wa Huduma ya Maji 2016 (%)
	2014		2015		2016		
Arusha	15,256,841	9,679,355,909	15,267,200	9,189,207,260	15,267,200	11,385,681,743	78
Babati	1,438,290	1,010,362,969	1,565,467	1,210,094,769	1,565,467	1,443,980,929	84
Bukoba	3,166,446	1,449,906,297	3,111,505	1,354,793,498	12,038,250	1,879,612,507	87
Dodoma	11,180,417	7,931,340,515	12,038,250	10,473,029,627	5,384,053	12,222,417,151	96
Iringa	5,681,451	3,907,585,966	5,384,053	4,402,847,990	481,226	5,726,246,072	70
Kigoma	4,420,717	1,488,432,082	2,693,846	1,411,612,380	15,680,862	1,495,898,490	97
Lindi	778,939	331,318,916	481,226	256,676,508	11,642,401	198,582,859	94
Mbeya	14,521,357	7,769,379,747	15,680,862	8,099,457,867	10,771,035	8,789,113,162	100
Morogoro	11,056,167	6,188,159,186	11,642,401	6,586,853,102	3,093,413	7,726,217,100	92
Moshi	10,166,113	5,215,821,127	10,771,035	6,142,186,713	3,391,420	7,616,200,285	82
Mtwara	2,906,891	1,731,569,647	3,093,413	2,037,164,193	3,818,506	2,652,851,020	78
Musoma	3,533,008	2,244,389,746	3,391,420	2,256,894,510	2,515,028	2,377,423,671	89
Mwanza	27,854,358	15,953,484,917	27,140,398	16,882,598,795	2,851,497	21,047,423,562	93
Shinyanga	3,605,506	3,014,107,752	3,818,506	3,554,969,593	4,786,207	4,416,379,733	86
Singida	2,867,025	1,279,081,037	2,515,028	1,658,438,213	10,288,619	2,137,392,972	99
Songea	3,538,968	1,817,808,585	2,851,497	2,109,228,289	1,342,230	2,352,913,720	52
Sumbawanga	1,816,822	808,748,215	1,598,912	776,913,969	192,467	940,707,565	40
Tabora	4,887,392	2,520,009,578	4,786,207	3,153,920,080	1,237,511	3,906,149,905	53
Tanga	10,205,227	7,554,448,254	10,288,619	9,453,232,952	91,479	10,752,460,576	54
Mpanda	1,007,100	242,286,893	1,342,230	321,938,674	27,140,398	399,069,657	94
Bariadi	164,554	66,373,476	192,467	97,084,376	3,111,502	113,235,333	76
Njombe	1,184,610	429,318,275	1,237,511	444,136,912	1,598,912	918,031,280	62
Geita	132,928	96,127,675	91,479	55,062,750	2,693,846	184,353,437	71
Jumla	141,371,127	82,729,416,764	140,983,532	91,928,343,020	140,983,529	110,682,342,730	86

Chanzo: Wizara ya Maji na Umwagiliaji

SURA YA 19

ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

Elimu ya Awali

387. Mwaka 2016, idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika elimu ya awali ilikuwa 1,562,770 ikilinganishwa na wanafunzi 1,069,823 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 46.1. Kati ya hao, wasichana walikuwa 775,027 sawa na asilimia 49.6 ya wanafunzi wote na wavulana walikuwa 787,743. Idadi ya wanafunzi katika shule za serikali ilikuwa 1,488,439 ikilinganishwa na wanafunzi 1,015,030 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 46.6. Kati ya hao, wasichana walikuwa 738,323 na wavulana 750,116. Aidha, mwaka 2016, idadi ya wanafunzi katika shule zisizo za serikali ilikuwa 74,331 ikilinganishwa na wanafunzi 54,793 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 35.7. Ongezeko la uandikishaji katika elimu ya awali lilitokana na mwamko wa wazazi na walezi juu ya umuhimu wa elimu ya awali.

388. Mwaka 2016, uwiano wa mwalimu mwenye sifa kwa wanafunzi katika shule za awali za serikali ulikuwa 1:177 ikilinganishwa na uwiano wa 1:92 mwaka 2015. Uwiano unaokubalika kimataifa ni 1:25. Ongezeko la uwiano lilitokana na uandikishwaji wa idadi kubwa ya wanafunzi ambao haukuendana na idadi ya walimu walioajiriwa katika kipindi hicho.

Elimu ya Msingi

389. Mwaka 2016, shule za msingi za Serikali na zisizo za Serikali zilikuwa 17,174 ikilinganishwa na shule 16,899 mwaka 2015. Kati ya hizo, shule za msingi za Serikali zilikuwa 16,109 ikilinganishwa na shule 15,966 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 0.9. Aidha, katika kipindi hicho, shule zisizo za Serikali zilikuwa 1,065 ikilinganishwa na shule 933 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 14.1.

390. Mwaka 2016, idadi ya wanafunzi wa elimu ya msingi iliongezeka hadi kufikia wanafunzi 8,639,202 kutoka wanafunzi 8,298,282 mwaka 2015. Kati ya hao, wavulana walikuwa 4,265,714 na wasichana walikuwa 4,373,488, sawa na asilimia 50.6 ya wanafunzi wote. Aidha, katika kipindi hicho, idadi ya wanafunzi katika shule za Serikali ilikuwa 8,342,284 ikilinganishwa na wanafunzi 8,011,229 mwaka 2015 ambapo wasichana walikuwa 4,226,289 na

wavulana 4,115,995. Idadi ya wanafunzi katika shule zisizo za Serikali iliongezeka hadi kufikia wanafunzi 296,918 ikilinganishwa na wanafunzi 227,992 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 30.2. Kati ya hao, wasichana walikuwa 147,199 na wavulana 149,719. Vile vile, idadi ya wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza iliongezeka hadi kufikia wanafunzi 2,120,667 mwaka 2016 kutoka wanafunzi 1,568,378 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 35.2. Ongezeko hilo lilitokana na kuanza kutekelezwa kwa utoaji wa elimu msingi bila malipo. Aidha, kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa rika lengwa (miaka 7-13) kimeongezeka kutoka asilimia 91.9 mwaka 2015 hadi asilimia 93.5 mwaka 2016.

391. Mwaka 2016, walimu wenye sifa katika shule za Serikali walikuwa 191,772 ikilinganishwa na walimu 178,242 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 7.6. Ongezeko hilo linafanya uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi kwa shule za Serikali na zisizo za Serikali kuwa 1:42 ikilinganishwa na 1:41 mwaka 2015. Kwa mujibu wa vigezo vya kimataifa, uwiano stahiki wa mwalimu kwa mwanafunzi ni 1:40. Pamoja na jitihada za Serikali za kusomesha na kuongeza ajira za walimu, uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi uliongezeka kutokana na utekelezaji wa elimu msingi bila malipo uliosababisha idadi ya wanafunzi kuongezeka zaidi.

392. Mwaka 2016, wanafunzi 789,479 walifanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi ikilinganishwa na wanafunzi 763,606 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 3.4. Kati ya hao, wasichana walikuwa 419,932, sawa na asilimia 53.2 na wavulana 369,547. Kiwango cha ufaulu kilikuwa asilimia 70.4 ikilinganishwa na ufaulu wa asilimia 67.8 mwaka 2015.

Elimu ya Sekondari

393. Mwaka 2016, idadi ya shule za sekondari za Serikali na zisizo za Serikali ilikuwa 4,759 ikilinganishwa na shule 4,708 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 1.1. Kati ya hizo, shule 3,614 ni za Serikali na shule zisizo za Serikali ni 1,145.

394. Mwaka 2016, idadi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita katika shule za Sekondari ilikuwa wanafunzi 1,806,955 ikilinganishwa na wanafunzi 1,774,383 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 1.8. Kati ya wanafunzi hao, wavulana walikuwa 905,896 na wasichana walikuwa 901,059,

sawa na asilimia 49.9. Aidha, wanafunzi waliojiunga na elimu ya sekondari kwa kidato cha kwanza mwaka 2016 walikuwa 538,826 ikilinganishwa na wanafunzi 448,826 mwaka 2015, sawa ongezeko la asilimia 20.1. Vile vile, mwaka 2016, walimu katika shule za sekondari walikuwa 100,636 ikilinganishwa na walimu 92,439 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 8.9.

395. Mwaka 2016, jumla ya watahiniwa 351,909 walifanya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne ambapo wasichana walikuwa 179,567, sawa na asilimia 51.0 ya watahiniwa wote na wavulana walikuwa 172,342. Ufaulu wa mwaka 2016 uliongezeka na kufikia asilimia 70.1 ikilinganishwa na ufaulu wa asilimia 68.3 wa mwaka 2015. Aidha, mwaka 2016, jumla ya watahiniwa 73,940 walifanya mtihani wa kidato cha sita ambapo ufaulu ulikuwa asilimia 97.3 ikilinganishwa na watahiniwa 35,176 waliofanya mtihani wa kidato cha sita mwaka 2015 ambapo wanafunzi 34,777 walifaulu, sawa na asilimia 98.9.

396. Mwaka 2016, wanafunzi 61,488 waliripotiwa kuwa watoro ikilinganishwa na wanafunzi 54,949 walioripotiwa kuwa watoro mwaka 2015, sawa na kuongezeka utoro kwa asilimia 11.9. Aidha, mwaka 2016, wanafunzi wa kike 3,439 walipata ujauzito ikilinganishwa na wanafunzi 3,281 waliopata ujauzito mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 4.8.

Elimu ya Ualimu

397. Mwaka 2016, kulikuwa na vyuo vya ualimu 127 kama ilivyokuwa katika mwaka uliotangulia. Kati ya hivyo, vyuo vya Serikali vilikuwa 35 na visivyo vya Serikali 92. Aidha, mwaka 2016, idadi ya wanachuo katika vyuo vya ualimu vya Serikali na visivyo vya Serikali ilikuwa wanachuo 19,825 ikilinganishwa na wanachuo 20,421 mwaka 2015. Kati ya hao, wavulana walikuwa 9,389 na wasichana 10,436.

398. Mwaka 2016, idadi ya wanachuo katika vyuo vya ualimu vya Serikali ilikuwa 14,057 ikilinganishwa na wanachuo 16,814 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 16.4. Kati yao, wasichana walikuwa 7,642 na wavulana walikuwa 6,415. Aidha, mwaka 2016, idadi ya wanachuo katika vyuo vya ualimu visivyo vya Serikali ilikuwa 2,794 ikilinganishwa na wanachuo 3,607 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 22.5.

Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu

399. Mwaka 2015/16, Serikali iliendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa sera, sheria na kanuni za elimu kwa lengo la kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa kwa ngazi zote inakuwa bora. Katika kipindi hicho, jumla ya taasisi 16,780 zilikaguliwa ikilinganishwa na taasisi 13,233 zilizokaguliwa mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 26.8.

Jedwali Na.19.1: Ukaguzi wa Taasisi za Elimu mwaka 2015/16

Taasisi/Shule/Vituo /Vyuo	Idadi ya Asasi (Machi 2016)	Idadi iliyolengwa kukaguliwa	Idadi halisi iliyokaguliwa	Kiwango cha utekelezaji (% ya idadi iliyokaguliwa)
Shule za Awali	16,273	9,973	6,412	64.2
Shule za Msingi	17,174	11,856	8,083	47.1
Shule za Sekondari	4,759	3,786	2,285	48.0
Jumla	38,206	25,615	16,780	65.5

Chanzo: Taarifa za Uthibiti Ubora wa Shule, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Elimu ya Ufundi na Mafunzo

400. Mwaka 2015/16, kulikuwa na wanafunzi 117,067 katika vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ikilinganishwa na wanafunzi 116,160 mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 0.8. Kati ya hao, wanaume walikuwa 57,895 (asilimia 49.5) na wanawake walikuwa 59,172.

Elimu ya Ufundi Stadi

401. Mwaka 2015/16, wanafunzi katika Vyuo vya Ufundi Stadi walikuwa 196,091 ikilinganishwa na wanafunzi 189,687 mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la asilimia 3.4. Kati ya hao, wanaume walikuwa 120,742 na wanawake 75,349 (asilimia 38.4).

Elimu ya Juu

402. Mwaka 2015/16, idadi ya wanafunzi katika vyuo vikuu vya Serikali na visivyo vya Serikali ilikuwa 189,857 ikilinganishwa na wanafunzi 220,531 mwaka 2014/15, sawa na upungufu wa asilimia 13.9. Kati ya hao, idadi ya

wanafunzi wa kike ilikuwa 67,209 (asilimia 35.4 ya wanafunzi wote) na idadi ya wavulana 122,648.

403. Mwaka 2016/17, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 411.3 ilitolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Vyuvo vya Elimu ya Juu kwa wanafunzi 113,442 ikilinganishwa na wanafunzi 99,069 waliopata mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 342.5 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 14.5. Katika kipindi hicho, Bodi ilipokea maombi ya mikopo 83,255 kutoka kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza katika ngazi ya stashahada, shahada ya kwanza na shahada za juu. Kati ya hao, waombaji 28,073, sawa na asilimia 33.7 walikidhi sifa za kupewa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 102.6. Aidha, wanafunzi 85,369 waliokuwa wanaendelea na masomo mwaka 2016/17 walipata mikopo ya masomo yenye thamani ya shilingi bilioni 308.6.

Jedwali Na. 19.2 -: Wanafunzi Waliopata Mikopo 2016/2017

Maelezo	Wanafunzi wapya		Wanafunzi wanaendelea		Jumla	
	Idadi	Kiasi	Idadi	Kiasi	Idadi	Kiasi
Stashahada			5,864	4,062,723,000	5,864	4,062,723,000.00
Shahada - Ndani ya	27,903	98,611,186,313	77,169	293,796,173,669	105,072	392,407,359,982
Nchi						
Uzamili/Uzamivu – Ndani ya Nchi	170	1,260,599,500	265	2,955,828,000.00	435	4,216,427,500.00
Nje ya Nchi	0	0	487	5,947,173,784.00	487	5,947,173,784.00
Jumla	28,073	99,871,785,813	83,785	306,761,898,453	111,858	406,633,684,266
Ruzuku			1,584	4,627,160,700	1,584	4,627,160,700
Jumla Kuu	28,073	102,637,618,313	85,369	308,623,226,653	113,442	411,260,844,966

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO

Jedwali Na. 80

(Namba)

Mwaka	I	II	III	IV	V	VI	Jumla
2000	43643	36734	31132	25456	6654	6143	149762
2001	47204	45078	30531	29188	7198	6601	165800
2002	56101	50371	36989	29045	7711	7126	187343
2003	52863	60643	36906	35653	7780	6885	200730
2004	98738	67294	46546	36385	8353	7572	264888
2005	134963	109398	46188	46489	9710	8444	355192
2006	196391	151448	72167	42584	18211	9691	490492
2007	401011	218060	105770	70796	21789	11668	829094
2008	395930	332393	175353	95214	25240	11743	1035873
2009	480529	308131	159789	167355	31201	12695	1159700
2010	382207	398870	293519	279995	26065	20674	1401330
2011	403873	396724	380528	279117	30265	25164	1515671
2012	457321	386250	355740	343376	31206	28859	1602752
2013	444532	506036	193901	302963	30581	26698	1504711
2014	479089	506170	356787	178246	33619	26899	1580810
Badiliko (%)							
2013 - 2014	7.8	0.0	84.0	-41.2	9.9	0.8	5.1

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi

IDADI YA WANAFUNZI NA WALIMU KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI KWA JINSIA

Jedwali Na.80A

	2012			2013			2014		
	Waume	Wake	Jumla	Waume	Wake	Jumla	Waume	Wake	Jumla
Elimu ya msingi									
Jumla ya wanafunzi wote walioandikishwa Darasa la I-VII	4086280	4160892	8247172	4066287	4165626	8231913	4047582	4175085	8222667
Jumla ya wanafunzi wanaosoma shule za Serikali Darasa la I-VII	3970502	4049246	8019748	3965572	4068354	8033926	3933130	4061545	7994675
Jumla ya wanafunzi wanaosoma shule za binafsi Darasa la I-VII	115778	111646	227424	100715	97272	197987	114452	113540	227992
Jumla ya walimu katika shule za msingi	87601	93386	180987	91253	98234	189487	92695	98262	190957
Jumla ya walimu katika shule za msingi za Serikali	82541	89445	171986	85525	93797	179322	86993	94012	181005
Jumla ya walimu katika shule za msingi za binafsi	5060	3941	9001	6631	4942	11573	5702	4250	9952
Elimu ya Sekondari									
Jumla ya wanafunzi wote Kidato I-VI	1010473	873799	1802810	939191	864865	1804056	997633	949716	1947349
Wanafunzi wanaosoma katika shule za Serikali, kidato I-VI	875480	727272	1542687	796895	707816	1504711	821697	759113	1580810
Wanafunzi wanaosoma katika shule za binafsi, kidato I-VI	134993	146296	260123	142296	157049	299345	175936	190603	366539
Idadi ya walimu katika shule za Serikali	33643	17826	51469	37291	20737	58028	41490	23900	65390
Idadi ya walimu katika shule za binafsi	10881	2736	13617	12261	3118	15379	12146	2993	15139
Jumla ya Walimu katika shule za Sekondari	44524	20562	65086	12101	3056	15157	53636	26893	80529

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi

IDADI YA TAASISI ZA ELIMU

Jedwali Na. 80 B

Aina ya Taasisi	2012			2013			2014			2015		
	Serikali	Binafsi	Jumla	Serikali	Binafsi	Jumla	Serikali	Binafsi	Jumla	Serikali	Binafsi	Jumla
Shule za Msingi	15525	806	16331	15576	767	16343	15705	788	16493	15966	933	16899
Shule za Sekondari	3508	1020	4528	3528	1048	4576	3692	1061	4753	3691	1108	4799
Vyuo vya Ualimu (Msingi na Sekondari)	34	91	125	34	92	126	34	92	126	35	92	127
Elimu ya Ufundi na Mafunzo	109	641	750	113	631	744	0	0	253	0	0	455
Jumla	19176	2558	21734	19251	2538	21789	19431	1941	21625	19692	2133	22280

MAFUNZO YA WALIMU KATIKA VYUO VYA UALIMU

Jedwali Na.80C

Aina	2011			2012			2013			2014		
	Waume	Wake	Jumla	Waume	Wake	Jumla	Waume	Wake	Jumla	Waume	Wake	Jumla
Stashahada (Pre-Service)	7222	4360	11582	7552	4808	12360	7188	4331	11519	6780	3081	9861
Astashahada (In - service)	1071	551	1622	729	327	1056	674	318	992	429	198	627
Daraja A	11905	12137	24042	14044	11582	25626	12855	10120	22975	14576	9533	24109
Elimu maalum	187	265	452	17	34	51	52	107	159	119	110	229
Mafunzo Kazini B/C-A	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Jumla	20385	17313	37698	22342	16751	39093	20769	14876	35645	21904	12922	34826

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi

IDADI YA WANAFUNZI NA WAKUFUNZI KATIKA VYUO VIKUU KWA MWAKA 2013/2014

Jedwali Na.80D

Jina la Chuo	Umiliki	Idadi ya Wanafunzi			Idadi ya Walimu		
		Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
UNIVERSITY OF DAR-ES-SALAAM (UDSM)	Serikali	13683	7066	20749	924	282	1206
ARDHI UNIVERSITY (UCLAS)	Serikali	2563	1432	3995	167	62	229
INSTITUTE OF SOCIAL WORK	Serikali	763	1709	2472	44	20	64
SOKOINE UNIVERSITY (SUA)	Serikali	6214	2635	8849	426	106	532
NATIONAL INSTITUTE OF TRANSPORT	Serikali	2511	942	3453	83	31	114
TANZANIA OPEN UNIVERSITY- OUT (Dar & Iringa Branch)	Serikali	23867	10980	34847	125	125	250
DAR ES SALAAM MARITIME INSTITUTE	Serikali	389	55	444	30	5	35
DAR-ES-SALAAM INSTITUTE OF TECHNOLOGY (DIT)	Serikali	6582	918	7500	168	32	200
MBEYA INSTITUTE OF SCIENCE AND TECHNOLOGY	Serikali	1309	164	1473	243	26	269
INTERNATIONAL MEDICAL AND TECHNOLOGICAL UNIVERSITY (IMTU)	Binafsi	409	347	756	18	8	26
KAMPALA INTERNATIONAL UNIVERSITY -DAR ES SALAAM CAMPUS	Binafsi	1534	1053	2587	161	48	209
MUHIMBILI UNIVERSITY OF HEALTH AND ALLIED SCIENCES	Serikali	1561	882	2443	207	92	299
WELL BUGANDO UNIVERSITY COLLEGE OF HEALTH SCIENCES (WBUCHS)	Binafsi	1384	898	2282	28	22	50
SAINT AUGUSTINE UNIVERSITY OF TANZANIA (SAUT)	Binafsi	5019	3085	8104	178	155	333
MWENGE UNIVERSITY COLLEGE OF EDUCATION (MWUCE)	Binafsi	2331	774	3105	83	23	106
MOSHI UNIVERSITY COLLEGE OF COOPERATION AND BUSSINESS STUDIES (MUCCOBS)	Serikali	1769	1517	3286	131	35	166
KILIMANJARO CHRISTIAN MEDICAL CENTRE (KCMC)	Binafsi	1077	704	1781	82	35	117
STEFANO MOSHI MEMORIAL UNIVERSITY COLLEGE	Binafsi	959	743	1702	43	17	60
INSTITUTE OF FINANCE MANAGEMENT	Serikali	3332	5514	8846	34	125	159
IRINGA UNIVERSITY	Binafsi	1914	1666	3580	63	28	91
SEBASTIAN KULOWA UNIVERSITY COLLEGE (SEKUCO)	Binafsi	799	473	1272	32	35	67
TUMAINI UNIVERSITY (Dar & Iringa)	Binafsi	903	1043	1946	38	14	52
MKWAWA UNIVERSITY OF COLLEGE EDUCATION	Serikali	2852	916	3768	114	38	152
TEOFILO KISANJI UNIVERSITY	Binafsi	1995	952	2947	34	11	45
THE AGAKHAN UNIVERSITY	Binafsi	68	41	109	11	11	22
MUSLIM UNIVERSITY MOROGORO	Binafsi	890	552	1442	45	11	56
UNIVERSITY OF MOROGORO JORDANI UNIVERSITY COLLEGE	Binafsi	1990	1323	3313	79	27	106
ST. JOHN UNIVERSITY	Binafsi	1625	1151	2776	66	37	103
MZUMBE UNIVERSITY	Serikali	5839	5196	11035	212	71	283
COLLEGE OF BUSINESS EDUCATION-DAR	Serikali	5815	5694	11509	88	14	102
LOCAL GVRNT TRAINING INST. DODOMA	Serikali	918	1391	2309	35	8	43
UNIVERSITY OF DODOMA INSTITUTE OF RURAL DEVELOPMENT PLANNING (MIPANGO)	Serikali	2201	1934	4135	81	25	106
MADINI INSTITUTE- DODOMA	Serikali	520	66	586	37	4	41
DODOMA UNIVERSITY (UDOM)	Serikali	13606	6065	19671	621	166	787
ECKERNFORDE TANGA UNIVERSITY	Binafsi	391	235	626	7	31	38
INSTITUTE OF ACCOUNTANCY ARUSHA	Serikali	1990	1621	3611	82	22	104
UNIVERSITY OF HORTICULTURE TENGERU	Serikali	34	39	73	13	5	18
CENTRE FOR EDUCATIONAL DEVELOPMENT IN HEALTH ARUSHA	Serikali	16	17	33	13	11	24
LIVESTOCK TRAINING INSTITUTE COLLEGE (LITA TENGERU)	Serikali	345	175	520	31	12	43
ARUSHA TECHNICAL COLLEGE	Serikali	1194	379	1573	90	10	100
EASTERN AFRICA STATISTIC CENTRE	Serikali	283	145	428	16	8	24
MOUNT MERU UNIVERSITY	Binafsi	240	405	645	20	10	30
DARES SALAAM UNIVERSITY COLLEGE OF EDUCATION	Serikali	3194	1394	4588	127	69	196
ST. JOSEPH COLLEGE OF ENGINEERING & TECHNOLOGY	Binafsi	3325	751	4076	110	20	130
TANZANIA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY	Serikali	7587	7389	14976	92	15	107
MWL. NYERERE MEMORIAL UNIVERSITY	Serikali	847	639	1486	110	60	170
RUAHA UNIVERSITY COLLEGE	Binafsi	3490	1859	5349	78	31	109
ARUSHA UNIVERSITY	Binafsi	1852	1197	3049	48	9	57
UNIVERSITY OF NELSON MANDELA	Serikali	184	65	249	77	21	98
Jumla		144163	86191	230354	5645	2083	7728

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

SHULE ZA SEKONDARI ZA BINAFSI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO

Jedwali Na. 81							(Namba)
Mwaka	I	II	III	IV	V	VI	Jumla
2000	30789	26601	23469	20430	5894	5011	112194
2001	36305	30820	25004	20762	5892	5116	123899
2002	41593	34209	27540	20681	6418	5534	135975
2003	46891	38506	26385	21650	6430	4859	144721
2004	48752	46167	33240	24476	8847	6229	167711
2005	45276	46321	32063	29248	9183	7046	169137
2006	46968	48013	42878	29796	9569	7956	185180
2007	47437	46927	41340	35746	11299	8667	191416
2008	42971	43232	43177	35980	12576	8594	186530
2009	44255	36384	37064	34061	11851	9096	172711
2010	56620	57876	50778	46820	12269	13006	237369
2011	63282	67205	65859	54521	11083	11926	273876
2012	65058	69403	64453	61209	9684	11713	281520
2013	70060	77407	67998	65637	8592	9651	299345
2014	109784	96732	76574	66898	8865	7686	366539
Badiliko (%)							
2013 - 2014	56.7	25.0	12.6	1.9	3.2	-20.4	22.4

SURA YA 20

AFYA

Kiwango cha Ukuaji

404. Shughuli ya utoaji wa huduma za afya ambayo inajumuisha utoaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii katika ngazi zote kuanzia zahanati, vituo vya afya, hospitali na hospitali za rufaa na huduma za afya zinazotolewa kwenye kaya pamoja na shughuli nyingine za kijamii zisizoshirikisha wataalam wa afya zilikua kwa kiwango cha asilimia 5.2 mwaka 2016 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.7 mwaka 2015. Hii ilitokana na juhudi endelevu za Serikali kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya zenye ubora unaokubalika. Mchango wa Shughuli hii katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.4 kwa mwaka 2016 ambayo ni sawa na mwaka 2015.

Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba

405. Serikali ilianzisha utaratibu wa kuviwezesha vituo vya kutolea huduma za afya kupata mikopo kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi nchini ambapo mwaka 2016 utaratibu huu ulionyesha mafanikio makubwa ambapo jumla ya vituo 226 vimeshafadika na mikopo hiyo. Aidha, vituo vinavyokopeshwa hutakiwa kurejesha mikopo hiyo baada ya miaka mitatu kupitia fedha wanazodai kutokana kuhudumia wanachama wa Mfuko. Vile vile, Serikali ilianzisha utaratibu wa hospitali kutumia mifumo ya kielektroniki katika utendaji kazi ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa, ukusanyaji na usimamizi wa mapato. Hadi Desemba 2016, Serikali ilikuwa imefunga mfumo wa kielektroniki katika Taasisi ya Mifupa (MOI) na hospitali za rufaa za mikoa ya Singida na Tabora (Kitete). Halikadhalika, Serikali ilikuwa ikiendelea na mchakato wa kufunga mfumo huu kwenye Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete na Hospitali ya Rufaa ya Mbeya.

Vituo vya Kutolea Huduma ya Afya

406. Mwaka 2016, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) kwa lengo la kuboresha huduma za tiba. Katika kutekeleza Mpango huo, idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya iliongezeka kutoka vituo 7,249 mwaka 2015 hadi vituo 7,346 mwaka 2016. Vituo hivi vinajumuisha hospitali maalum na za rufaa. Vituo 5,431 kati ya vituo vyote ni vya Serikali na vituo 1,865 ni vya taasisi binafsi na mashirika ya dini. Katika kuhakikisha ubora wa huduma katika vituo vya afya ngazi ya msingi serikali iliendelea kufanya tathmini na ukaguzi mara kwa mara katika mikoa yote 26.

407. Mwaka 2016, jumla ya watu 32,463,458 walihudhuria kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ikilinganishwa na watu 31,307,601 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 4.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za afya na kuwa karibu na jamii sambamba na jitihada za Serikali za kutoa huduma za kinga na kuhamasisha watu kupima afya zao. Mahudhurio ya wagonjwa wa nje yalikuwa mengi zaidi katika zahanati kwa asilimia 64.3, vituo vya afya (asilimia 20.1), hospitali (asilimia 15.3) na kliniki (asilimia 0.3). Aidha, idadi ya wagonjwa waliolazwa ilikuwa 1,775,835 ikilinganishwa na wagonjwa 1,858,956 waliolazwa mwaka 2015.

Mafunzo kwa watumishi wa kada ya Afya

408. Mwaka 2016, Serikali iliendelea kuboresha huduma za afya nchini kwa kufanya upanuzi wa vyuo ili kuongeza uwezo wa vyuo vya Afya kudahili wanafunzi. Vyuo vilivyoendelea kufanyiwa upanuzi na ukarabati ambao upo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji ni Mtwara (asilimia 90), Tanga (asilimia 80), Mirembe (asilimia 90) na Mvumi (asilimia 60). Vyuo vinavyoendelea na Ujenzi ni Vyuo vya Uuguzi vya Musoma na Morogoro. Kwa upande wa mafunzo ya afya, ngazi ya cheti, stashahada na stashahada ya juu, jumla ya wanafunzi 6,407 walidahiliwa ikilinganishwa na wanafunzi 4,961 mwaka 2015.

Afya na Uzazi na Mtoto

409. Mwaka 2016, Serikali ilitekeleza mipango mbalimbali ya kuboresha afya ya uzazi na mtoto kwa lengo la kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Utekelezaji wa mipango hiyo ilihamasisha wajawazito wengi kuhudhuria kliniki ambapo idadi ya wajawazito wanaohudhuria kliniki mpaka hudhurio la nne iliongezeka kutoka asilimia 30 mwaka 2015 hadi asilimia 42 mwaka 2016 na wajawazito waliopatiwa IPT2 ili kujikinga na malaria iliongezeka kutoka asilimia 57 mwaka 2015 hadi asilimia 60.4 mwaka 2016. Aidha, uhamasishaji wa matumizi ya njia za uzazi wa mpango uliongeza watumiaji wa njia hizo kutoka asilimia 37.5 mwaka 2015 mpaka asilimia 40.5 mwaka 2016. Vile vile, matokeo ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa mwaka 2015/16 yalionesha kuwa idadi ya vifo vitokanavyo na uzazi vilikuwa 556 kati ya vizazi hai 100,000

Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria

410. Mwaka 2016, maambukizi mapya ya malaria kwa watoto chini ya miaka mitano yalipungua na kufikia asilimia 15 ikilinganishwa na asilimia 18 mwaka

2015. Aidha, Serikali iliendelea kutekeleza hatua mbalimbali ili kudhibiti ugonjwa wa malaria zikiwemo: kunyunyizia viuatilifu ukoko aina ya *actellic* ndani ya nyumba 456,252 mwaka 2016 ambapo wananchi 2,296,260 walikingwa dhidi ya Malaria ikilinganishwa na nyumba 358,958 mwaka 2015 ambapo wananchi 1,794,945 walikingwa; kununua vitendanishi (MRDT) 17,566,750 na; dawa mseto dozi 19,084,230; na kusambaza chupa 1,150,000 za dawa ya sindano ya kutibu wagonjwa wa malaria. Aidha, mwaka 2015, jumla ya vyandarua 20,547,849 vyenye viatilifu vilisambazwa katika mikoa 18 ikilinganishwa na vyandarua 24,552,919 vilivyosambazwa katika mikoa 22 mwaka 2016.

Chakula na Lishe

411. Hadi kufikia Mei 2016, jumla ya viwanda vikubwa 13 vinavyosindika vyakula viliongeza virutubishi vya vitamini na madini katika unga wa ngano na mafuta ya kula. Vilevile, viwanda vitatu (3) vyenye uwezo wa kati vilianza kuongeza virutubishi vya vitamin A katika mafuta ya alizeti ambavyo viko katika mikoa ya Manyara, Singida na Dodoma. Jumla ya kilogramu 13,462 za *premix* ya vitamini A ilinunuliwa na viwanda vinavyosindika mafuta ya kula na kilo 497,243 za virutubishi kwa ajili ya kuongeza kwenye unga wa ngano unaosindikwa na viwanda vikubwa zilinunuliwa.

IDADI YA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

Jedwali Na. 84

Aina ya Vituo	2013			2014			2015			2016		
	Binafsi	Serikali	Jumla	Binafsi	Serikali	Jumla	Binafsi	Serikali	Jumla	Binafsi	Serikali	Jumla
Zahanati	1444	4469	5913	1390	4523	5913	1419	4724	6143	1421	4789	6210
Vituo vya Afya	222	489	711	208	505	713	211	507	718	259	508	767
Hospitali	130	124	254	130	124	254	128	124	252	146	119	265
Nyinginezo*			0	79	10	89	133	3	136	39	15	54
Maternity Homes												50
Jumla	1796	5082	6878	1807	5162	6969	1891	5358	7249	1865	5431	7346

Chanzo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

* Ni pamoja na kliniki

HUDUMA ZA AFYA : WALIOFAULU MAFUNZO YA AFYA

Jedwali Na.85

Aina ya Mafunzo	2011/12	2012/13	2013/14	2014/15	2015/16
Doctor of Medicine (MO)	278	174	-	-	-
Advanced Diploma in AMO Anaesthesia	4	2	-	3	3
Advanced Diploma in Clinical Dentistry	-	1	-	7	-
Advanced Diploma in Clinical Medicine	207	189	59	130	34
Advanced Diploma in Ophthalmology	6	6	-	10	3
Advanced Diploma in Vector Control	14	20	7	12	-
Diploma in Clinical Medicine	444	185	-	700	440
Diploma in Dental Laboratory Technology	4	4	4	4	4
Diploma in Dental Therapy	50	51	-	47	26
Diploma in Diagnostic Radiography	41	45	-	55	-
Diploma in Environmental Health Science	159	204	116	136	75
Diploma in Health Laboratory Sciences	148	188	44	-	-
Diploma in Health Personnel Education	37	38	23	29	-
Diploma in Medical Laboratory Sciences	133	174	44	194	40
Diploma in Nursing and Midwifery	878	1052	508	1156	-
Diploma in Occupational Therapy	6	14	-	12	-
Diploma in Optometry	13	16	-	11	10
Diploma in Pharmaceutical Sciences	130	118	40	184	137
Diploma in Physiotherapy	19	22	26	20	7
Certificate in Clinical Medicine	-	-	-	830	110
Certificate in Medical Laboratory Sciences	-	-	-	506	271
Certificate in Health Record Technology	-	-	-	48	16
Certificate in Pharmaceutical Sciences	-	-	-	150	-
Certificate in Nursing	-	-	-	2740	-
	2571	2503	871	6984	1176

Chanzo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

- Takwimu hazikupatikana

IDADI YA WAGONJWA KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

Jedwali Na. 86

Mwaka	Wagonjwa wa Nje			Jumla ya Wagonjwa waliolazwa
	Hospitali	Zahanati	Vituo vya Afya	
1995	355483	6785925	545921	240707
1996	604023	9530361	927606	541781
1997	711222	10003245	1052326	559949
1998	750465	10112305	1134242	-
1999	812891	10321654	1242354	626700
2000	989101	13697988	1874346	626700
2001	1167139	17218371	2511624	680263
2002	1328395	19695356	3258520	701568
2003	1491909	22935688	3659615	1390273
2004	1532028	23552460	3758027	2125388
2005	1619700	24900276	3973085	2237146
2006	1754925	26979136	4304787	2837252
2007	1842671	28328093	4520026	2979115
2008	1934805	29744498	4746027	3128071
2009	2128286	32718948	5220630	3440870
2010	2341114	35990843	5742693	3784957
2011	2622048	39917117	6431816	4239152
2012	2815529	41333522	6657817	4388108
2013	2903275	42682479	6873056	4529971
2014	5910725	14008692	475295	1665935
2015	4480781	25072487	6006466	1858956
2016	4984645	20859281	6515219	1775835

Chanzo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

IDADI YA WATAALAMU WA AFYA

Jedwali Na. 87

Kada	2016
Madaktari wote - MO (Wageni na Wazalendo)	2229
Madaktari Wasaidizi (AMO)	2156
Wafamasia (PH)	559
Watabibu (MA)	26788
Clinical Officers	7636
Environmenta Health Officers	508
Assistant Environmental Health Officers	1611
Laboratory Technologist	1415
Chemist	49
Record Management Assistants	142
Nurse	22,978
Assistant Nursing Officer	7,729
Scientists	25
Pharmaceutica Technologists	510
Dental Assistants	26
Dental Surgeon	134

Chanzo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

IDADI YA VITANDA KATIKA HOSPITALI ZOTE NCHINI KATIKA MWAKA 2016

Jedwali Na. 87A

Aina ya Huduma	Mmiliki				Jumla
	Serikali	Shirika la Umma	Shirika la Kujitolea/Dini	Binafsi	
Hospital za Mkoa	5158	260	0	0	5418
Hospitali za Wilaya	8693	0	6618	0	15311
Hospitali nyingine	935	154	2705	462	4256
Vituo vya Afya	8933	672	3993	1506	15104
Zahanati	12166	790	4127	2585	19668
Jumla	35885	1876	17443	4553	59757

Chanzo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

SURA YA 21

MAENDELEO YA JAMII

Mafunzo ya Maendeleo ya Jamii

412. Mwaka 2016, Serikali iliendelea kusimamia utoaji wa mafunzo ya maendeleo ya jamii katika vyuo nane vya maendeleo ya jamii na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Jumla ya wanafunzi 2,201 walidahiliwa kati ya hao, wanawake walikuwa 1,370 na wanaume 831 ikilinganishwa na wadhahiliwa 2,456 kati ya hao, wanawake walikuwa 993 na wanaume 1,463 kwa mwaka 2015, ikiwa ni upungufu wa asilimia 11.6. Aidha, kati ya wanafunzi waliodahiliwa mwaka 2016, ngazi ya astashahada walikuwa 1,820, stashahada 140, Shahada 239 na Stashahada ya Uzamili wawili (2) ikilinganishwa na ngazi ya astashahada 1,242 stashahada 1,105, Shahada 200 na Stashahada ya Uzamili 9 mwaka 2015 . Kwa upande mwingine, jumla ya wanachuo 3,576 walihitimu katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru pamoja na Vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii ambapo wanaume walikuwa 1,447 na wanawake 2,129 ikilinganishwa na wahitimu 4,502 ambapo wanaume walikuwa 1,743 na wanawake 2,759 mwaka 2015, sawa na upungufu wa asilimia 20.6. Aidha, wahitimu hao katika ngazi ya astashahada walikuwa 2,118, stashahada 1,181, shahada 190 na stashahada ya uzamili 10 mwaka 2016 ikilinganishwa na wahitimu katika ngazi ya astashahada 2,866, stashahada 1,515, shahada 117 na stashahada ya uzamili wanne (4) mwaka 2015.

Mafunzo ya Ustawi wa Jamii

413. Mwaka 2016, Serikali iliendelea kusimamia utoaji wa mafunzo ya ustawi wa jamii katika vyuo vya Serikali na binafsi ambapo jumla ya wanachuo 1,164 (wanawake 783 na wanaume 381) walihitimu ikilinganishwa na wanachuo 1,067 waliohitimu mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 9.1. Kati ya waliohitimu mwaka 2016, ngazi ya astashahada walikuwa 328, stashahada 368, shahada 432, stashahada ya uzamili 33 na shahada ya uzamili watatu (3) ikilinganishwa na wahitimu wa ngazi ya astashahada 310, stashahada 388, shahada 330 na stashahada ya uzamili 39 mwaka 2015.

Maendeleo ya Wanawake na Jinsia

414. Mwaka 2016, Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 87 zilizotokana na marejesho kutoka katika halmashauri ikilinganishwa na shilingi milioni 54 zilizotolewa kwa ajili ya mkopo mwaka 2015 ikiwa ni ongezeko la asilimia 61.1. Fedha hizo zilitolewa kwa wanawake wa halmashauri za Kisarawe, Busokelo, Gairo, Masasi na Iringa Manispaa. Aidha, Mfuko unafuata mwongozo wenye lengo la kuboresha uendeshaji, utoaji na urejeshaji wa mikopo na ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Mfuko. Vile vile, mafunzo yanayohusu faida za kujiunga katika vikundi vya kiuchumi yalitolewa kwa wanawake na wanaume takribani 450 katika halmashauri za wilaya ya Njombe na Ludewa ili lengo kuhamasisha wanawake kujiunga na SACCOS na VICOBA.

Maendeleo ya Watoto

415. Mwaka 2016, Serikali iliendelea kuzuia na kukomesha vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ambapo iliandaa na kuzindua Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 – 2021/22). Lengo la mpango huo ni kuzuia vitendo vya ukatili wa aina yoyote kwa wanawake na watoto kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2022 kupunguza tatizo la ndoa za utotoni kutoka asilimia 47 hadi asilimia 10, kupunguza mimba za utotoni kutoka asilimia 27 hadi asilimia 5 na kutokomeza ukeketaji wa watoto wa kike.

416. Katika kukabiliana na tatizo la mimba na ndoa za utotoni, Serikali iliadhimisha Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike mkoani Shinyanga. Lengo la maadhimisho hayo lilikuwa ni kuelimisha jamii wakiwemo watoto wa kike athari za mimba na ndoa za utotoni. Aidha, maadhimisho hayo yalifanyika sambamba na kutoa elimu kwa shule za sekondari kuhusu mtoto wa kike kujitambua na kujilinda dhidi ya vishawishi na mazingira yanayoweza kusababisha mimba za utotoni; kuendesha Kongamano la Mtoto wa Kike; kuelimisha wananchi wa vijiji vya kata ya Kizumbi; na kuendesha kongamano la viongozi wa Mkoa wa Shinyanga kuhusiana na mpango huu.

417. Mwaka 2016, Serikali iliendelea kukuza ushiriki wa mtoto katika maendeleo yao, ambapo iliwawezesha viongozi wa Kamati Kuu ya Baraza la Watoto kufanya ziara ya mafunzo kwenye mabaraza yanayofanya vizuri. Lengo likiwa ni kupata ujuzi na kuboresha ushiriki wa mtoto katika masuala mbalimbali yanayohusu haki na ustawi wa watoto. Aidha, Serikali iliwezesha

kuundwa kwa mabaraza 19 ya watoto ngazi ya mkoa na 108 ngazi ya wilaya kwa mwaka 2016 ikilinganishwa na mabaraza ya watoto 22 ngazi ya mkoa na 122 ngazi ya wilaya mwaka 2015.

418. Mwaka 2016, Serikali ilitoa elimu kwa jamii kuhusu madhara ya ukatili dhidi ya watoto na umuhimu wa kutoa taarifa za ukatili kwenye mamlaka husika. Aidha, Serikali kupitia namba ya simu 116 ya kuwasaidia watoto (Child Help Line – Na. 116) ilipokea taarifa 19,014 zinazohusu vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ikilinganishwa na taarifa 24,675 zilizotolewa mwaka 2015. Waathirika wa ukatili walipatiwa huduma mbalimbali za kibinadamu ikiwemo afya, ushauri, chakula, upelelezi na malazi.

Huduma za Ustawi kwa Watoto

419. Mwaka 2016, Serikali iliendelea kuratibu huduma za malezi ya watoto wa kambo na kuasili. Aidha, Serikali ilitoa leseni za makao ya watoto ili kuimarisha upatikanaji wa huduma za msingi (malazi, chakula, matibabu na mavazi) kwa watoto walio katika mazingira hatarishi. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya maombi 131 yalipokelewa, watoto 26 walifanyiwa usaili na wengine 74 walipatiwa walezi wa kambo ikilinganishwa na maombi 79 yaliyopokelewa na waombaji 17 walisailiwa mwaka 2015.

420. Mwaka 2016, Serikali iliendelea kutoa huduma za msingi za chakula, malazi, mavazi na matibabu pamoja na huduma za msaada wa kisheria kwa watoto 353, kati yao wavulana 322 na wasichana 31. Watoto hao, walikuwa katika mkinzano na sheria na walihifadhiwa katika mahabusu za watoto za Mbeya, Moshi, Tanga, Arusha na Dar es salaam. Aidha, Serikali ilifanya ukarabati wa majengo na miundo mbinu katika mahabusu ya watoto Dar es Salaam. Vile vile, Serikali ilitoa huduma za msingi ikiwa ni pamoja na elimu na mafunzo kwa watoto 617 waliobainika na makosa katika Shule ya Maadilisho Irambo Mbeya. Aidha, Serikali ilitoa mafunzo ya kujenga uwezo wa kuendesha kesi za watoto mahakamani kwa watumishi 123 ikilinganishwa na watumishi 67 waliopatiwa mafunzo mwaka 2015.

Huduma za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto

421. Mwaka 2016, Serikali iliendelea kusimamia utoaji wa huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kwa watoto wenye umri wa miaka mitatu (3) hadi miaka mitano (5) katika vituo vya kulelea watoto wadogo

mchana vya Serikali na binafsi. Aidha, Serikali ilisajili vituo 84 vya kulelea watoto wadogo wakati wa mchana na kufanya idadi ya vituo vya Serikali na binafsi kuongezeka kufikia vituo 841 mwaka 2016 ikilinganishwa na vituo 757 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 11. Vile vile, jumla ya watoto 67,240 waliandikishwa katika vituo vya kulelea watoto wadogo wakati wa mchana ambapo watoto 23,878 walikuwa wa kiume na watoto 43,362 walikuwa wa kike. Halikadhalika, Serikali ilitoa mafunzo ya kuwajengea uwezo walezi wanaotoa huduma katika makao ya watoto na vituo vya kulelea watoto wadogo mchana ambapo jumla ya walezi 713 walipatiwa mafunzo mwaka 2016 ikilinganishwa na walezi 604 waliopata mafunzo mwaka 2015

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

422. Mwaka 2016, mashirika yasiyo ya kiserikali 570 yalisajiliwa chini ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 24 ya Mwaka 2002, kama ilivyorekebisha mwaka 2005, ikilinganishwa na mashirika 563 yaliyosajiliwa mwaka 2015. Idadi ya mashirika yaliyosajiliwa katika ngazi ya wilaya ilikuwa 56, mkoa 15, taifa 469 na kimataifa 30 mwaka 2016 ikilinganishwa na mashirika 52 katika ngazi ya wilaya, 22 mkoa, 453 kitaifa na 36 kimataifa mwaka 2015. Mashirika haya yameendelea kutoa huduma na kuchangia kwenye jitihada mbalimbali za Serikali katika sekta za kilimo, afya, mazingira, elimu, maendeleo ya mtoto, haki za binadamu na utawala bora.

423. Mwaka 2016, Serikali ilipokea na kuchambua taarifa za kazi na fedha za mashirika yasiyo ya kiserikali 699 ikilinganishwa na mashirika 375 yaliyowasilisha taarifa mwaka 2015. Taarifa hizi zilisaidia Serikali katika kuimarisha usimamizi wa mashirika hayo. Aidha, Serikali ilitembelea mashirika yasiyo ya kiserikali 22 katika mikoa ya Mwanza, Arusha, Rukwa, Mara, Singida, Shinyanga, Dar es Salaam, Tanga na Morogoro kwa lengo la kuhakiki shughuli zinazofanyika. Vile vile, wadau 6,901,023 walitoa maoni kupitia tovuti ya taifa ya mashirika yasiyo ya kiserikali www.tnnc.go.tz na msajilingos.blogspot.com kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali.